

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Kumi – Tarehe 5 Februari, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 102

Watendaji Kutumiwa na Wanasiwa Kupandikiza Kesi

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkurugenzi au Afisa Utumishi ni Mtendaji wa Serikali na si mwanasiwa; na kwa kuwa, katika baadhi ya maeneo Watendaji hao hutumiwa na wanasiwa kupandikiza kesi kwa wananchi na kuwalazimisha watumishi kutoa ushahidi wa uongo:-

Je, Serikali itawachukulia hatua gani watendaji wa aina hiyo endapo watabainika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo langu la Siha naomba kuchukua nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kutimiza miaka yake 33 kwa mafanikio makubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mbunge wa Viti Malum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtumishi wa Umma anatakiwa kufanya kazi zake za kila siku kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na

marekebisho yake, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali, na kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma.

Inapobainika kuwa mtumishi wa Umma amekiuka taratibu hizo inabidi mwajiri wake amchukulie hatua za kinidhamu kulingana na utaratibu uliofanuliwa kwenye Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Taratibu hizo ni kumpatia hati ya mashtaka ili aweze kujitetea, kumsimamisha kazi ili kuruhusu Kamati ya Uchunguzi ambayo itapewa Mamlaka ya kumshauri Afisa wa Nidhamu (mwajiri) juu ya makosa yatakayobainika. Ushauri wa Kamati hiyo unaweza kumsaidia mwajiri kufikia uamuzi ama kutoa onyo kali au kumfukuza kazi mtuhumiwa kwa kuzingatia uzito wa kosa na ushahidi uliopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa raia yejote, ni kosa pia kwa Mtumishi wa Umma kutoa ushahidi wa uongo Mahakamani. Hivyo, mwananchi ambaye amebambikiwa kesi kutokana na Mtumishi wa Umma kutoa ushahidi wa uongo Mahakamani, yuko huru na anayo haki ya kumfungulia mtumishi huyo mashtaka Mahakamani ili Sheria iweze kuchukua mkondo wake. Aidha, endapo atapatikana na hatia na kufungwa atafukuzwa kazi kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa wakati wa Uchaguzi TAMISEMI au Serikali kwa ujumla hutoa mafunzo kwa watendaji wake pamoja na wananchi. Na kwa kuwa watendaji hawa naamini kwamba wanafahamu na wanaelewa, lakini wanakwenda kinyume cha hayo na mwananchi anapojoitokeza aliyepata mafunzo kama yeje kuelezea ukweli uliopo kumsingizia kesi kama hizo na kumlazimisha mtendaji akatoe ushahidi wa uongo Mahakamani na sisi tuko hapa kwa ajili ya kutangaza utawala bora na muda wote tunazungumzia utawala bora, je, huo ndio utawala bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nimekuwa nikitoa malalamiko ya aina hii katika maeneo yangu na nilikuwa najibowi hapa kwamba tutashughulikia, nitapiga simu sasa hivi nitaongea nao, lakini haya hayatokei. Je, Serikali haioni kwamba hii ndiyo sababu ya hawa watendaji kuendelea kututendea mambo kama haya kwa wananchi wa maeneo ambayo yana upinzani wa nguvu. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Kilwa nimekwenda na nimefika na Mheshimiwa Mbunge Mwanawetu anapozungumza hapa ninaelewa anayosema hapa. Lakini nataka niseme hapa kwa hawa watendaji anaozungumzia hapa swalii liliyokuwa limewekwa nilitegemea sasa kwamba atafika mahali atanitajia kisa maalum ambacho nitakichukua sasa nitaondoka nacho. Hapa anazungumza kuhusu watendaji ambao tunawapa semina na tunawapa mafunzo ili wakasimamie utaratibu wa Uchaguzi kama ilivyo elekezwa katika sheria za nchi. Nataka niseme hapa kwa maoni

yangu na ninavyofahamu Uchaguzi huu uliofanyika safari hii umefanyika vizuri na umesimamiwa vizuri na sisi tumeambiwa kwamba umekwenda vizuri.

Ninachosema sasa maana yake huyu ni Mbunge, Mbunge akisema jambo hapa siwezi kulichukulia tu kienyejenyeji analo tatizo maalum anajua kwamba kuna mtendaji ambaye amefanya hivi alivyosema. Ametoka Mtendaji akaenda Mahakamani akatoa ushahidi wa uongo Serikali hii haiwezi kukubali jambo la namna hii hata kidogo. Ni lazima tuchukue hatua kwa hiyo atuambie.

Hili la pili analolizungumzia la kupiga simu, kwamba nikitoka hapa ninasema nitapiga simu, huwa napiga na namwambia Mtendaji anayehusika, sasa nikishapiga simu, wako watu wengine wanaofanya kazi Ofisi ya Waziri Mkuu wako chini yangu, ndio wanatekeleza. Mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane kama kuna jambo lolote linampa taabu nataka nimthibitishie mbele ya Bunge lako kwamba tutachukua hatua.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora ni katika pande zote, upande wa uongozi pia upande wa wananchi. Sisi kama viongozi tukipewa Semina kwa watendaji wetu tunawaeleza Kanuni, taratibu na sheria. Na wananchi wanaweza wakapewa semina kama hiyo lakini sisi ndio wenyewe miongozo na kile ambacho tunakitoa ndicho chenye uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema Mheshimiwa Mwanawetu naomba kama ana *specific issue* angetuletea lakini mara nyingi maswali yake hayako *straight* huwa hayako moja kwa moja anazunguka. Sisi tunasema kama kuna kesi maalum ni vyema akatuletea tukaishughulikia na tukamaliza moja kwa moja na bila ya kujirudia.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inapotambua kwamba baada ya siku kadhaa kutakuwa na chaguzi au Uchaguzi Mkuu au Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa nini basi wasiwapeleke semina watendaji hawa mapema kulikoni kuwapeleka wakati wananchi wanatarajia kurudisha fomu na kukwaza wananchi kurudisha fomu kwa wakati muafaka wakikuta ofisi hizo zimefungwa. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na hili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa chaguzi mbalimbali ni kweli watendaji wetu huwa tunawapa semina ili kuwapa miongozo mbalimbali. Mara nyingi huwa tunafanya karibu na Uchaguzi ili waweze kukumbuka yale ambayo tunawaasa.

Sasa kama ilitokea kweli kwamba kuna tatizo la watendaji kufunga ofisi na watu wanarudisha fomu wakati huo huo kwa kweli labda hilo ni tatizo la sehemu maalum. Lakini ujumla Tanzania nzima tulikuwa na ratiba maalum ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na ilikuwa muda kwa muda, siku ya semina inakuwa tofauti na siku ya kurudisha fomu na kadhalika na kadhalika. Kama kulikuwa na suala maalum ningeomba Mheshimiwa Mbunge angetuletea ili tuone kwamba huko mbele ya safari tutarekebisha namna gani.

Sasa hivi Ofisi yangu imetoa waraka maalum kwamba vyama vyote via siasa, wananchi wote watuletee maoni yao kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Sasa kama kulikuwa na mapungufu ni vyema mkatuletea ili huko mbele ya safari tukawenza kurekebisha hizo kasoro ambazo zimejitokeza.

Na. 103

Kuhusu Utupaji wa Takataka Kwa Wasafiri wa Mabasi

MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza swali langu naomba nichukue fursa hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia iliyopatwa na msiba baada ya ndugu zao wapatao wanne kufariki kutokana na ajali ya moshi wa jenereta. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema. (*Amin*)

Baada ya kupata fursa hiyo naomba sasa kuuliza swali kama ifuatavyo. Kwa kuwa, Serikali iliahidi kuwa inao mpango kabambe wa kuwataka wenyewe mabasi kuweka kwenye mabasi yao vyombo vya kuhifadhi takataka wakati wa safari ili kuepuka utupaji hovyo wa takataka barabarani wakati wa safari:-

Je, hadi sasa mpango huo umefikia wapi; na kama umeanza ni mabasi ya kwenda wapi yanautekeleza mpango huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeanza jitihada za kudhibiti taka kwenye vyombo vya usafiri na usafirishaji nchini. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*), kwa kushirikiana na (*SUMATRA*) walizindua kampeni kabambe ya mpango wa udhibiti wa taka kwenye vyombo vya usafiri hasa mabasi yaendayo mikoani.

Aidha, Baraza kwa kushirikiana na wadau wameweka mikakati ya kukabiliana na tatizo la utupaji ovyo wa taka hasa mabaki ya chakula, chupa za plastiki na kwenda haja o vyo wakati wa safari maarufu kama kuchimba dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni inayohusu Viwango vya Ubora wa Magari pamoja na Huduma (*the SUMATRA – Technical Safety and Quality of Service Standards (Passenger Vehicles) Rules, 2008*) imeandaliwa. Aidha, kifungu namba 18 cha Kanuni hiyo, kinaagiza wasafirishaji kuhakikisha kuwa abiria wanapanda mabasi au wanapumzika/wanajisaidia katika vituo ambavyo vina huduma muhimu kama vivuli vya kupumzikia, huduma za vinywaji/chakula na vyoo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Kanuni hii na mpango wa uthibiti taka kwenye vyombo vya usafiri vinakwenda sanjari na utoaji wa elimu kwa umma katika maeneo mbalimbali kama vile kwenye vituo vikuu vya mabasi yaendayo mikoani, na vituo vikubwa vya mabasi (daladala) mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutekeleza mpango huu baadhi ya mabasi yaendayo barabara ya kaskazini mwa nchi yameanza kutekeleza mpango huu. Mpaka sasa makampuni ya mabasi sita ambayo ni *Dar Express, Hood, Mohamed Trans, Sumry, Saibaba na Scandinavia*, yanatekeleza mpango huu. Vile vile Makampuni ya Mabasi kumi yaendayo mikoa ya Mwanza, Tabora, Shinyanga, Dodoma, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Lindi na Mtwara yameanza kutekeleza mpango huu nayo ni *ABC, Hekima, Hood, Mohamed Trans, Najimunisa, Super Ferro, SABCO, Scandinavia, Saibaba na Sumry*.

Aidha, kwa Jiji la Dar es Salaam, baadhi ya daladala zimeweka vifaa vya kukusanya uchafu ndani ya mabasi. Hata hivyo juhudhi bado zinafanywa za kuboresha vifaa hivyo na kuendeleza ukaguzi. Tunataka mabasi yote yanayotoa huduma ya familia kuendelea na utaratibu huu na kutekeleza agizo hili. (*Makofî*)

MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa suala la kuweka mifuko kwa ajili ya kutupa takataka kwenye mabasi ni kitu kimoja, lakini suala la utekelezaji ni kitu kingine. Je, sasa Serikali ina mpango gani kwanza wa kuwaelimisha hao makondakta na madereva wao kwamba abiria anapoingia apewe *instruction* kwamba unapotaka kutupa takataka itupwe kwenye hifadhi inayohitajika kuliko kuacha kama ilivyo sasa hivi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Masolwa Cosmas Masolwa kwa jinsi alivyokuwa mfuatiliaji wa masuala haya ya mazingira.

Katika kumjibu swali lake la nyongeza kuhusu umuhimu wa kutoa elimi napenda kusema kwamba hili tumeliona ni jambo kubwa sana na ndiyo maana pamoja na kuwa

sheria inataka yule ambaye anavunja sheria kwa maana ya kutupa taka ovyo ama kujisaidia ovyo basi atozwe shilingi 50,000 hapo hapo ama adhabu ya kifungo cha miezi mitatu (3).

Lakini makosa ya uchafuzi wa mazingira faini yake inafika mpaka shilingi 50,000,000 na kifungo cha miaka saba (7) au vyote viwili kwa pamoja. Kwa hivyo sisi tunasema tutaendelea kutoa elimu, pale elimu ikionekana haijafikia wananchi vizuri adhabu itaanza kutumika na adhabu itaendelea kutumika pamoja na elimu vyote kwa pamoja. (*Makofi*)

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika Jiji la Dar es Salaam hivi sasa kuna adha kubwa ya taka kutupwa maeneo ya wananchi na kuhatarisha maisha yao na afya zao. Vile vile katika Jiji la Dar es Salaam limetafutwa eneo sasa la mbali ili kupeleka taka zile. Ni kikwazo gani kinachosababisha taka zisiondolewe maeneo ya wananchi na kupelekwa sehemu ambayo imetengwa na Serikali?

NAIBU SPIKA: Jamani hili swali lilikuwa kwenye magari, sasa wewe umesemea mambo ya uchafu. Mheshimiwa basi useme kwa manufaa ya wananchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyojuwa Mheshimiwa Mbunge ni Kiongozi pale Jiji la Dar es Salaam na ye ye tukishirikiana pamoja kubana Taasisi mbalimbali zinazoshiriki katika suala zima tutafanikiwa. (*Makofi*)

Lakini hata hivyo kwa mujibu au kwa faida ya wananchi wote suala la Dar es Salaam ni suala gumu kidogo na sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tumeona tushirikiane na wenzetu wa Jiji la Dar es Salaam katika kutoa ufumbuzi kwanza wa kutoa taka zote ambazo zimekuwa ziki *pile-up* kwa muda mrefu na kuweza kuwafanya sasa Dar es Salaam waendelee kufanya kazi ya utoaji wa taka.

Tunashirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri zote kuhakikisha kwamba kunakuwa na vifaa vya kuchukulia taka zile kupeleka katika dampo lile la Pugu Kinyamwezi lakini kuweza kuona kwamba hii ni kampeni ambayo tutaiendesha kwa miezi sita. Tumeomba ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Mazingira ya UNEP ili kuwa na programu kabambe ya *clean up Dar es Salaam* au Safisha Jiji la Dar es Salaam, kama walivyofanya wenzetu wa Kenya, Safisha Nairobi. Kwa hivyo huo ndio mkakati ambao tunataka tuufanye kwa pamoja halafu tulikabidhi Jiji letu na kuweza kuona kwamba wataendelea vipi?

Na. 104

Hitaji la Kiwanda cha Kusindika Samaki Kigoma

MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI aliuliza:-

Kwa kuwa, Ziwa Tanganyika lina rasilimali ya Samaki wa kila aina wanaopendwa nchi nzima pamoja na nchi jirani hivyo kuwepo uwezekano mkubwa wa kupata masoko mengi nchi za nje; na kwa kuwa, hivi sasa wakazi wengi wa Mkoa huo wanajishughulisha sana na uvuvi na wengi wana nyenzo duni:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaweka Kiwanda cha Kusindika Samaki katika Mkoa wa Kigoma?
- (b) Kwa kuwa, nyenzo duni husababisha uvuvi hafifu Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mradi wa kuwakopesha vifaa vya uvuvi pamoja na kuwapa mitaji ili wavuvi nao waweze kuendesha uvuvi wa kisasa na wenye tija?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kilontsi Mporegomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijihusishi moja kwa moja na uwekaji au ujenzi wa viwanda vikiwemo viwanda vya kusindika samaki. Kazi ya Serikali ni kuweka mazingira mazuri ya uzalishaji na kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda kwenye maeneo yote yenye fursa za uwekezaji yakiwemo maeneo ya uvuvi. Mazingira hayo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu.

Aidha, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Kuendeleza Maeneo ya uzalishaji kwa Mauzo Nje (*EPZA*), imebaini Mkoa wa Kigoma kuwa Kanda Maalum ya Kiuchumi (*Kigoma Special Economic Zone (KISEZ)*).

- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa nyenzo duni husababisha uvuvi hafifu na Serikali inalitambua hilo. Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali kupitia mradi unganishi wa Mkoa wa Kigoma (*Lake Tanganyika Regional Intergrated Development Programme*). Unatekelezwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, katika kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya uvuvi (*Beach Management Unit (BMU)*) ambapo watafundishwa uvuvi endelevu.

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Vile vile, mpango huo unalenga kusaidia katika upatikanaji wa mitaji, vifaa vya kisasa na mahitaji muhimu ya wavuvi kwa kadri vikundi hivyo vitakavyo elekeza kupitia maandiko ya miradi ya vikundi husika.

MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sekta ya uvuvi ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na kwa kuwa wengi wanajishughulisha sana na sekta hii ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini labda niulize tu kwamba zaidi ya tamko la Serikali la kuanzishwa kwa EPZA ni mazingira mazuri mengine yapi ambayo Serikali imeweka?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa ninapokwenda Mkoa wa Kigoma huwa natembelea wavuvi wengi kutoka jumboni kwangu na wengi wanaonekana hata huu mradi hawana taarifa nao. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatembelea Mkoa wa Kigoma ukanda wa Ziwa Tanganyika akazungumza na wavuvi hawa na kuwaeleza juu ya mradi huu maana hawana taarifa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ADB itatoa dola za Kimarekani milioni 6 ambazo zitasaidia katika kujenga mihalo, kujenga barabara, kujenga masoko madogo madogo na vituo vya afya. Vile vile *Nordic Development Fund* watatoa Euro milioni 6 ambazo zitasaidia kununua meli kwa ajili ya kazi hiyo na meli hiyo itaanza kutengenezwa Julai, 2010. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia kwamba kwa mazingira haya ambayo itawekwa, miundombinu ambayo itawekwa itasaidia sana kwa wawekezaji kuhamasika kuja kuwekeza katika Mkoa wa Kigoma. UNDP pia watatoa dola milioni 2.5 kwa ajili ya mazingira na ufahamu katika masuala ya majitaka na majisafi.

Swali lake la pili, kuhusu Waziri kutembelea, Serikali inakubali Mheshimiwa Waziri atatembelea maeneo hayo ili aweze kuwaelimisha kwa kusaidiana na Mheshimiwa Mbunge kuweza kuwaelewesha wananchi kuhusiana na mradi huo.

NAIBU SPIKA: Sio lazima Waziri hata wataalam wake maana yake sema hawaujui kabisa.

Na. 105

**Vikundi vya Wanawake Katika
Biashara Ndogo Ndogo**

MHE. AMEIR ALI AMEIR aliuliza:-

Kwa kuwa, wanawake wengi wameitikia wito wa Taifa wa kijiungu na vikundi kufanya biashara ndogo ili kujikwamua na umaskini; na kwa kuwa, wamekuwa wabunifu na kufanya bidhaa zao kuwa bora na kuipatia sifa nchi yetu katika Maonyesho ya Jua Kali yaliyofanyika Rwanda ambapo Tanzania imeshika nafasi ya kwanza kwa ubora wa bidhaa ingawa wanakutana na vikwazo vya urasimu mkubwa wa kupata vibali vya ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*):-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, urasimu huo ni usumbufu na unawanyima akina mama fursa ya kufanya biashara nje ya nchi na hivyo kuwapunguzia soko?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondolea kero hiyo akina mama hao ili wafikie matarajio na kufuta kauli kwamba nchi jirani zinatuzidi kibiashara?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA(K.n.y.
WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, wanawake wengi wameitikia wito wa Taifa wa kijiunga na vikundi, kufanya biashara ndogo ndogo ili kujikwamua na umaskini. Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wanawake wabunifu ambaa baadhi yao bidhaa zao zimekuwa bora na kuipatia sifa maonesho ya Jua Kali, yaliyofanyika Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni, *TBS* imetoa leseni za ubora zipatazo 109, kwa wajasiriamali mbalimbali kote nchini. Aidha, mwaka 2009 *TBS* ilianza utaratibu wa kutembelea wajasiriamali na kuwapa ushauri jinsi ya kutengeneza bidhaa zenye ubora na hadi kufikia Desemba, 2009 *TBS* imetembelea wajasiriamali mbalimbali nchini zilizowezesha wajasiriamali 9 kupata leseni za ubora.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2009 *TBS* ilitoa mafunzo katika Tamasha la Wajasiriamali Wanawake lilifanyika Dar es Salaam. Wajasiriamali 24 kati ya washiriki 78 walijaza fomu za maombi ya kukaguliwa kwa sehemu zao za uzalishaji wa bidhaa, inatarajiwa kwamba taratibu zikikamilika wahusika watapatiwa leseni za kutumia alama ya ubora kwenye bidhaa zao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mipango mingine ya kuwaondolea kero walengwa ni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo juu ya viwango na uthibitishaji ubora, kutumia Mfuko wa *SME Competitiveness Facility* (*SCF* ili kuwawezesha kuhimili ushindani na kuendelea kuimarisha asasi zinazohusika na masuala ya upatikanaji wa masoko ikiwemo:-

- (i) Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*); na
- (ii) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*).

Utekelezaji wa mipango hiyo pamoja na juhudzi zilizotajwa awali vitachangia katika kufikia matarajio ya walengwa na hivyo kufuta dhana kwamba nchi jirani zinatuzidi kibiashara.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imejitahidi kuwapa leseni vikundi 109 pamoja na mafunzo, je, Serikali imejipanga vipi kuwapatia masoko ya nje akina mama hawa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba upatikanaji wa masoko Halmashauri ya Bidhaa ya Biashara za Nje yaani (BET) pamoja na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) vitashirikiana na wajasiriamali hawa katika kuwatafutia masoko.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge hili kwamba suala la MKUKUTA liko kwenye Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na suala la MKUZA liko kwenye Ofisi ya Rais ya Zanzibar.

Bidhaa inapotoka ndani ya Jamhuri ya Muungano kwenda nje huwa inahesabika kuwa hii ni bidhaa ya Tanzania. Ofisi ya Rais kupitia MKUKUTA inashirikiana vipi na MKUZA ili bidhaa zinazotoka Zanzibar ziwe na ubora unaotakiwa na kuwasaidia akinamama katika kuendesha maisha yao ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimwa Naibu Spika, nadhani wazo lake ni zuri kama hilo halifanyiki mahusiano ya vyombo hivi kama hayahusiki basi nadhani wazo lake ni zuri tunalichukulia hapo tutalifanya kazi, lakini nadhani kwa sababu Serikali ni moja kazi hiyo inafanyika.

Na. 106

**Wahadhiri wa Vyuo Vikuu Kwenda Nje ya Nchi
Kutafuta Maslahi**

MHE. HALIMA J. MDEE (K.n.y. MHE. SUSAN A. LYIMO aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ni msingi wa maendeleo na kwamba elimu bora hutokana na vitendea kazi bora ikiwa ni pamoja na walimu bora; na kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la wahadhiri wa vyuo vikuu kwenda nje ya nchi hususan Rwanda na Burundi kwa kile kinachoitwa kufuata Mishahara Bora.

- (a) Je, ni kweli Serikali yetu imeshindwa kuwabakisha wasomi wetu nchini?
- (b) Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi kuhakikisha wasomi wetu wanaboreshwaa mazingira yao ya kazi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. GAUDENSIA M. KABAKA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vipindi tofauti katika miaka ya nyuma wanataaluma wachache huondoka kwenda nje ya nchi kwa lengola kutafuta maslahi kutokana na sababu zifuatazo:-

- Hali ya uchumi wa nchi yetu ambao haukuwa mzuri.
- Mishahara bora zaidi katika Vyuo Vikuu na Taasisi waendako.
- Mazingira bora zaidi ya kufundisha na utafiti huko waendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu haijashindwa kuwabakisha wasomi wetu hapa nchini. Aidha mwaka 2004/2005 Serikali ilipandisha viwango vya mishahara kwa Wahadhi na Maprofesa wa Vyuo Vikuu vya Umma pamoja na posho stahili zao. Serikali pia inawezesha vyuo vikuu kwa njia ya mikopo katika kujenga miundombinu, ofisi na kununua vifaa vya kufundishia kupitia kwa wabia wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukua hatua za makusudi kuhakikisha wasomi wanaboresha mazingira yao ya kazi kwa njia zifuatizo:-

- Kuwatumia wanataaluma wa Vyuo Vikuu kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali. Hali hii inawatia moyo sana kwa vile inawapa wao na vyuo vyao mapato zaidi na kuthamini taaluma zao.
- Serikali imekuwa inaongeza ruzuku kwa vyuo vikuu mwaka hadi mwaka kupitia kwenye Bajeti ya kila mwaka, misaada ya wabia wa maendeleo kwa ajili ya kufundishia na utafiti.
- Kuhakikisha kuwa ulipaji wa haki za wafanyakazi *Staturoty rights* zinaboresha na kulipwa kwa wakati.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru, hivi karibuni Serikali imemnyima mkataba Profesa Baregu ambaye ni Mtaalamu wa masuala ya uongozi na mahusiano ya kimataifa kwa sababu tu ana mahusiano na Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA):-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kwa kumnyima mkataba huu imewaondolea haki watoto wa Kitanzania kupata uzoefu wa Profesa huyu?

(b) Kuna ushahidi unaoonesha kwamba kuna Makada wa Chama cha Mapinduzi ambao wako kwenye nafasi za uongozi wa Chama na wao pia ni watumishi wa umma. Je, Serikali inaliambia Bunge hili ushahidi ukiletwa unaowahuisha Makada wa CCM na uongozi wa Chama, Serikali itakuwa tayari kuwavua kazi kama walivyofanya kwa Profesa Baregu? (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mdee, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza swali la msingi linaongea juu ya wahadhiri wanaondoka nchini kwa sababu ya maslahi kidogo. Sasa huyu Profesa anang'angania humu ndani nchini, hivi kweli kama maslahi yangekuwa madogo angeweza kung'ang'ania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Baregu alistaafu mwaka 1999 na amekuwa anaongezewa muda kwa kufanya kazi kwa mkataba tangu wakati ule. Sasa wakati umefika Mwajiri amejenga uwezo wa mtalaamu mwagine kuchukua nafasi ile na hivyo hakuna tena sababu ya Profesa Baregu kupewa nafasi ya kufundisha pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tena Profesa Baregu hakuondolewa kwa sababu eti tu ni kiongozi wa CHADEMA maana wako viongozi wa vyama vingine ambao pia tunao kwenye kazi na ambao hawajastaafu. Lakini *discretion* ya kumwongezea mtumishi muda ni *discretion* ya mwajiri. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri hajajibu swali langu la pili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa amejibu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa hajajibu swali langu la pili.

NAIBU SPIKA: Amejibu mimi nimesikia. Hukupenda kuridhika basi. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 107

Upungufu wa Walimu Shinyanga

MHE. AHMED ALLY SALIM aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga una upungufu mkubwa sana wa Walimu likiwemo Jimbo la Solwa; na kwa kuwa Serikali inapoleta Walimu Mkoa wa Shinyanga wengi wao hawaripoti kwa kutoridhishwa na mazingira yalivyo:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutuletea Walimu ambao wametoka maeneo yetu ili kupata Walimu ambao wamezoea mazingira haya na hivyo kuondoa tatizo la uhaba wa Walimu?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutuletea Walimu wa kutosha?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la uhaba wa walimu nchini na imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kutatua tatizo hili. Aidha imekuwa ikiwapanga walimu kuzingatia mahitaji ya sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kujenga utaifa na uzalendo, umoja na mshikamano baina ya wananchi wake bila kuzingatia maeneo wanayotoka au imani za kidini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutoa wito kwa Halmashauri kuweka mazingira bora ya mapokezi ya walimu wapya ili waweze kuvutiwa kubaki kufanya kazi katika Halmashauri nchini ikiwemo Wilaya ya Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu imepanga walimu 2330 katika Mkoa wa Shinyanga, kama ifuatavyo:-

Mwezi Oktoba, 2009 jumla ya walimu wenye Shahada 179 na walimu wenye Stashahada 233 walipangwa Mkoani Shinyanga katika awamu ya kwanza, awamu ya pili walimu wenye Shahada 31, walimu wenye Stashahada 32 na walimu wa Cheti 1,855 walipangwa huko na kufanya jumla ya walimu waliopangwa Mkoa wa Shinyanga kuwa 2,330.

MHE. AHMED ALLY SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Sina tatizo na utaifa au mshikamano wa nchi yetu, kwa kuwa tatizo lipo pale pale hivi juzi tumepata walimu 134 lakini walimu 19 wameingia mitini na kama bado wapo

Walimu ambao wanaweza wakatoka nje ya Mkoa wa Shinyanga wana uzoefu wa kuishi kwenye maeneo ya Vijijini.

(a) Je, Serikali inasema nini kutuletea Walimu hao ambao wametoka nje ya Mkoa wa Shinyanga wanaweza kuja kujenga umoja na mshikamano wa kitaifa katika Mkoa wetu na wakaja bila kuingia mitini?

(b) Kwa kuwa Halmashauri yetu inafanya kazi kubwa mno ya kujenga mazingira mazuri, lakini uwezo wa mazingira mazuri ni nyumba za Walimu. Je, Serikali inasemaje kuhusu kututengea fedha nyingi za kutosha katika mwaka huu wa fedha kupata nyumba za Walimu za kutosha kabisa katika Jimbo letu la Solwa na kuondokana na tatizo hili la upungufu wa Walimu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba kazi ya kushawishi na kuwapeleka walimu ambao wameridhia kwenda Shinyanga tunaifanya sana na Mheshimiwa Shibuda ni shahidi na Waheshimiwa wengine wa Mkoa wa Shinyanga kwa mfano Bukombe wanafahamu. Tatizo lililopo bado hata wale wanaotoka Shinyanga ambao Mheshimiwa anadhani wanapenda kwenda, ukweli ni kwamba ukiwabembelea wanakuambia tunapenda kubadili mazingira na ikifika hapo hakuna mahala wala mkataba tuliosainiana nao kwamba ametoka Shinyanga na lazima arudi Shinyanga na sisi tunasema kama wamependa kwenda walikopangwa basi ndiko tunakojenga utaifa na uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nyumba ni kubwa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa pamoja limepewa kipaumbele na ninaamini katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 suala hili litapewa kipaumbele. (*Makofii*)

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hapana ubishi kwamba Wizara ya Elimu imekuwa ikionesa jitihada kubwa za kupunguza tatizo la uhaba wa Walimu, lakini kwa bahati mbaya walimu wenyewe wakifika huko wanaamua kukwepa kwa sababu wanazozijua.

Je, isingekuwa jambo aula kabisa hivi sasa kuacha milango wazi kwa walimu wastaifu ambao wangependa kukaa katika maeneo hayo ambayo vijana hawayataki wakapewa ruhusa bila vikwazo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI -MHE. MWANTUMU B. MAHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ruhusa imetolewa kwa Wakurugenzi kuweza kuajiri wastaifu pale wanapoona mahitaji wanayo na uwezo wa kuajiri upo, hakuna kipingamizi kwa hilo. (*Makofii*)

Na. 108

Miundombinu ya Barabara na Reli

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO aliuliza:-

Kwa kuwa, ni ukweli usiopingika kwamba ile dhana ya Kilimo Kwanza iweze kufanikisha ni lazima miundombinu ya barabara na Reli iimashwe:-

- (a) Je, ni lini barabara ya Songea –Mbamba Bay itajengwa kwa kiwango cha lami?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga reli kutoka Mtwara –Mbamba Bay na Mbinga Makambako ili kukamilisha mtandao wa Reli nchini?
- (c) Kwa kuwa maeneo ya Nyoni Maguu na Langiro ni maeneo ya wakulima wa kuhawa. Je, ni lini barabara ya kutoka Likwere (Nyoni) Langiro itawekwa lami?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kumpata Mkandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara kutoka Peramiko mpaka Mbinga (km78) unaendelea. Makampuni 10 ya ujenzi yenye uwezo yamechaguliwa *pre-qualified* kwa ajili ya kupewa vitabu vya zabuni ili yajaze bei zao. Inatarajiwa kazi rasmi za ujenzi zitaanza mwezi Julai 2010. Ujenzi huu unagharamiwa na *MCC*. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje ili kujenga sehemu iliyobaki ya kutoka Mbinga hadi Mbamba Bay (km 66).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Reli ya Mtwara – Mbamba Bay na Mbinga – Makambako, Serikali inafahamu umuhimu wa reli hii kwani ni moha ya miundombinu muhimu katika Mtwara *Development Corridor* na ni moja kati ya reli zilizopo katika mpango kabambe wa *East Africa Railway Master Plan*.

Katika maandalizi ya ujenzi wa reli hii mwaka ujao wa fedha 2010/2011 tumepeanga kufanya upembuzi yakinifu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Likwere (Nyoni) Langiro. Kwa sasa tunaendelea kuiboresha kidogo kidogo kulingana na upatikanaji wa fedha kwa lengo la kuiimarisha kutoka barabara ya udongo ili ifikie kiwango cha barabara ya changarawe.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru majibu mazuri ya Serikali na hasa mchakato wa ujenzi wa barabara ya kutoka Peramiko kwenda Mbinga. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa wiki hii *TANROADS* wamefika Mbinga na kuanza mchakato wa kuanza kulipa fidia na kwa vile fidia hizo pia zinaonekana kuna watu wanapunjwa lakini pia ziko za aina mbili. (*Makofit*)

Kwanza kuna fidia itakayolipwa na MCC na pili fidia itakayolipwa na Selikali ambayo itachukua muda mrefu sana. Lakini wananchi wameambiwa tathimini iliyofanyika itabaki vilevile hata kama italipwa baada ya miaka mitano ijayao. Waziri yuko tayari kuchunguza jambo hili na kuelimisha Wanambinga hasa pale Mbinga Mjini?

La pili, kwa vile huu wimbo wa *Mtvara Corridor* ni wa muda mrefu na matunda yake ni kidogo sana; na kwa vile miradi hii ya kikanda ambayo inajengwa kwa nchi tatu au tano inachukua muda mrefu na kwa vile Mikoa hii hasa Mkoa wa Ruvuma ni Mikoa ya uzalishaji sana na usafiri ni ghali. Je, Serikali iko tayari sasa kuweka mkakati maalum wa kujenga reli hii kwa fedha za Serikali hata kama ni kwa kushirikisha sekte binafsi?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la kwanza nakubali ushauri wa Mheshimiwa Mbunge nitajitahidi kutumia *TANROAD* Ruvuma na wataalam Wizarani kuja kule Mbinga kwa ajili ya kutoa elimu ya utaratibu huu wa ulipaji fidia kwa wale ambao wameathirika na ujenzi wa barabara. Tatalifanya hili mapema iwezekanavyo.

Kwa swali la pili. Tunakiri kuelewa umuhimu wa ujenzi wa miundombinu ya reli kwa ukanda ule wa Mtvara. Tuna mpango thabiti kupita Ushirikiano wetu wa Afrika Mashariki; lakini kama ambavyo amependekeza Mheshimiwa Mbunge, tutaliangalia kwa umakini na pale ambapo fedha hazipatikani kwa njia nyingine pia tutajitahidi tutenge mafungu kupitia fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na mchakato wa ujenzi wa reli hilo.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri kwa swali liloulizwa na jirani wangu wa Mbinga ambaye ni jirani na Ludewa na kwa vile reli na barabara hizo anazozizungumza kwa kweli kwa namna fulani zinalenga kufikia machimbo ya Liganga na Mchuchuma. Mheshimiwa Waziri atatueleza hapa sasa ni juhudhi gani zitafikiwa katika mwaka ujao ku-*develop* reli, barabara au mawasiliano kwa ujumla katika Wilaya ya Ludewa?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika majibu ya swali la msingi ni kwamba. Katika mwaka ujao wa fedha tutaanza upembusi yakinifu kwa ajili ya reli hiyo. Fedha kwa ajili ya ujenzi baada ya mchakato huo wa upembusi yakinifu. Kwa sasa hatuna njia nyingine isipokuwa kufanya hivyo, na ujenzi wa barabara katika ukanda huu wa Mtvara uko katika ngazi nzuri, wenzetu Wamerekani wanatusaidia. Lakini najua kwamba imechukua muda mrefu isipokuwa taratibu za mfadhili zimehitaji hivyo sasa hivi tumefika katika ngazi nzuri ambayo ujenzi wa barabara utaanza hivi karabinu tuvute subira mambo yatakuwa mazuri. (*Makofit*)

Na. 109

Usafiri wa Bajaji Nchini

MHE. ANIA S. CHAUREMBO aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa Serikali katika jitihada zake za kupunguza tatizo la usafiri hapa nchini imeruhusu usafiri wa Bajaji na sasa zinafanya kazi:-

- (a) Je, usafiri huo wa Bajaji unatenda kazi kwenye maeneo maalum?
- (b) Je, ni kodi za aina gani zinalipwa kutokana na usafiri wa Bajaji?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge kufanya marekebisho katika sheria ya leseni za usafirishaji Na. 1 ya mwaka 1973, sheria hiyo iliidhinishwa kutumika na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipotia saini Muswada wa marekebisho tarehe 20 Machi, 2009. Sheria hiyo inaruhusu matumizi ya pikipiki na Bajaji kama usafiri wa umma.

Hakuna maeneo maalum ambayo yameshaanishwa kwa matumizi ya pikipiki na bajaji. Hata hivyo, Wizara yangu imeandaa rasimu ya Kanuni ambazo baada ya kupitishwa zitaelekeza matumizi bora ya bajaji za kawaida barabarani. Katika kanuni hizo ambazo ziliandaliwa kwa kujumuisha maoni ya wadau mbalimbali kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara, imependekewa kwamba Wizara yangu kupitia *SUMATRA* na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa watashirikiana kuainisha maeneo maalum ya pembezoni mwa Jiji na miji ambako Bajaji na pikipiki za kawaida zitakuwa zinafanya kazi. Tayari *SUMATRA* imekwishatoa elimu katika miji ya Bukoba, Songea, Singida, Mbeya na sehemu hizo nidhamu imejengeka ya kutoa huduma katika maeneo maalum. Aidha kwa vile vyombo hivyo vimeanza kutumika kabla ya Kanuni zake kupitishwa zitaendelea kutumika kwa kuzingatia sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 (*Road Traffic Act, 1973*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wamiliki wa Bajaji na pikipiki za kawaida ambao watahitaji kutumia vyombo hivyo kwa matumizi ya kufanya biashara ya kubeba abiria wanapaswa kulipa ada ya usajili wa chombo cha moto (*motor vehicle registration*), ada ya kila mwaka ya leseni ya chombo cha moto (*Motor vehicle license*) na kodi ya mapato kwenye mamlaka ya mapato Tanzania(*TRA*). Aidha watalipa ada ya leseni za usafirishaji kwa *SUMATRA* kuititia Halmashauri za Wilaya/Miji kwa mujibu wa Kanuni ya leseni ya usafirishaji ya pikipiki na Bajaji.

MHE. ANNIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Bajaji na pikipiki zimesaidia sana kupunguza tatizo la usafiri nchini na kwa kuwa vyombo hivi kwa muda mfupi tu vimekuwa vimesababisha ajali nyingi sana hapa nchini na kwa taarifa iliyokuwepo sasa hivi nchini kwamba waendesa Bajaji asilimia kubwa hawana leseni na ni vijana wadogo na vilevile hawajui Sheria za Barabarani. Je, zoezi linaloendeshwa na Wizara hizi ambazo Serikali imezitenga? Je, ziko tayari sasa kwenda sambamba na kuwasaidia vijana hawa wanaofanya biashara hii ya udereva ili na wao wapate elimu ya kupata leseni pamoja na kujua sheria za barabarani pamoja na hizo njia wanazosema wanatakiwa kupita?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba pikipiki na Bajaji baada ya kuruhusiwa kufanya biashara ya abiria imesababisha ajali nyingi sana. Kwa *report* ya Polisi ya mwaka 2009 jumla ya ajali 3945 zilihushisha pikipiki na Bajaji. Hii ni sawa na asilimia 13.8 ya ajali zote zilizotokea nchini Tanzania ambazo jumla yake ni 30,836. Hili ni tatizo kubwa na napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba kwa sababu hiyo na kwa sababu ya utekelezaji mzuri wa Sheria hiyo. Serikali inachukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kwamba waendeshaji bajaji na pikipiki ni wale ambao watakuwa wamefuzu na wanamafunzo ya kutosha kwa ajili ya kufanya biashara ya kusafirisha wananchi kwa kutumia vyombo hivi.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Majibu mazuri aliyoeleza Waziri napenda kuuliza kwa sababu pikipiki ni usafiri ambao unatumiwa na watu wengi hasa sehemu za vijijini ambako hakuna usafiri mwingine wowote na pia imekuwa ni chanzo cha mapato kwa vijana kujiajiri. Je, Serikali itakuwa tayari kuhamasisha hawa vijana kuunda vikundi vyta kiuchumi na kupewa mafunzo maalum ili wanapoendesha hizi pikipiki waendeshe kwa usalama zaidi lakini pia kuwasajili kwa namba kama nchi nyingine zinazofanya kama Rwanda?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba ni suala la muhimu sana kwa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi hawa na hasa vijana ambao wanajishughulisha na usafirishaji wa abira kwa kutumia vyombo hivi vyta pikipiki na bajaji kuwahamasisha wajunge pamoja ili kuhakikisha kwamba huduma wanayoitoa inaboreka kwa kuwezesherwa ndani ya vikundi vyao. Serikali itafanya hivyo lakini ninauhakika kwamba jukumu hilo tunalo sisi kama Wabunge katika Majimbo yetu kwa kushirikiana na Serikali tushirikiane ili kuhakikisha jambo hili limefanyiwa kazi vizuri na vijana wameweza kujiunga katika ushirika. Kwa upande wa kujiandikisha, kanuni zitakapokuwa tayari tutahakikisha kwamba tumeweuka utaratibu maalum wa

kuandikisha na kusajili wale wote ambao wanatoa huduma ya usafirishaji wa pikipiki na bajaji ili waweze kupata namba kamili watambulike na kuweza kudhibitiwa ipasavyo:-

Na. 110

Kuyumba kwa Uchumi Duniani

MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. MHE. ALOYCE B. KIMARO) aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na mtikisiko wa hali ya fedha na Uchumi Duniani; na kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa:-

- (a) Je, Tanzania kama nchi imeathirika kwa kiwango gani?
- (b) Kwa kuwa mashirika ya fedha kama *World Bank, IMF* na kadhalika, wametoa fedha za kusaidia uchumi wa Tanzania usiyumbe kwa sababu ya mtikisiko huo wa fedha. Je, ni kiasi gani tumepata kutoka wapi na zimetumikaje?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uchumi wa Tanzania hatimaye ulikumbwa na athari za mtikisiko wa sekta za ya fedha duniani ambao ulijidhihirisha kuanzia robo ya nne ya mwaka 2008.

Kupungua sana kwa uwezo wa ununuzi wa bidhaa na huduma duniani kote kulipunguza kiasi na bei za bidhaa na huduma zinazouzwa na Tanzania nje ya nchi.

Bei ya kahawa, pamba, karafuu na mazao mengine katika soko la dunia katika nusu ya kwanza ya mwaka 2009 zilikuwa chini ya zile za nusu ya kwanza ya mwaka 2008. Bei ya wastani ya kahawa aina ya robusta katika soko la dunia ilishuka hadi dola za Kimarekani 3.0 (Tsh.3900) kwa kilo kutoka dola za Kimarekani 3.2 (Tsh. 4160).

Bei ya wastani ya pamba ilifikia dola za Kimarekani 1.3 (Tsh.1690) kwa kilo ikilinganishwa na dola za Kimarekani 1.7 (Tsh.2210) katika kipindi kama hicho mwaka 2008. Vivyo hivyo bei ya wastani ya karafuu ilishuka. Bei za bidhaa za viwandani vile vile nazo zimeathirika kutokana na msukosuko wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utalii, athari kwenye uchumi zimejidhihirisha kutokana na watalii wanaoingia hapa nchini kupungua kufikia 303,219 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2009 ikilinganishwa na watalii 353,826 walioingia katika kipindi kama hicho mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kupungua kwa kiasi na bei za bidhaa na idadi ya watalii ni kuathirika kwa mapato kutokana na mauzo yetu ya nje ambapo mauzo yetu nje katika nusu ya kwanza ya mwaka 2009 yalikuwa na thamani ya asilimia 12. Chini ya thamani ya mauzo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, msukosuko wa fedha na uchumi duniani umeathiri maeneo mengine ya uchumi wetu na kupelekea kupungua kwa mapato ya Serikali ambapo makusanyo ya mwaka 2008/2009 yalifikia 90 tu ya lengo na hivyo kuilazimu Serikali kukopa kutoka vyanzo vya ndani ili kujaza pengo hilo. Athari hizi ndizo zilizotufanya pia tukapunguza makisio yetu ya ukuaji wa uchumi mwaka 2009 hadi 5.0% kutoka 7.4% mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na ilivyokuwa katika nchi zilizoendelea, sekta yetu ya fedha imendelea kuwa imara hata baada ya athari za msukosuko wa sekta ya fedha duniani kukumba uchumi wa Tanzania. Hii imejidhihirisha katika viashiria vya uimara wa mabenki na asasi za fedha hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imepata misaada kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) kwa ajili ya kupambana na madhara ya mtikisiko wa uchumi duniani:-

. Ili kupambana na athari za kupungua kwa mapato ya fedha za kigeni kufuatia kushuka kwa bei za bidhaa na huduma tunazouza nje ya nchi, Shirika la Fedha la Kimataifa limeipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu (*Exogenous Shock Facility*) wa jumla ya dola za Kimarekani milioni 336 (sawa na shilingi bilioni 440). Tayari dola za Kimarekani milioni 245.8 (shilingi bilioni 322) zimekwishapokelewa na kiasi kilichobaki kinatarajwa kutolewa Aprili, 2010. (*Makofi*)

· Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Fedha la Kimataifa ilipitisha mgao wa dola za Kimarekani bilioni 250 wa *special drawing rights* tarehe 7 Agosti, 2009 kwa nchi wanachama ili kuziongezea nchi hizo ukwasi wa fedha za kigeni ikiwa ni hatua ya kuzipunguzia makali ya athari za msukosuko wa sekta ya fedha duniani.

· Benki ya Dunia imetoa dola za Kimarekani milioni 252.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2009/2010, kati ya dola za Kimarekani milioni 359.9 ilizoahidi kwa mwaka mzima. Katika fedha zilizotolewa na Benki ya Dunia, zimo za program ya maendeleo ya kilimo, maji na uboreshaji wa mfumo wa kodi. Vivyo hivyo, Benki ya Maendeleo ya Afrika imetoa dola za Kimarekani milioni 62.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2009/2010 kati ya dola za Kimarekani milioni 98.9 ilizoahidi kwa mwaka mzima kwa Tanzania.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri, marefu ya Mheshimiwa....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lembeli, anza tena Mheshimiwa Lembeli.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi Naibu Waziri anakiri mbele ya Bunge hili kwamba sekta ya utalii ambayo ni moja ya sekta muhimu kwa uchumi wananchi hii, ilikumbwa na mtikisiko huu na hivyo kupelekea idadi ya watalii walioitembelea nchi yetu kupungua na pato la nchi yetu pia kupungua. Je, Serikali imesaidia vipi wadau wa sekta hii ya utalii hususan wananchi wanaojihusisha na biashara ya utalii katika kuhimili mtikisiko huu na katika mipango yao ya kurejesha hali au biashara ya utalii katika hali ya kawaida?

Pili, kwa kuwa kutokana na mtikisiko huu Tanzania itabidi ijpange upya katika kutangaza vivutio vyake vya utalii ndani na nje ya nchi; Serikali imejipanga vipi au Serikali itakuwa tayari kuipatia Bodi ya Utalii Tanzania (*TIB*) katika Bajeti ya 2010/2011 kipaumbele ili iweze kutangaza vilivyo biashara ya utalii wa Tanzania katika nchi za nje?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kimaro yaliyoulizwa kwa niaba yake kama ifuatavyo:-

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Maswali ni ya Lembeli, siyo ya Kimaro! Maswali ya nyongeza ni ya Lembeli, siyo ya Kimaro. Tunaelewana? Hakuna kwa niaba maswali haya ni yake. Kwa hiyo, mjibu Lembeli peke yake.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Lembeli kama ifuatavyo na ni kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi.

Kwanza, Serikali imesaidia vipi athari zilizotokana na mtikisiko huu kwenye sekta ya utalii, Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tarehe 10 Juni, 2009 hapa Dodoma Mheshimiwa Rais alitangaza hatua ambazo Serikali ingechukua ili kunusuru uchumi wa nchi kutokana na mtikisiko huo na ilikuwa ni pamoja na sekta ya Utalii.

Katika mambo ambayo Serikali ilitangaza ni kwamba hasara waliyopata wanunuzi wa mazao wangefidiwa, lakini vile vile katika sekta ya utalii hasara ambayo wangepata ingefidiwa. Isipokuwa sasa, kuna uataratibu wa kufuata, na kwa hiyo nina hakika kwamba ikiwa watakuwa wamefuata utaratibu ule, baasi hatua ambazo Serikali

ilikwishaahidi, zitachukuliwa. Kama hawajafanya na kama wana tatizo na uelewa wa nini wafanye, basi nitawaomba waje Serikalini na tutawaelekeza nini cha kufanya.

Kuhusu utangazaji wa utalii kutokana na mtikisiko huu wa uchumi na kwa hiyo kuanguka kwa sekta ya utalii. Tuko sasa katika maandalizi ya Bajeti na swali hapa ni Serikali itakuwa tayari kuupa utalii kipaumbele; na jibu ni ndiyo na nina hakika kwamba wakati Wizara husika itakapokuwa inapanga bajeti zao jambo hili litachukuliwa maanani.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kuongezea katika swali la pili kuhusu Serikali tumejipanga namna gani kwa ajili ya kuzidi kutoa kipaumbele kwa TTB kwa ajili ya *promotion* za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba zaidi ya bajeti kwamba itaongezwa, na pia tumeweka jitihada zingine za kuhakikisha kwamba wadau wote wale *TTB* inawafanya kazi katika kuwatangaza katika nchi mbalimbali, watachangia kwa *TTB* na kwamba mashirika yale makubwa yakiwemo *TANAPA* na Ngorongoro wenyewe watachangia *percent* 3 na ambapo mashirika mengine yote na wadau mbalimbali wenyewe watachangia *percent* moja ili kuhakikisha kuipa nguvu zaidi *TTB*.

Na. 111

Kufilisika kwa Mashirika ya Umma

MHE. LUCY F. OWENYA aliuliza:-

Kwa kuwa, Baba wa Taifa alitujengea msingi wa kujitegemea ambapo takriban mashirika 400 ya umma yalianzishwa; na kwa kuwa mashirika hayo karibu yote yameishauzwa au kubinafishwa kwa kigezo cha kuliingizia hasara Taifa:-

- (a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuanguka kwa mashirika hayo?
- (b) Je, menejimenti ya mashirika ilihuksika kwa kiasi gani kudhoofisha mashirika hayo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuanguka kwa Mashirika ya Umma kumetokana na sababu nyingi pamoja na zifuatazo:-
 - (i) Baadhi ya Mashirika yameanzishwa kwa mtaji mdogo.

- (ii) Mashirika kushindwa kuendana na mabadiliko ya teknolojia kutohana na udogo huo wa mitaji yao.
- (iii) Ghamama za uzalishaji kwa baadhi ya Mashirika kuwa kubwa.
- (iv) Mashirika mengi kushindwa kuingia katika soko la ushindani.
- (v) Uzalishaji mdogo na uduni wa viwango vya bidhaa zinazozalishwa na baadhi ya mashirika.
- (vi) Kushindwa kwa Serikali kuendelea kusaidia kwa njia ya ruzuku, misamaha ya kodi na dhamana za benki.
- (vii) Utandawazi na mabadiliko ya uchumi duniani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi huwezi kuihusisha menejimenti ya shirika pekee moja kwa moja katika udhoofishaji wa shirika. Hata hivyo, lazima tukiri kuwa baadhi ya watendaji wa baadhi ya mashirika hayo elimu zao na ujuzi hazikuweza kuendana na mabadiliko ya tekinolojia pamoja na soko na pamoja na mabadiliko ya uchumi duniani na hivyo kuchangia katika kudhoofisha baadhi ya mashirika.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba baadhi ya watendaji elimu zao hazimkuweza kuenda na tekinolojia za kisasa na kupelekea mashirika yale kutofanya vizuri.

Hata hivyo katika ripoti ya CAG kati ya Mashirika 160 yaliyobaki bado kuna Mashirika ambayo hayafanyi kazi vizuri kwa kuwa na Hati Chafu kwa mfano Shirika la TBC. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba watendaji au Wakurugenzi wa Bodi huteuliwa zaidi kisasa au kirafiki badala ya kuzingatia taaluma na kupelekea Mashirika yale yasifanye kazi kwa ufanisi?

Kwa kuwa tafiti zinaonyesha kwamba katika Mashirika ya Umma baadhi ya Wakurugenzi wa Bodi za Umma wakimaliza muda wao huwa inachukua muda sana kuteua wengine ambapo hupelekea mashirika yale yasifanye kazi vizuri kwa sababu hayana wasimamizi. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba wanateua Wakurugenzi wa Bodi wapya katika Mashirika ambayo Wakurugenzi wake wamemaliza muda wao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sina habari kwamba Mkurugenzi yeoyote anateuliwa kirafiki au kindugu. Mimi nina taarifa kwamba huwa wanachaguliwa kwa umakini mkubwa, kwamba taaluma zao zinapimwa na kwamba tunaridhika Serikalini kwamba wale wananchi wenzetu Watanzania tunaowapeleka kwenye mashirika haya wana uwezo wa kujaza zile nafasi kwenye Bodi.

Kuchelewa uteuzi wa Bodi, swali hili aliulizwa Mheshimiwa Waziri Mkuu jana na alitoa msimamo wa Serikali. Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri jibu la Mheshimiwa Waziri Mkuu lilitosha kujibu swali ambalo limeulizwa.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba wapo baadhi ya Wakurugenzi ambao walisababisha Mashirika hayo kufa. Je, Serikali iliwachukulia hatua gani ukizingatia wamelitia hasara taifa letu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nimesema na kwamba tunakiri kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba baadhi ya watendaji wa baadhi ya Mashirika ilitokezea kwamba walishindwa kufikia kiwango cha utendaji ambacho kilikuwa kimetazamiwa. Lakini cha kukumbuka ni kwamba katika shirika lolote kuna wadau zaidi ya menejimenti, siyo menejimenti tu inayoendesha shirika. Kwanza, kuna Bodi yenyewe, kuna menejimenti, kuna wafanya kazi, kuna wadai, kuna wadaiwa, kuna wateja wa shirika, kuna soko lenyewe. Kwa hiyo, siyo sahihi kusema tu shirika limedhoofika kwa sababu menejimenti imeshindwa.

Kwa hiyo, kama amedhihirika meneja ama kiongozi wa shirika kashindwa kazi, ni hatua gani zimechukuliwa. Hatua zitakuwa zimechukuliwa kulingana na mwongozo wa shirika husika.

Na. 112

Kituo cha Utafiti na Uendelezaji wa Sekta ya Madini

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Utafiti na Uendelezaji wa Sekta ya Madini (SEAMIC) kilichopo Kunduchi Dar es salaam kinachomilikiwa na nchi saba wanachama ambao ni Tanzania, Uganda, Kenya, Ethiopia, Comoro, Angola na Msambiji, kinaendelea kutoa huduma za kitalaam na mafunzo kwa sekta binafsi yanayohusiana na masuala ya madini katika nchi wanachama:-

- (a) Je, kwa upande wan chi ya Tanzania tumepata mafanikio gani kuwepo kituo hicho?
- (b) Je, mafunzo yaliyotolewa yametoa mchango gani wa kuwaandaa wazalendo kuwa na sifa ya kuwa watafiti wa madini nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana tangu kuwepo kwa kituo cha *SEAMIC* hapa nchini ni pamoja na Watanzania kutoka kampuni na watu binafsi kupata mafunzo ya fani mbalimbali.

Mafunzo hayo yanahu su mbinu za utafutaji na uchimbaji madini na namna bora ya uchenjuaji madini kwa wachimbaji wadogo wadogo na wa Kati. Kwa upande wa watalaan wa sekta ya madini, mafunzo yamekuwa yakinolewa katika mbinu na teknolojia mpya zinazogunduliwa duniani ili kuimarisha uwezo wao wa utendaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo mbalimbali yanatolewa na kituo cha *SEAMIC* yamekuwa yakiwasaidia Watanzania katika kuelewa namna bora ya kutafuta na kuchimba madini yanayopatikana nchini na hivyo kuwepo kwa fursa ya kuongezeka kwa kasi kwa Watanzania wanaojishughulisha na utafutaji na uchimbaji wa madini.

Maabara za kituo hicho zimekuwa zikiwasaidia Watanzania kufanya utafiti na uchunguzi wa madini yao wanayoyagundua katika maeneo waliiyomilishwa hivyo kupata uelewa mzuri wa mashapo yalivyo na kuweza kupata wabia katika uwekezaji kwenye kuchimba madini husika. Maabara za kituo hicho zina uwezowa kufanya utafiti wa sampuli zaidi ya 2000 kwa mwezi. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita wastani wa sampuli milioni 1.2 zimefanyiwa utafiti katika maabara za kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo kinao watalaan wengi wa Kitanzania kulinganisha na watalaan wengine kutoka nchi wanachama. Siku za karibuni kituo kimeanza kutoa mafunzo juu ya utunzaji wa mazingira ambapo jumla ya maafisa wa madini 11 kutoka Mikoa yote Tanzania Bara walipata mafunzo ya wiki mbili juu ya matumizi bora ya zebaki katika kuchenjua dhahabu. (*Makofī*)

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ya ufanuzi, ninauliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kituo hiki kimeanzishwa ni muda mrefu sasa na kimekuwa kikitoa mafunzo kwa ngazi ya vyeti na stashahada. Je, kwa upande wa wanawake kimewashirikisha kwa kiasi gani?

Pili, wahitimu wa chuo hicho ambao wanatoka sekta binafsi, pale zinapotokea kazi muhimu, Serikali inawatambua kwa maana ya kuwashirikisha ili kufikia lengo la kuongeza ajira nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa bahati nzuri hapa nchini kuna chama

ambacho kinajumuisha wanawake ambao wanajishughulisha na uchimbaji wa madini na sampuli zao huwa wanazipeleka katika kituo hiki. Hivyo, kituo hiki huwa kinahudumia wanawake wa Kitanzania kikamilifu. Serikali inatambua vyeti na stashahada zinazotolewa na kituo hiki kwa vile ni kituo ambacho kimeorodheshwa kama vituo vya elimu ya ya juu.

Na. 113

Serikali Kupeleka Umeme Kata za Pembezoni – Musoma

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo ya Kata za pembezoni mwa Mji wa Musoma kama Kata za Bweri, Nyakato, Kigera, Buhare na Makoko hayafikiwi na umeme; na kwa kuwa katika maeneo hayo kuna sekondari 15 ambazo zote hazina umeme japo umbali wa shule ni kati ya ya kilomita 0.5 na kilomita 2:-

- (a) Je, Serikali itawapatia lini umme watu wa maeneo hayo pamoja na shule hizo?
- (b) Je, Serikali haioni kuwanyima umeme hasa wanafunzi hao huwakosesha mafunzo kwa njia ya mtandao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, napenda kutoa maelezo mafupi ambayo ni kwamba:-

Kutopelekwa kwa umeme katika maeneo mbalimbali ya miji na vijiji kunakotokana na ufinyu wa Bajeti ya Shirika la Umeme *TANESCO* na vyanzo vingine vya Serikali vinavyofanya kazi hiyo, ukilinganisha na mahitaji ya umeme. Hata hivyo, Serikali inajitahidi sana kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kutosha zinakuwepo ili kuwapatia wananchi wake huduma hii muhimu sana. Baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa *TANESCO* wanafanya kazi maombi ya shule ya sekondari ya Makoko. Tunampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia suala hili. Aidha, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, viongozi na wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini kwa ujumla kwamba waendelee kushirikiana kwa karibu na *TANESCO* pamoja na Wizara yetu katika kushughulikia

maombi ya umeme kwa maeneo yaliyoombewa kwa kadri uwezo wa kifedha utakavyokuwa. Na wale ambao bado hawajawasilisha maombi yao, wayawasilishe *TANESCO* kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya gharama na kazi zitakazofanyika.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kuwafikishia umeme wananchi wake wote kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa sasa wananchi wa mjini hasa wakiwemo wa Mjini Musoma wanazuwa kutumia mkaa pamoja na kuni kwa ajili ya kulinda mazingira. Je, Serikali haioni kwamba kwa kutowapelekea umeme na huku ikiwazuia kutumia hizo nishati mbadala, inawafanya wananchi waendelee kuwa na maisha magumu?

Pili; gharama za umeme kwenda kwenye hiyo shule moja ya Makoko ambayo haizidi kilomita moja kutoka mahala umeme ulipo, imegharimu zaidi ya shilingi milioni tano(5). Endapo kila shule itafanya tathmini ya peke yake, gharama hizo zitakuwa ni kubwa sana kiasi kwamba hizo shule hazitaweza. Je, ni lini Serikali itafanya kwa pamoja tathmini ya gharama ambazo zitaunganisha shule zote hizo pamoja na wananchi walioko katika hayo maeneo ya shule ili shule hizo ziweze kupata umeme kwa gharama nafuu kuliko kila shule kujitegemea?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni azma ya Serikali kusambaza umeme hasa maeneo ya mjini ili kulinda mazingira yetu na hivyo kwa maeneo kama ya Musoma tuna hakika jitihada hizi zitazaa matunda.

Kwa upande wa gharama; kwa kweli kusambaza umeme gharama yake ni kubwa hasa kwa maeneo ya mbali kama shule ya Makoko kwa ajili ya vifaa kama vile *transfoma*. Kwa shule ambazo ziko vijijini, nashauri wananchi watumie umeme wa jua au pia watumie umeme kutohana na vianzio vingine kwa vile kusambaza umeme nchini kote ni gharama kubwa.

MHE. MCH. LUCKSON MANJALLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru. Kwa kuwa tatizo lililopo katika Kata zilizoko pembezoni mwa Mji wa Musoma ni sawa na tatizo lililoko Mbeya Vijijini hasa kuhusu umeme. Ninaomba niulize kwamba ni lini kazi ya kupeleka umeme Mbeya Vijijini hasa maeneo ya Ilembo na maeneo mengine yaliyoko Mbeya Vijijini itaanza?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Mkoa wa Mbeya umeorodheshwa chini ya Mpango wa MCC wa kusambaza umeme vijijini; na kwa vile kazi hiyo itaanza hivi karibuni, tunaamini

kwamba maeneo aliyoyataja pia yatafikiriwa kupewa umeme kwa utaratibu wa Mpango wa *MCC* wa Serikali ya Marekani.

NAIBU SPIKA: Ahsante, tuangalie muda jamani! Tunaendelea, Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa...., naomba tufanye mabadiliko ya jina la Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, ameishaenda Hija, kwa hiyo anaitwa Hajat Zuleikha Yunus Haji. Atauliza swali yeye! Mahajat wengine wapeleke majina kwa Spika kusudi majina yabadilishwe. (*Makofi/Kicheko*)

Na 144

Hospitali kubwa za Madhehebu ya Kidini Nchini

MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI aliuliza:-

Kwa kuwa hapa nchini zipo Hospitali kubwa za madhehebu ya Kidini kama vile *KCMC* Moshi, Bugando – Mwanza, na kadhalika.

Je, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ina ushirikiano gani na Hospitali hizo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Zuleikha, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana kwa kuweza kwenda kuhiji Macca na kuwa Hajat. Mungu amsaidie sana ili aweze kuzingatia madili ya dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hajat Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali nyingi za Mashirika ya Dini, zikiwemo Hospitali za *KCMC* na Bugando zinaendeshwa kwa ubia wa Serikali. Hospitali za *KCMC* na Bugando zinatumika kama Hospitali za rufaa za Kanda. Katika Hospitali Serikali inachangia kulipa mishahara ya watumishi wote, fedha, dawa, vitendanishi, vifaa na vifaatiba. Aidha, Serikali inatoa fedha za matumizi mengine ya kawadia (*Other Charges*) na fedha za miradi ya maendeleo katika hospitali hizo.

Mheshimiwa Spika, jukumu la hospitali hizo ambazo zinatumika kama hospitali za rufaa za kanda sawa na zile za Serikali ni kutoa huduma za ngazi ya rufaa kwa wananchi wote kulingana na Sera ya Taifa ya Afya na miongozo mbalimbali inayohusiana na utoaji wa huduma za afya. Hospitali hizo pia zinatumika kutoa mafunzo kwa wataalam mbalimbali wa kada za Afya na Utafiti wa magonjwa ya binadamu.

Aidha, hospitali hizi zinashirikishwa katika kupitia sera za afya, kuandaa mipango mkakati na miongozo pamoja na tathmini mbalimbali za kisekta.

MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naona pamoja na swali lilivyokuwa, amenielimisha zaidi kuhusu hospitali ya Bugando na *KCMC*, je, vipi uhusiano kuhusu hizi baadhi ya hospitali kama kule Makyungu, Singida, Mchukwi iliyoko Rufiji na Kipatimo iliyoko Kilwa na nyingine. Je, wanauhusiano gani na Hospitali kama hizi?

NAIBU WAZIRI WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, Sera yetu ya Afya ni kwamba tuna ushirikiano mzuri sana na hospitali zile nyingine ambazo si za Serikali, ziwe za Mashirika ya Dini au ya binafsi. Hizi hospitali ambazo amezitaja za Makyungu, Kipatimo na zingine alizozitaja tunahusiana nao. Kama itakuwa ni hospitali Teule basi na yenyewe tunaifanyia kama tunavyofanya katika hospitali za Bugando. Lakini vilevile zile hospitali zingine za Mashirika ya Dini ambazo zinatoa huduma kwa wananchi, huwa tuna utaratibu wa kuweza kuwasaidia kuweka nao mikataba katika yale maeneo wanayotoa huduma, Serikali huwa inalipia. Vilevile katika zile hospitali ambazo pia zinatoa mafunzo kama vile vyuo na kadhalika, Serikali huwa inachangia ili kuweza kuona kuwa huduma za vyuo hivyo inakuwa bora, Serikali huwa inachangia katika maeneo mbalimbali.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha.

Sasa tuna wageni ambao wako Bungeni kwa ajili ya kushuhudia shughuli za Bunge. Tuna wageni wa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda ambao ni Dr. Richard Chatora Rufaro, yeche ni raia wa Zimbabwe, *if you are there, can you rise please! Thank you very much.* Yeye ni mwakilishi wa Shirika la Afya Ulimwenguni, Ofisi ya Tanzania. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna Dr. Martin Ovberedjo, raia wa Nigeria, yeche ni Afisa Mshauri Masuala ya Rasilimali Watu katika Shirika hilo. Tuna Bwana Emmanuel Mntenga, ambaye ni Afisa Uhusiano na Uhamasishaji Masuala ya Afya. *We welcome you into our House, I am sure you are following up our Swahili discussions here and we want you to feel at home here in Dodoma.* (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza ambaye ni Kijoli Said na Johari Kapufi, wako wapi, wote hao ni wadogo zake, karibuni, kama hawapo, basi watakuja baadaye. (*Makofi*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila ambao ni Mrs Faith Sakila, mke wake. Ahsante mama, tunafurahi kukuona. (*Makofi*)

Tuna wageni 40 wa Mheshimiwa Kayombo kutoka Umoja wa Wanavyuo Vikuu Dodoma wakiongozwa na Stanslaus Mdetele, Mwenyekiti kwanza asimame halafu

Jumuiya yote pale walipo wasimame, karibuni sana. Huyu Mdetele huyu ni kama anatoka Njombe maana majina yanafanana na huko. Ahsante sana wanafunzi wa Vyuo Vikuu, tunawatakieni masomo mema na nyie ndiyo warithi wa shughuli zote hizi. Tunaamini amani, utulivu na nidhamu, zitaendelea kule shulen i kwenu ili tuweze kujenga Taifa lenye nidhamu. (*Makofi*)

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini ambao ni Wajumbe wa Serikali ya Kijiji na Mtaa, Kata ya Nzuguni, wakiongozwa na Mchungaji Moses Sibeti, Mchungaji Sibeti yuko wapi na ujumbe wenyewe wote uko wapi, aah! Ahsanteni sana, nyie wenyeji wetu, tunashukuru sana. Sasa katika kundi, yuko Mchungaji Sibeti, Mheshimiwa Diwani Mwalimu, yuko Mtendaji wa Kata, Vicent Leo na yuko Mwenyekiti wa Kijiji cha Nzuguni, Ndugu Wilson Daudi, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Jiji la Mbeya, nao ni Mheshimiwa Halima Mwampyate, Kata ya Forest, Mheshimiwa Neema Nyangwale, Kata ya Itanganu na Mheshimiwa Agatha Ngole, Kata ya Ilemi, karibuni sana Wahemiwa Madiwani na tunafurahi kuwaoneni. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dr. Mathayo David, naye ana wageni wake kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, sijui wako pamoja na wale wa mwanzo, sina uhakika. Yupo Ndugu Saimon James, Ndugu Nelson Sanga, Ndugu Projesta Amos, Ndugu Emmanuel Lukwalo, Ndugu Davi Onesmo, Ndugu Emmanuel Edmund, Ndugu Baraka Mbwambo na Ndugu Riziki Sanga. Wote mnakaribishwa na kama nilivyosema tunawatakia masomo mema kwa sababu nyie ndiyo rasilimali ya Taifa sasa na siku zijazo. (*Makofi*)

Kuna matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa George Simbachawene, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 5/2/2010, saa saba mchana katika ukumbi namba 133, ghorofa ya kwanza, jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Abdisalaam Khatibu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati leo saa saba mchana katika Ukumbi namba 219.

Kuna tangazo ambalo limetolewa na Katibu wa Chama cha Wabunge Wanawake (*TWPG*), Mheshimiwa Switi, kuwa anapenda kuwataarifu Wabunge Wanawake wote na Wanachama wa *TWPG* kuwa leo siku ya Ijumaa, tarehe 5/2/2010, saa saba mchana, kutakuwa na kikao katika ukumbi wa *Basement*, nafikiri mnaufahamu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dr. Zainabu Gama, ye ye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge wa Kupambana na Rushwa (*APNAC*), anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho tarehe 6/2/2010, saa tano asubuhi kutakuwa na Semina inayohusu Muswada wa Gharama za Uchaguzi na itafanya katika Ukumbi

wa *African Dream*. Narudia hapo, wenzetu APNAC wameandaa semina kwa Wabunge wote kuhusu Muswada wa Gharama za Uchaguzi lakini semina hii itafanyika kule *African Dream*. Kwa hiyo, mnakaribishwa kule saa tano asubuhi. Kesho ni Jumamosi hatuna shughuli za Bunge.

*(Hapa kulikuwa na minong'ono kutoka
kwa Waheshimiwa Wabunge)*

NAIBU SPIKA: Mbona naona mnashangaa kwa nguvu, kwa mujibu wa ratiba mpya, kesho hakuna kikao, kwa hiyo, wanaotaka watakwenda semina hiyo lakini itahusisha masuala ya Gharama za Uchaguzi kama ambavyo imefanyiwa marekebisho mbalimbali na Kamati na pia Serikali.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Katibu wa Wanawake wa CCM Bungeni, anawatangazia kutakuwa na kikao leo saa saba Mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Katibu wa UWT maana yake Wanawake wa CCM, nadhani ni kujipongeza kwa siku ya CCM, leo ni siku ya kuzaliwa CCM. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza Wanachama wote wa CCM kwa sikuu ya kuzaliwa kwa Chama chao. (*Makof*)

Tangazo linguine, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, anaomba niwatangazie Wabunge wa CCM wote kwamba siku ya Jumapili ambayo ni tarehe saba, saa tano asubuhi kutakuwa na mukutano wa Wanachama wa CCM kwenye ukumbi wa Msekwa. Ni siku ya Jumapili, saa tano, tarehe saba Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi wana kikao ukumbi wa Msekwa.

Nafikiri nimemaliza matangazo yote sasa tunaendelea, Katibu!

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi Nyongeza wa Mwaka 2010
(Supplimentary Appropriation Bill, 2010)

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, jana baada ya kipindi cha maswali, mimi nilitoa tangazo kwamba hoja ya Waziri wa Fedha, Hati iliyowasilishwa Mezani kwamba haikuwa imepita kwenye kikao cha Kamati na kwamba Kamati itaendelea na shughuli yaani kikao cha Kamati halafu leo tutaletewa Hoja hiyo. Mheshimiwa Chenge jana akahoji kwamba ile hoja haikuweza kupitia katika ngazi zote kwa mujibu wa Kanuni ya 105. Mheshimiwa Mbunge alikuwa sahihi kwamba inapokuja tunapitisha Muswada wa Nyongeza hatukai kwenye Kamati bali inapitishwa moja kwa moja na Muswada maana yake hiki kikaratasi kidogo ambacho mlishagawiwa. Lakini kuna kitu kinaitwa Hati ya Matumizi ya Nyongeza yaani *Supplimentary Estimates of Expenditure*, hii ndiyo ambayo haikuwa imepitia kwenye Kamati na nikasema kwamba wanapitisha kwenye Kamati.

Kwa hiyo, asubuhi hii mmegawiwa *Supplementary Order Paper*, ndiyo hoja aliyosoma Katibu Mezani inahusu *Supplimentary Oder Paper* na hii ni kwamba tutaijadili. Waziri atawasilisha na Mwenyekiti aliyehusika na Hati hii, atazungumza na Upinzani watatoa maoni yao, tunaenda kama kawaida ya hoja, tukimaliza hoja hiyo, tutaingia hata kwenye Kamati ya Matumizi kupitia hoja hiyo, halafu Waziri atakuja na Muswada na Muswada huu hatutaujadili, atasoma na nitawahoji basi kwa sababu ni sehemu ya Miswada ya Fedha tuliyopitisha mwezi Juni, fedha zile zilikuwa kwenye *Consolidated Fund Account* sasa zinatoka mle zinaingizwa kwenye shughuli maalumu ambayo itaelezwa na Waziri. Kwa hiyo, tunashughuli za namna hiyo asubuhi hii.

Baada ya kusema hivyo, sasa tunaendelea, Mheshimiwa Mtoa hoja!

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Hati ya Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza ya mwaka wa Fedha 2009/2010 (*The Supplementary Appropriation (For Financial Year 2009/10) Act, 2010*), wenyewe lengo la kuwasilisha makadirio ya matumizi ya nyongeza ya Serikali kwa mwaka 2009/2010 ya kiasi cha shilingi bilioni 19 yaliyo nje ya bajeti ya Serikali iliyyoidhinishwa na Bunge, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hati inayowasilishwa ni kwa mujibu wa Ibara ya 99 ikisomwa pamoja na Ibara ya 137(3) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambazo zinaelekeza kwamba Serikali inaweza kufanya matumizi ya ziada ya yale yaliyoidhinishwa na Bunge kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kupata idhini ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kushukuru Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili hoja hii jana Alhamisi tarehe 4 Februari 2010. Napenda kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge wa Kamati kuwa michango yao tumeifanyia kazi kwa lengo la kuboresha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyowasilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 21 Agosti, 2008, Mheshimiwa Rais alielekeza kwamba fedha za *EPA* zitakazorudishwa Serikalini ziingizwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya shughuli za maendeleo ya nchi ikiwemo kuongeza fedha katika Mfuko wa Ruzuku ya Mbolea kwa wakulima, madawa ya mifugo na kwa ajili ya mikopo katika sekta ya kilimo kupitia Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia agizo hili la Mheshimiwa Rais, napenda kuwasilisha Muswada huu ili kupata idhini ya matumizi ya nyongeza ya kiasi cha shilingi bilioni 19 kwa ajili ya kuongeza fedha katika Mfuko kwa ajili ya mikopo katika sekta ya kilimo kupitia Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha hizi zitaingizwa katika bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi; (Fungu la 50) ambapo ndio mkondo wa Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*), kupata fedha zake za bajeti ya kila mwaka kuitia Idara ya Msajiri wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matumizi haya ya nyongeza, jumla kuu ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010, imeongezeka kutoka shilingi trilioni 9,513,685,000,000 hadi shilingi trilioni 9,532,685,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili:-

Sehemu ya Kwanza yenyе kifungu cha 1 hadi cha 5, inahusu masuala ya utangulizi, kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada wenyewe, mamlaka ya Hazina kutumia kiasi cha shilingi bilioni 19 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kulipia gharama za Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na mamlaka ya kisheria ya Waziri wa Fedha na Uchumi kukopa ndani na nje ya nchi kiasi kisichozidi shilingi bilioni 19.

Sehemu ya Pili, yenyе jedwali, inabainisha nyongeza ya shilingi bilioni 19 kuitia Fungu la 50 (Wizara ya Fedha na Uchumi) kwa kuwa bajeti ya Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) inakasimiwa chini ya Idara ya Msajili wa Hazina ambayo ipo chini ya Fungu la 50 (Wizara ya Fedha na Uchumi).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako likubali kuitisha Hoja hii na kuidhinisha Matumizi haya ya Nyongeza ya Shilingi bilioni 19 kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ajili ya maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAIBU SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti aliyeshughulikia hoja hiyo, namwona mwakilishi wake Mheshimiwa Mwenegoha.

MHE. HAMZA A. MWENEGOHA – (K.N.Y. MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati juu ya hoja ya Serikali ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007, niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Hoja ya Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha

2009/10 (*The Supplementary Appropriation (For Financial Year 2009/10) Act, 2010*), wenyе lengo la kuwasilisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ya kiasi cha shilingi bilioni 19 yaliyo nje ya bajeti iliyo idhinishwa na Bunge, kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kiasi cha fedha hizi zitakazoidhinishwa zinatoka katika Akaunti ya Madeni ya Nje ‘External Payment Arrears’ (EPA) ambazo zitatumika kwa ajili ya kuongeza fedha katika Mfuko kwa ajili ya mkopo katika sekta ya kilimo kupitia Benki ya Rasilimali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kamati yangu inakubaliana na maombi haya yaliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ya kiasi cha shilingi bilioni 19. Ni matumaini ya Kamati kwamba fedha hizi zitatumika kwa uangalifu mkubwa hasa katika kuwasaidia wakulima wadogo wadogo kupitia mikopo. Serikali kupitia Benki ya Rasilimali ya Tanzania (*TIB*) iandae utaratibu mahususi wa kuwakopesha wakulima wadogo ili waweze kujikwamua katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hapo awali, Serikali iliamua kutoa mikopo kwa wakulima kupitia Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) na Bunge kuidhinisha kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya shughuli hiyo ni vema fedha hizi zikaidhinishwa ili kuongeza mtaji kwa *TIB* ili iweze kuhudumia idadi kubwa ya wakulima amba wengi wao wapo maeneo ya vijijini; hali hii itasadia kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa tuna kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, ni vema Serikali ikafuatilia kwa umakini matumizi ya fedha hizi ili kilimo chetu kiwe na faida kwa wakulima na kuleta tija kwa nchi nzima. Ni lazima tubuni mfumo endelevu wa muda wa kati hadi muda mrefu ujao utakaojenga misingi ya kuwa na wakulima mahususi wenyе sifa zote zinazohusiana na uzalishaji mali kwa kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeona kiasi cha fedha hizi zitakazoidhinishwa zitasaidia kuongeza fedha katika Mfuko wa Ruzuku wa Mbolea kwa wakulima, kununua madawa ya mifugo na mbegu bora. Hali hii itasaidia kuongeza thamani ya uzalishaji kwa wakulima pamoja na *TIB* ambayo inasimamia utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia maoni na ushauri wa Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti na Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti. (*Makofî*)

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Dr. Anthony M. Diallo, Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Athumanı Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Monica Ngenzi

Mbega, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Damas Pachal Nakei, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Dkt. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi, Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla na Mheshimiwa Charles Kajege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Manaibu Waziri, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa utendaji wao mzuri wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Makatibu wa Kamati, Ndugu Lawrence Makigi na Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mwenegoha, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu hoja hii, Mheshimiwa Salim kwa niaba ya Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.N.Y MSEMADI MKUU KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA FEDHA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 (*Supplementary Appropriation (For Financial Year 2009/2010) Act, 2010*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 96(6), naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kabla ya kuridhia nyongeza hiyo ya matumizi, inaitaka Serikali kutoa ufanuzi kuhusu fedha hizo zinazotakiwa kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu lilielezwa kwamba fedha ambazo zilirejeshwa na watuhumiwa waliochukua fedha za Malipo ya Akaunti ya Madeni ya Nje (EPA), kuwa kiasi fulani cha fedha hizo ambazo ziliikuwa ni Tshs 62 bilioni zitapelekwa kwenye Benki ya Rasilimali (TIB) kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa, je, ni kiasi gani kilipelekwa kwenye Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali kabla ya hizi

zinazoombewa idhini ya Bunge? Tokea Serikali itangaze mpango huu wa *TIB* kuwa na Dirisha Maalum la Kilimo hadi leo hakuna mwongozo wowote uliotolewa. Dirisha hili si litakuwa sawa na lile la kawaida ambalo urasimu wake hautatofautiana na huu wa kutoa mikopo ya kilimo? Ni vema Waziri aliahidi Bunge hili kwamba kabla hatujamaliza mkutano huu, Wabunge watagawiwa utaratibu wa kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Waziri akalielezea Bunge lako Tukufu, je, kiasi cha Tshs.19 bilioni kinachoombwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina, ni sehemu ya zile zilizokuwa zimerejeshwa na watuhumiwa wa *EPA* au ni marejesho mapya kutoka kwa watuhumiwa ambao walikuwa hawajamaliza kurejesha fedha walizochukua katika akaunti hiyo? Kwani Bunge lako Tukufu lilikwishapitisha matumizi kwa fedha zote ambazo zilikuwa zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo ambavyo vilikwishaelezwa na Serikali wakati wa uidhinishwaji wa Bajeti Kuu ya Serikali. Mtazamo wa Kambi ya Upinzani kuhusu fedha hizo zingeelekezwa kwenye kilimo cha Mpunga na Mahindi kwa kuainisha wakulima na taasisi kama JKT, Magereza ambazo zitaweza kuzalisha kwa wingi ili kupunguza tatizo la njaa linalotukabili kila mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hizi zisifanywe kuwa ni za sadaka kama zilivyofanywa za Mfuko wa JK, hizi zinatakiwa zirudi kwenye mzunguko mzima wa uchumi na hasa ikizingatiwa kuwa zinatakiwa kulipwa pindi wenyewe wakijitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutafuta maeneo kati ya zile hekta 2.3 milioni zinazofaa sana (*high potential*) kwa kilimo cha umwagiliaji, ili watu wafanye kazi na kuondoa kabisa tatizo la mfumuko wa bei na pale pale tukilitumia vyema soko la Afrika ya Mashariki vizuri. Kwa njia hii, tunaamini kuwa tutafanikiwa kujikwamua katika baadhi ya nyanja za uchumi ambazo zinakwama kutohana na kushindwa kuthubutu kutenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, nimepata wachangiaji wawili, Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Ruth Msafiri.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo!

NAIBU SPIKA: Mwongozo!

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Nilileta karatasi yangu ya kuomba kuchangia.

NAIBU SPIKA: Kama nilivyosema Muswada hatutachangia isipokuwa hoja hii ndiyo tutachangia.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya kuongeza shilingi bilioni 19 kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kuidhinisha au kuamua kwamba pesa zote za *EPA* zitumike kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Ni kweli kwamba zile pesa zilikuwa zimekaa muda mrefu bila kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, ndiyo sababu namshukuru sana Mheshimiwa Rais alipoamua pesa hizi zitumike kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia jambo kubwa hapa ni kuongeza pesa kwa ajili ya shughuli za kilimo na mifugo pamoja na kupeleka pesa zaidi kwenye mbolea. Hili ni jambo muhimu kwa sababu kwa maeneo mengi katika nchi hii ambayo yanalinwa mazao ya biashara na chakula bado mbolea inabaki kuwa muhimu sana. Ni kweli uwezo wa Serikali haukuwa mkubwa sana kupeleka mbolea ya ruzuku kwa wakulima lakini baada ya ongezeko la pesa hizi za *EPA*, Serikali imejitahidi kupeleka mbolea walau ya kutosha kwa kiasi fulani ingawa tunaendelea kutoa rai kwa Serikali ione umuhimu wa kuendelea kuongeza pesa zaidi kwa ajili ya mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa katika suala hili ni mikopo katika sekta ya kilimo kupitia Benki ya Rasilimali ya Taifa (*TIB*), hili ndiyo kubwa na tunaidhinisha pesa hizi ili ziende huko. Naiomba Serikali na wenzangu walioangulia kusema kwa maana ya Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wamelisema hilo, tunapeleka pesa tuongeze zile zilizoidhinishwa kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010 kwa maana ya shilingi bilioni tatu kwa maana hiyo bajeti nzima au pesa zote zinazopelekwa kwenye sekta ya kilimo kupitia *TIB* kwa ajili ya mikopo zitakuwa bilioni 22. Ninachoomba na Serikali itilie maanani, tunapeleka pesa hizi kwa nia nzuri, ninaomba pesa hizi zifanye kazi ambayo imekusudiwa. Wakati mwingine ni vizuri Serikali itueleze kwenye Bajeti inayokuja kwamba hizi pesa ambazo zimeidhinishwa kuanzia zile bilioni tatu kwenye bajeti iliyopita na hizi bilioni kumi na tisa jumla shilingi bilioni 22 zimefanya kazi iliyokusudiwa, kwa sababu tumekuwa tunaidhinisha pesa halafu hazifanyi kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kujua, hivi hadi sasa ni wakopaji wangapi ambao tayari wameshapewa pesa kwa sababu tayari kuna hela ambazo zilishaidhinishwa, shilingi bilioni tatu. Ni wangapi wameshapewa kati ya walioomba, kwa sababu mimi nina wakulima wangu kadhaa walioomba mikopo hii, Wilaya ya Mbozi na wamekuwa wanani fuatilia sana kwamba tunaomba Serikali itimize ahadi yake ya kutoa mikopo kwa ajili ya sekta ya kilimo. Lakini wakopaji hawa pamoja na mimi mwenyewe, tulipofuatilia Benki ya Rasilimali Dar es Salaam ni kwamba bado tupo kwenye mchakato kati ya *TIB* na Wizara na kati ya Wizara na *BOT*. Tangu tunapitisha fedha mpaka zianze kutumika zinachukua muda gani? Leo tumebakiza miezi michache kumaliza mwaka wa fedha huu, fedha zilizoidhinishwa kwenye mwaka huu, hazijaanza kutumika kwa sababu kuna watu ambao wanataka kukopa bado hawajapata, wakati mwingine tunatoa matumaini makubwa kwa Watanzania lakini matumaini hayo hatuwezi kuanza kuyatekeleza kwa muda unaostahili. Waziri awaeleze Watanzania na hasa wale wanaolima na ambao

wanafikiri mkopo huu ulikuwa uwe na manufaa sana, ni lini sasa wataanza kufaidika na mikopo hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kama nilivyosema, maelezo yako bayana, naomba Waziri atueleze Watanzania na Bunge lako Tukufu, ni masharti yapi ambayo yanapaswa yafuatwe kabla ya mkopaji hajapata mkopo wenyewe? Nina wasiwasi kama hatutakwenda kwenye masharti yale yale ambayo kimsingi yamekuwa magumu sana, maana tunesema benki hii tunaianzisha maalumu kwa ajili ya wakulima, sasa isije ikawa na masharti yanayolingana na benki za kibiashara ambako masharti yake kimsingi siyo mazuri hata kidogo. Wakati wote yamekuwa yanawabana wakulima ambao tunawakusudia. Mimi sitarajii benki hii ikawa na taratibu zile zile kama mabenki yale mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri, ni vizuri Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ikaandaa masharti ya mikopo hii na kuyasambaza nchini kote kupitia kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Vyama vyta Ushirika waliko wananchi ili waelewe masharti yanayohusika katika kukopa pesa hizi za *EPA* ambazo zinapelekwa *TIB* ili wananchi wasisumbuke kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kwamba ni vizuri tupunguze urasimu katika *ku-process* mikopo yenye. Tumekuwa na taabu, unapeleka maombi ya mikopo kwenye mabenki unaambiwa hili halijakamilika, njoo kesho, njoo kesho kutwa na bahati mbaya sana benki ya *TIB* iko Dar es Salaam. Waziri pia awaeleze Watanzania watatumia utaratibu gani, je watakuwa na Kanda au itategemea mtu anatoka Mbozi afuate mkopo (benki) Dar es Salaam? Kwa hiyo, naomba tufikirie pia mtu anapokopa atalazimika kutumia gharama zake yeye mwenyewe, anatoka Mbozi, Mpanda, Kagera kwa hela zake lakini anakuja kukopa pengine shilingi milioni mia mbili, sasa akizunguka mara mbili mara tatu ameshatumia pesa ambayo katika hali ya kawaada ingeweza kumsaidia kufanya mambo mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili nimeliunga mkono ninachoomba kusisitiza kwa kweli ni uaminifu kwa viongozi wenzetu ambao tumewapa kazi hii ya kuwashughulikia Watanzania. Lakini pia niombe pesa hizi ziende kwa wakulima kule vijijini, tusije tukakuta tena wanaofaidika ni wakulima wakubwa peke yake, tutakuwa hatujafanya jambo la maana sana kwa sababu zaidi ya asilimia themanini ya wakulima wote katika nchi hii ni wakulima wadogowadogo, kwa hiyo, zisipokwenda kwao, bado kusudio la kuanzisha benki hii litakuwa halijatimia hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri pia kupitia Bunge hili na Watanzania, Waziri akatueleza nini hasa riba kwa mikopo hii ambayo itatozwa na benki hii. Ni moja ya masharti ambayo nimesema kwamba ni vizuri Watanzania wakaelezwa kwamba riba yake itakuwa kiasi gani au itaanzia kutoka mahali fulani kwenda mahali fulani, kwa sababu tunaelewa riba nydingi za mabenki zinaanzia asilimia 15 mpaka asilimia 30. Kwa hiyo, ni vizuri atueleze ili kweli tuseme hii benki inakusudia kuwasaidia wakulima na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka kusema mambo hayo machache ili Watanzania pia wafaidike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, ninaiunga mkono hoja hii ya kupitisha nyongeza ya makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona kwamba huu ni utekelezaji au ni kukamilisha utekelezaji wa uamuzi wa Rais wa kutumia fedha za *EPA* kwa ajili ya kuendeleza kilimo, kwa hiyo, hoja hii naiunga mkono kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukumbusha Bunge lako Tukufu kwamba mwaka 2008 nilileta hoja hapa ya kujadili Taarifa ya Benki ya Rasilimali (*TIB*) na katika kujadili, nilitoa hoja ya kuanzisha Benki ya Kilimo na hoja hiyo ilikubalika na tukaahidiwa kwamba Benki itaanizishwa. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kutoa maelezo, atueleze hatua zilizofikiwa katika kuanzisha Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu Rais aliagiza kwamba lianzishwe Dirisha *TIB*. Nia hasa ni kuanzisha Benki kamili ya Kilimo na hili linaungana na hoja aliyotoa mwenzangu aliyetangulia, Mheshimiwa Zambi, kuwa hizi Benki zilizopo Dar es Salaam, kwa kweli zina gharama kubwa sana ya mikopo, kwa hiyo, Benki hiyo ianzishwe ili iweze kufika vijijini kwa Wakulima Wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masharti, nitapenda kwa kweli hata sisi Wabunge pengine tungeyajua kwanza kabla hayajatolewa. Tuyaone na tutoe michango yetu kwa sababu, suala la kilimo ni tofauti kabisa na shughuli zingine za uzalishaji, za uwekezaji na kadhalika. Kwa mfano, kwa Wakulima ambao wako kwenye maeneo ya kahawa, chai, mfano, mimi nipo katika eneo la kulima chai, kuanzia kwenye kitalu cha chai pale unachukua mwaka mzima halafu kupanda miche mpaka kuvuna ni miaka mine. Kwa hiyo, kuna miaka minne ambayo huna mapato yoyote. Je, mkopo huo utazingatia hali hii, kwamba si mkopo wa kurudisha kesho kutwa lakini uzingatie kuanzia kupanda mpaka wakati wa kuvuna? Hiyo kwa kweli kwa Sheria ya *TIB*, hakuna nafasi pale. Kwa hiyo, hii Benki ya Kilimo kwa kweli ndiyo ambayo ingekuwa ni benki maalum ambayo ina riba maalum na inahudumia zaidi Wakulima Wadogo, kwa sababu hawa Wakulima wakubwa wana uwezo mkubwa sana na wameendelezwa kwa muda mrefu, hawa wadogo ndiyo nadhani msisitizo ungekuwa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwamba sasa matumizi hayo tuyapitishe kwa mujibu wa Sheria na uamuzi wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, kwa taarifa yako, hata mimi ninazungumza na *TIB* kuhusu Wakulima wa Chai wadogo wadogo, shida yangu ni kama hiyo hiyo, kwa hiyo, mwenzio nimeanza mazungumzo, tukiwa pamoja tunaweza tukawa na nguvu. (*Makofii*)

Sasa namwita Mtoa Hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru sana kwa hoja zilizotolewa...

NAIBU SPIKA: Mtoa hoja unasogea mbele, vipi hapo tena. (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuwashukuru wale wote waliochangia hoja hii, tukianzia na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa William Shellukindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kama alivyosema Mheshimiwa William Shellukindo, hoja hii inaletwa hapa kama utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoatoa tarehe 21/08/2008, kwamba fedha zote zile ambazo zimetokana na *EPA*, zinazorudishwa, zitumike kwa ajili ya masuala ya kilimo. Sasa wakati tulipoleta hoja ya kwanza wakati ule pesa zilizokuwa zimerudi zilikuwa shilingi bilioni 53, kwa hiyo, zikaidhinishwa kwamba shilingi bilioni 40 zipelekwe kwenye sekta ya kilimo kwa ajili ya mbolea, pembejeo na mambo mengine, shilingi bilioni 10 zipelekwe kwenye sekta ya mifugo kwa ajili ya madawa ya mifugo na mambo mengine na zile shilingi bilioni tatu zipelekwe *TIB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi ule ulishatekelezwa na kilimo ilipewa shilingi bilioni 40, mifugo shilingi bilioni 10 na *TIB* ilipewe shilingi bilioni 3. *TIB* ilicheleweshwa kupelekewa pesa zile kwa sababu walikuwa bado hawajaandaa utaratibu na ilibidi utaratibu uandaliwe, nadhani ndiyo wakati ule mlikuwa mnapiga simu kuuliza kwamba hawajapata pesa, walikuwa hawajaandaa utaratibu. Sasa hizi shilingi bilioni 19 ambazo tunaziombea kibali leo ni zaidi ya zile shilingi bilioni 53 ambazo zilishaidhinishwa. Kwa hiyo, kwa ujumla, pesa zote ambazo tumezipata kutokana na *EPA* na wale ambao wamerudisha kwa sasa hivi jumla yake ni shilingi bilioni 72, shilingi bilioni 53 zilishaidhinishwa, shilingi bilioni 19 ndizo ambazo tunaziombea kibali leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kilichelewesha? Kwanza, tukumbuke kwamba agizo la Rais ni kwamba tufungue Dirisha kwa sababu Benki ya Kilimo hatuna, kwa hiyo, tufungue dirisha katika Benki ya *TIB* ili iweze ku-*facilitate* kutoa hii mikopo ya kilimo. Kwa hiyo, kilichopo sasa hivi pale *TIB* ni Dirisha Dogo, *TIB* bado ni Benki ya Maendeleo ya Viwanda, utaalam wao na kila kitu ambacho wao wamezoea ni kutoa mikopo ya maendeleo ya viwanda lakini tumewaomba waandae Dirisha Dogo la kuanzisha hii mikopo ya kilimo. Sasa kwa sababu ni Benki, inabidi zile taratibu ziidhinishwe na Benki Kuu. Taratibu zile ziliandaliwa, Benki iliidhinisha, zililetwa kwangu kwa kufuata Katiba na mimi nimeshazidiidhinisha na zimesharudishwa tayari kwa utekelezaji. Kwa hiyo, watakapopata hizi shilingi bilioni 19 pamoja na zile shilingi

bilioni tatu, ndiyo Benki itakuwa tayari kulitumia lile dirisha la kilimo kuanza kutoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti gani? *TIB* ina masharti yake na Bodi yake lakini tumetoa mwongozo wa jinsi gani wanaweza kutoa ile mikopo. Nisingependa kusema kitu ambacho si sahihi na maudhui ya ule mwongozo ambaao tumeutoa. Lakini nataka niwahakikishie kwamba tumetoa mwongozo wa namna gani *TIB* ishughulikie mikopo katika dirisha lile la mikopo ya kilimo kwa sababu mikopo wanayoitoa siyo ya kawaida. Ni mikopo maalum kwa ajili ya kufanikisha kilimo. Sasa hizi shilingi bilioni 22, kwa mikopo, ukinipa mie ni pesa nydingi sana na sitegemei kuzipata katika uhai wangu kama Mustafa Mkulo, sijui baraka gani zitokee huko mbele ya safari lakini sitegemei kwamba kuna siku mimi nitakuwa na shilingi bilioni 22 kama zangu lakini kama Benki, ni pesa ndogo sana. Kwa hiyo, tusijipe matumaini kwamba sisi wote tunaweza kwenda *TIB* na maombi ya mikopo wa shilingi milioni 200 maana ukiomba shilingi milioni 200 katika shilingi bilioni 22 maana yake unazungumzia watu 11. Kwa hiyo, watu 11 wanaweza wakapata hizo pesa lakini Wabunge tuko 323, achilia mbali wananchi milioni 40 ambaao wanangoja kuzipata hizi pesa. Kwa hiyo, ninachopenda kushauri ni kwamba Serikali imeona tuanzishe angalau hilo Dirisha la kuwapa uzoefu *TIB* kwa mikopo ya kilimo ili uzoefu wa dirisha hili ndiyo uje uwe *spring body* ya kuanzisha Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Kilimo tumefika wapi? Nataka nikuhakikishie kwa sababu mimi mwenyewe nimehusishwa, tumefikia hatua nzuri sana. Tunategemea kupata pesa nydingi kidogo sio hizi shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kuanzisha benki hiyo ya kilimo. Siwezi kuzitaja maana wale ambaao wanakaribia kutusaidia wanaweza pengine wasifurahie. Lakini tunategemea kupata pesa za kutosha kwa ajili ya kuweka mtaji kwenye Benki ya Kilimo lakini tukishaweka mtaji pia tuweze kupata watu ambaao wanaweza kuikopesha ile Benki. Kwa sababu mtaji wa Serikali hauwezi kuwa na pesa nydingi sana lakini tukishaweka pesa fulani kama mtaji tayari tumeshapata maeneo kadhaa ambapo wako tayari kutukopesha ikiwa sisi wenyewe kama Serikali tutakuwa tumewekeza pesa kiasi fulani. Kwa hiyo, Benki ya Kilimo itakuja wakati wowote lakini mpaka tutakapokamilisha zile taratibu ambazo tunaziandaa. Ninachoweza kuahidi ni kwamba hatua zimefika mbali na tukishakamilisha na Serikali ikishaidhinisha, tutahakikisha kwamba tunaleta hapa Bungeni tupate idhini ya Benki hii ianzishwe lini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala kati ya *TIB*, Hazina na *BOT*, ni kweli kulikuwa na mjadala lakini kama nilivyoeleza ni kwamba *TIB* hawakuwa na uzoefu wa kutoa mikopo ya kilimo. Sasa wafanye nini? Ndiyo ikabidi *Supervision* ya Benki Kuu na *TIB* wenyewe wakae chini wajue nini tunachotaka kukifanya na baadaye kufuatana na Sheria, Wizara ya Fedha iidhinishe. Mjadala ule umekwisha, taratibu zimeshaandalisha na Wizara ya Fedha tumeshaidhinisha. Kwa hiyo, japokuwa imechukua muda lakini kitakachofanyika sasa kitakuwa ni kitu ambacho kina faida kuliko tungefanya haraka halafu hizo pesa zote zipotee kama Mheshimiwa Zambi alivyosema kwamba pesa hizi zisije tu zikaenda, kwa hiyo, nasema tunasikitika kwamba tumechelewa kidogo lakini nataka kuwapa faraja kwamba hata baada ya kuchelewa kitakachokuja kitakuwa ni kitu kizuri chenye faida kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti, nimeeleza kwamba kwa kweli Benki yenyewe itaandaa na Bodi yao itaidhinisha. Serikali itakachoweza kufanya ni kuwaomba *TIB* wakubali kwamba Dirisha hili ni maalum hawakulanzisha wao, limeanzishwa na Serikali. Kwa hiyo, ile mikopo itolewe kwa masharti ambayo tutakubaliana baina ya Serikali na *TIB* ili yasiwe yale masharti ambayo wanayatoa kwa mkopo wowote ule wa kaida. Kama tulivyofanya kwa ile pesa ya JK kwamba ukienda *CRDB* kukopa pesa utapewa masharti ya *CRDB* lakini ukienda kukopa zile pesa za JK, utapewa masharti ambayo ni nafuu kuliko yale ya *CRDB*. Nisingependa kusema kwamba riba kiasi gani, maana nikisema hilo litaingia kwenye *Hansard* sasa lisipotekelzeza nitapata matatizo. Nadhani tukubaliane kwamba tutajadiliana na *TIB* kuhakikisha kwamba mikopo hii inatolewa kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Shellukindo na swal lako la Benki ya Kilimo nimelijibu, tulilipokea lile wazo na limefanyiwa kazi wakati wowote tukishakamilisha, Benki ya Kilimo inaweza ikaanza wakati wowote. Ninachoweza kuwashakikishia ni kwamba *response* katika maeneo fulani fulani duniani yamekuwa mazuri ila tuna tahadhari tusije tukakimbiza vitu tukaja tukapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa ujumla ndiyo yaliyojitokeza kama jinsi nilivyotoa muhtasari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu na heshima zote, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunatumia hati hii.

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Uchumi

Kif. 2003 - Msajili wa Hazina Shs.19,000,000,000/-

MHE. DKT. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sitarajii kutoa shilingi kwa sababu na mimi ni mkulima pia isipokuwa nataka ufanuzi. Wakati ninamaliza na kupeleka ule mchango wangu wa maandishi, ulishamsimamisha Mheshimiwa Waziri kwenda pale mbele kwenda kutoa maelezo, kwa hiyo, naona ile karatasi yangu imekwenda kule nyuma kwa wataalam lakini sina hakika kama Mheshimiwa Waziri aliipata hiyo taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lenyewe ni kwamba kule Morogoro tuna kampuni inaitwa Demaco ambayo ina uhusiano mzuri na mabenki, mojawapo ni *Federal Bank of the Middle East Limited* ambayo wanashirikiana na *SACCOS* mojawapo, *SACCOS* yangu

ya Malindi. Wanapata mkopo wa matrekta kwa kiwango cha ku-*deposit* shilingi milioni 5. Lakini sasa naambiwa kwa kupitia hizi fedha za *TIB* wanatakiwa waweke shilingi milioni 10 kwa trekta ya shilingi milioni 40 yaani asilimia 20, jambo hili kwa wakati huu na hawa watu walisha-*deposit* ili wapate mikopo ya matrekta, haitawezekana kwa sababu wakati huu ndiyo wa kupalilia mpunga, kutia dawa na kadhalika. Kwa hiyo, naomba kwanza ufanuzi kama hili jambo ni kweli, kama ni kweli kwa nini sasa Serikali inaweka kima cha juu hata kupita zile benki pamoja na hata ule Mfuko wetu wa Pembejeo ambao unaweka asilimia 10. Sasa kwa nini Serikali/Wizara inaweka kiwango kikubwa kama hiki? Ahsante.

MWENYEKITI: Hizi *specific questions* una uhakika kweli anaweza kujibu Waziri? Jaribu hiyo ya trekta.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyeekiti, lazima nikiri kwamba mchango wake wa maandishi sikuusoma lakini kwa swali ambalo ameliuliza katika majumuisho yangu nimesema kwamba *TIB*, mwongozo wameshaandaa tayari, sasa wanaandaa masharti. Nikasema kwamba itabidi Serikali na *TIB* tukae chini tuzungumze ili kuelewana kwamba mkopo huu au Dirisha hili Maalum, masharti yake na mambo mengine yawe maalum na siyo yale ambayo wanayafanya kwa mikopo mingine ya kawaida. Sasa hili tutalizungumza na *TIB* na tutaeleza nini kitafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hilo kwamba *specific* kwamba *FMV*, wanafanya nini, hilo kwa kweli siwezi kulijibu hapa.

MWENYEKITI: Utamjibu kwa maandisho.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyoye*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya shilingi bilioni 19 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa Fedha 2009/2010 (*The Supplementary Appropriation for financial year 2009/2010*) sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

(*Bunge liliafiki Muswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza wa Mwaka 2010 na Kuyapitisha*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(*Kusomwa Hatua zake Zote*)

(*Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza wa Mwaka 2010 (The Supplementary Appropriation Bill, 2010)*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, niliidhinisha kwamba tumejadili nakala hii ambayo ilikuwa Hati ndiyo tumejadili, tumemaliza. Sasa upo Muswada wa kuidhinisha hizi fedha sasa, huu hatujadili maana naona wengine wameomba kujadili Muswada, hatujadili sisi. Waziri akishasoma tunapitisha hapa, soma Muswada kama ulivyowasilisha.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome kwa Kiingereza.

An Act to apply for a further some of 19 billions shillings out of the service of the year ending on 30th June, 2010 and to appropriate the supply granted.

This Act may be cited as Supplementary Appropriation for the financial year, Act, 2009/2010 and shall be read as one with Appropriation Act 2009.

The expressions used in this Act shall have the meaning as described under the Public Finance Act. The Treasurer may issue out of the Consolidated Fund and apply towards the supply granted for the service of the year ending on 30th June, 2010 the some of 19 bilions shillings. The some granted by section 3 shall be appropriated for the purposes and in the amount specified in the third and fifth columns of the schedule to this Act.

Schedule, ambit expenditure, Ministry of Finance and Economic Affairs, recurrent expenditure 19 billion, total 19 billion, development expenditure nil, total sum 19 billion.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza wa Mwaka 2010 (The Supplementary Appropriation Bill, 2010)* ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmechanganyikiwa hapa ehee!

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

NAIBU SPIKA: Tunakwenda taratibu. Kwanza kabisa, niliwaambia mwezi wa sita tulipitisha Bajeti ya Serikali ambapo kulikuwa na Muswada wa Sheria ya Fedha. Tuliupitisha huo ambao ulitoa maelezo yote kwamba Serikali itatumia kiasi gani na itatoa kiasi gani. Lakini katika hiyo pia walitoa taarifa wakati huo katika *Consolidated Fund Account* kwamba kutakuwa na fedha zitakazopelekwa *TIB* nyingine zilipelekwa na kwamba zingeongezwa. Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba tusingeingia kwenye Muswada huu moja kwa moja hapa akasema Waziri halafu tukapita kwa sababu ina *interest* ya wananchi. Kwa hiyo, Serikali ikaleta hoja kwa Waraka huu, hii Hati kubwa, ndiyo hii ikajadiliwa na Kamati zinazohusika na Kambi ya Upinzani, wametoa maoni na mmeputa maoni ya kuweza kujadili. Kwa hiyo, mmejadili hoja ya mwanzo kwamba zile fedha tulisema zinaingia katika Mfuko huu kusudi zikafanye kazi gani, kwa sababu wananchi wajue tumefanya kazi ya namna hiyo na fedha zimetoka wapi, zimetoka kwenye fungu la *EPA*. Tumemaliza kama kawaida hoja ya fedha. Sasa ili kukamilisha iwe Sheria kamili ndiyo tumekuja tutoe kifungu kidogo hiki kwamba sisi sasa tumeidhinisha hiyo shughuli kwamba iende huku ndiyo maana tunasema hamtajadili kwa sababu tayari mmeshaujadili huku sasa hapa ni kutoa idhini kwamba sasa Hazina itafanya hivyo. Kwa hiyo, nadhani hapo ndiyo shughuli ambayo tumefanya. (*Makofi*)

Jana Mheshimiwa Chenge alipohoji kwa sababu tulitumia huu Muswada kwenda kujadiliwa, Muswada huu haujadiliwi, kilichokuwa kinajadiliwa ni ile Hati.

Kwa hiyo, baada ya kusema hivyo, shughuli imekwisha Mheshimiwa Waziri kwa maana ya kukamilisha bajeti, tumekamilisha, tunaingia tena sasa kwa mwongozo wetu na kwa sababu muda mwingi umetumika, kwa hiyo, orodha ni kubwa sana tutakuwa na wachache halafu tutampa Waziri mchana ajiandae kwa ajili ya kuweza kujibu baadhi ya maoni aliyoyakuta.

HOJA ZA SERIKALI

(*Mapendekezo ya Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Taifa kwa mwaka wa Fedha 2010/2011*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kwa kuweza kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu. Kwanza kabisa, niipongeza

Wizara, Waziri pamoja na timu yake yote kwa maandalizi mazuri ya mwongozo huu wa bajeti ambao uko mbele yetu, nawapongeza najua ni kazi kubwa sana. Lakini pamoja na hayo, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida, napenda pia nitoe mchango kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lolote linapokuwa linaandaliwa lazima kunakuwa na dhana yake na dhana hiyo naamini kabisa wenzetu hawa walizingatia. Lakini kama ninavyojua mimi lazima kunakuwa na malengo, lakini pia kunakuwa na tathmini. Sasa sielewei kama wenzetu walifanya tathmini ya kutosha katika kuanda mwongozo ambao utatupelekea kuanda bajeti yetu, maana ukizingatia bajeti iliyopita kuna mambo mengi sana ambayo tulikuwa tumeyazungumza hapa na tukawa tumeyapitisha lakini sina hakika sana kama yote yalikuwa yamekwenda barabara kama tulivyokuwa tumepitisha. Hivyo, ninaamini kwamba tathmini lazima ifanyike na tuje kwamba sasa tunataka kufikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza kwa kuamini kwamba, tangu nikiwa mdogo nilikuwa nasikia maneno yafuatayo; kwamba adui wa nchi yetu ni ujinga, maradhi, pamoja na umaskini. Ninapenda zaidi kama tungejikita katika kuyaondoa haya. Tukiyaondoa haya, Taifa letu litakuwa ni Taifa lililoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia suala la ujinga, ni lazima mtu atoke kwenye ujinga kwa kupata elimu, nimeshangaa kuona kwamba Kilimo Kwanza imepewa kipaumbele sielewi kipaumbele cha elimu kimefikia wapi ambacho ndio tulikipa kipaumbele cha kwanza. Kwa sababu Kilimo Kwanza bila elimu sidhani kama kinawezekani kikafanikiwa wananchi wake wanatakiwa wawe na elimu ili waweze kuwa na kilimo cha kisasa ambacho kitaleta tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na mpango wa elimu, tukaweka shule za sekondari katika kata zetu, lakini bado kuna matatizo makubwa sana katika maeneo yale, haiwezekani tukawa tuna madarasa na wanafunzi lakini hakuna vitendea kazi, Walimu hakuna hawatoshi, bado Wizara hii ina mzigo mkubwa sana kuongeza Walimu, bado vifaa havitoshi, nikizungumza vifaa ni pamoja na vitabu na maabara, haiwezekani ukajenga nyumba usiweke mlango ukasema sasa una nyumba imekamilika unaishi ndani. Kwa hiyo, naomba sana tuzidi kuangalia upande wa elimu ili tuzidi kukidhi mahitaji mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka katika adui ujinga lakini bado kuna maradhi, ukasema Kilimo Kwanza. Tukizungumzia kilimo, asilimia kubwa sana ya Watanzania wanaolima ni wanawake, lakini tukizungumza upande wa wanawake ndio wanaolea watoto wachanga na wakubwa, wao wenyewe na wazee pia, mzigo mzito anaopata mwanamke huyu, bado na maradhi yote akiugua mtoto, akiugua yeze mwenyewe mama, akiugua baba, hata wazee jukumu kubwa ni la mama. Kwa hiyo, nafikiri katika sekta ya afya pia lazima tuiangalie, haiwezekani ukasema Kilimo Kwanza, wakati afya za watoto zinakuwa bado hazijatengewa bajeti ya kutosha kwa ajili ya kupunguza vifo vya watoto, kina mama wanahangaika kwenda hospitali, lakini bado pia uzazi sio salama. Akina mama hawa wajawazito ndio wanaokwenda kulima pia lakini anapofikia kuja kujifungua

bado Serikali yake inakuwa haijamwekea kipaumbele. Vifo ya kinamama ni vingi, ikitokea ajali sasa hivi wakifa watu 100 inakuwa ni *issue* ya Taifa zima lakini kwa mwaka mzima akina mama mia tano wanakufa, Taifa linakuwa bado halitoi kipaumbele. Bajeti inayotengwa kupelekwa katika Wizara ya Afya, inachanganya tu yote hakuna bajeti maalum inayotengwa kwamba hii ilenge afya ya mama na mtoto kwa ajili ya kupunguza vifo. Sasa tutajenga Taifa la namna gani kila mwaka kupoteza watu, nguvu kazi na watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi bado nataka kusema kwamba ni lazima tuangalie afya ya mama na mtoto, tutenge bajeti iende kama ilivyo isipelekwe tu kama kwenye kapu moja kwa moja. Inapopelekwa kwenye Wizara ya Afya basi ile bajeti ya mama na mtoto kwa ajili ya kupunguza vifo iende, kina mama wanapata shida, wanabebwa kwenye matela ya ng'ombe, hawafiki, wahudumu hata hawa waliopo, Wakunga wetu hawawezi kufika kwenye vituo kwa ajili ya kuhudumia kwa sababu ya miundombinu ambayo sio mizuri, vitendea kazi hakuna, usafiri hakuna, hakuna kitu chochote wanabaki kuandika takwimu tu tunapunguza vifo, tunapunguza vifo. Kwa hiyo, naomba sana katika upande wa maradhi, izingatiwe hasa katika kulenga kupunguza vifo vya mama na mtoto ili tuje kwenye dhana ya kuinua uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika suala la umaskini tunaweza kusema kwamba sasa kilimo ndio kinaweza kikatoa umaskini, umaskini huu hauwezi kutoka bila kukuza uchumi wa nchi hauwezi ukakua. Kwa hiyo, mimi ninataka kuzungumzia ni namna gani Serikali yetu iweze *ku-focus* kwenye kukuza uchumi wa nchi yetu. Nchi yetu ya Tanzania imezungukwa na Mataifa manane, kama tutatumia vizuri miundombinu yetu, miundombinu ya kiuchumi, tukaboresha bandari yetu, wazungumzaji waliopita walisema wenzetu Kenya pamoja na matatizo makubwa ya kisiasa waliyoyapata lakini hawasahau, wanaangalia ni wapi pa kuweza kupata pesa kwa ajili ya kukuza uchumi wao. Sasa hivi wanajenga bandari kubwa sana pale Mombasa wanatatupiku sasa hivi tutabaki sisi na bandari yetu. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie ni namna gani tutakavyoweza kuikuza bandari yetu iweze kuongeza pato la Taifa pia kuongeza ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari haiwezi kwenda bila barabara na reli, kwa hiyo mimi naomba sana tuangalie ni namna gani tutatenga bajeti kwa ajili ya kukuza uchumi kwenye nyanja hizi za barabara, reli lakini pia nishati. Umeme tunaowasha hapa Tanzania ni mdogo ukilinganisha na matumizi tuliyoyanayo. Sasa huwezi ukasema kwamba utapata maendeleo bila kutumia umeme na umeme wetu hasa kwa ajili ya viwanda, unapozungumzia viwanda na kilimo huwezi ukasema kilimo kwanza wakati umesahau ni namna gani unaweza ukapata umeme wa kutosha Tanzania. Ili tuweze kuwa na viwanda na vifanye kazi, umeme wa kukatikati tu hata vile vidogo vidogo ndio kabisa havina umeme. Kwa hiyo, naomba sana katika suala la umeme, nimeambiwa kwamba kuna *master plan* ya kuzalisha umeme. Sielewi kama hiyo *master plan* imetengewa fungu la pesa, naomba pia tuzingatie sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba nizungumzie kidogo kuhusu upande wa michezo. Miaka mingi sana mimi tangu nimeingia hapa Bungeni, Wizara ya Michezo, huwa naona kama vile ni Wizara inayojibanza sana, imejibanza tu, ni Wizara ambayo

kama ilikuwa haitakiwi hivi. Tukizungumzia michezo, Kenya wao wametangaza Taifa lao kupitia michezo, hapa tukikaa tunasema kwamba michezo imeshuka, sijui Serikali imefanya nini, tunatenga nini kwenye michezo? Inatakiwa kila Wilaya kuwe na viwanja vya michezo, kila Wilaya kuwe na ma-hall kwa ajili ya wasanii. Wenzetu Kenya kupitia michezo, Mchezaji Maarufu wa Tenes Duniani, Serena William, anajenga Shule ya Wasichana Kenya, hii yote ni kwa sababu ya wanariadha wanawake waliojitokeza katika ulimwengu wa michezo duniani. Sasa michezo inaweza ikatangaza utalii, haiwezekani tukasema kwamba tunapeleka tu hela kwenye CNN sijui na wapi michezo ndio inatangaza utalii wa Taifa. Kwa hiyo, naomba sana tusiweke mbali hii Wizara, tutawapata wapi kina Ronyadino, sijui nani, wachezaji wa kimatifa kama tumewaacha kule vijijini Singida, mwanariadha utampata wapi Shinyanga, Kigoma kule utawapata wapi ni lazima tuwekeze, kwenye michezo na hii michezo ianzie mashulenii, huwezi ukasema sijui soka likue, sijui wasanii, sijui kitu gani lazima tuwekeza mashulenii ndiko vipaji vinakoanzia. Kama ni riadha, wakimbiasi wako kule mashulenii, wako wasanii, waimbaji wazuri kule mashulenii, kama ni wacheza mpira wazuri wako kule mashulenii. Kwa hiyo, hii Wizara naona kama imewekwa pembeni sana hasa katika upande wa michezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa kwa sababu naona muda wangu umekwisha. Zaidi ya yote, ninaunga sana mkono, mzingatie sana suala la elimu pamoja na afya ya mama na mtoto, zitengwe pesa kwa ajili hiyo pamoja na michezo mashulenii na Wizara nzima kwa ujumla, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii iliyo mbele yetu, kwanza kabisa, ninapenda nikubaliane na michango ya wenzangu wengi katika hoja hii lakini ninayo haya ya kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumetoa azimio maalum la Kilimo Kwanza ambalo lina maeneo matatu, kilimo, uvuvi na ufulgaji, natumaini sasa mipango yetu itajielekeza katika maeneo haya na hasa maeneo ambayo yanatoa matunda kwa haraka. Hata katika kilimo, kuna maeneo yanayotoa matunda kwa haraka. Uvuvi, pia unatoa matunda kwa haraka, nadhani wenzangu wa Zanzibar, Mafia watakubali kwamba unaweza kulala leo maskini kesho ukatupa nyavu ukarudi nyumbani una samaki wanaofika shilingi milioni moja. Lakini katika maeneo ambayo yamepuuzwa, ni hili eneo la uvuvi, ukizingatia kwamba tuna bahari yaani zile *opportunities* hatuzitumii. Wengine wamesema Tanzania iko katika eno ambalo kijiografia tu ni biashara. Lakini pia ukichukua maziwa, mito na ukanda wa bahari, pale ni eneo mojawapo tungelitumia, tungetoa mazao ya haraka bila hata kutumia pembejeo nyingi. Kwenye maji hatuweki mbolea, hatupalilii, ni kutafuta tu dhana zinazofaa na zinazofanya uvuvi endelevu na katika mipango tukiliweka hilo basi tutaweka na umuhimu wa kuzalisha hizi dhana hapa nchini ili eneo hili nalo liweze kuwa na mchangano mkubwa. Kwa hiyo, Kilimo Kwanza iwe ndio dira basi ya kutuonyesha ni nini tunachofanya na miundombinu inayohusiana na

kuendelezwa kilimo, uvuvi, ufugaji viwekewe umuhimu wa pekee ili tuweze basi kuvuka pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niliunganishe na sera za mwanzo tu baada ya uhuru, tulikuwa na sera ya kujitegemea yaani hatimaye nchi hii iweze kujitegemea. Nadhani hili wazo limekuwa hata sisi tunapozungumza hapa sisikii watu wengi tunazungumza juu ya kujitegemea, wengi tunazungumza juu ya wahisani, ugonjwa wa kuomba wahisani umeenea mpaka vijijini, Mbunge ukionekana ni katika kutoa hisani, badala ya kuelekeza namna ya kujitegemea. Kwa hiyo, mipango yetu turudi pale pale, haya mambo ya omboomba haya yananiudhi halafu wanatukejeli wakati mwingine Mawaziri wetu wananyanyasika nchi nzima, wanatuona sisi tunatembea na vibakuli vyta omboomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huo ni msingi mkubwa, tutake tusitake hatuwezi kuwa na maendeleo tegemezi, haiwezekani kabisa hata tulete umeme, hata tufanye nini, kama tutaendelea kutembea na vile vibakuli vyta omboomba vile, heshima ya Taifa hili itarudi chini. Ndio maana zamani Mwalimu Nyerere alikuwa hajali, anaweza hata akamfokea Mmarekani akamwambia ondoka na mimi katika lugha yetu tunamsemo “*ukundisya*” kama hunilishi wewe unaninyanyasa nini lakini leo tunaweza kusema “*ukundisya*”, wote tunaomba ombo. Kwa hiyo, ninataka mipango ijayo ionyeshe jinsi tunavyoondoka kwenye omboomba, tunaenda kwenye kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nitoe mfano tu, maeneo yote yenyе njaa ukiweka mbegu bora, ukasaidia wakulima wale kuzalisha vizuri, hatuhitaji kuomba chakula cha mtu lakini tusipofanya hivyo, tutaendelea kuwa omboomba, zile nguvu tunazozitumia katika kuombaombia, tuzitumie katika kujikomboa na kuweka mkakati wa kujitegemea na mkakati huu uende mpaka ngazi za familia, familia ikijitegemea kijiji kinajitemea na Wilaya imejitegemea, Mikoa itajitegemea. Tuanze kwanza kujilisha, turudishe heshima yetu ya kujilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu nimepata tabu sana, Wilaya yetu ya Ukerewe imepata ugonjwa wa mihogo ambayo ilikuwa zao kuu la chakula. Suala la kupigapiga magoti limeniudhi sana, unamwomba huyu anakwambia tutafanya hivi, unamwomba huyu anakwambia tutafanya wakati watu wanaumwa njaa. Uombaomba nauchukia kweli kweli, miaka yote tangu niwepo sijaona Wilaya yetu ya Ukerewe tunaombaombia chakula, kumbe watu wanaoombaombia wana shida kubwa sana, nimeiona mwaka huu katika Wilaya yetu. Unakwenda kwa Waziri huyu anakupiga chenga, unakwenda kwa huyu anakupiga chenga. Kuombaombia ni kubaya kabisa na Taifa hili lazima tuliondoe katika hali ya kuwa omboomba. Hapo kweli tutafanya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kusema viwanda, maeneo tunayoyaona hayo, juhudhi kubwa ilikuwa ni kuweza kujitegemea. Nchi hii sasa tunaletewa matakataka kutoka nchi mbalimbali, *junk*, manguo *junk*, hatuzalishi, tulikuwa na pamba yetu, tulikuwa na viwanda vyetu vyta kutengeneza katika nia ile ile ya

kujitegemea kwamba tuvae kama tunavyotaka sio tukavae pamba ambayo wengine wametengeneza nguo wakatuletea *second hand*, ni matusi, wakati tuna pamba, wakati viwanda tulivitengeneza. Nasema sawa tumebinafsisha, sasa tukishakuwa tumebinafsisha basi tusimamie hao waliochukua viwanda nya nguo ambavyo ndiyo ilikuwa dhamira yetu, watengeneze basi hizo nguo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliochukua viwanda nya viatu watengeneze viatu, wale waliochukua viwanda nya kuzalisha vifaa nya kilimo, watengeneze hivyo vifaa. Kila mahali ukiangalia katika historia ya nchi hii tulikuwa tunakwenda sawa sawa, sijui vurugu hii imetokea wapi, halafu mnasema wazee tutoke hili mvuruge zaidi, wala hatutoki humu humu tutabanana na nyie mjue wazee wenu tumo. Huko tulikotoka tulikuwa tunakwenda barabara isipokuwa tumerudi nyuma na sisi wengine tukae humu humu, wazee wote mkae humu humu, mtukumbushe mpaka turudi kwenye njia tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kusema ni kwamba kama tunataka kupiga hatua, kuna misingi ya kupiga hatua katika mipango, mipango inaweza kuwa mizuri lakini hata ungekuwa na mamilioni ya pesa kama watendaji sio madhubuti hufiki. Hebu tutazame tu mifano midogo, shule zipo tunazojenga kwa pesa za Serikali, kuna shule zinajengwa kwa pesa za watu binafsi, pesa ile ukimpa mtu binafsi ambayo wewe unatumia kwa madarasa mawili anaweza kukutolea matatu. Sasa tusipokuwa makini watendaji wakawa ni wale *committed*, wale amba wana moyo wa uzalendo, sio kila mtu anaweza kuwa Mkurugenzi, sio kila mtu anaweza kuwa Mtendaji wa Kijiji, sio kila mtu anaweza kuwa Nesi, sio kila mtu anaweza kuwa Daktari, sio kila mtu anaweza kuwa Mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo linatupa matatizo sana, tuna Wakurugenzi, pesa za umma zilizotoka kwa wananchi maskini zinavurugwa, zinapotea na tunapata kigugumizi kusema. Kwa nini mtu akishapoteza pesa mwaka huu na mwaka kesho akapoteza inakuwa kazi kubwa kumuondoa huyo mtu mahali alipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mpango huu utaendaje? Kama tunataka uende vizuri lazima wafanyakazi na watendaji wote wajipange vizuri amba wana *commitement*, wana *professionalism* na wanaweza kuamini ni nini sera ya nchi hii. Si ajabu wengine wako kwenye *position* walizopewa ambazo ni muhimu lakini ukimwambia hebu soma mpango wa miaka mitano haujui. Kwa hiyo ye ye anasubiri pesa zitoke *treasury* aje atumie anavyotaka, hajui kujipima kwamba mwaka jana tulifanya kazi kadhaa, mwaka huu tunafika wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tena haraka niseme, siku hizi kuna kitu kimetokea, badala ya nyaraka ni semina, hivi ni kusema tuliajiri wote amba hawakwenda shule? Kwa sababu hizi semina tuseme ukweli zinatusaidia kuganga njaa, lakini ukweli ni kwamba kuna mambo mengi ya maelekezo. Zamani ilikuwa ni waraka wa Serikali. Ukitumwa huo waraka ndiyo unatoa maagizo na ndiyo *reference point*, tukienda kwenye semina yamekwenda na hewa, lakini ukiwa na waraka amba ni imara, ortalinda matumizi na mtu akikiuka huo waraka ni mara moja wala hangoji tena kwenda

ku-negotiate, ooh mniache kwenye kazi, ikawa vile, ikawa hivi, ilikuwa ukikiuka, umekiuka moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukali huu tuuveke lakini tukilindana lindana, nataka nitumie Wilaya yangu kama mfano, watu wa pesa wanashindwa kuweka mapesa vizuri, sisi ndiyo tunanyimwa lile fungu la pesa za kusaidia maendeleo. Wale Wakerewe wavuvi wamekosa nini? Aliyefanya vurugu ni mtu anaye-deal na *profession* ya pesa. Mnakuja mnatwambia sisi hatuwapi msaada na hivyo katika Wilaya nyingi hasa hizi za pembezoni, watu wakifika kule wanajitawala kwa sababu wanajua hata wakubwa wanapata tabu kufika katika maeneo hayo kuwakagau.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine matumizi ya muda. Hilo ndilo kabisa halina mpango. Watu hatuna muda, *timeframe* ya kusema katika maendeleo hili litafanyika kwa miezi kadhaa *full stop*. Hapa tuna mikataba mingapi ya makandarasi, anakwenda kila siku wanaongeza muda badala ya kusema ikifika tarehe fulani tuliyokubaliana hujawenza kufanya kazi kwa sababu ulipokuwa una-sign mkataba ulijua mvua zipo, ulijua matatizo mengine, yote hayo ndiyo unayaweka katika programu yako ya kuomba ukandarasi, lakini tuna *drag* mpaka muda, mradi unakuwa mara mbili, tatu, tunapoteza rasilimali za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kero. Watanzania hawa wasipokuwa na raha katika nchi yao, kila mara mlango ukigongwa unasema sijui majambazi hao, kila mara unapopita njiani huna uhakika kama utafika nyumbani. Unakuwa ni mtu wa wasiwasi, sasa tunajenga maendeleo ya watu wa wasiwasi, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho. Taifa lisilokuwa na watu walioelimika haliwezi likapiga hatua. Elimu ya watu wazima tumeua ya nini? Usipoiweka kwenye mipango hii kilimo kwanza na nini hakiendi. Kilimo kwanza kitakwenda kama mkulima anajua kulima kwa mistari *simple*. Turudi kwenye zana za zamani zile za vitu kuviweka katika lugha nyepesi, katika mkakati mwepesi.

Tulikuwa tunasema mvua za kwanza ni za kupandia, watu wakaelewa lakini *complication* na *jagon*, haya ma-documents leo nikibeba kupeleka kijijini, nani anayaelewa? Kwa hiyo, nataka turudi pale kujitegemea. Pili, utegemezi, tuache kabisa, tuna dhahabu, tuna almasi, tuna maziwa, tuna kila kitu nadhani watu wamesimama tu wanatuangalia hawa nao vipi? Lakini mwisho kuheshimiana kama Watanzania, hizi vurugu za kwenye magazeti hizi, zitaua watu. Rwanda waliuana milioni sijui ngapi kwa sababu ya viredio. Sasa kama tunataka maendeleo waandishi wa habari mtusaidie jamani, watu wasome vitu vinavyowapa matumaini, watu wasome vitu vinavyowapa ujuzi mpya, maarifa mapya, sio wasome malumbano ya sisi wanasiwa, nani anakwenda kugombea wapi, acha wakagombee tutafia huko huko, lakini watu wapate matumaini, wajukuu zetu sisi waweze kupata maarifa. Siku hizi magazeti unanunua huthubutu kuliacha *sitting room* mjukuu akalisoma, atakuuliza maswali wakati huna majibu kwa sababu mengine ni matusi matupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, waandishi wa habari mnanguvu sana, mtalikomboa Taifa hili tunapoelekea kwenye maendeleo ya nchi hii

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nishukuru na niseme kwamba, namtakia kila la kheri Waziri wa Fedha, lakini pia ajaribu kutumia wataalam nje ya Wizara yake tutampa mawazo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, uzee dawa. Sasa namwita Mheshimiwa Jenister Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Fred Mpandazoe na Mheshimiwa Diana Chilolo pia atafikiwa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kabla hata muda haujaniishia kwanza niseme kwamba, naiunga mkono hoja hii. (Makofsi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema, ni kweli kwamba, tunahangaika kuona namna gani tunaweza kusaidia maendeleo ya nchi yetu. Lakini kimoja naweza kusema kwamba, tumepega hatua ukilinganisha kule tulikotoka na hapa tulipo kwa namna moja ama nyingine, nchi yetu imepiga hatua na hata ukienda nje, unaona kabisa kwamba yako maeneo sisi tunatolewa kama mfano mzuri wa utekelezaji. Hiyo kwa kweli lazima niseme na ni lazima hapo kwanza tukubaliane na haya yote yanatokana na uongozi bora wa Chama chetu tena Chama Tawala

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo mazuri ambayo tumekuwa tukijivunia na sifa tunayoipata, bado tunatakiwa kuendana na changamoto ambazo zinatukabili kwa sasa. Dunia hii kwa sasa hivi ni kama kijiji, kipindi cha huko nyuma dunia ilikuwa si kama kijiji, kwa hiyo tulikuwa tunajitazama sisi na mambo yetu tuliyonayo, lakini sasa hivi dunia ndiyo imekuwa sasa kama kijiji kwa maana wote tunaelewana na kila kinachoendelea katika ulimwengu kiko wazi. Sasa hapo ndipo changamoto zinapoanza kuja. Sasa tunapopata changamoto hizi ni kuangalia hali halisi tuliyonayo, mazingira tuliyonayo na namna gani tufanye ili tuweze kuondokana na changamoto hizo na kujaribu kuwaweka Watanzania waweze kwenda kwa *speed* zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kusema, naunga mkono kabisa *agenda* ya mwongozo wa mpango huu kwamba kilimo kichukue nafasi ya kwanza. Naomba kwanza niseme kwa nini naunga mkono hilo. Nilikuwa kwenye mkutano mwaka jana mwezi wa kumi na mbili na nilikuwa naongea na Mkurugenzi wa Fedha wa Afrika wa Benki ya Dunia, aliniambia kitu kimoja ambacho nimejaribu kukifikiria sana. Alisema katika fedha zilizotolewa na Benki ya Dunia kusaidia maendeleo ya nchi na hasa nchi za Afrika, fedha zilizokwenda katika sekta ya kilimo angalau zimeweza kutoa matunda yanayoonekana kulinganisha na miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaona kwamba kuna kiashiria kinachotwambia kama tutakitumia kilimo kama *agenda* ya kwanza inaweza kutusaidia sana na hii ilikuwa ni ripoti ya mwaka 2006. Lakini unaona kabisa kwamba hata malengo ya kimilenia, lengo namba moja ni kupambana na njaa na kupambana na umaskini. Utakapozungumza

habari ya njaa ina maana kwamba kilimo huwezi kukiacha nje. Kwa hiyo, hata kama wenzetu mpaka ulimwengu mzima wakaona umuhimu wa kuweka lengo la kwanza la kimilienia ni suala zima la kupambana na njaa na umaskini, ina maana uchumi *per se*, ni suala la umasikini na ni suala la kilimo, halafu mengine yote yataendelea kuwepo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kusisitiza kwamba, nakubalina na naunga mkono na hoja ya kwamba kilimo ndiyo kituongoze. Lakini bado niendelee tu na utangulizi wangu, unaona ongezeko la watu duniani linaendelea kuwa kubwa sana, inatazamiwa mpaka kufika miaka ya 2060 idadi ya watu duniani inaweza kufikia karibu bilioni tisa na nukta ngapi huko.

Lakini bado wataalam wanatwambia asilimia sabini na tano ya ongezeko hilo la watu, watu hao bado wataendelea kuwa wanaishi vijijini, lakini asilimia hiyo sabini na tano, watu hao wataendelea kuwa na tatizo kubwa la umaskini. Sasa asilimia hiyo hiyo ya watu sabini na tano kama wako vijijini hatuwezi kukwepa kwamba watu hao ni wakulima. Kwa maana hiyo basi tusipofanya maamuzi katika sekta hii tunawenza kujikuta kwa muda mrefu tunaendelea kupiga *mark time* ya kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme, pamoja na haya yote niliyoyapitia, ushauri unatolewa ili sasa hicho kilimo katika sekta ya mifugo, katika sekta ya uvuvi watu wamekuwa wakisema uvuvi, hapana uvuvi na sekta hiyo ya kilimo kwa maana ya mazao, sasa ni kiasi cha kuangalia Serikali imesema nini. Serikali katika kutwambia kwamba kilimo ni sekta kiongozi, wao wamesema katika kilimo wataangalia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, umwagiliaji, uvuvi, kilimo na mifugo, sawa. Lakini nataka kusema hayo ni kweli, akisema uvuvi, umwagiliaji, kilimo na nini hiyo yote ni kilimo. Sasa chini ya hayo ndiyo sasa Serikali ilitakiwa kupunguza ule mlolongo wa vipaumbele na kusema sasa sekta zinazoambatana na kilimo ni sekta zipi ili sasa kuoanisha sasa kilimo na sekta nyingine ambatanishi zifanye kazi kwa pamoja kwa maana sasa ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo badala ya kuanza kui-*define* sekta nyingine huko chini, wangesema sekta ya kilimo sasa, sekta ya uvuvi, sekta ya mifugo iendane na suala zima la miundombinu ya kimasoko, iendane sambamba na suala zima la miundombinu ya viwanda, vyote vikaambatanishwa hapo hapo, iendane na suala zima la miundombinu ya umeme, vyote vikawekwa kwenye sekta ya kilimo, iendane sambamba na miundombinu ya barabara. Kwa hiyo ungeona kwamba, tunazungumza kilimo lakini kikiwa na sekta ambatanishi vyote vimekaa pamoja kama vichocheo vya kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ndiyo nafikiri tunapotakiwa kupajadili na tukiweza kuviambatanisha hivi, kwanza tutakuwa tumeondo ile dhana ya kwamba tumeshatafuta vipaumbele vingi tumevileta. Nilichogundua na nimejaribu kufuatilia ripoti mbalimbali za Umoja wa Mataifa za Shirika la Chakula Duniani, unaona kabisa hata wao wanasema hicho kitu na wamesemaa kwamba katika hiyo miaka niliyosema ya ongezeko la watu, kama nchi itajitahidi angalau kwa asilimia sabini na tano kuunganisha

sekta ya kilimo na haya niliyoyasema kwamba sekta hiyo ya kilimo ikaendana na viwanda kama tunavyokubaliana kwenye ufugaji, tungeongeza uzalishaji wa nyama, uzalishaji wa ngozi ungeona kabisa tungesaidia hata kuifanya shilingi yetu isiende chini kwa sababu tungepata fedha za kutosha ambazo tungeweza kuwekeza hata nje ya nchi na tunaona shilingi yetu imeanza kwenda chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia mfumo mzima wa kilimo chetu, tunalima sana, tunalima pamba, tunalima mazao ya chakula, tunalima kahawa lakini hatuna viwanda vingi vya kufanya *processing* ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo tungekuwa sisi tunauza nje bidhaa ambazo tayari zimeshatengenezwa ndani ya nchi yetu na tungeweza kuingiza mapato zaidi kutoka nje ya nchi yetu na hivyo basi umaskini ungepungua kama vile *millennium goal* namba moja inavyosema: “Ni lazima uhakikishe kwamba umaskini lazima utaendana na kilimo”.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini miundombinu kama barabara, kama bandari hivi vyote vinaendana sambamba kabisa kama nilivyosema, tukishazalisha kwa wingi kama hatuna barabara za kutosha tutashindwa kufanya kazi. Tusipoimarishe bandari zetu hatutaweza kufanya kazi. Sasa ukishayapanga hayo kwa utaratibu huo ndiyo linakuja sasa swalii zito. Wapi tunapata fedha za kuhakikisha hizo barabara zinakwenda vizuri, viwanda vinawenza kufunguliwa, Bandari zinaimarishwa na vitu vingine vyote vinafanyiwa kazi? Sasa tukifika hapo ndiyo tutengeneze kipaumbele namba mbili kitakachotufanya tupate fedha za ku-*facilitate* hayo ili yaweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kipaumbele namba mbili ndiyo tungeangalia ni maeneo yapi ndani ya nchi yetu yanaweza kutupa fedha kwa haraka kuweza kutekeleza hayo? Tumeona sekta ya utalii inaongoza sana katika mapato ya nchi yetu. Kwa hiyo, ndiyo tujiimarishe kwenye sekta hiyo ya Utalii ili tupate pesa kwa haraka, tuweze sasa ku-*sustain* hiyo *agenda* yetu, namba moja ambayo itatupa uchumi. Tunaangalia sekta ya madini, tufanye nini kwenye sekta ya madini inayoweza kutuongezea pato la kutosha? Halafu pato lile likishapatikana kazi ya haraka, matunda ya haraka kwenye kilimo ni yapi, halafu tuone matunda ya muda mrefu tufanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaona kwamba tunakuwa na sekta nyingi inayo-*facilitate* sekta inayotuongoza halafu tunakwenda mbele. Kwa hiyo, naomba kusema hakika tumeanza vizuri, nitolee mfano wa kitu kimoja, taarifa ya Mheshimiwa Waziri imeeleza hapa, kwa mfano suala la pembejeo, kweli tunashukuru sana Serikali imefanya vizuri sana kwenye suala la ruzuku, lakini niseme tu kwamba bado tunatakiwa kuangalia zaidi. Tumepata matatizo kwa mfano, wakulima wamepewa ruzuku safari hii lakini badala ya kupewa mifuko miwili ya mbolea kwa ajili ya kukuzia wamepewa mifuko mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaona mawazo yanakuwa mazuri, lakini utekelezaji hauendani na dhana nzima ya kilimo chenyewe, nchi nzima hii kero ya mbolea mifuko mmoja kwa ajili ya kukuzia mazao imesumbua sana karibu katika nchi nzima. Sasa na hiyo ni kwa sababu hatuna pesa za kutosha za kuwezesha wananchi hao wakapata mbolea mifuko miwili miwili kwa mpango ule wa ruzuku. Sasa lazima tuwe

na sekta nyingine itakayotusaidia kupata fedha na sasa hivi bila fedha huna sauti mahali popote na fedha hiyo iwe ya kwako wewe mwenyewe. Hata mimi nikitegemea fedha za Mama Mongella ndiyo nizipangie bajeti, hakika ni matatizo makubwa sana. Nijidai wakati nina fedha zangu katika mfuko wangu kwamba sitegemei cha mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiwa mama nyumbani ukiwa na fedha kidogo utaona hata baba anapenda mshauriane shauriane mipango, mpeane mawazo. Kwa hiyo sisi jeuri yetu itakayotusaidia katika kujiipanga na kufanya mambo yetu ndani ya Tanzania ni kutafuta sekta kiongozi kama tulivyosema, lakini sekta ambazo zitakuwa kichocheo cha kutupa fedha na fedha zile zitatusaidia. Tukimaliza hapo suala la elimu halitakuwa shida, tutajenga mashule tutamaliza, suala la afya halitakuwa na matatizo, fedha tutakuwa nazo, kila kitu kinachotusumbua tutamaliza na watu watatuuheshimu sana katika nchi yetu. Kwa hiyo, niseme kwamba, wenzetu wanajitahidi sana, lakini tuombe wazibe mianya ya maeneo yanayotufanya tusipate fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji mmoja jana alisema kitu kizuri sana. Kila siku tunapokuja kwenye bajeti vyanzo sigara, bia, maji ya kunywa ya chupa na soda. Kwa Taifa hili lenye wasomi walibobebe hebu safari hii waje na mipango mipya ambayo ndiyo hiyo tunayowaambia ya kutafuta vichocheo vingine. Rasilimali nyingine kama Bandari, reli, madini, maliasili tutapata fedha katika nchi hii na hakika maendeleo yetu yatakuwa ni ya kasi sana. Naamini wataalam wanaweza, wakiamua kutulia na wakaamua kutusaidia. Nina imani tulikotoka ni mbali, tulipofika hapa tumefika mahali pazuri, hapana matatizo, kinachohitajika sasa ni utashi wa kutoa maamuzi, kila mtu mahali alipo alifanye hilo kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Tunashukuru kama ingekuwa hivyo lakini bado urasimu ni taitizo. Sasa namwita Mheshimiwa Fred Mpêndazoe namwona hapa Mheshimiwa Diana, nafikiri tutafikia na Mheshimiwa Mushashu.

MHE. FRED T. MPENDAZOE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo tunaojadili kama ilivyoonesha kwenye ili kabrasha tulilopewa dira ya Taifa, Maendeleo ya Milenia, MKUKUTA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Naona programu hizi zina mikakati haina utata ndiyo mwanzo kabisa nimeamua kuunga mkono hoja hii. Lakini nina maeneo ambayo ningependa sana niyasisitize katika mchango wangu. Kwanza mwongozo umebainisha vipaumbele vingi ni kama vitano kama ilivyoonesha katika ukurasa wa 32 na 33, vipaumbele hivi ni vingi sana, ingekuwa ni vyema vikapunguzwa vikabaki vichache. Maana ukiwa na vipaumbele vingi ina maana huna kipaumbele kabisa, kwa hiyo ni vyema vipunguzwe tu na nisingeanza kuzungumzia vipi viondolewe na vipi vibaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kulingana na vipaumbele vilivyooneshwa, naona nizungumzie mambo matatu. La kwanza kabisa, naomba nizungumze kwamba, wakati wanaangalia vipaumbele ambavyo watavibakiza, lakini nilikuwa nadhani Serikali yetu iendelee kuimarisha suala la utawala bora, ni muhimu sana kuimarisha utawala bora katika nchi yetu. Usimamizi wa maisha ya wananchi na furaha yao ni lengo pekee na lengo la kwanza la Serikali yoyote bora duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo hili linaweza kutimizwa tu kama kuna utawala bora. Tukiangalia ripoti ya Mkaguzi wa Fedha ya Mwaka 2007, alieleza kwamba asilimia 37 ya fedha zilizotoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa hazikutumika. Zilitoka Serikali Kuu zikaenda Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri zetu, hazikuweza kutumika kutokana na uhamasishaji hafifu uliofanywa na watendaji wetu ma-WEO, ma-VEO na viongozi wengine katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni suala zito sana, asilimia 37 ya fedha kutoka Serikali Kuu hazikutumika zimefika kule, ukiacha fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali, lakini kwa nini uhamasishaji umekuwa ni hafifu, la kwanza ambalo nilikuwa naona lizingatiwe sana, sehemu nyingi vijiji ni vikubwa sana, ma-VEO hawawezi kumudu kushughulikia shughuli za maendeleo katika vijiji vyao. Ma-WEO wanashindwa kutimiza wajibu wao katika Kata zao kutokana na Kata hizo kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kuna masuala la vitendea kazi kwa ma-VEO, hawana vitendea kazi vya kutosha, kwa mfano, usafiri na kadhalika wakiwemo vile vile ma-WEO hawana vitendea kazi vya kutosha. Ina maana katika kuhamasisha wananchi katika maeneo yao ili waweze kuibua miradi kama sera inavyosema kwamba wananchi wataibua miradi ili kuungana na Serikali katika kutekeleza shughuli za maendeleo katika maeneo hayo, wanashindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji vyenye kaya mia tisa, hata elfu moja vinafika, VEO asie na vitendea kazi hawezo kwenda kuhamasisha na hata kukiwa na mkutano wa hadhara inashindikana kualika, kwa hiyo kuna uhamasishaji haffifu matokeo yake asilimia 37 ya fedha zilizopelekwa kutoka Serikali Kuu hazikuweza kutumika, kwa hiyo ipo haja kubwa sana kugawa Vijiji, kugawa Kata na kugawa Wilaya ili wananchi waweze kuwa na maamuzi na kufikiwa na viongozi wao kwa wakati unaohitajika. Niliomba vijiji ishirini na nne viweze kuanzishwa katika Wilaya yangu, nadhani na naamini Serikali itatimiza kama ilivyoniahidhi kwamba mwaka huu itafanya hivyo. Lakini na maeneo mengine kuna haja ya kuzingatia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala lingine la kuweka mazingira na kuimarisha uongozi bora katika nchi yetu. Katika ngazi zote pasipo uongozi bora maendeleo hayawezi kupatikana. Ripoti ya CAG ya mwaka 2008 inaeleza, bilioni 6 za fedha za bajeti zilitumika bila nyaraka, ina maana ziliibiwa kwenye Halmashauri zetu. Ukiacha fedha zingine ambazo hazikutumika bila taratibu nzuri kutoka kwa wafadhili. Mwongozo tunaoujadili sasa imeonyesha kwamba vyanzo vya kodi havikufanya vizuri katika kuleta mapato ya ndani ya nchi yetu. Lakini vile vile imeonyesha misamaha ya kodi inayofikia bilioni 324 ilitolewa. Haya mambo mawili ya

kutofanya vizuri kwa ukusanyaji wa kodi, na misamaha ya kodi inayofikia bilioni 324 inaonyesha kuna umuhimu wa kuimarisha uongozi bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la rushwa katika nchi yetu na lenyewe linatakiwa kuzingatiwa na kutokomezwa. Nimesoma mahali fulani inasema hivi, Serikali yoyote duniani inayotokana na kula rushwa haikusanyi kodi. Inatumwa na matajiri na inaabudu matajiri. Tusipoweka kipaumbele cha kupiga vita rushwa na kuiondoa na kuwa na utawala bora na uongozi bora katika nchi maendeleo hayawezi kupatikana. Hivyo kutokomeza rushwa na suala la kuimarisha uongozi bora katika nchi yetu, pamoja na kuchagua vipaumbele vizuri sana kama rushwa itaendelea kuwepo katika chaguzi zetu suala la maendeleo litakuwa ni ndoto sana katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala lingine la mwisho kuhusu uwajibikaji. Nadhani ilikuwa ni jana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu aliweza kuzungumzia na kufafanua akasema kwamba tunalo tatizo kubwa sana la kulindana katika nchi yetu. Alilisema yeye jana, *Hansard* itaonyesha, Namnukuu: "Suala la kuwajibika ni suala muhimu sana katika nchi yetu na tutawajibika kila mtu katika nafasi yake kama hatatalindana. Lakini tutawajibika vizuri zaidi kama tutaiangalia Katiba yetu. Katiba yetu ambayo ndiyo Sheria Mama ndiyo iliyozaa mifumo ya uendeshaji wa nchi yetu. Ni dhahiri inahitaji marekebisho ili tuimarishe suala la uwajibikaji katika kuendesha nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja, limezungumzwa sana, nadhani lazima tulikubali, tuliangalie na ikiwezekana tuangalie Katiba yetu na tuiureka. Waziri kuwa Mbunge hamna tija sana. Ni vema Mawaziri wasiwe Wabunge. Ni eneo moja ambalo natolea mfano ambalo linaweza likaimarisha uwajibikaji katika nchi yetu. Lakini kuna mambo mengi ya kuangalia katika Katiba yetu, tukiifanya marekebisho nadhani inaweza ikaimarisha uwajibikaji na kiongozi anapokuwa amepewa dhamana ya kuongoza, akiona Katiba anaweza akaona hapa nisipowajibika baadaye nitawajibishwa. Nadhani Katiba yetu ni nzuri lakini inahitaji kufanyiwa marekebisho ili tuweze kuendana na changamoto tulizonazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile matokeo ya Zanzibar yaliyotokea kule yanaweza kuonyesha kwamba tunahitaji kuwa na Katiba ambayo itaweza ku-accommodate yaliyotokea huko ambayo dhahiri ni mazuri. Lakini nadhani wakati wa bajeti hii sasa ni kuweza kuangalia mambo yote hayo ya kuimarisha utawala bora, kuimarisha uongozi bora na kuimarisha uwajibikaji na kuangalia changamoto tulizonazo kwa sababu tunakwenda kwenye uchaguzi haya yote ni muhimu sana ambayo yanaweza kusababisha kuzaa Serikali bora zaidi na wananchi wakaweza kunufaika na Serikali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona ya kwangu ambayo nilipenda niyazungumze yamekwisha. Sasa naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mapendekezo ya mwongozo wa utayarishaji wa mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri. Kwa kweli utaratibu huu waliouanzisha wa kuwasilisha mwongozo mapema ni mzuri sana kwa sababu ni imani yangu kwamba michango yote mizuri ya Waheshimiwa Wabunge iliyotolewa itafanyiwa kazi wakati wanaandaa bajeti nzima ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri, sasa nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali, ni vizuri sana tukawa na takwimu sahihi za uchumi wa mikoa yetu. Huwezi ukamsaidia mtu kama hujui yeye mwenyewe anajitahidi kiasi gani katika kuzalisha pato lake. Nikisema hivi nina maana yangu. Kwa mfano Mkao wa Singida tuna shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Tunalima vitunguu, wakati wa mavuno, tunasafirisha magunia ya vitunguu. Lakini hakuna takwimu zinazowekwa tunasafirisha vitunguu kwa kiwango gani. Tunasafirisha kuku kila siku Singida hakuna takwimu zinazoonyesha kwamba kila siku kuku wa Singida wanatasafirishwa kwa kiasi gani. Tunalima alizeti, hakuna takwimu zinazoonyesha kwa zao la alizeti tunazalisha kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata ukitaka kupima pato la mwananchi wa kawaida wa Mkao wa Singida utapataje? Kama hujaweka kumbukumbu sahihi za uzalishaji mzima wa wananchi wa Singida. Tuna mifugo ya kutosha Mkao wa Singida, tunapeleka minadani kila siku, hakuna takwimu za kutosha kuonyesha kwamba katika kila gulio wanauzwa ng'ombe wenye uzito gani na wenye ubora gani. Naomba Serikali kama kweli inataka kupata *data* za uhakika za uchumi wa nchi hii iwe na takwimu za kutosha ndani ya Mikoa yetu ili tuweze kujua wananchi wetu wana vipato gani ili tuweze kujua tuwasaidie wananchi hao kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuwatengenezea wananchi barabara kutoka mahali mpaka mahali wakati hujajua huko ninakopeleka barabara ina wananchi wa wingi wa kiasi gani na kuna wakulima na wafugaji wengi kiasi gani. Naomba takwimu zipewe kipaumbele katika bajeti ya Serikali yetu. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, naomba niongelee jinsi ya kuwapa unafuu wananchi wa Tanzania wakiwemo akina mama. Akina mama wa karne hii wako katika mstari wa mbele sana katika kuzalisha mali na akina mama hao wanahitaji Serikali iwasaidie katika kupata mikopo. Lakini mabenki hayawasaidii kabisa kabisa, hayana urafiki kabisa na mteja maskini. Kwa sababu riba zake ni kubwa, ni kubwa, ni kubwa. Ni wananchi wachache wanaonufaika na mikopo hii. Labda sana sana ni wale wafanya biashara wakubwa wakubwa. Naomba sana itazame upya riba za mabenki yetu na mashirika yanayokopesha. Unakuta mashirika yanakopesha riba ni nusu ya mkopo wake, nusu kwa nusu, hivi kweli huyo mwanamke mbangaizaji anayejitalihidi

kuondokana na umaskini utakuwa umemkomboa kwa kiasi gani. Naomba riba katika benki zetu zitazamwe upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo riba tu pamoja na muda wa ukopaji, mikopo mingi inakuwa na muda mfupi sana. Hivi mtu kakopa mkopo kwa ajili ya kilimo, mnajua hatua za kilimo, uandae shamba, sijui ufanye nini, utafute mbegu, utafute pembejeo. Unapompa mtu mkopo kwa kulipa kwa muda mfupi huyo umemsaidia ama umeamua kumtesa. Naomba sana sana muda katika ukopaji upewe kipaumbele, kuwe na muda mrefu. Kuna mikopo ambayo inahitaji hatua nyingi kwa ajili ya kukamilisha huo uzalishaji. Hata ujenzi wa nyumba, mtu anakopa pesa kwa ajili ya kujenga nyumba, unamwambia arejeshe ndani ya miezi sita. Hivi huyu atakuwa amejenga nyumba muda gani na atakuwa ameanza kuizalisha lini hata aweze kurejesha huo mkopo. Naomba sana sana pamoja na kupunguza riba vile vile tuangalie muda, wakopaji wapewe muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee bajeti ya ziada. Naiomba Serikali katika kuandaa bajeti, tuwe na bajeti ya ziada, dharura ni nyingi. Nataka nitoe mfano, kwa mfano, ndani ya Mkoa wa Singida, Bodi ya Barabara imekaa, ikapandisha daraja barabara nyingi tu. Kila Wilaya labda barabara moja moja. Barabara hizo tayari zimeshahama kwenye Halmashauri, zimehamia kwa Wakala wa Barabara. Unamkuta Wakala wa Barabara anakwambia mimi sasa hivi sina bajeti yake sijapewa bajeti yake, barabara hiyo itabaki inaning'inia, tunahangaika, zinachimbika, zinasubiri mpaka kipindi cha bajeti ndiyo bajeti za barabara hizo zipangwe. Naomba kila sekta iwe na bajeti ya ziada kwa ajili ya kunusuru matatizo yanayojitokeza ya dharura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu namna ya kuwasaidia wazalishaji pamoja na wauzaji. Katika nchi yetu kuna mzalishaji kwa mfano, *let say* mkulima, halafu kuna mtumiaji na kuna muuzaji. Watu hawa yupo mtu mmoja hapa anakandamizwa sana hasa yule mzalishaji, mkulima anayefanya kazi ya kuzalisha. Unakuta anatumia fedha nyingi sana katika kuzalisha zao ambalo analilima. Lakini unakuta zao hilo analiuza kwa bei ya chini sana. Zao hilo faida inahamia kwa muuzaji. Nina hakika hili nalo linatakiwa litazamwe kwa kina sana ili tuweze kumpa unafuu mwananchi wa chihi badala ya kumnufaisha mfanyabiashara ambaye kazi yake ni nyepesi kuliko kazi ya mzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la watumishi wa chini. Watumishi wa chini kwa kweli wanahaaulika sana hasa kwa upande wa vitendea kazi, hawana pikipiki, hawana balskeli, wakati mtu huyo huyo unataka ahimize kilimo bora ili uchumi ukue, utakuaje kama huyu mtu hajawezeshwa? Hebu tumwangilie askari, askari wa chini hata hapa Dodoma, hana nyumba, anakaa mtaani, hivi huyu mtu atafanya kazi yake kikamilifu? Hivi kweli atadhibiti mali ya nchi hii? Hivi kweli huyu mtu atatulinda? Tunaomba sana sana tunapoandaa hebu tujaribu kuwatazama kwa karibu sana watumishi wa chini, tuwasaidie kuwawekea mazingira mazuri ya kufanya kazi ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Tukiwafanya hayo ama kweli wataweza kutusaidia kuinua uchumi wa nchi yetu na kuleta ulinzi wenye tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu wafanyakazi. Wafanyakazi wanafanya kazi nzuri sana, lakini wanachopata tabu ni maslahi. Maslahi yao ni duni hawaboreshewi mishahara yao. Hivi sasa mwenzangu hapa anapambana sijui na wizi, sijui kitu gani, sasa utapambana na vitu vyote hivyo wakati mtu hujamboreshea maslahi yake. Nina hakika kabisa wafanyakazi tukiwaboreshea maslahi yao, tukiwapa mishahara mizuri, tukiwapa hela zao labda za likizo, tukiwapa huduma muhimu, nina hakika watu hawa tutakuwa tumewakata mikono ya wizi. Uchumi wa nchi yetu unapotea kwa sababu watu wanapopata nafasi wanasema chukua chako mapema. Kwa sababu pato wanaloapata ni dogo, mtu anaona bora achukue hicho aweze na yeze kupata nyumba nzuri ya kulala na kumbe hapo anaififisha Serikali katika uchumi wake wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu hawa Maafisa wa Serikali, huwa wanapewa nyumba na samani na kila kitu na Serikali. Nawapongeza Mawaziri wangu, wengi nimewatembelea kwenye nyumba zao. Wana nyumba za kawaida, wana samani za kawaida, lakini Watendaji Wakuu wa Serikali, Mtendaji Mkuu anapata madaraka leo anakwenda kuingia kwenye Ofisi anaangalia fenicha anasema hii siyo *test* yangu. Hivi kweli tunakwenda na ushabiki. Anakwenda kwenye nyumba aliyohamishiwa, anaangalia rangi, labda yeze ni mshabiki wa Yanga, kuna rangi nyingine anasema hiyo siyo rangi yangu. Nyumba inaanza kupakwa rangi upya, nyumba inabadilishwa samani. Hivi hawa wenzetu wana mkataba na nyumba hizo? *Test* zetu tuzipeleke kwenye nyumba zetu tulizojenga wenyewe, tukifanya hivyo tutasaidia sana kuokoa fedha zinazopotea za nchi hii bila utaratibu. Nimeyaona haya si kwamba najisemea, nina ushahidi wa kutosha, tuache mambo ya ushabiki. Tuache mambo ya *test*, twende na mambo yenye kuleta tija katika nchi hii. Tuokoe mali ya nchi hii, ili tuweze kumwinua huyu mwananchi wa chini kwa kutumia fedha hizi ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie.....

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda
wa kuchangia wa Mheshimiwa Mbunge*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Ooh! Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite msemaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali kwa mafanikio makubwa tuliyoyapata. Kwanza kabisa mnakumbuka wote Serikali iliahidi kwamba itatoa ajira zipatazo milioni moja na watu wakafikiri kwamba haitawezekana. Lakini nimefurahi kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri, alipotwambia kwamba ilipofika mwaka 2008 tulishafikisha ajira mpya milioni moja laki mbili na kadhalika. Nawashukuru sana

Serikali kwa jitihada zetu. Lakini vile vile ningependa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa wanawake kwenye nafasi mbalimbali za maamuzi. Nimesoma kwenye taarifa hii vile vile kwamba na sisi tumeona kwamba uteuzi mbalimbali unapotokea kati ya wale wanaoteuliwa wanakuwemo wanawake kwenye nafasi za maamuzi na sasa hivi ilipofika mwaka 2008 tumeambiwa wameshafika asilimia 29. Tunamshukuru kwa busara zake na utashi wake wa kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hoja kwa kuzungumzia vipaumbele. Hoja hii imebainisha kwamba vipaumbele vilivyopo ni kilimo na mifugo, miundombinu, huduma za jamii, ardhi na viwanda. Lakini ukiangalia ndani ya kilimo na mifugo na miundombinu kuna vile vipengele vidogo vidogo nilivovichambua nimeona vinagusa kama Wizara tisa hivi. Kwa hiyo nataka kusema kwamba, *na-feel strongly* kwamba bado vipaumbele ni vingi, vinaweza vikapunguzwa vikawa vichache zaidi kusudi tukiwa na fedha kiasi kidogo basi kiweze kufanya kazi itakayoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilishatamkwa na nakubaliana na wale waliotamka kwamba kipaumbele cha Taifa hili kwa muda mrefu kinapashwa kuwa elimu. Kama kuna kitu ambacho tunaweza kujivunia Serikali ya Awamu ya Nne kwa mambo makubwa yaliyofanyika ni ndani ya Sekta ya elimu. Tumepata mafanikio makubwa tu, shule nyingi zimejengwa mpaka kwenye ngazi ya kila Kata, Kata nyingine zina zaidi ya shule moja. Madarasa mengi sana yamejengwa, wanafunzi wengi wamo mashulen, wanafunzi waliofikia umri wa kwenda shule kuanza darasa la kwanza, wengi wao wameanza. Umri wa wanafunzi wengi waliofikia umri wa kwenda sekondari wamekwenda. Kwa hiyo, tumepata mafanikio makubwa. Lakini pamoja na mafanikio hayo kwa sababu sekta ya elimu imepanuliwa kwa ghafla ghafla bado kuna changamoto nyingi. Kwanza kuna uhaba mkubwa wa walimu. Bado tunazo shule zenye mwalimu mmoja, walimu wawili, bado tuna madarasa ambayo hayajamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko kwenye Kamati ya *LAAC* tunazunguka kwenye Halmashauri mbalimbali, unakuta wananchi wamejitahidi, wamejenga maboma manne, matano pale. Unakuta Serikali imejitahidi, wamejenga madarasa, hayajawekwa milango, hayajawekwa madirisha. Unakuta kwamba mahali pengine maabara zipo, lakini katika sehemu nyingi hakuna maabara. Lakini kwenye shule hizo hizo tulizojenga unakuta kwamba kuna majengo muhimu kama Maktaba, kama *computer labs* hakuna. Lakini bado unakuta katika Halmashauri ambao hawakuchangamka mapema hata madeni ya walimu yapo bado hayajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapohamisha kipaumbele, elimu yenewe haijatengemaa, tukataka kuleta kipaumbele kingine cha kwanza, hata hii kazi nzuri tulioanza haitaonekana. Naishauri Serikali kwamba tuendelee na elimu iendeleee kuwa kipaumbele, tukamilishe vile viporo, tupendezeshe, tutengeneze mazingira mazuri ambayo yanafaa kutoa elimu bora kwa Mtanzania na wote mnatambua kwamba elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Tukishakuwa na elimu bora kila kitu kitajileta tu. Hata hicho kilimo kwanza, kwa sababu tutakuwa na wataalam wa kutosha wa kuweza kushauri namna gani ya kukuza hicho kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie mtikisiko wa uchumi. Sababu ya mtikisiko wa uchumi duniani bei za mazao kama kahawa, pamba ziliteremka sana, wanunuzi wa kahawa wakiwemo wafanyabiashara binafsi na vyama vyaya ushirika walipata hasara kwa sababu wao walinunua kutoka kwa wakulima kwa bei za juu lakini walipokwenda kwenye soko la dunia bei zikawa zimeteremka na mkumbuke kwamba kwa sababu hiyo basi walishindwa kulipa madeni na mikopo walijokuwa wamechukua benki. Lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 10 mwezi wa sita mwaka jana, mwaka 2009 akihutubia hapa Dodoma alieleza kuwa kutakuwa na mkakati maalum wa kuhami na kunusuru uchumi ili kukabili matatizo ya mpito na ya dharura na katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha vile vile alitoa ahadi zifuatazo:-

Kwamba watafidia hasara waliyopata wanunuzi wa kahawa na pamba na kwamba watalipa mikopo ya benki au ambayo mashirika haya walikuwa wameshindwa kuyalipa. Lakini vile vile walisema watatoa udhamini wa kuainisha ulipaji wa mikopo ya walioathirika na waliahidi kutoa ruzuku kwenye bei za mazao hayo. Nasikia kwamba wanunuzi wa pamba wamekwishalipwa, lakini wanunuzi wote wa kahawa walio Mkoa wa Kilimanjaro, Mbinga na katika Mkoa wa Kagera hawajalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoolewa huu ulipaji ulikuwa unapashwa kuwa ni mpango wa dharura wa kunusuru uchumi kwa hao wanunuzi wetu. Kwa mfano vyama vikuu vyaya kama kwetu *KCU, KBCU* na wafanyabiashara binafsi. Ukiuliza wanakwambia kwamba bado wako kwenye mchakato. Sasa nauliza huu mchakato utaendelea mpaka lini? Hebu tuangalie Amerika walifanyaje, si mtikisiko ulianzia kule. Lakini baada ya Rais Obama kutangaza mkakati, *economic stimulas plan* mara moja waliweka hela kwenye mzunguko, waliweka hela kwenye *system* na juzi nimesikia wakitangaza kwamba sasa uchumi wao umeanza kurudi kwenye *track* ndiyo maana wamejihakikishia na wametangaza kwamba ifikapo Desemba mwaka huu watakuwa wameweza kutoa ajira mpya milioni tatu na nusu kwa sababu gain? Kwa sababu walichukua hatua za haraka, lakini sisi bado tuko kwenye mchakato mpaka leo.

Mheshimiwa Rais alikuwa na nia nzuri lakini watendaji wa Serikali mnatuangusha, michakato inachukua muda mrefu. Sasa angalia matokeo yake na athari zake ni nini. Kwa mkoa wa Kagera maandalizi ya msimu mwingine unaofuata yameanza. Kwa sababu ndugu zangu katika kuuza kahawa hawaandai tu, yaani hawatoi hela za kwenda kununua kahawa lazima uandae na viwanda vyaya kukoboa na lazima vifanyiwe *rehabilitation*. Lazima uandae kununua vitendea kazi hizo *consumables* wameanza msimu. Hata hela za *stimulas package* hazijafika huko. Lakini mkumbuke ili waweze kuandaa hivyo viwanda wanahitaji hela ambazo huwa wanakopa benki. Hawakopesheki kwa sababu kwanza madeni yameshakuwa makubwa sana. Kwa sababu hayakulipwa kwa wakati. Kwa hiyo watakosa fedha za kununua kahawa na hatari itakuwaje kwa wakulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wana kahawa wanachohitaji ni fedha. Kwa sababu vyama vyaya ushirika havitanunua na wafanyabiashara wa Tanzania hawatanunua, wako walanguzi jamani watatoka Uganda watakuja kununua hii kahawa na sisi tutakuwa tumepoteza pato la Taifa. Swali kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa wanunuzi hawa

watakeleze wa ahadi yao na mnawasa idiaje Mkao wa Kagera katika maandalizi ya msimu wa kahawa unaokuja? Tumeona jinsi msukosuko wa dunia, uchumi wa dunia ulivyoathiri uchumi wetu kwamba wametwambia kwamba pato la Taifa limeteremka kutoka kwenye asilimia 7.4 zimefika 5. Mfumko wa bei ulipanda mpaka *GDP* 2. Shilingi imeshuka kujua katika mpango huu mliotuletea wa bajeti, kuna mkakati gani wa kulinda uchumi wetu usiathirike sana na mtikisiko kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kilimo kwanza kifanikiwe lazima kuwe na miundombinu ya barabara, reli, viwanda na viwanja vya ndege. Ili kutaka kuufungua Mkao wa Kagera tunacho kiwanja kimoja tu cha ndege ambacho ni kikubwa kidogo kiko pale Bukoba Mjini. Serikali iliahidi kwamba itakitengeneza kile kiwanja, wakaanza kukipanua, lakini tulivyoahidiwa tulijua kwamba kinatengenezwa kwa kiwango cha lami kwa sababu mvua za Mkao wa Kagera mnazijua, kuna wakati zinaweza kunyesha tangu asubuhi mpaka jioni, jioni mpaka asubuhi kwa muda wa siku tatu mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonishangaza sasa naambiwa kiwanja kile kinatengenezwa kwa kiwango cha matope. Au wengine mnaita changarawe. Sasa tutakuwa tumetatua tatizo au tutakuwa tumepeoteza hela za Serikali. Naomba nielezwe katika mwongozo huu tunaouandaa wa bajeti, unaweza kuandaliwa kiasi kwamba ukaelekeza hela nyingi zaidi zikaenda kwenye kutengeneza ule uwanja ukawa kwa kiwango cha lami kuusaidia Mkao wa Kagera kusudi katika kilimo kwanza wawewe kupata mahali pa kupitishia hayo mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napendekeza baada ya elimu, kipaumbele cha pili kiwe kilimo kwanza, kwa sababu Watanzania wengi ni wakulima na wako vijijini. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa mwongozo wa bajeti nikitegemea michango yetu itasaidia kuboresha maandalizi ya bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, nawashukuru wote waliopata nafasi kipindi cha asubuhi kuweza kutoa mjadala wao. Sasa Waheshimiwa hii hoja lazima iishe leo na wachangiaji walioomba kwa siku nzima wako 24. Asubuhi tumeweza kupata watu saba tu. Kwa hiyo mchana kwa sababu inatakiwa saa 12.30 tuanze kuwapa nafasi watoa hoja waanze kujibu. Kwa hiyo nitawenza tu kuwa na watu wafuatao:- Mheshimiwa Dr. Mahenge, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Anastazia Wambura na labda Mheshimiwa Omar Kwaangw'. Ndiyo hawa tu wanaweza kupata nafasi jioni.

Baada ya kusema hayo naomba tutakiane mchana mwema. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni.

(*Saa 07.00 Mchana Bunge lilisitishwa
hadi saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11 :00 Jioni, Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana, nilishataja ambao watachangia. Lakini kabla sijawataja ningependa kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hayupo Dodoma. Kwa hiyo, badala yake anayekaimu shughuli za Serikali ni Profesa Mark Mwandosya. Ahsante sana nina-hope Miswada haitarudishwa, hakuna hata Muswada wa kurudishwa. (*Makofi/Kicheko*).

Sasa nilikuwa nimewaita Waheshimiwa Dokta Mahenge, sijamwona, Mheshimiwa Mwandoro, sijamwona, Mheshimiwa Halima Mdee, sijamwona, Mheshimiwa Omar Kumchaya, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw', nimemwona. Haya ahsante, tuenze na hao.

MHE: SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mwongozo huu wa uandaaji wa bajeti yetu inayokuja. Pili, kwa kuwa nasimama kwa mara ya kwanza katika mkutano huu, basi na mimi pia kwa unyenyekevu mkubwa napenda nitoe salamu zangu za rambirambi kwa kifo cha Mzee wetu, Mzee Rashid Kawawa, kwa familia na Watanzania wote kwa ujumla. Amefanya mambo mengi, ametuachia uhuru, ametuachia upendo, ametuachia amani, umoja na mshikamano. Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumeingia mwaka mpya, ningependa pia kutoa salamu za heri ya mwaka mpya kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Lulindi na kwa Watanzania wote kwa jumla. Mwenyezi Mungu atujalie, atuongezee heri na fanaka ili tujenge mazingira mazuri ya kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa nichangie katika mwongozo huu. Siku moja mtu mmoja alikuwa anasafiri ndani ya ndege. Bahati nzuri alikaa na mzungu mmoja ambaye anaifahamu vizuri sana Tanzania. Yule mzungu alipomwona mwafrika amekaa pembeni yake akamuuliza kwa Kiingereza, nitanukuu: “*Where are you coming from?*” akamjibu, “*I am coming from United Republic of Tanzania.*” Akamjibu tena katika Kiingereza, “*Ooh! You are coming from the richest country in the world.*” Yule Mtanzania akafikiri ni utani, akakasirika. Akasema hapana, “*No! No! I know what I am talking about*”. Akasema tulia, najua ninachokizungumza. Akatoa *document*, anajua mwenyewe alizipata wapi. Akaelezea madini yaliyokuwepo katika nchi hii, ni mengi kuliko nchi nyingi katika Bara la Afrika pamoja na *South Africa*. Akaelezea maeneo ambayo yanaweza kulimwa yakaondoa njaa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Yule Mtanzania akatuliza moyo wake, akawa rafiki yake mpaka aliposhuka ndani ya ndege ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini nimeyasema haya? Nimeyasema haya kwa sababu katika nchi yetu ya Tanzania, tuna kila kitu cha lazima cha kuifanya nchi hii ipige hatua katika maendeleo na kuwa mfano katika bara la Afrika. Kwa hiyo, ni matarajio yangu basi katika mwongozo huu, bajeti hii inayokuja yatazingatiwa hayo. Mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, ni ukweli mtupu na mimi nitagusia baadhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni miundombinu. Kama kuna nchi ambayo imebarikiwa katika Bara la Afrika kwa upande wa bandari, ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuna bandari ya Tanga, *potential* bandari ya Bagamoyo, Dar-es-Salaam, Kilwa, Lindi na Mtwara, *the deepest* katika eneo letu hili mpaka *Cape Town*; hakuna bandari yenye kina kirefu kama bandari ya Mtwara. Tuna bandari Kigoma, *Mbamba-Bay*, Mwanza, Musoma, Zanzibar. Tuna migodi ya kutosha kabisa, hata kama tusingekuwa na madini, madini tunayo, yanatosha kabisa, lakini tumekuwa tukiimba wimbo huu kwa muda mrefu sana. Hapa ningependa kuishukuru na kuipongeza Serikali kwamba sasa kuna kitu kinaitwa *master plan* ya kutaka kukuza bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee nyingine; *intergrated master plan*. Kwamba bandari hizi tutakapoziendeleza msisahau miundombinu ya barabara na reli. Mtwara imekaa mahali pazuri sana kwa maana ya Tanzania yenyewe, upande wa Kaskazini wa Msumbiji ama Mozambique, Malawi, Zambia na hata upande wa Kusini wa Kongo *DRC*, tunaweza kabisa kuitisha mizigo yetu kutokea Mtwara na wakati huohuo tusisahau Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nakumbuka ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkullo pale Arusha, kwamba Wachina wameonesha dalili ya kutaka kujenga reli hii kutoka Mtwara–Liganga mpaka Mchuchuma. Kama nitakosea mtanisahihisha, lakini nina hakika hili linafahamika. Tunaijenga reli hii kwa sababu tuna chuma, tuna makaa ya mawe ambayo yanatakiwa sana katika Bara la Afrika na duniani kwa ujumla hasa wenzetu wa Jamhuri ya watu wa China. Naomba sana bajeti hii itilie mkazo hilo. Ukija Dar-es-Salaam, bandari. Naomba iende sambamba na uibuaji wa reli yetu ya kat, iende mpaka Kigoma. Ikaendelee kufanya kazi ya Rwanda, Burundi, *DRC*. Nasema jamani uwezo tunao, tatizo letu ni moja tu la kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwakumbusheni ndugu zangu. Mwaka 1978 tulipoona kwamba mambo ni magumu katika barabara ya Kusini, tuliweka mkakati wa kuchangiana. Pale Lumumba tulijaa tele, tukaanza kuchangiana watu wote walikubali, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, Edward Moringe Sokoine, akasema hapana Serikali itajenga. Mimi mwenyewe nilikuwa katika msafara wa kwenda kuweka jiwe la msingi pale Nangurukuru, kwa hamasa tu ya wananchi wa Kusini. Leo hii reli ya kat tunahangaika usiku kucha, *RITES* ondoka *RITES* baki, leo hii tukiwaambia Watanzania tena wote kwa ujumla wao, wanaojua nini maana ya maendeleo; watakuwa tayari kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba bajeti hii izingatie hilo. Bandari ya Tanga, ile reli iwemo kwenye bajeti. Itoke Tanga, Musoma, mpaka Uganda kukatisha maziwa. Tumelizungumza sana hili, naomba bajeti hii ianze kushughulikia bandari ya Tanga na reli hiyo. Yamezungumzwa mengi sana na ndugu yangu pale Mheshimiwa Rished, mali iliyokuwepo hapo katikati tunaweza sana kufaidika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndio uti wa mgongo. Ndio utajiri wa watu wengi katika Tanzania. Naomba sana tuwe makini katika kilimo, sasa hivi tuna kilimo kwanza, tusambaze mbegu kwa haraka na kwa uhakika. Tuendeleze vituo vyetu vya

utafiti hasa Naliendele ili tupambane na mabadiliko ya hali ya hewa. Usambazaji wa *power tillers* uende mpaka vijijini, kule Mkaliwata, Namyeme hadi Manyoli, ufile kule usikae Wilayani tu, yasitazamwe tu kama mapambo. Tusicheze na kilimo hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuzungumzia viwanda. Hakuna nchi ambayo imeweza kuendelea bila kuwa na viwanda. *Import and export*, viwanda vinachukua sehemu kubwa sana. Naomba bajeti hii inayokuja eneo la viwanda itiliwe mkazo na naweza kusema viwanda mama, vitengenezwe viwanda vingine, malighafi ipo, Mchuchuma ipo, Liganga ipo na maeneo mengine yapo. Leo tunakaribia miaka 50 bado tunapeleka korosho ghafi nje! Tupunguze kwa kasi sana. Leo tunakaribia miaka 50 bado tunauza pamba kwa wingi nje! Hatuna viwanda vya nguo, ni hatari sana hiyo; dunia itatuacha. Tufike mahali tuanze kuyapunguza mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu, isiwe kila siku tukija Bungeni hapa tunazungumza mambo hayo hayo tu. Tujisikie aibu, sisi ni binadamu kama binadamu wengine na hasa katika nchi kama ya Tanzania ambayo ina malighafi nyingi. Sasa hivi tumesema mengi tu, uzalendo tunao, nia tunayo, sababu tunazo na nguvu tunazo. Naomba sana hayo ndio maeneo ambayo yatajenga msingi mzuri wa maendeleo. Tusipoyafanya hayo tusije tukafika mahali tukasema maendeleo ni ndoto katika nchi yetu hii ya Jamhuri ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofî*).

NAIBU SPIKA: Asante sana. Nakumbuka wakati tunachangia barabara ya kule zilichangwa shilingi 97,000/= kujengea barabara ya Kusini. Ndio Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema, jamani 97,000/= zinajenga barabara kweli? Kwa hiyo, ni kazi.

Nilimwita Mheshimiwa Omar Kwaangw', wengine walikuwa hawajafika, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, halafu Mheshimiwa Mwandoro.

MHE. OMAR S. KWAANG'W: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu mwongozo wa bajeti 2010 mpaka 2012 mpaka 2013. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta mwongozo huu ambao kwa kweli tunaona unajaribu kuainisha mambo ambayo Serikali inaona kwamba ni vizuri ianze nayo katika mipango inayokuja. Lakini vilevile nitume nafasi hii kwa kweli kuipongeza Kamati ya Fedha na Uchumi kwa pendekezo lake kubwa sana ambalo nimeona ni zuri la kuwa na Kamati ya Bunge ambayo itakuwa inahusika na bajeti, hili ni jambo zuri sana na nadhani litatusaidia sana katika kuona kwamba mwelekeo wetu ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye mwongozo huu Mheshimiwa Waziri ametwambia kwamba dira inatuelekeza kwenye mambo kama matano. Moja amesema ni maisha bora na mazuri; pili amesema ni uchumi imara ambao unahimili ushindani; lakini vilevile akasema jamii iliyoelimika na ambayo itaendelea kujifunza zaidi. Na nne, kwamba katika mwongozo huu kwenye dira inatuelekeza tuendelee kulinda amani, utulivu na umoja wetu na mwisho utawala bora. Sasa katika mapitio ya mpango huu, ya

mwenendo huu wa uchumi Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba pato linakua kwa 5%, pamoja na kwamba 7.4% ndio ilikuwa mwaka 2008, limeshuka kidogo lakini anasema litaendelea kukua na kuongezeka kufikia 6.1%. Sasa pato linakua, lakini umaskini unazidi kwa wananchi wetu! Sasa hapa ndio jambo la kujifunza, kwamba tunasema pato linakua lakini umaskini unazidi kujikita, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge, sasa mimi nigosie jambo moja tu ambalo naona kama halijasemwa, nalo ni idadi ya watu. Nchi hii ni kubwa, eneo ni kubwa *square kilometres* zaidi ya 945,000 idadi ya watu sasa tunakaribia 40,000,000. Hatulinganishi ongezeko la idadi ya watu na pato la nchi, kwa hiyo kuna tatizo hapo kama hatuzungumzi habari ya kuongezeka kwa idadi ya watu, nadhani tutaendelea kupata tatizo kubwa. Sikuona kama jambo hili limesisitizwa sana, lakini naona nitumie nafasi hii kuzungumza jambo hilo kidogo, kwamba tusipoweka malengo, kila Mkoa, kila Wilaya. Je, kwanza tuna ongezeko kiasi gani? Katika ongezeko hilo tunaweka juhudhi gani kuhakikisha kwamba tunaongeza pato la Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa maana yangu ni kwamba, watu wetu wengi hawafanyi ndani ya nchi hii. Tunayo nguvu kazi kubwa ambayo inazurura tu, vijana wako tu mijini, wanatembea na biashara ndogondogo ambazo hazina tija, hatuoni hili, hapa ndio mahali pa kuangalia zaidi. Nenda kwenye miji utashangaa! Vijana wengi kabisa, lakini wote tunawaona wanauzu vitu vidogo vidogo, lakini nchi hii ina ardhi kubwa, hatuwapaleki huko! Sasa sijui kwenye mpango huu wa kilimo kama tunaweza kuwaondoa vijana wote mijini wakaenda kwenye kilimo kwanza, labda hapo tunaweza tukajaribu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tatizo kubwa ni kwamba mikono inayofanya kazi ni michache lakini midomo inayokula ni mingi mno. Sasa hili ni tatizo kubwa sana ndani ya nchi. Kwa hiyo ni vizuri sana tuangalie eneo hili la watu kufanya kazi. Nadhani ukiangalia saa 4:00 hivi ukaiangalia Tanzania, ukaenda ukaangalia kwenye miji yote na katika maeneo mengi utaona jinsi watu wasivyofanya kazi. Wakati huo huo tunasema kwamba hatuna chakula, hatujitoshelezi, tuko maskini, lakini kumbe idadi ya watu hatuiangalii vizuri na kazi pia hatuiangalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri, eneo hili liangaliwe kwa mapana na mrefu. Kwamba utakuta ukienda kwa mfano vijijini, watakwambia watu wenyewe uwezo wa kufanya kazi katika kijiji chenye watu 3,000 labda watakwambia ni 500 au hata 1,000. Sasa inakuwa ni tatizo kubwa kabisa, lakini utakuta watu wengi hawana kazi. Sasa eneo hili ndio lifanyiwe kazi. (*Makofit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, sizungumzii ajira, hii ya ajira ambayo tuliahidi 1,000,000 nadhani tulishavuka, lakini jambo kubwa ni kwamba sehemu kubwa ya vijana na watu wenyewe uwezo wa kufanya kazi hatufanyi kazi ipasavyo. Lakini hata sio kwa wananchi tu, hata Serikalini sasa hivi kuna tatizo. Kazi mara nyingi zinaanza kwenye saa 04:00. Siku hizi wameanzisha mtindo, asubuhi kwanza wanafanya mkutano. Kwa hiyo mtu mwenye shida haanzi kusema shida yake mapema pale saa 1:30, anaambiwa asubiri mpaka karibu saa 3:00, wanamaliza

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana hata katika ofisi nyingine wameandika kabisa, kumwona Mkurugenzi, kumwona fulani, ni kuanzia saa 3:00 au saa ngapi. Sasa hivi kweli tunaweza kweli tukafanya kazi kwa namna hii? Kwa hiyo nayo tuangalie vilevile kwenye Serikali jinsi tunavyofanya kazi na jinsi tunavyowahudumia wananchi. Hili ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona eneo hilo niliwekee mkazo kwa sababu naona ndilo eneo ambalo halijasemewa sana. Jambo la pili ni suala la misaada ambayo ameeleza Mheshimiwa Waziri, misaada na mikopo. Tayari ameshatueleza ziko nchi ambazo sasa zimepunguza misaada yao, zipo nchi wamekataa kutoa kabisa kwa sasa na ziko nchi wamepunguza. Sasa kama misaada hii imepungua na sisi hatuna mipango ambayo ni endelevu hasa kwenye sekta ya afya, ni tatizo kubwa sana. Kwenye sekta ya afya eneo la magonjwa ya *TB, malaria, HIV & AIDS*, ndio maeneo yanayochangiwa sana na *Global Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwelekeo sasa unaonesha kwamba Marekani ambao ndio wachangiaji wakubwa katika eneo hilo katika miaka mitano ijayo wanapunguza misaada yao, haitaongezeka. *Global Fund* vilevile misaada yao haitaongezeka wala haitabiriki. Sasa kama 96% ya fedha zote zinazohudumia katika eneo hili la sekta hasa upande huu wa magonjwa kama *HIV & AIDS* inategemea *Global Fund*, kama hatutaweka mipango endelevu, hatutaweka kwenye bajeti yetu, maana yake wananchi wetu watapata matatizo. Kutakuwa na vifo vingi sana. Kwa hiyo, ni muhimu tukawa na mipango ambayo kwa kweli ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya afya sasa hivi, wakati tulipokuwa tunazungumza hapa ule Muswada wa Uuguzi na Ukunga, tulizungumza kwamba inakabiliwa na 62% ya upungufu wa wataalam. Sasa leo katika mwongozo huu katika mapendekezo ya vipaumbele, huduma za jamii imewekwa ya tatu! Kama ni 38% tu ambayo ndio ipo na 62% haipo ya wataalam kwenye sekta ya afya, hawa wananchi afya wataipatia wapi? Tayari umekwishaondoa kutoka kwenye sehemu ile ya *priority* umeshashusha chini, hii maana yake ni nini? Tutakuwa na tatizo kubwa sana na huku tumeshajiwekea utaratibu kwamba kila Kijiji kuwe na Zahanati, kila Kata kuwe na Kituo cha Afya, tuimarishe Hospitali za Wilaya, Mikoa na za Rufaa. Sasa tunafanyaje eneo hili? Ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo langu kubwa sasa katika maeneo haya ya vipaumbele na kwa kweli nilikuwa sina sababu ya kusema lakini sasa naomba nizungumze kwa sababu hiyo, kwamba huduma za jamii hasa sekta ya elimu ambayo ilikuwa ya kwanza kwa miaka hii miwili iliyopita, sasa tumeiteremsha ni ya tatu. Sasa ujumbe ni nini kwa wananchi? Hivi ujumbe ni nini wa kuondoa elimu kutoka kipaumbele cha kwanza kwenda mpaka cha tatu? Hii ndio sekta ambayo inamgusa kila Mtanzania. Ni nyumba gani ambayo mtoto haendi shule hapa? Hebu tukubaliane hapa, kila nyumba mtoto anatakiwa kwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni tatizo na hii mantiki yake ni kwamba ile mipango mikubwa tulioanzisha chini ya miradi ile ya *MMEM* ya kuimarisha elimu ya msingi, *MMESS* elimu ya sekondari, maana yake ni ile mipango sasa, ni lazima mingine iachwe kwa sababu sasa umeshusha elimu imekuwa kipaumbele cha tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya upanuzi mkubwa sana, *rapid expansion* katika *primary education*, *secondary education* na hata *higher level*. Kwenye *higher education* nako tumefanya *expansion* ya kutosha. Lakini sekta hii inahitaji sana wataalam, kila siku tunazungumza hapa shule za Kata zina walimu wawili, mmoja, hatuna maabara, hatuna vitabu, hatuna nini. Sasa ukishafanya kuwa ya tatu maana yake ni kwamba sasa ni lazima vitu hivi vingine viachwe, sasa tutakwenda vipi na hii sekta! Vyuo vikuu kama kile cha Dar-es-Salaam kimechoka, majengo yamechoka yanahitaji ukarabati wa zaidi ya *billions of money*. Tutakwenda kufanya nini huko sasa? Vyuo vya ualimu, nendeni mkaviangalie, vimechoka kabisa, vinahitaji kujengwa upya wala hata sio ukarabati. Tunahitaji kuwa na walimu wengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunashukuru kwamba angalau mashirika yetu haya ya *NSSF*, ya Pensheni na nini yamesaidia sana kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma, sasa sijui kama na Serikali nayo itapunguza huko, maana sasa ukienda kuangalia pale kazi iliyofanywa na haya mashirika, kwa kweli ni kazi nzuri ya ajabu na ya kupongezwa sana

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mashirika mengine haya ya simu, sijui yanachangia wapi? Mnawafanyaje? Maana wao wanafadhili vitu ambavyo, aah! Kwenye jamii ni tabu. Sina haja ya kusema sana, lakini tunaona jinsi ambavyo kuna zawadi nyingi zinazotangazwa, jamani fedha hizi basi tuzielekeze zikasaidie kuimarisha elimu au afya. Tuwaambie haya mashirika, lakini kufadhili mambo mengine ambayo kwenye jamii kwa sasa sio lazima sana ndio hapo tunapopotea sasa kwenye vipaumbele vyetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka na eneo hili, kwa kweli kwangu mimi ningesema kipaumbele cha elimu kiendelee tena kwa miaka 15 au 20 ijayo, tubaki hapo. (*Makofi*)

Nikisema hivi maana yake sipingi kwamba tusitilie mkazo kilimo, twende na kilimo lakini sekta itakayokiokoa kilimo ni Sekta ya Elimu, maana nina hakika kilimo cha kijana aliyemaliza kidato cha nne, hakiwezi kufanana na kilimo cha kijana ambaye hakwenda shule. Lazima tukubaliane ni tofauti hata iweje; ukitaka kujua hili nenda ukaangalie kwenye magereza ni watu gani wengi wako kule, utakuta wengi ni wale amba wamepata elimu ya chini. Hii ni kwa sababu hawazifahamu vizuri sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninataka kusema kwamba; ni meseji gani tunapeleka tunapofanya elimu kuwa kipaumbele cha tatu badala ya kuwa cha kwanza? Naomba mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, japokuwa leo koo langu lina tatizo kidogo, kwa hiyo, ukiona mambo hayaendi vizuri, tunaweza tukavunja japo kanuni tupate maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, ningependa kutoa salamu za pole kwa Familia ya Marehemu Mzee Kawawa na vilevile Familia ya Maleko, kwa kumpoteza mtoto wao kipenzi na mke, Bibi Habiba Kawawa. Kimsingi, msiba huu umenigusa kwa sababu Habiba nilisoma naye Chuo Kikuu, alikuwa amenitangulia darasa lakini ndiye aliyenipokea nikiwa mwaka wa kwanza na tulikaa naye bweni moja. Kwa hiyo, ndiye aliyenikaribisha mimi katika maisha ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na msiba huu kwa kweli umenigusa, naamini Mwenyezi Mungu akisaidia, tutashiriki kwenye mazishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia suala zima la hali ya uchumi inavyokwenda. Mimi siyo mchumi ni mwanasheria, lakini nimepitia vitabu vyao vya kiuchumi, ambavyo vinatuonesha kwa kadiri miaka inavyokwenda ndivyo kasi ya uchumi kukua inavyopungua. Ninatumia Kitabu cha Serikali hapa, kwa hiyo, kama kuna chochote cha uwongo, itakuwa wao ndiyo wametupotosha. Kwa kutumia Kitabu hiki, tunaona kwamba, katika mwaka 1993 mpaka 1996, uchumi ulikuwa unakua kwa kasi sana, tulivyokuja mwaka 1997 mpaka 2002 kasi ilianza kupungua taratibu. Tulivyofika 2004 mpaka 2007, kasi ikapungua zaidi kuliko kipindi kilichopita na sasa hivi tuko 2008/2009, kwa hesabu za kawaida kwa sababu Ripoti ya Serikali bado haijatoka, inaonekana hali inaweza ikawa mbovu kwa sababu ya mtikisiko wa uchumi na kwa sababu sisi ni wategemezi, kwa hiyo *expectation* ni kwamba, japokuwa tunapokuwa tunachangia tunaonesha kwamba kuna mafanikio makubwa sana, lakini kumbe takwimu zinaonesha kwamba, kasi ya uchumi kukua inapungua sana kwa kadiri ambavyo miaka inakwenda.

Kitu hicho pia kimethibitishwa zaidi na Ripoti ya Wataalam wetu hawa wa RIPOA, ambao walikuwa wanajiliza kitu ambacho na sisi huwa tunajiliza siku zote, tunaambiwa uchumi unakua. Hii hapa Ripoti yenu ya mwisho, watu wanasesma takwimu zinatuonesha uchumi unakua lakini hatuona kama kuna *impact* yoyote kwa Watanzania wa kawaida. Naomba kunukuu *findings* zao kama utaniruhusu: “*The finding from the simultaneously exercise indicate that the incidence of poverty has slightly but smoothly decline since 2001, at the same time, however, the share of government consumption in GDP has rapidly increase.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokiona hapa ni kwamba, japokuwa tunaoneshwa kitakwimu fedha zimeongezeka kidogo, lakini wakati huo huo kuna matumizi makubwa mno kwa Serikali, hali ambayo inafanya sasa kile kipato kidogo ambacho kinapatikana badala ya kwenda kwa mwananchi wa kawaida kupunguza umaskini, tunaishia kugawana wenyewe Serikalini. Sasa hili ni tatizo la msingi na tukiwa tunapanga mpango ni muhimu tuangalie ni kwa namna gani Serikali inapunguza ku-*consume GDP* na basi ile sehemu ambayo ilikuwa ina-*consume* kuzidi kiasi, waipeleke kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vipengele mbalimbali watu wamevizungumzia sana na tumekuwa tukizungumza sana; juzi Waziri wakati anatupa *briefing*, alitutajia vipaumbele ambavyo ukivikokotoa viko kama kumi na moja. Sasa kwa taifa maskini kama hili, mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine, tukiwa na tunavipaumbele kumi na moja maana yake ni kwamba, tutakitekeleza kipi kwa ufanisi? Kwa hiyo, lazima ifike mahali tuamue kama kipaumbele chetu ni elimu, basi tuwekeze kwenye kilimo na elimu.

Marekani pamoja na utajiri wake wote, juzi nilikuwa nasoma *summary* ya bajeti yao, wameweka vipaumbele katika maeneo mawili tu; eneo la kwanza, wameamua watengeneze ajira kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha. Eneo la pili, wameamua waangalie kwenye afya. Pamoja na utajiri wao wameona kwamba, lazima tuwekeze kwenye maeneo mawili ambayo ni ya msingi, ambayo kufanikishwa kwake kutawenza kusaidia maeneo mengine. Ninakubaliana na Mheshimiwa Kwaang'w, elimu ina umuhimu lakini kilimo hatuwezi kukiacha kwa kuwa kinaajiri asilimia 75 ya Watanzania. Kwa hiyo, tunaweza tukasema *priority* zetu ni mbili; elimu na kilimo; hivi vingine sasa vitafuatia huku chini taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kufanikisha, lazima tuangalie Malengo ya Milenia, Malengo ya MKUKUTA na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ndiyo chama kinachotawala hivi sasa. (*Makofî*)

Ukiangalia malengo kama yamefanikiwa, nikichukulia mfano wa Malengo ya MKUKUTA; ukiangalia MKUKUTA, *target* yake kwa kilimo kwa mwaka 2010 ambayo kwa hivi sasa ilikuwa kilimo kiwe kinakua kwa asilimia kumi, lakini kwa mujibu wa Taarifa za MKUKUTA ambazo zipo ndani ya Ripoti ya Serikali, kilimo chetu kimekua kwa asilimia 4.7 tu, hakijafikia hata nusu ya ile *target*. Tatizo ni nini? Mwaka jana tumepitisha bajeti tukaambiya Kilimo Kwanza, lakini kama kawaida yetu kwenye Bajeti ya Maendeleo ambayo katika mazingira ya kawaida unategemea kwamba, kilimo maana yake Bajeti ya Maendeleo, ndiyo inaenda kusaidia miundombinu ya kilimo, imetengewa milioni 12 kwenye Wizara ya Kilimo. Ukiangalia hizi Wizara Shirikishi ambazo zina *linkages* na Wizara ya Kilimo katika suala zima la maendeleo ya kilimo, kwa ujumla wake bilioni 36. Katika vitabu hivyo hivyo, ukiangalia fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kusafiri, yaani kwa ajili ya safari za Watumishi wa Serikali ni zaidi ya bilioni 300 katika vipindi vya miaka miwili. (*Makofî*)

Sasa tunajiuliza; tunasema ndani ya Kilimo Kwanza tunatenga bilioni 130; katika hizoz bilioni 130, asilimia 95 tunategemea wafadhili, wakati huo huo tumetenga bilioni 300 ambazo hizi fedha za maendeleo zinaingia mara mbili kwa ajili ya watu kusafiri ndani na nje ya nchi; we are not serious kwa sababu kama sisi ni maskini, tunaweza tukaamua kujibana hata hizoz safari tukaziacha tukaamua *ku-focus* ndani. Tumeshasafiri sana, kama hatujajifunza sijui kama tutajifunza; mwaka jana tumezungumzia hapa bajeti za viburudisho na *hospitality* ya zaidi ya bilioni 33. Matokeo yake ni kwamba, Reli ya Kati ambayo tunaona sasa hivi ina matatizo kwenye Bajeti ya Maendeleo, imetengewa

bilioni 3, ninyi mnajipa *hospitality* na *entertainment* wakati Reli ya Kati imetengewa bilioni tatu za maendeleo; huo sijui niite ni uupuzi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe na ngozi ngumu, ni kukosa akili kabisa, lazima tufike sehemu hizi ngonjera, ngonjera hapa ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa hebu sahihisha maneno yako, katika vitabu vyetu vya kanuni hakuna kukosa akili, tafuta neno lingine.

MHE. HALIMA J. MDEE: Haya ili kukoa muda ni kukosa busara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo ndiyo hilo, lazima tuwe makini katika matumizi yetu na mipangilio yetu ya fedha.

Vifo vya akinamama wanaojifungua; ninasikitika sana nimempoteza rafiki yangu kutokana na tatizo hilo. Taarifa zinaonesha kwamba, hali inazidi kuwa mbaya; kwa hiyo, tunatarajia Wizara ya Afya itakapokuja, katika mipango yao nao wataangalia ni kwa namna gani hizi fedha zinazotengwa mabilioni ya shilingi kwa ajili ya kuzuia vifo vya akinamama ambapo katika kila saa 24 anakufa mama mmoja, zinatumika ipasavyo kunguza vifo hivyo. Lazima tupangilie ili vifo vya watoto wadogo walio chini ya mwezi mmoja, ambapo sasa hivi ndiyo vinaongoza kati ya vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano vipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la *Gender Budgeting*, naona muda hautoshi; takwimu zinaonesha kwamba, hali ya Mwanamke wa Kitanzania kuanzia mwaka 2006 hadi 2009 na nafasi ya Tanzania kidunia katika masuala ya *gender gap* au tofauti ya kipato kati ya mwanamke na mwanaume, Tanzania imeshuka kutoka nafasi ya 26 mwaka 2006 mpaka nafasi ya 73 mwaka 2007 kati ya nchi 134. Hii inaonesha kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne katika kipindi chake cha miaka mitano, imeshindwa kabisa kumwondolea mwanamke matatizo yake. Sasa tuko kwenye Kilimo Kwanza na sote tunafahamu kwamba, asilimia 87 ya wanawake katika ile asilimia 51 ambayo ndiyo jumla ya *population* ya wanawake nchini, wanashiriki kwenye kilimo. Kwa hiyo, kwa namna yoyote hatuwezi kumuweka huyu mwanamke katika Kilimo Kwanza, lazima tuangalie namna gani Kilimo Kwanza kinam-*target* yule mwanamke maskini, mkulima wa kijijini, hilo hatuwezi kulikwepa. Tulikuwa tunazungumza Kilimo Kwanza kumbe tuna-*target* matajiri wenye matrekta, hiyo haina maana na wala haitakuwa na *impact* au *effect* yoyote katika kumwondolea umaskini Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua wewe ni *gender archivist*, nilikuwa napendelea Wizara zote zitakapokuja kutuelezea mipango ya bajeti yao, watueleze katika miaka mitano iliyopita au *at least* katika mwaka mmoja uliopita ni kwa kiasi gani bajeti zao zimeweza ku-*impact* maendeleo ya mwanamke katika nchi hii. Ni aibu, mwaka 2006 tulikuwa nafasi ya 26 kati ya nchi 134, leo mwaka 2010, miaka mine, tumeshuka hadi nafasi ya 73 wakati tunaimba uchumi unaenda; huu siyo ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya kuingiza masuala ya jinsia kwenye bajeti ni muhimu, ukizingatia nchi yetu ilikuwa ya kwanza kuridhia dhamira ya kuingiza masuala ya jinsia kwenye bajeti. Tuache maneno tuje kwenye vitendo, mwanamke ndiyo mzalishaji mkubwa kwenye suala zima la kilimo akombolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna programu kubwa imekuja ya *Clean Development Mechanism*, kutokana na dunia kukumbwa na machafuko ya hali ya hewa. Nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Kifua kimekuhurumia wala hukunywa maji.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii muhimu. Ningependa kuchukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu wake, pamoja na Wataalam wote Wizarani, kwa hotuba nzuri waliyondaa kwa mwongozo mzuri waliouandaa na kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Ni jambo la faraja kubwa sana kwamba, pamoja na mtikisiko mkubwa wa kiuchumi duniani, pamoja na hali ngumu ya ukame iliyotokea nchini kwetu, uchumi wetu haukuyumba kwa kiasi kikubwa kama ambavyo ilikuwa. Hii ni dhahiri inatokana na kazi nzuri waliyofanya; nawapongeza sana, naomba waendelee na jitihanda hizo. (*Makofi*)

Mwongozo huu unatupelekea katika mipango yetu na bajeti kwa miaka miwili, mitatu inayokuja. Katika kuzungumzia suala hili, Kamati ya Fedha na Mipango na Uchumi, imeona hakuna *consistency* wala hakuna utaratibu ambao umefuatwa vizuri kwa namna moja au nyingine.

Katiba yetu haikufuatwa, kwa sababu ilitakiwa Kamati hii ya Bunge itazame mapendekezo ya bajeti halisi, lakini tunatazama miongozo. Sasa pendekoz lao kwamba tuwe na Kamati ya Bajeti, mimi ninalafiki moja kwa moja, napendekeza kwamba tuwe na Tume ya Mipango iliyo imara. Nalafiki suala hili kwa sababu unapokuwa na Wizara ya Fedha inayoangalia masuala ya mipango, mara nyingi linamezwu linatazamwa zaidi suala la *fiscal policy* badala ya *fiscal planning*, ambayo intakiwa tutazame mwenendo wa sekta mbalimbali na tufanye mambo yetu namna gani. Kwa hiyo, naamini kwamba, tukiwa na Tume ya Mipango yenye nguvu, shughuli hii itatazamwa kwa ubora zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Sasa napenda kutofautiana na baadhi ya wasemaji waliotangulia kuhusu suala la vipaumbele. Mimi napenda kuafiki vipaumbele vilivyotolewa na Wizara katika mwongozo huu. Kwa sababu mipango yetu au misingi ya mipango yetu tumesema sasa hivi ni Dira ya Maendeleo 2025, *Millennium Development Goals*, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya 2005/2010. Kwa ufupi, mipango yote hii inalenga kupambana na maadui wetu wa asili; ujinga, umaskini na maradhi. Yameelezwa kwa namna mbalimbali katika vipengele mbalimbali, lakini misingi hii *theme* yake ni kupambana na maadui hawa watatu. Sasa tunapozungumzia suala la *persistence* na *consistency*, tunazungumzia juu ya masuala haya matatu ya ujinga, umaskini na maradhi, ambayo yamekuwa *addressed* kwa namna mbalimbali.

Suala la vipaumbele, vimewekwa kwa kisekta kuweza kupambana na maadui wetu watatu hawa. Mimi naamini tulichukua hatua sahihi katika miaka mitatu, minne, iliyopita kuweka elimu kuwa kipaumbele cha kwanza, kwa sababu elimu ndiyo ufunguo wa maendeleo ili kuendelea unataka rasilimali watu waliopata elimu, walioelimika na kubobe katika taaluma hizi na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na maendeleo makubwa katika sekta mbalimbali. Hilo nafikiri tumelifanya kwa mafanikio mazuri sana chini ya MMEM, MMES na pia chini ya Programu za Kuendeleza Elimu ya Juu. (*Makofi*)

Sasa katika kutazama jambo hili katika kutathmini, tutakumbuka kwamba, hili suala la Kilimo Kwanza kuwa kipaumbele cha kwanza tujikumbushe lilitokea wapi. Suala hili mara ya kwanza lilizungumzwa katika semina ambayo ilihuisha baadhi ya Wabunge na Wataalam mbalimbali wa sekta mbalimbali. Baada ya kutazama hali ya uchumi ilivytetereka na kusema kwamba, madhali misingi yetu maendeleo ni kujitegemea na madhali Ilani yetu ya Uchaguzi ina shabaha kuu moja ambayo ina malengo mawili, shabaha hiyo ni maisha bora kwa kila Mtanzania. Halafu malengo makuu chini ya Iani, moja ni kujenga uchumi wa kisasa unaoendelea kwa kasi kubwa, endelevu na uchumi usiokuwa tegemezi. Pili ni kuwawezesha wananchi kumiliki na kuendesha njia kuu za uchumi kwa faida yao na kwa faida ya Taifa. Sasa katika kutazama hivi vipaumbele, ilipofikia hali ya uchumi kutetereka, ilionekana kwamba, uwezo wetu wa kuendesha uchumi wetu unategemea sana hatua madhubuti za kuendeleza uchumi wetu.

Pamoja na kwamba, elimu inachangia sana katika kuendeleza uchumi na kuleta watu wenyе maarifa na teknolojia nzuri, lakini msingi mkubwa wa uchumi wetu katika nchi yetu ni kilimo. Zaidi ya asilimia wananchi ya 80 wanategemea kilimo kwa maisha yao. Kwa hiyo, ukitaka kuendeleza uchumi ambaо kama ilivyotokea athari hii, tusingeweza kuathirika kwa njaa na kutegemea msaada kutoka nje. Msingi mkubwa wa kujiedeleza na uchumi wetu huu, ndiyo utawezesha kutupatia mapato ya kuendeleza sekta nyingine za huduma za jamii na nyingine zote kama zilivyoolezwa.

Sasa basi kwa hilo, mwaka jana baada ya hali ya uchumi kutetereka ilitishwa semina Kunduchi Beach, yakaelezwa masuala haya, ikaelezwa dhana hii ya Kilimo Kwanza. Wengi tulikuwepo pale, tukaelezwa sababu hizo. Mheshimiwa Rais alikuja Kilimani akatueleza hali halisi ilivyo na tukaona kwamba ili tuweze kujikombua na kuendelea vizuri katika hali ya kujitegemea, hatuna budi kuchukua hatua thabiti za kuendeleza kilimo. Wengi wetu tulisema kwamba, umuhimu huo kweli upo, lakini bahati mbaya kilimo hakikupewa bajeti inayostahili, hakikupewa kipaumbele kinachostahili, tukasema kwamba kipewe kipaumbele hicho.

Ndani ya Bunge hili Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Fedha na Gavana, walikuja na kuzungumza nasi juu ya masuala ya haya na sisi tulikubaliana juu ya suala hili. Leo ni kitu cha kustaajabisha kwamba, hili suala limetoka wapi. Hili suala tumelijadili si muda mrefu tumekubaliana na nafikiri Serikali yetu sikivu imelisikia hilo na kufanya mipango kutokana misingi hiyo. Kilimo Kwanza tukikifanya

kwa misingi iliyoelekezwa, kwa hali nzuri na kwa uangalifu, ndicho kitatuwezesha kuwa na misingi imara ya uchumi wetu ambao utatuwezesha kuendelea.

Sasa vipaumbele vimeelezwa, Kilimo Kwanza na hatua zake thabiti zimeelezwa katika mipango mbalimbali. Kipaumbele cha pili kimeelezwa kuwa ni miundombinu, tutazame *logic* na mantiki ya masuala haya ili kuendeleza kilimo muhimu sana kuwa na miundombinu thabiti, ambayo itawezesha kilimo kukua kama inavyotakiwa. Tumezungumzia miundombinu ya barabara, bandari na viwanja vya ndege. Miundombinu mingine kiuchumi ni pamoja na malambo na mambo mengine chungu nzima, ambayo yanahitajika kuendeleza kilimo. Kwa msingi huo, mimi naona kipaumbele cha pili kuwa miundombinu ni sahihi ili kuweza kusaidia uchumi uwe unakua kwa kasi endelevu, usiokuwa tegemezi. Sasa kwa dhana yetu inayotaka maisha bora kwa kila Mtanzania, huduma za jamii zinafuata hapa. Hatukusema kwamba, maana yake zote ziko katika vipaumbele siyo kama zimeachwa, lakini huduma za jamii; imetajwa elimu, maji na afya na haya majanga yanamgusa kila mwananchi wetu.

Lazima tukubaliane kwamba, kazi ya kupanga ni ngumu sana. *Resources* zetu ni chache sana. Katika *level* yetu ya maendeleo, sisi tuko chini sana, sekta zote zina kiu zinahitaji maendeleo. Sasa katika kupanga ni lazima tuhakikishe kwamba, tunaipa kipaumbele ile sekta ambayo italeta msukumo mkubwa wa maendeleo au inaitwa *investment drive*. Katika masuala hayo, kilimo kinasaidiwa na miundombinu. Huduma za jamii zinasaidia kuwa na wananchi wenye elimu bora, wenye afya na wenye kupata maji safi na salama, ambayo yatawezesha kuchangia ujenzi wa kiuchumi kadiri inavyotakiwa. Sasa ni ukweli kwamba, kilimo kimebadilisha huduma za jamii kutokana na msingi huo ambao umeelezwa na ambao tumekuwa tukiuzungumzia wakati wote.

Pia kipaumbele cha nne nashukuru kwamba, Wizara hii au Serikali kwa ujumla, imeona umuhimu wa ardhi na kuweka ardhi kama kipaumbele cha nne. Vilevile imeona umuhimu wa viwanda na kuweka viwanda kama vipaumbele cha tano. Mimi nafikiri ardhi kama ninavyoolewa ni msingi mkubwa sana wa maendeleo. Bahati mbaya hapajakuwa na matumizi mazuri ya ardhi au kutokana na MKURABITA ambao unahusika sana haujaweza kufanya kazi kama ilivyostahili, kwa sababu tu ya upungufu wa bajeti na upungufu mwengine wa kiutendaji. Kwa hiyo, kipaumbele kilichotolewa ni sahihi ili tuweze kutumia ardhi yetu vizuri kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Sasa viwanda, kama baadhi yetu ambavyo wamezungumzia, kwanza ndiyo soko kuu la Kilimo Kwanza, mazao yale ambayo yatatoka kwenye kilimo mengi yatakwenda viwandani kutengenezwa na kupatiwa thamani zaidi na kuongeza thamani katika uchumi. Viwanda ndiyo vinavyozalisha pembejeo, malighafi za kilimo na shughuli nyingine za kilimo nyingi na huduma za jamii zinatokana na viwanda. Sasa kipaumbele hicho tulichopewa ni sahihi na kwa kuamini kwamba, itapewa *allocation* kubwa zaidi ili kuweza kuondoa upungufu ambao umekuwapo mpaka hivi sasa. Upungufu ambao sekta hii ya viwanda na biashara imekuwa ikitabiliwa nao ni mchache sana na Wizara yenye, pamoja na taasisi zake, imekuwa ikipata ugumu sana kuweza kufanya maendeleo yanayotakiwa kuendeleza viwanda. Kuna taasisi za utafiti, taasisi za

maendeleo na taasisi za ukuzaji biashara, ambazo ni muhimu sana katika shughuli hizi za kimaendeleo.

Sasa kutokana na kipaumbele chetu tulichopewa hiki, naamini itawezekana sasa hivi kwa taasisi hizi kuweza kufanya kazi zake vizuri zaidi ili tuweze kuwa na tija katika uzalishaji wa viwanda ili tuwe na ufanisi katika kazi zetu za viwanda ili tuweze kuwa na viwanda bora zaidi na mazao bora zaidi yanayoweza kuhimili ushindani. Tumesema kwamba, kuhimili ushindani, lakini huwezi kuhimili ushindani kama viwanda, masoko na biashara haviko katika hali nzuri.

Kwa hiyo, hii naamini itatuwezesha kutoka kwenye hali hiyo, lakini pengine kuna haja kubwa ya kutazama suala hili la viwanda kuokoa watu. Sote tunakumbuka, Mheshimiwa Mongella ametukumbusha hapa kwamba, zamani tulikuwa na msingi mzuri sana wa viwanda; tulikuwa na taasisi kama karibu 400, viwanda sijui zaidi ya 50 vya aina mbalimbali, tulivijengea misingi mizuri tukaendelea lakini hatimaye karibu vyote vimekufa; sasa hivi jitihada kubwa zinafanyika za kujenga upya na kufufua viwanda hivyo na shughuli mbalimbali.

Katika kufanya shughuli hizi, hatuna budi turudi nyuma tutazame, kwa nini viwanda hivi vilikufa? Kwa nini uwekezaji ambaou umekazaniwa humo ndani kwamba tuuendeleze unapungua? Kwa nini mauzo yetu nje yanapungua? Haya ni masuala muhimu ambayo yanahitaji kutazamwa. Sasa basi katika kuandaa mwongozo huu ni vizuri Sera zetu za Fedha zikaangalia masuala haya mbalimbali ya jinsi gani ya kuvilinda na kuviendeleza viwanda vyetu vya ndani. Baadhi ya masuala haya ni kwamba, Sera zetu za Kodi zinakazania zaidi kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofī*)

NAIBU SPIKA: Nilisema nitamwita Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, atafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia Wambura.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii na napenda nianze kwa kuungana na wale wanaosema tuwe na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kujikita zaidi kwenye suala la vipaumbele, lakini nikipata muda nitazungumzia na masuala mengine mwishoni. Ninataka nikokotoe vipaumbele kwa kuwa na mtazamo wa kimazingira, nitaliangalia kutoka upande wa mazingira, kwa sababu mazingira ni mtambuka, yanakaa pale juu na unaweza kuona sekta nyngine zote hapa chini.

Ninapenda kulizungumzia hili kutokana na kipengele kilichoko kwenye mwongozo katika kifungu cha 42, ukurasa wa 29, kuhusiana na hatua zinazochukuliwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwenye ukurasa wa 30 wameeleza mabadiliko makubwa ya tabianchi ambayo yameleta athari kubwa kwa maisha ya wananchi wetu kwenye miundombinu, kilimo na mambo mengi sana, tumeathirika na hakuna mtu anayebisha hilo. Namna ya kushughulikia matatizo haya kwenye vipengele vya (1), (2)

na (3) kwenye ukurasa ule wa 30 anazungumzia kutafuta fedha kwa ajili ya kukarabati, kununua mazao ya chakula kwa ajili ya kuwalisha wananchi, kuwaomba watu wengine kama Mashirika wachangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kutatua matatizo haya kwa kufanya hivi, haitoshi; juhudhi hizi siyo endelevu kwa sababu zitatokea mwaka kesho na mwaka keshokutwa, kazi yetu itakuwa ni kukarabati na kuendelea kutafuta hela kwa ajili ya kukarabati barabara, reli na kadhalika, hatutafika mbali. Mimi nilidhani *solution* ni kujua kwa nini mabadiliko ya tabianchi yanatokea? Kwa nini athari za mazingira zinatokea zinaleta uharibifu kwenye miundombinu; maji mitoni yanakwisha; mito inakauka kwa hiyo hata tukianzisha umwagiliaji, hakutakuwa na maji na hakutakuwa na tija kwenye umwagiliaji. Sasa ni lazima tufanye kitu ambacho kitatusaidia kuhakikisha kwamba, miradi hii iwe ya kilimo, iweze kuleta maji kwa wananchi, viwanda vinavyohitaji maji ambayo ni lazima yawepo, tuhakikishe kwamba kuna uendelevu wa namna fulani kuhakikisha kwamba, vitu hivi vinakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani vyanzo vikubwa vya mabadiliko ya tabianchi kama alivyozungumza Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', kimoja kikubwa ni ongezeko kubwa la watu, yaani *population growth*; yaani watu wanaongezeka sana lakini ardhi haiongezeki. Kila mara nimesema, hakuna anayetaka kuzungumzia suala hili na hata kwenye mwongozo huu Wizara hii haizungumzii habari ya kuongezeka kwa watu, ambalo ndiyo tatizo kubwa.

Kuongezeka kwa watu kunaendana na matumizi makubwa na duni ya ardhi, watu wanahitaji ardhi zaidi, wanafungua mashamba na kwa sababu hawana uwezo wa kutumia mbolea, wanatafuta maeneo oevu, maeneo yenye rutuba ya asili, wanafyeka misitu, wanalima kwenye miteremko kule ambako wanadhani watu hawajawahi kulima, kwa sababu ardhi bado ni *virgin*. Maeneo ambayo tulitegemea yasilimwe ndiko watakakolima, ndivyo tunavyofanya, ina maana hakuna *land use plan*. Sasa matatizo yamejikita hapo, lakini tungekuwa na matumizi bora ya ardhi, yaani *land use planning*, tungekuwa tumeweka utaratibu wa wapi tutalima na tuhakikishe watu wanafuata utaratibu huo. Kwamba, huku ni kwa kulima na huku ni kwa kufuga, hivi ni vyanzo vya maji, hii ni misitu ambayo inatuletea maji ili mito yote itiririke. Tukizingatia kwamba, ardhi yote ya Tanzania imepangwa, hatuwezi kuwa na matatizo, maji yatakuja, mito itajaa na mvua inaweza kunyesha kwa sababu misitu itakuwepo na hatutakuwa na matatizo na Kilimo Kwanza kinachozungumzwa hapa, lakini sasa hivi hatufanyi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishukuru sana kuona kipaumbele namba nne ni cha ardhi, tunakozungumzia mambo ya *land use plan* nzuri sana. Kwa mawazo yangu, nilidhani *that is the starting point*, kama nchi yote ya Tanzania imepangwa vizuri, matumizi bora ya ardhi yanaelewaka, *it may take time* kupanga kwa nchi nzima, lakini tukiwa na dhamira hiyo na ardhi ikipangwa na matumizi yake yakipangwa vizuri na tukaweka Sheria za kuhakikisha kila mtu anaafuata Kanuni na Sheria hizo; kipaumbele cha kwanza (kilimo) na cha pili (miundombinu) na kadhalika, kwangu mimi vinakuja baadaye.

Kwa hiyo, kipaumbele changu cha kwanza ni ardhi, yaani tuangalie ardhi na tupange matumizi ya ardhi vizuri, tutenge fedha tufanye hiyo kazi. Waziri wa Ardhi amekuwa akisema hapa kwamba, tufanye hiyo *exercise* vizuri na tupange wapi kwa kulima, wapi kwa kufuga na wapi tuache maeneo oevu, tuache misitu ili tuwe na mvua ya uhakika. Tukifanya hivyo, kwangu kipaumbele cha pili ni mchanganyiko wa vipaumbele namba moja ya sasa mliyopendekeza ninyi ambayo ni kilimo, kilimo hakitafanikiwa bila mipango mizuri ya kilimo, umwagiliaji hautafanikiwa kwa sababu mito itakuwa haina maji; tutamaliza *ground water reserves* kwa sababu tumekausha kila kitu. Kwa hiyo, ni lazima tuzingatie kipaumbele cha kwanza kiwe ni hicho. Kwangu kilimo ni kichochezi tu, kwa sababu kilimo ni pamoja na mazao ya kuuza. Viwanda kwangu ni vichochezi, miundombinu ni vichochezi, tunahitaji reli na barabara kuchochea ili kuhakikisha kwamba hali ya uchumi ni nzuri. Kwanza ni lazima tupange matumizi ya ardhi na tusimamie. Vipaumbele vingine vinavyofuata pamoja na viwanda, vyote navikubali ni kitu kimoja.

Kipaumbele cha tatu kwangu ni Ustawi wa Jamii, kwa kuwa unahitaji hela kwanza na kwa hiyo ni lazima uwe na vichochezi nya uchumi, unatengeneza pesa kutoka kwenye madini, viwanda na kilimo na kuipeleka pesa kwenye ustawi wa jamii. Elimu na afya ni vitu ambavyo havizalishi hela moja kwa moja, bali vinazalisha Wataalamu. Kwa hiyo ni lazima *u-generate* pesa kwanza na ndiyo maana tumejenga shule nyingi lakini Walimu hakuna, majengo mengine ni magofu; kwa nini? Hatuna fedha, kwa hiyo, lazima tuzalishe fedha na fedha itatokana na vichochezi nya uchumi kama viwanda na miundombinu. Kilimo kwangu ni kichochezi. Kipaumbele cha tatu ndiyo mambo ya jamii, yaani elimu, afya na kadhalika.

Kwa hiyo, nitakuwa na vipaumbele vitatu, wenzangu wanasema vipaumbele ni vingi, lakini mimi nitasema ninavyo vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nimemaliza mambo ya vipaumbele naingia kwenye mambo mengine. Nataka nizungumzie habari ya nishati mbadala. Mbadala maana yake ni badala ya kile kitu ambacho tumekizowea. Nishati tunayoitumia sana sana ni ya maji, juzi tumeanza gesi, lakini zaidi ni maji. Kwa hiyo, tunapozungumzia nishati mbadala maana yake ni kitu zaidi badala ya maji, kwa sababu hatuna maji ya uhakika na hatujapangilia matumizi ya ardhi. Mito haitoi maji ya kutosha inakauka, hatuwezi kuendelea na umeme wa maji twende kwenye makaa ya mawe.

Kwa hiyo, nakubali kwamba pawepo *development* ya Mchuchuma ili tupate umeme kutoka pale, lakini kama ni lazima twende kwenye maji, twende *Stigler's Gorge*, kwa sababu Mto Luwegu unatoka Selous Game Reserve, eneo lake kubwa ni *protected* hawalimi kule, ukiacha wenzetu wa Kusini sana hawaja-*open up* sana. Mto Kilombero unatoa 50% ya maji, Luwegu 30%, Great Ruaha ambayo ndiyo tunaijua 15% tu ya maji. Kwa hiyo, eneo lililohifadhiwa vizuri ni Kilombero na vyanzo vyake nya Luwegu. *Stigler's Gorge* inaweza kuwa *developed* tukawa na umeme wa uhakika. (*Makofi*)

Ndege anayekupa yai la dhahabu mheshimu. Kwa hiyo, kama tutakuwa na uhakika na Migodi ya Liganga, basi ni lazima tuhakikishe kwamba, tunaweza kufanya

kazi maeneo hayo. Lazima tutumie fedha tuwekeze miundombinu Ludewa ili tu-*develop* Liganga na Mchuchuma, ndicho kitakachotupa *golden egg* kwa sababu *impact* kwenye uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nizungumzie habari ya kuwa tegemezi. Tumeona hapa kwamba, misaada inazidi kupungua, lakini niseme wahisani wanatupa *false hopes*, tunapanga bajeti na mikakati tukitegemea watatupa hela halafu hawatupi; wanatuvurugia bajeti, hatuwezi kuendelea namna hiyo. Mimi nadhani ni vema sasa kidogokidogo tuanze na sisi kuvuta soksi, tutegemee fedha zetu wenyewe tunapofanya bajeti badala ya kuandaa bajeti wakati tunategemea wafadhili. Wametuathiri vyakutosha, tufike mahali tuseme *enough is enough* tuendelee kujitegemea sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Anastazia Wambura, halafu nitamwita Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo na ndiye atakayekuwa msemaji wetu wa mwisho kwenye kundi letu.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji jioni hii.

Awali ya yote, nami napenda niungane na wenzangu, kutoa pole kwa Familia ya Mzee Rashid Mfaume Kawawa, kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Simba wa Vita, Mzee Rashid Mfaume Kawawa. Vilevile natoa pole kwa wote waliopata misiba kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ajali, maafa ya mafuriko na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Wizara nzima, kwa kuandaa Mwongozo wa Mpango na Maandalizi ya Bajeti ambao wameuleta kwetu. Kimsingi, Mwongozo huu umezingatia maeneo muhimu kabisa katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu.

Mwongozo huu vilevile umezingatia kuonesha wazi malengo ya *Vision 2025*, pamoja na Malengo ya Milena na nguzo tatu za MKUKUTA kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niipongeze Kamati ya Fedha, kwa kuwa makini na kutokana na umakini huo, imeweza kubaini kwamba, tulichokuwa tunakijadili kwa miaka ya nyuma kama Kamati ya Mipango ya Bunge ni Mwongozo badala ya mipango yenyewe. Kwa hiyo, nami naungana nao kusema kwamba, itakuwa vizuri sasa utafutwe utaratibu wa kuliwezesha Bunge kama Kamati ya Mipango kuwa tukijadili Mpango wa Serikali wa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, niseme tu kwamba, nakubaliana na vipaumbele ambavyo vimeletwa na Serikali kwa sababu vinazingatia maeneo muhimu ambayo yataweza kuiendeleza nchi yetu kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hayo basi, niseme kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, wasiwasi wangu upo katika eneo moja tu na hili ni jinsi ambavyo rasilimali fedha zitakavyoweza kugawanywa katika Wizara tisa ambazo zinaonekana ku-*overlap* ndani ya vipaumbele hivi vitano.

Labda nitoe mfano, utakuta Wizara ya Maji na Umwagiliaji, inaonekana kwenye kipaumbele kile cha kwanza cha kilimo na maendeleo ya mifugo inakuja kuonekana tena kwenye kipaumbele cha tatu cha Huduma za Jamii. Wakati huo huo utakuta kipaumbele cha kwanza kina Wizara tatu na hicho cha tatu kina Wizara tatu vilevile.

Kwa hiyo, nina pendekezo moja kuhusiana na eneo hilo kwamba, pengine Wizara ilitazame hili kwa makini na hasa kwa kuzingatia tatizo la maji katika nchi yetu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji isimame peke kama kipaumbele kinachojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pendekezo hili kutokana na sababu zifuatazo; nazo ni nne: Sababu ya kwanza ni hawa *New Partnership for Africa's Development*, yaani *NEPAD* kwamba, katika taarifa zake inaeleza wazi kwamba, uhaba wa maji ni moja ya vikwazo vikubwa katika maendeleo ya Afrika. Vilevile inasema kwamba, upatikanaji wa maji ndiyo lengo moja kubwa katika kuleta maendeleo katika Afrika na hivyo nchi za Afrika zimekubaliana kwamba, zitajitahidi kuhakikisha kwamba, wananchi wake wote wanapata maji ndani ya umbali wa mwendo usiozidi dakika 15. Wakati huo huo hata Serikali yetu ya Tanzania nayo ina mpango kwamba, kufikia mwaka 2015, Watanzania wote, yaani kila Mtanzania, apate ndani ya mita zisizozidi 400. Hiyo ni sababu yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili inatokana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambayo inatuambia kwamba, ndani ya miaka miwili, yaani 2006/2007 hadi 2008/2009, upatikanaji wa maji safi vijijini uliongezeka kutoka 53.7% hadi 58.3%. Hili ni ongezeko dogo sana, ni ongezeko la wastani wa kama 2.2% kwa mwaka na waathirika wakubwa utaona hapa ni wanawake.

Kutokana na hilo, naona kwamba, inahitajika nguvu ya ziada ili tuweze kufikia hilo lengo katika mwaka 2015, kwa sababu najua tumebakiza miaka kama mitano hivi; sasa hiyo 40% ya wananchi wasiopata maji angalau tukiwa na ongezeko la 8% kwa mwaka itakuwa ni rahisi kufikia hilo lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo sababu nyingine ya tatu ambayo ni ushuhuda uliotolewa na *UNDP*. *UNDP* imewawezesha wananchi wapatao 4,000 wa kijiji kimoja kinachoitwa Lusala kupata maji kwa mpango shirikishi kwa thamani ya dola 40,000 za Kimarekani; lakini kwa mujibu wa taarifa, wananchi wenyewe wamethibitisha kwamba, maradhi yamepungua, wameweza kupata muda wa kushiriki katika kilimo, uzalishaji mali kwa njia ya ufgaji na wameweza pia kujenga nyumba za matofali badala ya nyumba za tope, ambazo walikuwa wakiishi mwanzoni kabla hawajapata mali.

Vilevile watoto pia wameweza kupata muda wa kujisomea na hivyo elimu imeweza kuboreka. Kwa hiyo, kwa mtazamo huo inaonekana wazi kwamba, upatikanaji wa maji una matokeo mapana zaidi na vilevile ukosefu wa maji una athari kubwa zaidi au nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina sababu nyingine ya nne ambayo imenipelekea niseme kwamba, maji na umwagiliaji yatazamwe kwa umakini. Hili ni suala ambalo katika bajeti ya mwaka 2009/2010, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia suala la maji. Katika majibu yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikiri kabisa kwamba, kweli maji ni tatizo katika nchi yetu na akasema katika bajeti ya mwaka huu, Serikali itafikiria ili iweze kuona kwamba maji yanapewa nafasi katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011.

Kwa hiyo, kwa msingi huo, ninapenda tu nijue je; kauli hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imezingatiwa katika Mwongozo huu au haikuzingatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba, pamoja na kwamba, tumeweka Kilimo na Maendeleo ya Mifugo kama ndiyo kipaumbele chetu, lakini hata maji kwa mtazamo wangu naona tukiweka kama ndiyo kipaumbele cha kwanza, *yata-play part* kubwa katika maendeleo ya kilimo, vilevile yataboresha afya, elimu, uchumi na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwa upande wa afya; katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumeona kwamba, mafanikio ya MKUKUTA, kupungua kwa vifo vya watoto wachanga na vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano, imeonekana lakini haikutajwa kabisa kwamba vifo vya akina mama vimepungua. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, inaonekana bado kuna changamoto ya kupunguza vifo vya akinamama. Ninadhani katika afya, suala hili liwekewe kipaumbele zaidi kuliko mambo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme naunga mkono hoja, lakini niombe suala la maji na umwagiliaji lipewe kipaumbele cha kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mjadala huo na sasa ninamwita Mheshimiwa Juma Njwayo.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii kama mtu wa mwisho kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuipongeza Serikali kwa mambo mbalimbali ya msingi iliyoifanyia Taifa hili na tumeona kwenye Mwongozo huu mafanikio mengi; kwa mfano, kwenye elimu, maji na maeneo mengine mbalimbali. Kwa kweli napenda kupongeza sana juhudzi zilizofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, ningependa niseme kwamba, vipaumbele vilivyotolewa na Serikali naviunga mkono moja kwa moja, kwa asilimia mia moja.

Nimesimama ili nitoe ushauri kwenye vipaumbele hivyo. Kwanza, naomba kutoa ushauri wangu kwenye suala la kilimo. Kweli kilimo ndiyo kwanza na Tanzania imekuwa nchi inayotegemea kilimo, maisha ya Watanzania wengi yanategemea kilimo, lakini wakulima wetu pamoja na kulima vizuri, wamekuwa wakilalamika sana kwenye maeneo wanayofanya kazi hii ya kilimo hasa kuhusiana na tatizo la bei ndogo ya mazao wanayoyazalisha. Kwa hiyo, natoa ushauri na rai kwamba, Serikali ifanye jitihada za kuhakikisha viwanda vidogovidogo vitakavyosaidia kuongeza thamani ya mazao yetu yaweze kuleta tija na kuleta uchumi wa wananchi wetu.

Tusiendelee kurudia mambo ya miaka iliyopita. Naweza kutoa mfano wa Kahawa na Korosho kule kwetu; leo Mtanzania wa Tandahimba, Newala au Mtwara Vijijini, anatumia gharama kubwa kwenye kuzalisha Korosho na Muhogo lakini wakati unapofika wa kuuza Korosho zenyewe, pamoja na kupata ruzuku kidogo ya Serikali, bado bei ya Korosho hiyo inakuwa ya chini na hivyo haimsaidii sana ukilinganisha na gharama zilizotumika. Kwa hiyo, natoa rai kwa Serikali kuongeza bidii hapa, viwanda viwe vingi, utengenezwe utaratibu ambao utasaidia wakulima wetu na mazao yetu kuwa na bei yenye tija. Yapo mambo madogo madogo ambayo yakizingatiwa, inaweza kusaidia sana.

Kwa mfano, kule kwangu Muhogo ndiyo chakula anachokitegemea kila mmoja na wanazalisha ziada, lakini leo ile ziada ambayo pengine ingewaletea pesa za kumudu maisha yao, imekaa tu pale haina soko; kuna haja kwa Serikali kuongeza bidii hapa kutafuta masoko. Haiwezekani Nigeria wauze Muhogo mbichi nje ya Nigeria, lakini sisi Watanzania tunalima Muhogo kwa kiasi kikubwa hatuvezi kuuza. Wakati ufike tuwekeze kwenye maeneo kama haya na kwa kweli yangeweza sana kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu; wenzangu wamesema zipo barabara maalum na kadhalika, lakini mimi nasema karibu kila maeneo kuna barabara maalum na barabara zenyewe kusaidia kuongeza uchumi kwa nchi. Kwa mfano, kule Mtwara, Barabara ya Mtwara kuititia Tandahimba, Newala na Masasi, imekuwa ikisaidia kukuza uchumi wa Mkoa wa Mtwara na Uchumi wa Taifa.

Kwa hiyo, ukisema kwamba, barabara ziko Magharibi tu peke yake; unakosea. Rai yangu ni kwamba, Serikali iangalie zile barabara ambazo zimekuwa chachu ya kusaidia kuongeza uchumi wetu nazo zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye suala la bandari. Mimi natoka kwenye Mkoa wenye bandari na kwa kweli inanisikitisha sana, ile bandari imeachwa tu ni kama kuku asiye na mwenyewe na jitihada za Serikali hazitoshi. wenzangu walisema hapa jana kama Mheshimiwa Rished Abdallah alichukua muda mwangi kweli kuongelea suala hili.

Labda nitoe mifano, Bandari yetu ya Mtwara ina kina kirefu kuliko bandari yoyote hapa nchini, imefanyiwa *heavy duty paving* kwa ajili ya kuweka kontena 1000, ina *container handling facilities* za kutosha kabisa, ina eneo la bandari lipatalo ekari 80,

ina eneo lipatalo hekta 2700 kwa ajili ya *Special Economic Zone*, bandari hiyo iko kilomita 940 hadi Malawi ukilinganisha na Dar es Salaam ambako ni kilomita 1680, ipo kilomita 600 tu kutoka Songea na kilomita 1040 kutoka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari hii kama ingetumika ipasavyo, ingetusaidia Watanzania wote. Sisemi hivi kwa sababu ipo Mtwara tu; na kwa hali hiyo ingekuwa rasilimali muhimu ya Taifa; ingesaidia ajira, ingesaidia kupunguza msongamano uliopo Dar es Salaam. Naambiwa hapa kwamba imepungua, lakini kwa kweli maelezo hayatoshi kwamba; kuna upungufu pale kwani bado adha zipo. Tusiweke mayai kwenye kapu moja, tusambaze mayai maeneo tofauti na yasайдie kujenga uchumi. Kwa hiyo, mimi naiomba Wizara na Serikali, kwenye jambo hili la miundombinu hasa bandari, kila kwenye bandari tutengeneze mazingira mazuri ili yasaidie kujenga uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la umeme wa gesi asilia ya Mnazi Bay. Wakati fulani tulikuwa tumeelezwa kwamba, upo mpango wa kujenga *line* ya umeme ambayo ingeweza kuzalisha megawatt karibu 300 mpaka pale Kibaha na kwa hiyo ingeingizwa kwenye Gridi ya Taifa, kwa sababu kwenye mikakati lipo suala la kusaidia miundombinu ambayo ni pamoja na umeme ule wa megawatt 300. Mimi nadhani nia au maamuzi ya makusudi sasa yafanywe ili umeme ule utumike kwa ajili ya kuendeleza taifa letu.

Rasilimali hizi tunazo, tuzitumie vizuri ili zisaidie kujenga nchi, tusizicheechezee tu kwa sababu Mwongozo huu nauona ni mzuri lakini ninachojaribu hapa na ndio maana tangu mwanzo nimesema, nataka kuunga mkono vipaumbele vilivyotolewa, lakini najaribu kuongeza chachu kwa kushauri kwamba, jitihada za makusudi zifanywe kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi tena kwenye kilimo; kule kuna *Rufiji Basin*, kuna *Ruvuma Basin* na *erable land* kubwa inayoweza kutusaidia sisi kuzalisha mazao mbalimbali tukajenga uchumi wetu, lakini Ukanda wote wa Ruvuma sasa hivi hautumiwi ipasavyo. Ukanda wa Rufiji na maeneo mengine ya nchi hii hayatumwi ipasavyo. Jitihada za makusudi zifanywe ili uchumi wa Taifa hili usonge mbele. Haipendezi, wenzetu wanatutania hata majirani zetu kwamba, tuna kila kitu, tuna *potentials* mbalimbali, lakini namna ya kutumia *potentials* hizo imekuwa sisi hatuwezi, kwa nini mbona wasomi tunao na watu wa kila aina?

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la maji, elimu na afya. Nianze na maji; eneo hili kwa mtazamo wangu ni eneo ambalo hatujafanya vizuri katika miaka mitano. Tulipokuwa tunaingia kwenye kampeni tulisema, asilimia 65 vijijini, asilimia 90 mijini, lakini kila mahali sasa ni kelele, kila mahali ni malalamiko. Kwa kweli naweza kusema tumeingizwa mjini kwenye maeneo mengine, kwa sababu ya wajomba tuliokuwa tunawategemea. Nilikuwa ninafikiri tufanye uamuzi kama tuliofanya kule Mwanza - Kahama wa kuweka kwenye bajeti yetu wenywewe ili suala la maji liwe la kwetu. Kweli ni gharama, lakini suala la maji tulifanye lilotokane na hela zetu za ndani. Tukiwategemea wajomba watatuangusha. Ule Mradi wa Vijiji 10 kila mwaka mmoja hadi leo haujaanza

kufanya kazi, kwa sababu ya kutegemea wajomba. Mimi natoa rai, kwenye eneo hili tutenge pesa zetu wenyewe ili mambo yaende vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu tumepiga hatua sana, sasa hivi tuna vyuo vikuu vingi kuliko mwaka 2005, tunazalisha wasomi wengi, lakini nina wasiwasi mmoja; Mbunge mmoja wa Shinyanga jana jioni alikuwa anachangia hapa akasema, kwake kuna tatizo la walimu na linafanana na Tandahimba. Tumepangiwa walimu 156, lakini walioripoti sasa hivi ni 56, maeneo ya Wilaya za Vijiji ndiko waliko Watanzania wengi, lakini hawa tunaowasomesha hawaendei kule, wakisha-graduate wakapata shahada zao, hawaendi.

Kwa hiyo, naiomba Serikali wakati hili jambo tunaliweka kama kipaumbele chetu, tutengeneze na mikakati thabiti, tuweke mikataba kabisa na watu wetu tunaowasomesha, kwa sababu hii Tanzania ni ya wote kwamba, ukimaliza masomo yako lazima uende kule. Tumejenga shule nyingi za kutosha, kila Kata sasa ina shule, hivi inakuwaje sasa wataalam hawapo? *Investment* gani ile tumeifanya ambayo haikamiliki sawasawa?

Kwa hiyo, ninatoa ushauri katika eneo hili kwamba, lazima tuangalie mara mbilimbili, tuhakikishe wataalam wetu wanakwenda vijiji; lakini hii ya kwamba, mtu unamsomesha anarudi anasema sina mkataba naye na tumewakopesha mkopo wa hela za Watanzania wote, maana Mtanzania wa Tandahimba amechangia kwenye kodi hizo, Mtanzania wa Shinyanga, wa Moshi na kwingineko amechangia. Sasa inapokuwa wanakaa mijini tu vijiji hawaendi, haitusaidii na kwa kweli hatujengi uchumi wetu kuwa imara, tutaendelea ku-mark time hapo hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la afya, wananchi wa maeneo mbalimbali wamekuwa wakijitahidi kujenga zahanati, hivi sasa kata nyingine zimeanza kujenga vituo vya afya na ni mpango wa Sera yetu; lakini nako kuna tatizo. Lipo tatizo kubwa, wafanyakazi hawapo! Kwa hiyo, kwa sababu Mwongozo huu unaweka kipaumbele kwenye huduma za jamii ikiwa ni pamoja na maji, elimu na afya, mimi nataka kuishauri Serikali iongeze udahili kwenye maeneo ya vyuo vya afya tupate wauguzi wengi, wakunga wengi, madaktari wengi na *clinical officers* wengi. Utaratibu uliopo huu, mimi ninachelea kwamba, bado tutapata wataalam wachache wasioweza kufika vijiji, majengo tumejenga yasitumike kwa mambo mengine, yalenge kusaidia kutoa huduma tunazozitarajia kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Hakika, nataka niipongeze Wizara kwa kutuletea Mwongozo huu wa Bajeti. Mimi nimeusoma kwa makini, lakini nilitaka nijikite katika suala la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii ina mabonde mengi, ikilimwa sawa sawa inaweza ikalisha Tanzania na Afrika nzima. Katika mfumo wetu wa kutaka kuleta

mabadiliko ya kilimo (*Tanzania Green Revolution*), hilo haliwezi kutimia hata kidogo na njaa haiwezi kukosa kutuadhibu hata kidogo mpaka tutakapoamua kufanya umwagiliaji mkubwa wa kilimo katika nchi yetu. Nami nasema, mabonde tuliyonayo hasa Bonde la Mto Rufiji ambalo lina ukubwa wa *square kilometres* 170,000, ni sawa sawa na asilimia 20 ya nchi nzima, lina maji, linaweza kabisa kutumalizia matatizo ya njaa, linaweza kabisa likatupa tija katika kuuza mazao tutakayolima katika Bonde hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mara tukisoma historia, tunaelezwa umuhimu wa maji, soma historia ya Nile, utakuta Waingereza baada ya kujua umwagiliaji ndio muhimu kwa Misri, jangwa, walitengeneza Protocol ya 1923 kukataza sisi wote ambaa Nile inaanzia tusitumie maji yale. Mwaka 1957 wakaiingiza na Sudan, mtu asitumie maji ila Sudan tu. Mpaka tulivyopata uhuru, Mheshimiwa Baba yetu wa Taifa katika kitu kinachoitwa *The Nyerere Doctrine*, kukataa kukubalina na mikataba iliyoingizwa na wakoloni, ndiyo tukafunguliwa maji yale. Sasa naona na Mheshimiwa Prof. Mwandsosya ananitazama, tulikuwa pale Shinyanga/Mwanza wakati wa uzinduzi wa Mradi tunaweza kuyatumia na tumeanza kuyatumia hivi karibuni katika mradi wa Maji wa Shinyanga toka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, umwagiliaji uliopo sasa hivi ni *small schemes*, hauna tija kwa nchi, umwagiliaji unaendelea lakini njaa tunayo. Mwaka huu karibu Wilaya 57 za nchi yetu zina njaa pamoja na Rufiji. Aibu kubwa, maji yapo, ardhi ipo, lakini tuna njaa na naishukuru Serikali kwamba imetupatia chakula. Naomba Serikali hii ikubali sasa kusahau mambo mengi madogomadogo ikijua tu kwamba, ukiwa na chakula una kitu kinachoitwa *political power*. Ukiwa na chakula utatawala nchi ndogondogo. Marekani, Waziri wa *Agriculture* aliiomba *Congress* nipeni fedha nimwagilia, niweze kupata chakula kingi Marekani *and that will be my political power*. Ninaomba mpeni hela nydingi sana Mheshimiwa Prof. Mwandsosya ili aweze kumwagilia; mto mkubwa tunao, ardhi ya kumwagilia ipo, maji yapo, tunachohitaji ni miundombinu na elimu ya umwagiliaji. Mheshimiwa Profesa Mwandsosya, uliniahidi kwamba utakuja Rufiji hivi karibuni na mimi nitakuwa pale kukuonesha hiyo kitu inayoitwa *The Rufiji Basin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile utaona kwamba, kama ukiweza kuboresha kilimo ambacho asilimia 75 ya Watanzania wako kazini sasa hivi kwa kutumia kijembe kidogo, utaboresha maisha ya asilimia 75 ya Watanzania. Kwa hiyo, hii ni habari kubwa. Hivi leo tunasema kama unapigana na magonjwa, ukifanya chanjo kwa watu asilimia 50 katika nchi ile, basi ugonjwa ule huondoka. Ukiweza kuboresha kilimo kwa asilimia 75 ya Watanzania, maana yake umaskini umeshaondokana nao na ukiondokana na umaskini, maana yake utajenga barabara, utatoa huduma za jamii, utaweza kabisa hata kununua *jet fighters* na kufanya mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, nilikuwa naomba nizungumzie juu ya nyenzo ya kufanya viwanda vyetu vifanye kazi, nayo ni hapo hapo Mto Rufiji kuna kitu kinaitwa *The Stigler's Gorge*. *Stigler's Gorge Hydro Power* ndiyo mkombozi wa nchi hii kwa ajili ya umeme.

Nakumbuka miaka ya 1960 au 1970 hivi, Wa-Norway walifanya *study* pale, wakasema huu ndio ukombozi wenu. Wakatokea kama kawaida wasomi, wakamwambia

Mwalimu Nyerere hapana; *we will have too much power, we have no where to sell acha tufanye mambo madogomadogo tu.* Sasa tumepata balaa kubwa, nchi yetu tunatishwa kuingia katika giza saa yoyote.

Kama mipango itapangwa vizuri, tukajenga *Stigler's Hydro Power*, viwanda vyetu vitapata umeme, faida yake viwanda vikiwa na umeme, *production cost* (ile gharama ya utengenezaji vifaa vyetu viwandani) itashuka. Kwa hiyo, bidhaa zetu zitauzwa vizuri sana katika masoko yanayotuzunguka hapa *East Africa (EAC)* na vilevile na *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hiyo haitoshi, ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, amezungumza juu ya kuhifadhi mazingira, ukiweza kutumia umeme kwa Watanzania wengi kupika, maana yake utanusuru misitu yetu kwa sababu mkaa na kuni zinatoka huko. Jambo hilo ukishalifanya, maana yake unahakikisha kwamba, misitu itakuwepo, mvua zitanyesha na ardhi yetu itaendelea kupata rutuba. Ama hiyo haitoshi, lakini angalia viwanda vidogovidogo, angalia maembe ya Rufiji yanavyoharibika wakati wa msimu wa maembe kwa kukosa viwanda vidogovidogo. Kwa hiyo, viwanda vidogovidogo nchi nzima vitachipua na sisi tutakwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninaomba nimalizie kwa suala la elimu. Hata tukiwa na matatizo gani, elimu ibaki kuwa ndiyo dira ya mambo yetu yote. Nawea nikatoa mfano wa kibiblia kwamba, Mtume Suleiman alipewa na Mwenyezi Mungu vitu vitatu achague kimoja; alipewa achague elimu, utajiri au achague ufalme. Mtume Suleiman alichagua elimu, baada ya kuchagua elimu alipata utajiri na alipata ufalme.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na Manaibu wake, kwa maelezo ya kina kuhusu Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2010/11 – 2012/13.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia, pamoja na mambo mengine, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, dira ambayo inategemea nchi yetu iwe *middle-income country*, yenye maendeleo katika kilimo na viwanda kufikia 2025. Suala la kuimarisha na kuongeza ugavi wa umeme wa bei nafuu nchini halikwepeki, lazima lipewe kipaumbele. Bila kutatua tatizo la upungufu wa umeme nchini linalotukabili na bila kupunguza gharama za umeme kwa watumiaji, si rahisi kuendesha kilimo cha kisasa kinachoendana na uwepo wa viwanda vya mazao (*processing plants*) na viwanda vingine muhimu kiuchumi. Utoaji kipaumbele kwa Sekta ya Nishati kunahuisha uimarishaji wa njia za kusafirishia umeme, uboreshaji wa vyanzo vya nishati hiyo na utafutaji na utumiaji wa vyanzo vipyta vya umeme kama jua na upepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kuona kuwa moja ya maeneo ya kipaumbele katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni kilimo na maendeleo ya mifugo. Hatuna njia nyingine zaidi ya kutenga fedha zaidi kwa sekta hii ili tuendane na Malengo ya AU ya kutenga si chini ya asilimia 10 ya bajeti ya nchi kwa kilimo. Ongezeko la fedha kibajeti kwa sekta hii, litaongeza ruzuku kwenye mbolea na zana mbalimbali za kilimo zenye ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwenye taarifa yake, mikakati mbalimbali ya kuboresha ukusanyaji wa mapato na TRA. Ningependa kumtahadharisha

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala mawili ambayo yanachangia katika ukusanyaji mdogo mapato. Kwanza, suala la TIN. Kwa uelewa wangu, niliamini kuwa uanzishwaji wa TIN ulikuwa na lengo la kuwatambua walipa kodi na kufuutilia au kwenda sambamba na shughuli zao za biashara na kazi, lakini leo hii kuna watu wenye TIN zaidi ya moja. Wapo wafanyabiashara wenye TIN hadi 10! Sasa lengo la kuwa na TIN ni nini?

Pili, upo umuhimu kwa maeneo yanayozalisha mapato makubwa nchini kupewa kipaumbele na TRA. Tuchukulie eneo la biashara la kariakoo, ambalo linazalisha mapato makubwa kwa nchi kupita sehemu nyingine yoyote nchini, lakini lina wafanyakazi wachache wa TRA wa kusimamia shughuli zinazofanyika pale. Matokeo ni makusanyo yasiyordhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anajua kuwa, kupata chumba kidogo cha biashara Kariakoo lazima uwe na fedha si chini ya shilingi 600,000 kwa mwezi. Taarifa zinazofanyiwa kazi TRA zinaonesha gharama za vyumba Kariakoo zisizozidi shilingi 200,000 kwa mwezi hata kwa vyumba vikubwa vya shilingi milioni moja hadi mbili kwa mwezi! Udanyanyifu huu unatokana na TRA kuzidiwa nguvu na mbinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa serikali inadanganywa kwenye suala wazi la kodi ya pango, serikali ina uwezo gani kufuutilia biashara lukuki za kariakoo za mabilioni ya fedha?

Kwa kumalizia, serikali inatumia njia gani kuwafuutilia na kujiridhisha kuwa wafanyabiashara wanaoaminika kuwa waadilifu (*compliant traders*), wanabakia na kuendelea kuwa waadilifu ili nchi isiibiwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALIM YUSUF MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia maisha mema na kufikia mwaka huu wa 2010. Mwenyezi Mungu, azidi kutupa maisha ya kheri na salama na zaidi kutupa uwezo mkubwa wa kufanikisha majukumu yetu. *Aamin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, pamoja na Wataalam wao wote, kwa kutuletea kazi hii, ambayo naamini kwa ushirikiano wao na usikivu wao, wataweza kutuletea bajeti ambayo itakuwa na maslahi makubwa kwa wananchi wetu.

Naipongeza pia Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kazi kubwa waliyofanya katika kutoa ushauri mzuri juu ya namna gani tufanye ili kufanikisha lengo tunalolikusudia. Pia nampongeza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa maelekezo yake mazuri juu ya Mpango na namna gani tunawenza kuutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukura wa tatu inaonekana Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 5.0 mwaka 2009. Hii ni dhahiri kuwa, ipo kazi kubwa mbele yetu katika kuhakikisha uchumi unakua, kwani tayari tulikwishazidi asilimia sita. Pamoja na kuwa kuna mtikisiko wa uchumi duniani, lakini hapana budi tujipange vizuri ili hali kama hiyo inapotokea isituathiri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 5 kifungu cha 8, mfumko wa bei hutokeza ikiwa kuna uhaba wa upatikanaji wa chakula na hali hii ilijitokeza mwaka 2009; na kwa hiyo mfumko wa bei ulikuwa uwe mkubwa zaidi kuliko ule wa mwaka 2008; mbona hali imeelezwa tofauti?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 22, miongoni mwa mafanikio ya MKUKUTA ni kuboreka kwa hali ya upatikanaji wa maji safi na salama kutoka asilimia 73.0 hadi 83 mwaka 2008/09. Wakati kwa vijijini hali imeongezeka kutoka asilimia 53.7 hadi 58.3 mwaka 2008/09 na Dar es Salaam kutoka asilimia 50 hadi 68 mwaka 2010. Sasa hii asililima 83 imekusudiwa vipi wakati bado kilio cha wananchi wengi ni maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo wa juu juu tu, utaona vipaumbele katika bajeti hii ni vitano tu kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 32/33. Ukweli ni kwamba ni zaidi ya 10. Sasa kipaumbele hasa ni kipi? Kwa hali hii nadhani tutashindwa kupiga hatua katika kipaumbele chochote. Ni vema basi, tuchague vichache ili tuweze kuvishughulikia kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali yetu isiyoridhisha ya kiuchumi, nadhani umefika wakati serikali ipige marufuku uagizwaji wa samani kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, kwa sasa magari ya anasa yamekuwa mengi mno na yanapigiwa kelele na wananchi wengi na hata baadhi ya viongozi. Hivyo, nafikiri ni vema serikali isitishe ununuzi wa magari ya anasa (mashangingi) na inunue magari kwa mahitaji kama vile hospitalini, yaani *Ambulances*.

MHE. MAGRARET AGNES MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo machache, lakini kabla ya kutoa mchango wangu, naipongeza Wizara kwa kuleta hoja hii kwa vile itatoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa mawazo kwa niaba ya wananchi ili kuboresha kabla ya kujadili Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, serikali imeeleza mafanikio na changamoto mbalimbali, lakini kwa maoni yangu nimeshangazwa kuona vipaumbele vya mwaka 2008/09 tayari vimepanguliwa na kupangwa upya. Kwa mfano, mwaka 2008/09, elimu iliyokuwa kipaumbele cha kwanza, mwaka 2010/11 ni kipaumbele cha tatu.

Ninalotaka ufanuzi ni je; katika elimu ambayo ndiyo msingi wa maarifa ya jamii; changamoto zilizojitokeza zitaweza kushughulikiwa kwa fedha chache? Nashauri elimu iendeleee kuwa kipaumbele cha kwanza kwa vile ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yoyote ile. Taifa la watu wenye elimu ya kutosha, huweza kutenda mambo yake kitaalum zaidi katika kila nyanja ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maana kwamba, vipaumbele vingine havina maana la hasha, ninachoshauri ni kipi kitaleta *multiplier-effect* ya haraka ndani ya Taifa letu; kwa mfano, huwezi kuboresha hali ya maisha kwa makundi maalum kama wenye ulemavu bila makundi hayo kupata elimu.

Kipaumbele cha pili kiwe miundombinu, cha tatu kiwe kilimo, ardhi na maendeleo ya mifugo na hatimaye viwanda mama na vya usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. PHILEMON SARUNGI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na timu yake, kwa kuandaa Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63(3)(c), chini ya Kanuni ya 94 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mwongozo wa Mpango umetayarishwa kwa utaalamu kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 na Malengo mabalimbali na Taarifa za Utekelezaji wa Sera. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, napenda kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha Mwongozo huu kama ifuatavyo:-

Mapendaakezo ya vipaumbele katika Mpango na Bajeti 2010/11 – 2012/13:-

(a) Napenda kutoa ushauri kuwa Serikali iandae orodha ya maeneo yote hasa mabonde yanayofaa kuendelezwa kwa kilimo cha uwagiliaji, kwa lengo la kuendeleza maeneo hayo kushirikiana na wananchi wa maeneo husika na wawekezaji.

Serikali imejitahidi sana katika kutoa msukumo katika ujenzi wa mabwawa kwa ajili kilimo cha umwagiliaji, nashauri mabwawa yote yaliyojengwa na serikali na yanayochangia Pato la Taifa na ajira kwa wananchi, yaboreshwe kwa kujenga miundombinu ili yaweze kutoa mchango katika Pato la Taifa. Mabwawa hayo yachapishwe katika orodha ya mabwawa yaliyotajwa katika ukurasa wa 18 ya Mwongozo.

Wananchi wa Wilaya ya Rorya wanaipongeza serikali kwa kuwajengeea mabwawa matano na bwawa la sita linaanza kujengwa. Mabwawa hayo yatatoa tani 6,373 ya mpunga kila mwaka.

(b) Serikali iandae mpango wa muda mfupi, wa kati na muda mrefu kuhusu ujenzi wa viwanda vya usindikaji nyama, viwanda vya ngozi na bidhaa zinazotokana na mifugo kama chakula cha kuku katika maeneo ya mikoa ya wafugaji. Katika Mkoa wa Mara, wezi wa mifugo wameshamiri kutokana na nchi jirani kujenga viwanda vingi vya kusindika nyama mpakani. Kiwanda cha nyama na ngozi kitakapo jengwa, thamani ya mifugo itaongezeka na mapato ya serikali yataongezeka.

(c) Asilimia 73 ya eneo la Wilaya ya Rorya ni maji ya Ziwa Victoria na kuna mitaro 34 inayotumika kwa ajili ya uvuvi katika kata 10.

Serikali inapoteza mapato yanayotokana na Sekta ya Uvuvi kwa kutokuwa na mpango wa ukusanyaji ushuru wa samaki. Ninaishauri serikali iboreshe Vituo vya TRA katika Bandari ndogo ya SOTA, maeneo ya Mihalo, kwa kutoa nyezo za utendaji kazi kwa watumishi wake kama vile maboti, magari, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri.

MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja hii ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu wake, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara, kwa Hotuba nzuri na kazi nzuri kwa jumla. Kwa kuzingatia mazingira magumu yaliyosababishwa na kuyumba kwa Uchumi wa Dunia na ukame, Serikali inastahili pungezi kwa hatua thabiti walizochukua, kuulinda Uchumi wa Tanzania na kuepusha na uzorotaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na nchi kuweka mkazo maalumu kwa mipango. Hapana budi pakawepo mfumo wa utaratibu wa kuipa shughuli ya mipango uzito maalumu ama kwa kuiimarisha Tume ya Mipango au kwa namna nyingine yoyote ambayo itatoa uzito stahiki kwa mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mazingira yetu, ninakubaliana na vipaumbele kama vilivyoainishwa na Mheshimiwa Waziri. Hatuna budi tutambue kwamba, Dira ya Taifa 2025, MDG, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM, yote yana madhumuni ya kupambana na maadui ujinga, umaskini na maradhi. Hivyo

consistency na *persistence* ni katika kupambana na maadui hawa kwa ukjumla wake bila kutaka *permance and perpetuality* za vipaumbele kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwa zaidi ya miaka kumi tumetoa kipaumbele cha kwanza cha kutosha kwa Sekta ya Elimu na tumefanya mengi chini ya MMEM na MMES, pamoja na maboresho ya Elimu ya Juu. Maboresho zaidi (*Qualitative Chance*) kwa Sekta ya Elimu, yanaweza yakapatikana chini ya mapendekezo ya elimu kuwa na kipaumbele cha tatu kama ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso la kilimo kupewa kipaumbele cha kwanza ni sahihi, misingi yake ilielekezwa katika Warsha ya Kilimo Kwanza Kunduchi Hoteli. Kwa mara ya pili, Mheshimiwa Rais alitoa ufanuzi mzuri Kilimani Dodoma wakati wa kuelekeza Sera za Uchumi kufuatia kuyumba kwa uchumi Duniani.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Gavana wa Benki Kuu, walifafanua haya Bungeni mara kadhaa; kwa mara zote hizo, Wabunge waliona umuhimu wa kilimo na kuhimiza kwamba, kimpango na kibajeti, kilimo kipewe kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, changamoto zetu kimipango na kibajeti, hazitokani na ujinga bali zinatokana zaidi na umaskini. Hivyo, kimantiki baada ya kuwekeza vya kutosha kwa Sekta ya Elimu na kutoptana na haja ya kujihami dhidi ya njaa na kujenga uchumi imara unaojitegemea kuendelea kwa kasi kubwa, kilimo kwa sasa ndicho kinachostahili kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa kizingatia kwamba, miundombinu ya kiuchumi ndio mhimili mkuu katika kuchochea na kuhakikisha kasi kubwa ya maendeleo ya uchumi, kipaumbele cha pili kupewa miundombinu ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kizingatia mchango wa huduma za jamii kwa maisha bora kwa Watanzania ni sahihi kabisa kwa eneo hili kuwa katika kipaumbele cha tatu. Naamini sekta hii itapata rasilimali tosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la faraja kubwa sana kwamba, Serikali imeona umuhimu wa ardhi na viwanda kuzipa sekta hizi vipaumbele na 4 na 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ningependa kujikita katika masuala ya sera na utendaji ambayo ni muhimu yakatupiwa macho katika mchakato mzima wa mipango na bajeti ili kuweza kupata kasi endelevu ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara 41(iv), ukurasa wa 29, kwa usahihi kabisa imesisitiza kuhusu kulinda uwekezaji muhimu, mafanikio ya azma hii yatategemea sana uwekaji na utekelezaji bora wa Sera za Kodi kwa viwanda vyetu zaidi ya yale yanayojitokeza kwenye Ibara 46 (ukurasa wa 33). Baadhi ya hatua muhimu ya kuvilinda ni pamoja na:-

- Hatua thabiti za kupunguza gharama za uzalishaji zikiwemo za umeme, malighafi, usafirishaji na urasimu usio wa lazima. Mradi wa *BEST* ulete manufaa yanayotarajiwu.
 - Upatikanaji wa maji na nishati kwa uhakika ni muhimu.
 - Sera ya kodi ipunguze mlolongo wa kodi hasa katika upande wa uzalishaji na kuzihamisha kodi hizo kwa mlaji ili viwanda vyetu nya ndani viweze kuhimili ushindani.
 - Vivutio vyta uwekezaji kama vilivyoainishwa katika Sheria ya TIC vitekelezwe ipasavyo ili kidhibiti kasi ya upunguaji wa uwekezaji na kukimbiza uwekezaji kutoka Tanzania.
 - Zaidi ya samani (*paragraph* ya 35 (xvii, ukurasa wa 39), upendeleo maalumu upewe bidhaa zinazozalishwa nchini kwa misingi ya kulinda viwanda vichanga kama inavyoruhusiwa na kanuni za wito.
 - Misamaha ya kodi kwa bidhaa zitokazo nje itolewe pale ambapo bidhaa hizo hazizalishwi kabisa nchini au hazizalishwi kwa kiwango stahiki.
 - Wigo wa vivutio vyta EPZ au EDZ, pamoja na ECGS na vivutio vingine kwa wauzaji bidhaa nje upanuliwe ili kuboresha ushindani na kuongeza mauzo nje.
 - Hatua thabiti zichukuliwe kulinda wawekezaji wetu dhidi ya ushindani usio wa haki.
 - Mgao wa rasilimali chache upewe kipaumbele kwa viwanda mama na viwanda vinavyozalisha pembejeo (*Intermediate Goods*).
 - Pawepo mfumo wa ushindanishaji wawekezaji kisekta na motisha kwa wanaofanya vizuri zaidi kuliko wenzi wao.
- Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hayo yote yakitekelezwa kwa ufanisi, tutajenga na kulinda uchumi wa nchi yetu kwa mafanikio makubwa.
- Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi serikalli iangalie jinsi ya kuweka vipaumbele vyetu vizuri ili mwananchi wa kawaida na yule maskini kabisa, ambao ni wengi wasiweza hata kumudu mlo mmoja kwa siku, waweze kufaidika

na rasilimali zetu. Tanzania kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametujalia rasilimali nyingi kuanzia chini ya ardhi tuna madini ambayo najua hayapatikani mahali popote duniani zaidi ya Tanzania. Juu ya ardhi tuna ardhi yenyе rutuba nzuri ambayo kilimo chochote kinakubalika katika sehemu tofauti nchini. Tuna mito, bahari, vivutio vya utalii, mlima pekee wenye theluji (Kilimanjaro) ambaо upo kwenye sehemu za joto; lakini cha kusikitisha tunashindwa kuzitumia vizuri.

Ningeshauri tuendelee na kipaumbele cha mwaka jana cha Elimu Kwanza badala ya kilimo. Watu wakielimishwa tutapata maafisa ugani na hata hivyo tukiwa na watu wenye elimu tutaendelea. Mfano, nchi jirani ya Kenya wao walihakikisha wana-*invest* na kuwa na *capital* na tunaona wenzetu walivyoendelea.

Kipaumbele cha pili baada ya elimu, kuwepo na nishati ya umeme ya uhakika ili viwanda vidogovidogo na vikubwa viweze kufunguliwa mpaka vijijini, badala ya kuza malighafi wauze mazao na bidhaa ambazo zimekwishafanyiwa *process* hapa hapa. Kwa njia hii wakulima watafaidi, ajira zitaongezeka na kuiongezea Tanzania Pato Taifa na hatimaye kupunguza au kuondoa kabisa umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango yetu badala ya kuwa na vipaumbele vingi, tumalize kwanza kimoja na kufanya tathmini tumefanikiwa kwa kiasi gani na tuliposhindwa ni wapi badala ya mtindo wa sasa wa kubadilisha vipaumbele vyetu kila mara na kutufanya tushindwe kufikia Malengo ya Milenia.

Tafadhali zingatia kipaumbele cha kwanza kiwekwe kwenye elimu. Bila kutoa ujinga na dunia ya sasa ya teknolojia na sayansi, hatuvezi kubaki kama kisiwa, lazima tuendane na dunia hii ya utandawazi.

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Ningependa kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuongeza fedha za ununuzi wa pembejeo za ruzuku. Hii inaonesha ni kwa namna gani Serikali inajali maendeleo ya wakulima. *Support* inayotolewa na Serikali katika Kilimo Kwanza itatuwezesha kufikia azma ya Serikali ya kujitosheleza kwa chakula.

Miradi ya *Millenium Challenge Corporation (MCC)*; Serikali yetu inayo miradi mingi inayohusu Sekta za Barabara na Umeme. Kazi nyingi zimefanyika na baadhi ya miradi ipo katika hatua mbalimbali, tatizo ni kwamba, hakuna mradi hata mmoja wa ujenzi ambaо umeshaanza. Nashauri hatua zichukuliwe ili kuona miradi hiyo inatekelezwa haraka ili kuimarisha imani kwa wananchi.

Hifadhi ya chakula: kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa na upungufu wa chakula baadhi ya maeneo yetu, lakini wakati huo chakula huwa kipo cha kutosha katika baadhi ya mikoa kama vile Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma; tatizo ni kwamba, *NFRA* hawapati fedha za kutosha kwa ajili ya kununa chakula cha akiba. Ninaishauri Serikali itoe fedha za kutosha kwa *NFRA*. Aidha, wananchi walio mpakani katika Mkoa wa

Rukwa, Serikali iweke utaratibu wa kuwawezesha waweze kuuza mazao yao katika nchi jirani ambao wana mahitaji ya chakula.

Naomba Serikali pia ifanye jitihada za kuuboresha Uwanja wa Ndege wa Lindi, ambao zaidi ya kuwa ni uwanja mzuri na mkubwa, lakini una historia kubwa toka enzi za Vita kuu ya Pili ya Dunia.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Utayarishaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2010/11 - 2012/13, umejikita zaidi kwenye Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Aidha, kutokana na Dira hiyo kumezaliwa ilani ya uchaguzi ya CCM 2005, maendeleo ya milienia na dhana ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango hii imejijenga katika vipindi vifupi, vya kati na vya muda mrefu. Kinachoonekana katika Mipango hii, hakuna muunganiko ulio bayana, ambao utaihakikishia mipango hii utekelezaji wake uwe kwa manufaa ya wananchi. Nadhani ipo haja ya makusudi ya kuiunganisha Mipango hii ili iweze kuleta tija kwa nchi na Watanzania wawe na maisha bora na mazuri.

Kutokana na kuparamiana (*overlapping*), kwa Malengo ya Dira na Mipango mbalimbali, kunapelekea nchi kuwa na vipaumbele tofauti na hali halisi na vinabadilika mwaka hadi mwaka. Mara nyingi vipaumbele hivyo huwa vingi kuliko uwezo wa Serikali. Hatimaye fedha chache tulionayo, inagawanywa kidogo kidogo na ni mara chache tunafikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, Serikali ingelichagua vipaumbele vichache ili rasilimali ya fedha iliyopo ieletekezwe huko ili kuleta mabadiliko yaliyokusudiwa. Mathalani, nchi hii mara kwa mara inakabiliwa na tatizo la njaa, miundombinu mibovu na iliyochakaa. Ingekuwa busara zaidi tukaanza na vipaumbele hivi na baadae mbele ya safari tukahudhuria vizuri vipaumbele vingine baada ya kuwa na tathmini ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kuvihudumia vipaumbele ambavyo Serikali huvichagua hapana budi kwa Serikali kusimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali. Aidha, Serikali iangalie upya utaratibu wa misamaha ya kodi, kwani misamaha hiyo imekuwa minge ni inalipotezea Taifa fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikalil ikiweza kuzingatia ushauri huu, basi fedha nyingi zitakusanywa na hivyo kusimamia vema utekelezaji wa vipaumbele tulivyojipangia. Serikali ingelichagua vipaumbele vichache ili rasilimali na fedha iliyopo ieletekezwe huko ili kuleta mabadiliko yaliyokusudiwa. Mathalani, nchi hii mara kwa mara inakabiliwa na tatizo la njaa. Eneo lingine ambalo linahitaji kupewa kipaumbele ni uimarishaji na uanzishaji wa viwanda vya kusindika malighafi za kilimo ili kuzingatia thamani na kumwongezea fedha mkulima. Uimarishwaji wa viwanda ni muhimu, siyo tu

unaongeza thamani ya mazao, bali pia unapunguza upotevu wa mazao na kufanya yasiharibike baada ya kuvuna au yakiwa shambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yataweza kusimamiwa vema iwapo rasilimali watu itazingatiwa ipasavyo. Kumekuwa na tatizo kubwa la upungufu wa watumishi wenye sifa mahususi kwa kazi wanazofanya. Hii ni sehemu ambayo ina umuhimu wake katika kukuza uchumi wa nchi na kutoa huduma iliyo bora kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja kwa Serikali ifanye utafiti wa kina kujua rasilimali watu au wataalamu tulionao na fani zao ili hatimaye kujua upungufu uliopo. Taarifa hiyo itawezesha Serikali kujaza upungufu uliopo. Hatua hii itapelekea kuwa na matumizi mazuri ya rasilimali watu iliyopo. Ahsante.

MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyez Mungu, kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kuichangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukupongeza wewe kwa kuweza kuliongoza Bunge hili kwa umakini mkubwa. Mwisho na kwa umuhimu mkubwa, napenda kuzipongeza taarifa zote zilizotolewa mbele yetu za kuweka Mpango Mkakati wa Bajeti yetu ya Mwaka 2010 - 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge iliona umuhimu wa kuweka Ibara hii ya 94 katika Kanuni zetu kukidhi ile dhana ya Bunge kushiriki katika mpango mzima wa bajeti, lakini Ibara hiyo imeonekana ina ipungufu kidogo, tunaiomba Serikali ishirikiane na Bunge hili ili kuondosha utata huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaonekana imebadilisha kipaumbele chake na kuwa Kilimo Kwanza na inaweka elimu nyuma, wakati kipindi hiki kina changamoto nyingi zinazoikabili Wizara ya Elimu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni muhimu sana na tumeshapoteza fedha nyingi sana kwa kujenga madarasa, maabara na kadhalika. Vitu vyote hivi vina mambo muhimu yanayotakiwa kukamilishwa, lakini leo tunaacha tunaimarisha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanadai fedha zao nyingi sana hawajalipwa; je, Serikali kweli iko makini katika kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu iliyo bora au bora elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mara nyingi inafanya kazi kwa utashi wa kisiasa zaidi kuliko kitaalamu; naiomba Serikali iache mambo hayo. Nchi yetu ni kubwa sana na Mwenyezi Mungu ametujalia vitu vyote muhimu vimo humu, kwa mfano, milima, mabonde, mito, maporomoko, madini, gas, mafuta na ardhi kubwa kabisa; kwa hiyo, tunahitaji miundombinu mizuri na ya uhakika ili nchi hii ipate maendeleo. Nchi hii haiwezi kuendelea bila kupata miundombinu ya reli, bandari, barabara, viwanja vyatundege na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha mvua kubwa, kumejitokeza mafuriko na kuharibu miundombinu ya barabara na reli na fedha nyingi sana zinahitajika kufanya matengenezo. Kwa hiyo, Serikali inatakiwa ifanye mipango kabambe ili miundombinu hiyo irejeshwe kwa haraka kwani dhana zote hizo tunazozipanga, haziwezi kufanikiwa bila ya barabara, reli na bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakandarasi wengi wanadai fedha zao nyingi na vile vile tumeingia katika mikakati mipyä bila ya kuzingatia uwezo wetu wa kifedha na ndiyo nasema Serikali iache kutanguliza siasa zaidi kuliko utaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha dharura, ninaungana na Wabunge wenzangu kuiomba Serikali ipunguze OC katika Mawizara mbalimbali ili kuiwezesha Wizara ya Miundombinu kufanya ukarabati reli na barabara zetu ambazo hata hiyo elimu au kilimo haviwezi kufanyika bila miundombinu iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelekezo hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuipongeza Serikali kwa juhudzi zake za kusukuma maendeleo katika nyanja mbalimbali.

Pamoja na juhudzi hizo, Serikali huwa inakabiliana na uhaba wa fedha ambapo hutegemea wafadhili, tunashukuru kwa jitihada hizo za wafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja kwa Serikali yetu kuweka mikakati mahususi ya bajeti ya ndani katika mambo makuu muhimu yanayoweza kufanyika bila ya kutegemea sana wafadhili, kwani ucheleweshwaji wa fedha/misaada toka kwa wafadhili, isituzuwie kutekeleza mipango yetu.

Je; ni lini au ni kwa vipi Serikali imejiandaa katika utekelezaji wa vipaumbele hivyo hata kama hatuna wafadhili?

Naomba nipatiwe maelezo.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kupata nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu kwa maandishi.

Pamoja na shukrani hizo, namshukuru Waziri na timu yake yote, kwa kutuletea Mwongozo wa Bajeti hapa Bungeni ili nasi tuweze kutoa maoni yetu. Aidha, nawapongeza wataalamu waliouandaa Mpango huu kwani ninajua ni kazi ngumu kidogo, wanatoa taswira ya bajeti yetu iweje, nasi tunapata pa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe mchango wangu kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wowote wa jambo ni lazima huwa kuna mwanzo na malengo yake. Hivyo, ningependa kujua lengo hasa la bajeti itakayokuja ni nini? Isiwe tu kwamba, kumewekwa vipaumbele bila kuwa na lengo mahususi. Pamoja na malengo, lazima kwanza ifanyike tathimini ya bajeti iliyopita na kuangalia nini Malengo ya Bajeti iliyopita na kipaumbele chake; wapi palipofanikiwa na wapi palipokwama; na kwa sababu hii ni wapi tulitereza na ni kwa kwa sababu gani. Je, bado tunataka kufikia lengo lile ama la halina umuhimu tuanze lingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ndipo tunaweza kuanzia. Kwa maoni yangu, naomba niseme kwamba, Tanzania tangu Uhuru imekuwa ina maadui watatu; ujinga, maradhi na umasikini na maadui hawa wote wanaongozwa na kamanda ujinga. Hivyo, kama tukiendelea kupambana na kuutokomeza ujinga ni wazi maradhi na njaa vitatoweza. Hivyo, bado kipaumbele cha elimu ni kikubwa mno, ni lazima tusimame hapo. Mambo yote haya yatategemea uchumi wa nchi. Uchumi wa nchi hauwezi kuja kama watu wake hawajapata elimu nzuri na bora, kwani hata ukijenga barabara nzuri, zahanati, masoko na kadhalika, hawatavitumia ipasavyo. Elimu *must be number one*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhakikisha kuwa nguvu zote zinaelekezwa katika kukuza uchumi ni lazima kuweka juhudzi zote katika miundombinu ya uchumi, ambayo ni nishati, barabara, reli na bandari. Tanzania imezungukwa na nchi nane, mimi naona ni sawa na mgodi kabisa, kwani wote hawa kama watatumia bandari, barabara na reli yetu, uchumi utakua, Pato la Taifa litaongezeka na ajira na fedha za kigeni vitaongezeka.

Tukiwa tunapiga *marktime* kila mwaka, wenzetu Wakenya, pamoja na matatizo waliyokuwa wameyapata ya siasa, bado wanaendelea kujenga bandari kubwa sana Mombasa na hiyo itatumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa nchi hauwezi kukua bila umeme, lakini hapa Tanzania umeme tunaowasha ni mdogo sana kuliko mahitaji. Sasa sijui kama fedha za kuzalisha umeme zitapewa umuhimu, kwani nasikia kuna *Master Plan* ya kuzalisha umeme. Bila umeme wa kutosha, viwanda vitakwama tu na pia lazima viwepo viwanda vidogovidogo ili kukidhi dhana ya Kilimo Kwanza. Kilimo na viwanda ni watoto pacha. Hii itaongeza ajira na pato litaongezeka.

Suala la kukuza uchumi ni pamoja na kuitangaza nchi yetu ikae katika Ramani ya Dunia. Njia pekee iliyio rahisi kulitangaza Taifa letu na maliasili zake ni michezo. Nchi ya Kenya wametumia michezo zaidi kutangaza Taifa lao. Hivi sasa Serena William, mchezaji maarufu wa tennis Duniani, anajenga shule mbili Kenya na hii ni kwa sababu wanawake walishiriki mbio mbalimbali.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa maelezo aliyoyatoa kuhusu Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2010/11- 2012/13. Naunga mkono Mwongozo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hoja yangu ipo katika maeneo ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia, sehemu inayohusu kuondoa kabisa umaskini uliokithiri na njaa. Pamoja na nia nzuri hiyo, hatutafanikiwa bila kutoa kipaumbele katika maeneo ya kuboresha afya ya uzazi; kupunguza vifo vya watoto; na kuukabili UKIMWI na Malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hayo kwa sababu suala la ongezeko la idadi ya watu ukilinganisha na kukua kwa uchumi, hata ufanyeje umaskini wa nchi hii hautapungua.

Naelewa mhe Waziri anaewela kuwa kasi ya ongezeko la watu kwa asilimia 2.9 (*approx 3*), ukilinganisha na kukua kwa uchumi kwa asilimia 5.6 badala ya uchumi kuongezeka kwa angalau asilimia 8 hadi 9. Hali hii haiwezi kuongeza jitihada ya kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri hatua zifuatazo ziandaliwe katika Mpango ufuatao wa 2010/11: Fedha kwa ajili ya uzazi salama ziongezwe kuititia Wizara husika; na fedha kwa ajili ya UKIMWI na Malaria ziongezwe katika Mpango badala ya kuendelea kuwatumia wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hali ya fedha zinazotolewa na wahisani, kwa masuala ya UKIMWI ni asilimia 96, wakati sisi tunatoa asilimia 4. Je, kwa nini nasi kwa kipindi hiki tusiongeze kidogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida inaonekana yataongezeka sana kuliko matumizi ya maendeleo, licha ya kutambua kuwa bado madeni ya nyuma katika shughuli za miradi ya maendeleo hayajalipwa na yanaweza kuathiri sana utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Waziri afuatilie madeni ya makandarasi wa barabara (Shs.212 bill) bado ni madeni tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atupatie maelekezo kwa ufupi kuhusu Mpango wa Serikali ya China, inayotoa fedha za mikopo kwa Nchi za Afrika ambazo tunasikia sisi Tanzania tulichelewa kuitumia na kuipeleka nchi nyininge. Jitihada zipi zinatumika kuziomba zirejeshwe tena kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MAIDA H. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na kwa Kamati iliyojadili Mwongozo kuu kwa ufanuzi wa kina.

Naomba nianze na suala la MKUKUTA; lengo la Mkukuta ni kuwapunguzia wananchi umaskini wa kipato na huu ni mwendelezo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Lazima hapa Serikali ijikite katika masuala mazima yanayohusiana na jukumu la kuondoa umaskini.

Serikal imejitahidi kutoa fursa mbalimbali za fedha ili wananchi waondokane na umaskini wa kipato.

Kinachoendelea kufanyika katika baadhi ya Halmashauri/Wilaya au Mikoa imekuwa ni tatizo kubwa, kwani wananchi walio wengi wanalamika kwa kutofikiwa na fedha hizo. Serikali Kuu nayo pale malalamiko yanapotokea, inashindwa kufanya utafiti na ufuatiliaji katika maeneo yanayolalamikiwa. Hivyo, wananchi nao wanajenga imani kuwa wanaofaidika na fedha hizi siyo maskini kama wao na kupelekea kutokuwa na imani kwa Serikali yao vilivyo. Pia tuangalie Tanzania tokea tumeanza kutangaza Mkukuta, umasikini umepungua kwa kiasi gani ili kujiweka vizuri na kuangalia kasoro zilizopo na kujirekebisha katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumko wa bei; katika bajeti zilizopita tulikuwa tunajadili mfumko wa bei na hii inajulikana kabisa kwamba, mfumko wa bei unatokana na ukosefu wa mazao ya chakula. Serikali imetangaza Kilimo Kwanza, mikopo kwa wakulima, kuondokana na kilimo cha kizamani na kulima kilimo cha kitaalamu cha umwagiliaji. Hivi sasa yapo maeneo mengi wakulima wanalamikia mikopo ili kufikia lengo la Kilimo Kwanza.

Je, Serikali itahakikisha kuwa wakulima walio wengi wanapata mikopo hiyo na kujali jinsia zote ili kufikia lengo la Kilimo Kwanza? Tunayapongeza mashirika yaliyoimarisha umwagiliaji katika baadhi ya maeneo ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa kutangaza msamaha wa fedha za kugharimia mitihani ya darasa la saba kutokana na kuwa na idadi ya wanafunzi wengi nchini, ambao hawafanyi mitihani hiyo kutokana na kushindwa kulipia gharama hizo.

Kumejitokeza mtindo kwa baadhi ya shule kukusanya fedha wakati wa uandikishaji au kila ifikapo mwanzo wa mwaka, kwa maana ya kuchangia majengo, lakini wanafunzi hawapatiwi risiti yoyote ili kuonesha au kujulikana kuwa fedha hiyo imeingia katika makusanyo yanayotambulika.

Je, Serikali inalitambua hilo kama haitambui imojiwekeua ukaratibu gani wa kufuatilia mahesabu ya fedha zinazokusanywa shulen humo ili kuweza kujuu matumizi yanavyofanyika kulingana na makusanyo; wananchi wakiwemo wazazi na walezi, wanaoendelea kutoa malalamiko kwa Serikali, waweze kujenga imani na Serikali yao? Naiomba Serikali kupitia Wizara husika, ilifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie maafa yaliyotokea Mbagala kuhusu waathirika wa mabomu. Naipongeza Serikali kwa kuweza kutoa fedha nydingi kwa ajili ya kuwasaidia waathirika hawa wa mabomu. La kushangaza, sasa hivi kuna malalamiko kwa wananchi walio wengi, ambao wamepata athari hizo lakini hadi leo hii hawajafaidika na fedha hizo. Je, Serikali imeshakwenda kufanya usahihi wa wale waliokusudiwa na kuona kama wamefaidika au hawakufaidika?

Kama hazijawafikia walioathirika kama ilivyokusudiwa; fedha hizo zimekwenda kwa nani?

Hilo pia imekuwa ni tatizo kwa wananchi ambao wanapoteza imani kwa Serikali, kwani wale watendaji wachache wanaosababisha laana kwa Serikali Kuu.

Naomba Serikali ifuatilie kwa kina pale wananchi wanapolalamika kwani wananchi ndio wapiga kura katika chaguzi zote mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha, lakini kasoro zirekebishwe pale zilipojitokeza.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Kwa nini maandalizi ya kutoa mikopo kupitia Benki ya TIB kwa ajili ya wakulima inachukua muda mrefu?

Kwa nini TIB isiendeshe semina kwa Wabunge juu ya masharti ya kukopa ili kuongeza ufahamu na maandalizi mema kuwezesha ukopaji?

Kwa kuwa kilia kijiji kinalazimika kuchangia TSh. 714,000 ili wananchi wake wapimiwe mashamba yao na kupewa hati za kimila; je, kwa nini Serikali isivilipie vijiji kiasi hicho cha fedha ili kumuwezesha kila mkulima kupata hati miliki ya kimila na kukidhi sharti muhimu la kibenki kukopesheka?

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi ya kuchangia mawazo juu ya Mwongozo uliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi.

Pamoja na kumshukuru Waziri wa Fedha kwa kutoa mawazo yake mazuri kuhusu Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti, nina mawazo kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, katika Mpango wowote ni muhimu kuwa na vipaumbele, lakini mabadiliko ya kila wakati hayana tija. Huwezi kuona matokeo ya mambo unayofanya, unagusagusa tu. Hivyo, nashauri kuwe na *consistency* katika upangaji wa vipaumbele. Wakati huo huo, vipaumbele ambavyo ni *catalyst* ya maendeleo ya kiuchumi ni muhimu, ikiwa ni pamoja na vile vinavyojibu kero kubwa za wananchi ambao wanafanya kazi ya kuchochea maendeleo ya nchi. Si vema kupuuzia kero kubwa kama ya maji; leo ni miaka 48 tangu tupate Uhuru, lakini mpaka sasa katika vijiji vingi wananchi hawajapata maji safi ya kunywa.

Tungependa wazalishaji wetu wawe na afya nzuri, waishi bila kushambuliwa na maradhi yatokanayo na kukosa maji au kutumia maji machafu. Wanawake wengi vijijini bado wanatembea mwendo mrefu na kushindwa kufanya kazi za uzalishaji. Ukiliangalia suala la umuhimu wa maji kuwekwa katika kipaumbele cha juu, sambamba na kupunguza magonjwa ya kuambukiza na kumsaidia mwanamke asipoteze muda mrefu wa kazi kutafuta maji, unapunguza bajeti ya matumizi.

Serikali isisitize mambo muhimu yafuatayo katika kilimo:-

(a) Mkazo uwekwe katika kuongeza maeneo ya kilimo kwa kuwapa uwezo wakulima wengi wamiliki matrekta wenyewe kwa kuwapa mikopo. Benki ya Rasilimali ya Tanzania, ipewe fedha ya mtaji wa kutosha kwa mikopo hiyo. Kwa dhana ya kumiliki matrekta yatadumu kwa muda mrefu badala ya kununuliwa na Serekali kama ilivyokuwa kwa *Power Tillers*.

(b) Kusisitiza juu ya kulima mazao ya kuuza nje pamoja kujitosheleza kwa chakula.

(c) Serikali iendelee kwa nguvu kubwa kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya mazao, ikiwa ni pamoja na usindikaji wa matunda. Pia viwanda vya zana za kilimo.

(d) Kuunga mkono na kusukuma kwa nguvu kubwa kilimo cha mboga, ikiwa ni pamoja na matunda na maua. Sekta hii hivi sasa ina matatizo makubwa ya njia ya usafirishaji wa mazao yao kwenda nje. Kwa kuwa Serikali imeanzisha utaratibu wa kutoza VAT kwa mazao hayo kabla hayajasafirishwa pale Uwanja wa Ndege KIA, matokeo yake, wawekezaji wanalazimika kusafirisha mazao yao kwenda Nairobi, Kenya. Ni kazi kubwa na ya kuwakatisha tamaa wakulima. Hali hiyo irekebishwe ili mazao ya Tanzania yasafirishwe kutoka viwanja vyetu. Hatupati ndege za kutwa hapa nchini.

(e) Kilimo Kwanza – mkazo mkubwa utolewe katika kilimo cha umwagiliaji miradi mikubwa na kufufua *traditional furrows*.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa “Kilimo kwanza” na pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dokta Mkullo na Manaibu wake wote wawili Mheshimiwa Ommary Juma na Jeremiah Sumary kwa kazi nzuri iliyoandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi naunga mkono mwongozo huu kwa sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli kama una wajumbe wanne na wote wanatakiwa kuhudhuria m Kutano wakiwa wamevalia sare ya Suti, Tai na Viatu vyeusi na *column* ni watu wawili, wakati huo huo uwezo ni kununua suti mbili au *pieces*, ni bora kununua suti mbili na m Kutano ukaendelea kuliko kumgawia kila mmoja suruali au shati tu, kwa miaka miwili na ndipo wajumbe wote wafanye m Kutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wetu ni m dogo, miradi tunaitisha mingi kwa pesa kidogo, yote inachelewa, bei au thamani ya mradi inaongezeka na kuchelewesha mradi kujilipa kutokana na faida zake za kiuchumi (*pay back period/profit yield*).

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia zaidi ya 80% ya Watanzania ni wakulima na wapo vijijini na ndio wenye watoto wanaokosa huduma kutokana na umaskini wa wazazi

wao. *Main source of income* ni kilimo. Njaa, hakuna mwenye kiburi kwa njaa. Kilimo kwanza ndio mkombozi, kupata ziada na tujitosheleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, miundombinu – *Economic drivers*, bila miundombinu haitusaidii tuachenii siasa, tuchague miradi michache kwa mwaka au *short term* iihe, lakini pia mipango ya *planning* iendelee. Ni aibu kutoka jasho kila siku kujadili jambo hilo hilo, ni sawa na *retail purchases*.

Mheshimiwa Naibu Spika, malizeni tatizo la reli kwani linaleta msongamano wa malori Dar es Salaam na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme hakuna sababu ya mgao kila siku, fumbeni macho kwa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Songea *tank* la mafuta tu pale *airport* mpaka leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu Elimu, Afya na Maji. Kwa kuwa tulishawekeza sana kwenye majengo ya elimu, ni vema kufuatilia ubora wa elimu na Zahanati. *Actually* hapa ndipo kwenye maboresho ya rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia haya mabo moja, mbili na tatu yanategemeana sana. Nasema kwa mwaka huu wa uchaguzi nyie malizeni mambo yaliyoanzwa kwenye maeneo mengine bila kuongeza mapya kwanza. Jipya liwe ni uchaguzi Mkuu tu ni rahisi hata kufuatilia na kuona *progress*. *MSMES* watakuwa wamejengewa mazingira mazuri. Pia utaratibu wa kujadili mipango uboreshwe kama Kamati ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina zaidi, naunga mkono hoja, CCM idumu na iendelee kuongoza chini ya Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini ninayo maoni machache:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni vipaumble. Katika uboreshaji wa Miundombinu tumeacha suala la Miundombinu ya mawasiliano (simu na posta). Baada ya Ujenzi wa mkongo wa Taifa, ili uwe na maana na kuleta tija unaendana na ujenzi wa *infrastructures* mbalimbali, uboreshaji wa *communication information technology counter part finding* kwa miradi ya pamoja kati ya Serikali na Mashirika/Makampuni makubwa ya *information technology*. Uboreshwaji huo ndio utakaotoa nafasi kwa wananchi kutumia fursa zitokanazo na *ICT*, kufanya biashara na kuongeza tija kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, utafiti. Tunaongea tu lakini hatutendi. Nchi ukitaka iendelee lazima itoe uzito katika tafiti mbalimbali zenye tija na zitakazoleta mageuzi makubwa katika fani ya sayansi, fani ambayo inayo nafasi kubwa katika kuchangia uchumi wetu iwapo tutawekeza ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais aliahidi kutoa asilimia moja ya *GDP* iende katika fani ya *Research* – hatujaona matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watafiti sasa wanatumia *technology* kwa kuzalisha nafaka ambazo zinadumu na kutoliwa na wadudu. Watafiti wetu bado hawajawezeshwa kutumia nafasi yao kufanya utafiti na kusaidia nchi kuondoka hapa tulipo na kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni ubunifu. Hivi tunaona aibu gani kutoa *priority* katika eneo hili. Hadi lini tataendelea kutegemea nchi za wenzetu kununua matrekta, magari, vifaa vya umwagiliaji na kadhalika. Tunayo nafsi kubwa ya kuwasaidia wabunifu wetu kwa kulipa *priority* suala la ubunifu. Watafiti na wabunifu wa ndani wakishirikiana na wa nje wakiwezeshwa na kupewa kipaumbele wanaweza kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya viwanda, kilimo na afya. Tuanze sasa tusiseme tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni kuhusu uboreshaji mkubwa wa Kigoma *port* na reli yake ili ku – *capture* mizigo ya nchi za jirani.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa mpango wa maendeleo ya nchi umejikita katika programu zifuatazo: (a) Mpango wa kati na (b) Mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo makuu yaliyozingatiwa katika programu hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;
2. Maendeleo ya Milenia;
3. Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005; na
4. Mkukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa undani malengo yaliyowekwa katika mipango yote hiyo yametajwa kwa muhtasari katika malengo ya Mkukuta. Mipango iliyotangulia inatoa mchanganuo kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa mipango tulijoipangia bado nchi yetu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Upungufu wa chakula nchini;
2. Upungufu wa Umeme;

3. Kushuka kwa Viwango vya Elimu;
4. Uhaba wa upatikanaji wa Maji;
5. Miundombinu mibovu na iliyochakaa;
6. Utawala bora na Uwajibikaji; na
7. Mabadiliko ya Tabia Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUKUTA Na. I uliasisiwa 2006. Tokea wakati huo Serikali imejikita kutekeleza malengo ya MKUKUTA. Tumeelezwa mafanikio na changamoto zake, lakini naona changamoto ya kwanza ya MKUKUTA ni kutoeleweka ipasavyo mipango yake ndani ya Jamii. Tofauti na ilivyokuwa Azimio la Arusha ambapo Waasisi wake walihakikisha kwamba jamii inalifahamu Azimio ipasavyo na kwamba kila Mtanzania kwa nafasi yake alikuwa na fursa ya kushiriki katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba ni lazima jamii ielimishwe ipasavyo kuhusu dhana nzima ya MKUKUTA Namba II ili kila mtu afahamu na awe na nafasi ya kushiriki katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, bado Serikali haijatupa tathmini ya kina ya utekelezaji wa Mkukuta Namba I. Serikali inapaswa kutwambia katika utekelezaji wa vipaumbele tulivyojiwekea tumevitekeleza kwa asilimia ngapi. Hii itatupa fursa ya kujua ni vipaumbele gani tuendelee kuwa navyo na vipi vya kuvacha njiani kwa kuzingatia hatua za utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni tatizo la Serikali kutokuwa na uwezo au kutotilia maanani utabiri wa hali ya hewa duniani (*forecast*), majanga mbalimbali kama mafuriko, ukame na kadhalika. Kutotumia vyema taarifa za utabiri wa hali ya hewa kunapelekeea kukumbwa na majanga hayo bila ya kuwa na mbinu za kujinasua mapema iwezekanavyo. Ni dhahiri sasa Serikali ijikite katika kutumia taarifa mbalimbali za tabiri za hali ya hewa tuweze kujiweka tayari kuyakabili ipasavyo yanapotokea bila kuathiri uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ni tatizo la kutokuwa na Tume ya Taifa ya Mipango. Kuwa na Tume ya Mipango ni jambo la msingi sana. Tume hii itakuwa na majukumu ya kuandaa mipango ya Serikali katika viwango vya muda mrefu na vile vya muda wa kati. Tume ndio itapanga vipaumbele ambavyo Serikali itavipangia mikakati ya utekelezaji.

Kadhalika, itakuwa inatoa tathmini ya mwaka hadi mwaka wa utekelezaji wa vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja sasa kwa Serikali kuunda Tume ya Mipango ya nchi ambayo itakuwa imetamkwa kwenye Katiba yetu.

MHE. MWANTUMU B. MAHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mpango wa kuleta Bungeni vipaumbele vya bajeti. Hata hivyo inashangaza kuona Elimu imeondolewa katika kipaumble cha awali, jambo hili linashangaza. Madarasa yaliyojengwa hayajakamilika, shule hizo hazina majengo ya utawala, hakuna maabara, maktaba na nyumba za walimu hakuna za kutosha. Vitabu na vifaa vya kufundishia havitoshi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, tukamilishe kazi tulioianza ili tuweze kusonga mbele. Endapo tutaacha na kubadili kama mlivyoonyesha, basi tusitarajie maajabu katika elimu. Shule bila maabara si shule ni kubangaiza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kwanza bila elimu ya kutosha tusitarajie ufanisi. nawaomba tuwekeze zaidi katika elimu. Nawatakia heri.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kupongeza Wizara kwa kuleta mwongozo huu. Maoni yangu ni kwamba:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kilimo kwanza na maendeleo ya mifugo kipaumbele cha I. Kipaumbele kiwe kilimo kwa sababu ni chakula. Nchi ikiwa na kilimo kizuri chakula kitakuwepo na watu watakuwa na Afya nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, maji na umwagiliaji. Maji yanaendana na kilimo, bila maji huwezi kuishi kwa hiyo maji ni kipaumbele cha pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha tatu ni huduma za Jamii, Afya, Elimu. Huduma hizi ndizo zinazostawisha jamii (binadamu). Kwa hiyo, huduma za jamii ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha nne ni Viwanda haswa vya kusindika chakula ili kuleta ubora zaidi. Viwanda vya kusindika vyakula huendana na kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumble cha tano ni miundombinu, barabara, Reli, Bandari, Viwanja vya ndege na Nishati. Hivi ni kwa ajili ya kuleta uchumi. Miundombinu ni muhimu sana kwa kuleta uchumi, unatafuta uchumi ili uzalishe zaidi. Kwa mfano, tuchukue nishati tukitumia rasilimali ya chuma cha Liganga au mali ya Mchuchuma ni rasilimali kubwa ya kuleta uchumi, au Bandari. Bandari peke yake ni uchumi mkubwa sana kwani tutafanya biashara na Rwanda, Burundi, Malawi na nchi zote za Afrika ya kati ambazo hazina Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa tukiangalia bandari ya Dar es Salaam utaona kuwa ina mzigo mkubwa, kazi haiendi kwa sababu imeja sana. Sasa ni wakati wa kuongeza bandari zingine, kwa bahati nzuri Tanzania tuna uhakika wa kupata mwambao wa Bahari mzuri wa kutengeza bandari, Bagamoyo, Tanga, Mtwara na Lindi. Mfano, hivi sasa bandari ya Mtwara ina uwezo mkubwa sana wa kuhudumia meli na vile

vile ni njia ya mkato ya kutoka Tanzania kwenda Afrika ya kusini. Kwa hiyo, Mtwara ni Bandari nzuri kwa kufanya biashara, kwa hivyo miundombinu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono kwa asilimia mia moja.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Bariadi Magharibi, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hoja yake aliyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa na niharakishe kusema hapa kuwa naiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukweli kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi iliyopelekewa hoja hiyo ambayo taarifa yake imewasilishwa asubuhi ya leo na Mwenyekiti wa Kamati yetu, napenda kuongeza maeneo machache ili kukazia hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kanuni ya 94 ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo inasimamiwa na Ibara ya 63(3)(c) ambayo inasema: “Kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.”

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Serikali kwa tafsiri yake hiyo ndiyo inayozingatia Katiba *that is* Serikali kupitia mpango wake wa muda mrefu au mfupi (Serikali iliamua kuondokana na mpango wa muda mrefu kama ilivyokuwa huko nyuma) na kutumia *Medium Term Expenditure Framework* ya miaka mitatu mitatu.

Hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, kinachopaswa kuletwa Bungeni ni mapendekezo kuhusu Mwongozo wa utayarishaji wa mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha unaofuata 2010/11 – 2012/13. kwa maana hiyo, Bunge likikaa kama Kamati ya Mipango linapaswa lijadili na kuidhinisha mapendekezo yanayowasilishwa kwake na Serikali. Yawezekana kabisa muda uliowekwa na kanuni ya 94 *that is* Mwezi wa Februari na kuisogea mbele hadi mwezi wa Aprili kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni lile la vipaumbele. Naungana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliosema kuwa ni vingi mno. Nashauri *emphasis* yetu iendelee kubaki katika Miundombinu kwa maana ya reli, bandari, barabara, viwanja, umeme, kilimo katika dhana pana ya inayojumuisha mifugo na uvuvi, Walimu, Afya na Maji. Kama tunaona ipo haja ya kuongeza Ardhi na Viwanda iwe ni kwa maelewano kwamba kwa upande wa ardhi kuongeza kasi ya ya upimaji wa ardhi ya vijiji ili kuharakisha upatikanaji wa hati miliki za ardhi na hivyo *indirectly to empower our people in the rural areas*. Kwa upande wa Viwanda kwa maana ya kuendelea kutekeleza mpango wa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya shughuli za viwanda, kilimo, utalii na TEKNOHAMA na kujengea mazingira mazuri yatakayowezesha sekta binafsi (*Public Private Partnership*) ili kusaidia kuharakisha maendeleo ya sekta binafsi na hivyo kuongeza mchango wake katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isiwe kigeugeu katika vipaumbele tulivyojiwekea kwa kubadili badili vipaumbele na mikakati ya utekelezaji katika kila mwaka wa bajeti. Iwe hivyo hivyo kwa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara Tanzania (MKUMBITA).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwengine huwa na wasiwasi kama kubadili badili vipaumbele na mikakati yetu siyo *Conspiracy* ya washindani wetu ili tubaki nyuma na wao wapige hatua mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo katika mapana yake naamini kwa kuandaa nguzo kumi za mapinduzi ya kijani tumeanza vizuri. Changamoto zilizopo, ni kusimamia kwa karibu utekelezaji wake, pamoja na upatikanaji wa rasilimali ardhi kwa ajili ya wawekezaji wakubwa wa ndani na wale wa kutoka nje. Tusipokuwa makini ardhi yote nchini itageuzwa kuwa ardhi ya vijiji. Tusitumie kisingizio cha *administrative boundaries* ya vijiji ndani ya Wilaya na Mkoa kugeuza ardhi yote kuwa ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa *to put to productive use* ardhi kubwa inayomilikiwa na Serikali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa na Magereza ambayo sasa ni *idle* ili kupitia *joint ventures* na wawekezaji, ardhi hiyo iendelezwе kikamilifu na kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa H. Mkullo; Naibu Waziri Mheshimiwa Sumari, Naibu Waziri; Mheshimiwa Yusuph Mzee, Naibu Waziri; Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa mpango huu wa bajeti bila kuwasahau Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Abdala Kigoda na Kamati yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa michango yao ya pamoja ndiyo iliyowezesha mpango huu wa bajeti kuwasilishwa leo hapa Bungeni, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti izingatie hali ya uchumi wa kila mkoa. Ni ukweli usiofichika kuwa hali ya uchumi wa kila mkoa unapishana sana kupitia takwimu zinazotolewa. Mimi huwa nasikitika sana ninapoona bajeti za mikoa iliyoendelea ni kubwa na mikoa ambayo ipo chini kiuchumi ni ndogo. Naishauri Serikali iwe inapata takwimu sahihi ili huduma kubwa ipewe mikoa yenye uchumi duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iwe ya kumwinua mwananchi mwenye kipato duni. Ni imani yangu utaungana na mimi kuwa mara zote bajeti imekuwa inampa unaafuu wa maisha mwananchi wa chini kwa kiasi kidogo sana, kwani hata pale anapozalisha faida yake ni ndogo sana mfano, wakulima wa Singida wa mazao ya vitunguu, alizeti, dengu, pamba, ufuta, mbogamboga na kadhalika. mazao haya hununuliwa kwa bei ya

chini sana kwani wengi wao hawana uwezo wa kusafirisha. Hivyo ni vyema Serikali inawatafutia soko au kutenga fedha za kuwafidia, bei inakuwa ya chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti itoe kipaumbele cha miundombinu. Suala la miundombinu ni kikwazo sana kwa wananchi mfano, barabara, reli na kadhalika, mfano, Halmashauri zinapopewa jukumu la barabara wakati vyanzo vyao ni vidogo, ama barabara zinapopandishwa daraja wakati wakala wa barabara wa mkoa hana bajeti. Hapo mtumiaji huteseka muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vya Serikali. Ni kweli Serikali inajitahidi sana kujiletea maendeleo, bali vipaumbele vinakuwa vingi sana karibu kila mwaka unakuwa na kipaumbele wakati kipaumbele kingine hakijawa na tija kwa Watanzania. Nashauri tunapokuwa na kipaumbele kimoja au viwili basi tuhakikishe tumefikia hatua nzuri kama sio kukamilisha mfano Maji, Elimu, Afya, Miundombinu na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, riba kwenye mabenki na *NGO*'s. Vilevile benki zetu bado hazimsaidii mwananchi wa chini kwani matawi mengi yapo mijini, riba ni kubwa na haimjui mteja maskini. Naishauri Serikali itazame uwezekano wa kumpa nafuu, mwananchi maskini kwa maana ya kupunguza riba na kumsogezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuangalia uwiano wa faida, bado kuna tatizo kubwa sana katika kutoa fidia sawa kwa watu wafuatao: Mzalishaji, mtumiaji au mfanyabiashara. Naomba Serikali itoe haki sawa kwani mara nyingi kati ya watu watatu mzalishaji hupata faida, mtumiaji hana faida bali muuzaji ndiye anayefaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo la huduma ya pembejeo kwa wakulima, kwani wananchi wetu hawana uwezo wa kulingana. Hivyo, naishauri Serikali kwamba, pembejeo kila mwananchi apate kwa wakati inayolingana na uwezo wake, vile vile wakopeshwe walipe baada ya mavuno.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya wafanyakazi yaboreshwe. Ni ukweli usiojificha wafanyakazi wote wanafanya kazi kubwa sana bali utendaji wao hufifia pale maslahi yao inaposhindikana kuboreshwa na hali hiyo itaondoa tatizo kubwa wafanyakazi kutoa au kupokea rushwa. Ninaposema Maslahi nini maana ya mishahara na stahili zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee kuhusu maliasili tulizonazo ndani ya nchi. Nchi yetu ina maliasili nyingi sana mfano madini, wanyama, misitu, vivutio vya utalii, mazao na kadhalika, nchi yetu ina maliasili nyingi sana bali uzalishaji wetu kuitia vyanzo hivyo ni duni sana, tunawanufaisha sana wawekezaji na wengi wao ni kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu takwimu. Naiomba Serikali iweke utaratibu wa kuweka takwimu za uzalishaji wetu mfano, Mkoa wa Singida kila mnada ng'ombe wenye uzito gani wameuzwa, kuku kila siku wangapi wameuzwa, vitunguu wakati wa msimu kila ziku vinauzwa vya kilogramu ngapi, hivyo hivyo kwa kila bidhaa tuliyonayo

na uzalishaji wake, hapo tutapata *data* za kila mkoa kwa usahihi. Hii iendane na takwimu zingine mfano, watoto yatima, waishio mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti kwa makandarasi. Wakandarasi wengi wanatucheleweshea maendeleo pia wanatuletea hasara kwani wengi wao hawatekelezi masharti ya mikataba hasa ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magari ya thamani kwa viongozi na watendaji wakuu. Ni ukweli kuwa viongozi na watendaji wakuu wa Serikali wanatumia bajeti kubwa sana kwa magari ya mara kwa mara kubadilisha, ukarabati wa nyumba kila anapohamia nyumba ya Serikali hata kama sio chakavu, vilevile thamani za nyumba anapohamia kwa mara ya kwanza kwenye nyumba hiyo hata kama zipo anasema sio chaguo lake. Hili Serikali itazame upya. Hii itasaidia fedha kufanya kazi zenyé maslahi na jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii nikiwa na imani kuwa hoja zangu zitachukuliwa.

MHE. CASTOR B. LIGALLAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara kwa mapendekezo mazuri ya vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu kilimo na maendeleo ya mifugo. Kama tulivyoainisha katika azma ya Kilimo Kwanza, kilimo tunachokusudia kuweka kama kipaumbele ni kilimo cha umwagiliaji, chenye kutumia mbegu bora, mbolea, zana za kisasa za kilimo na utaalam wa kisasa na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi iko mikoa ambayo ina fursa ya kuwa na rasilimali muhimu kwa utekelezaji wa kilimo kama vile ardhi yenyé rutuba, maji mengi na hali ya hewa nzuri. Kwa hiyo mikoa hiyo ipewe kipaumbele kwa kuzalisha mazao ya chakula kwa wingi, kwa kutengewa ruzuku ya pembejeo za kilimo, kujengewa miundombinu ya umwagiliaji na kuwekewa mazingira rahisi ya kuweza kukopeshwa kwa masharti nafuu.

Kwa mfano mikoa sita ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Morogoro na Kigoma wapewe bajeti kubwa ya kilimo ili mchango wa mikoa hiyo iwe na *impact* kuliko kutawanya fedha nchi nzima kidogo kidogo na hatimaye kukosa *impact*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu miundombinu. Uzalishaji lazima uendane na masoko. Popote penye uzalishaji mkubwa lazima masoko yataibuka, kuna hitaji la kuuza mazao. Barabara hifuata bidhaa. Uzalishaji wa mazao asipoweza kuza mazao yake aliyozalisha hatutaweza kumwendeleza mkulima huyo. Kwa hiyo kama tutachochaea uzalishaji katika mikoa hiyo sita, kipaumbele cha pili katika maeneo hayo iwe ni barabara ili wakulima hao waweze kwenda kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu nishati. Nishati ni muhimu sana kama kichocheo kingine ambacho kinaendana na mlolongo wa kuchochea uzalishaji wa chakula au mazao katika eneo fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati inachochea uzalishaji wa viwanda vidogo na vikubwa. Katika vijiji viwanda hivi vitaongeza thamani ya mazao yanayozalishwa kule kule kijijini na kuweza kuuza kwenye soko unga wa mahindi badala ya mahindi, au mchele badala ya mpunga, juisi ya maembe badala ya maembe *raw*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi bila chakula haiwezi kuwa na amani. Hebu tujaribu kwa makusudi kwa mikoa hiyo inayolisha nchi tuipe bajeti ya kutosha kutekeleza kilimo kwanza, fedha za kuweza kujenga miundombinu ya barabara za lami na tuhakikishe kila mkoa unapata umeme na baada ya miaka mitatu tutaona *impact* yake. Kwa kusema hivi sina maana bajeti yote iende katika mikoa hiyo, lakini nina maana asilimia kubwa ya kila *budget* ya sekta iende huko ili nchi ijihakikishie usalama wa chakula na mengine yatafuata. Kilimo ninachoongelea ni cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni kuhusu huduma za jamii. Sina tatizo na kipaumbele cha huduma za jamii, isipokuwa huduma ya maji ipande juu kwenye kilimo ili kipaumbele hiki cha maji kiungane na kile cha umwagiliaji kwa sababu kilimo ni maji na umwagiliaji pia ni maji.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutuletea mwongozo huu. Ni jambo la busara kwa Bunge kupitia mwongozo wa bajeti lakini ni muhimu kuangalia kanuni inatuelekeza nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la kilimo ambalo ni sehemu ya uti wa mgongo wa maendeleo yetu. Ni vyema Serikali iangalie itawasaidiae wananchi wa vijijini kwa kuwapatia hati za kimila ili iwe rahisi kwao kupata mikopo, iwe matrekta, pembejeo na kadhalika. Ili kilimo hicho kiwe na tija kuna haja ya kuweka utaratibu wa kuongeza na kufufua viwanda ambavyo mazao yatakayovunwa yatapelekwa viwandani. Hii itasaidia wakulima wetu na nchi kuingia katika ushindani na hasa tunavyotaka kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna umuhimu wa kuimarisha barabara zetu ambazo zitatuwezesha kurahisisha uchumi wetu kwa nchi nzima mathalan Dar es salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Mtwara, Lindi na Pwani. Mbali ya kurahisisha usafiri wa watu na biashara. Vile vile utawezesha kufanya biashara na nchi jirani, bandari na viwanja vya ndege vitafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila huduma bora ya afya na maji bado kutakuwa na tatizo katika maendeleo ya nchi yetu. Yote haya yakizingatiwa tutakuwa tumepiga hatua katika mwongozo wetu.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake wawili kwa kuleta hoja hii

Bungeni ili Wabunge waichangie kabla ya kutengeneza bajeti kamili. Sina hakika kuwa michango ya Wabunge itatiliwa maanani katika bajeti maana Serikali haina utamaduni wa kutekeleza hata zile ahadi zake yenyewe seuze zile ambazo wameshauriwa. Hivyo Serikali haina umaskini wa mipango bali mapungufu makubwa yapo katika utekelezaji wa mipango yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sote tunakubaliana kuwa hakuna mkulima atalima kwa ufanisi bila kukopa tena katika Benki ya Kilimo yenyeye masharti nafuu na riba ndogo. Lakini bado tunaendelea kuimba tu hatujaona Benki ya Wakulima. Hivyo tunahitaji Benki ya Kilimo leo wala sio kesho na kwa kuwa hatuna (sisi wakulima) rasilimali pesa, zana bora na kujikita katika kilimo cha umwagiliaji tija inashuka na tunaendelea kuzungumzia vifaa kila mwaka jambo hili linaongezeka *inflation* na hivyo maisha yanakuwa ya tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapendekezo ya vipaumbele, naipongeza Serikali kwa kuchagua vipaumbele vichache na kilimo kuwa cha kwanza. Katika mtikisiko wa uchumi ulioikumba dunia suala la Tanzania kujikita katika Kilimo ni la umuhimu wa pekee. Kilimo hicho sio tu kwa kulisha watu wetu lakini pia tusafirishe nje ya nchi na uwezo huo tunao. Lakini cha kushangaza ni kuwa Kilimo ni cha kwanza katika mapendekezo ya Vipaumbele, sawa, lakini kwa nini Maji imewekwa nafasi ya tatu tukijua kuwa kilimo hakiwezi kufanikiwa bila ya maji. Kwa hivyo, kilimo na maji lazima, vyote viende pamoja, vinginevyo bila maji hakuna kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hekta 2.3 milioni zenyne uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa. Eneo hili lina uwezo wa kuzalisha tani 11.5 milioni za mpunga sawa na tani 8.0 milioni za mchele. Hii itapatikana kwa kulima mara moja tu. Tukiweza kulima mara mbili tutapata tani 16.0 milioni ikiwa mahitaji ya mchele kwa mwaka ni tani laki sita (600,000). Hivyo tuna ziada ya tani 15.4 milioni kwa mwaka ambazo zinaweza kuuzwa nchi jirani zenyne njaa tena kwa bei nzuri. Tunaweza kufanya hivyo kwa nafaka zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua na lazima tufanye maamuzi magumu ikiwa tunataka tuendelee. Ahsante.

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi hoja ya Mpango wa Bajeti ya Serikali 2010/11-2013. Nampongeza Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango iwe ya muda wakati na muda mrefu na pia kuwe na vipaumbele, ambavyo tunahitaji kuvitekeleza ili kufikia mipango tuliojipangia. Kilimo ndio njia pekee ya kuinua uchumi wetu, lakini tujiulize, baada ya kupata mafanikio katika kilimo, soko la mauzo ya bidhaa hizo lipo? Lakini hebu, tuangalie sekta ambazo zinatakiwa, kuboreshwa sambamba nacho, miundombinu ni muhimu na dhamira ya kujenga na kuunganisha barabara za Mikoa kwa kiwango cha lami, tunaweza kusaidia

wakulima kuuza kwa urahisi, mkoa kwa mkoa na nchi jirani zitatumia barabara kibiashara na kuinua uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka jana elimu ndio ilikuwa kipaumbele na tumefanikiwa, lakini hatujafanikiwa katika kukamilisha baadhi ya matatizo kwa mfano, nyumba za Walimu, Maabara, vitabu, Walimu na kadhalika ili kukamilisha mpango huu wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari zetu ziangaliwe na kuboreshwa, tusiwe tunazungumza na kujadili tu, ziboreshw sambamba na Reli zetu, ifike mahali kuwe na utekelezaji. Kwa kweli tuko nyuma katika kuweka mipango na kujipanga katika ushindani wa kibiashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwaondolea wananchi tatizo la usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya mambo katika sekta muhimu, mfano sekta ya Afya. Pamoja na juhudi za Serikali kuiboresha Afya lakini bado Zahanati na Hospitali hazipo katika viwango vinavyostahili na vile vile kuna upungufu wa Madaktari.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii muhimu iliyo mbele yetu. Pili, naomba nichukue fursa kutoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na maafa kupitia mvua kubwa ambayo zimesababisha mafuriko na kusababisha hitilafu kubwa za miundombinu katika makazi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pole sana kwa wananchi wa Zanzibar kwa matatizo makubwa ya Umeme ambayo yamesababisha kushuka kwa uchumi wa Zanzibar na watu wake, hasa kwa akina mama amba ni wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika hili ni kuunga mkono hoja hii hasa kwa kuanzia na kilimo kwanza, kwa sababu uchumi wa nchi hii hauwezi kukua kwa kuchangiwa na asilimia thelathini na kuacha asilimia ya wakulima amba ni asilimia sabini. Katika hili lazima kilimo hicho kiambatane na viwanda vidogo vidogo ambavyo vitasindika na kuuza nje ambapo ongezeko la fedha za kigeni litakuwa ni kitu cha kuchagua. Sambamba na hili lazima kilimo chetu kiendane na *irrigation* ambapo fedha tutakazozivekeza zitakuwa na uhakika wa kurudi kwani kilimo ni maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi huu tunaoujadili hapa lazima tufahamu ni endelevu, tusitegemee tunapopanga mwongozo huu *impact* yake tutaipata kesho au mtongogoo, ni lazima tuelewe hapa tunapanga nini na kipaumbele chetu ni nini? Balozi SATO alisema: “Tanzania itapiga hatua ya haraka kiuchumi ikitoa kipaumbele katika Kilimo”. Maana ya lugha, tuichukulie lugha hii kwa kuichambua na tafsiri yake itafaa katika kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukua kwa uchumi lazima pia tusome kutoka kwa wenzetu duniani, tuijulize, Malasyia wamepiga hatua vipi? Indonesia wamefanyaje mpaka hapo walipo? China wapo watu robo ya dunia lakini hawafi njaa, hawaagizi

chakula na wanasaadia wengine, jawabu tutalipata. Katika hatua hii mtazamo wetu lazima uangalie na kuboresha Bandari, *Airport* na Reli, tukifanya hivyo tutafika katika uchumi wa kisasa ingawa sio leo au kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa mchango wangu naomba Watanzania tupunguze maneno na tuthubutu kutekeleza yale tunayopanga kinadharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika misamaha ya kodi lazima iangaliwe upya, kwa sababu inapunguza mapato ya ndani kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado suala la utawala ndani ya Serikali haujawa mzuri kwa baadhi ya taasisi, ambapo kuna wafanyakazi hewa. Hili hatuliangalii kama ni tatizo kitu ambacho mabilioni yanaliwa bila jasho wakati fedha hizo zingechangia bajeti ya matumizi ya Serikali.

MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA: ili bajeti iweze kwenda vizuri lazima tuwe na mtazamo wa kufikia kile kitu ambacho kinatupa maendeleo ya haraka katika nchi yetu kutokana na mazingira na vitu ambavyo ni asilia Mungu ametujalia. Kwa hivyo basi, rasilimali watu ukizingatia na mazingira alisia inahitajika, pamoja na teknolojia nzuri ambayo itatusaidia kufanikisha malengo yetu. Kwa mfano, unataka kuhamisha chakula toka Kilwa kuja Dar es Salaam utafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi kwa mtazamo, kwa kuwa mazingira alisia yapo, tatizo tulilokuwa nalo ni rasilimali watu na teknolojia. Kwa hali ya kawaida, rasilimali watu tunayo ila hawana ujuzi wa jinsi gain ya kutumia maliasili tuliyonayo na pia wanakosa au hawana vifaa vyta kisasa ambavyo vingesaidia kurahisisha shughuli au kazi zote ambazo zingefanyika kwa ustadi mkubwa. Kwa hiyo basi, mazingira asilia yote lazima tuyatumie ipasavyo, tukizingatia zaidi rasilimali watu pamoja na teknolojia ili kuondoa au kupunguza ujinga, maradhi na umaskini tulionao katika nchi yetu (Tanzania).

Mheshimiwa Naibu Spika, nini tufanye sasa? Elimu jinsi ya kutumia maliasili zote tulizonazo ni lazima itolewe kwa wananchi wote hasa kwa wale wanaokaa au kuishi sehemu zenye uoto huo wa asili, mfano, misitu na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kutunza na pia kulinda uoto wa asili tulionao. Pia Serikali, kupitia Wizara yake ya Miundombinu, lazima iwe na Bajeti nzuri hasa kwenye vifaa vyta kisasa zaidi ambavyo vitatumika au kutumiwa na wananchi kwenye suala zima la kukuza na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo basi, elimu pia inahitajika kutolewa kwa rasilimali watu kuhusu jinsi ya kutumia vifaa hivyo maalum na vyta kisasa zaidi. Pia matumizi ya vifaa vyta kisasa lazima yaangaliwe kwa undani zaidi ili kurahisisha shughuli zote za maendeleo. Kwa mfano, ukienda nchi za Ulaya samaki wa kopo wanapatikana kwa wingi sana, wakati sisi hapa tuna bahari, ina samaki wa kila aina ila tunashindwa kuwahifadhi.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi kutoa maoni yangu. Kamati ya *PAC* tulitembelea Uganda, tumejifunza mambo mengi kuhusu bajeti, wana bajeti ya wakati na bajeti endelevu, ni kila mwaka na ndio maana

mambo yao mazuri. Pamoja na mipango mizuri je, kwa nini tusiwe tunaiga nchi za wenzetu tukaachana na matatizo kulinganisha na rasilimali tulizonazo hapa nchini? Tunacheckwa na majirani zetu hata matatizo yasingekuwa yanatupata kwa mfano, ukosefu wa madawa hospitali, malipo ya wastaafu, Madaktari, Walimu migomo mara kwa mara, itafika mahali hawa wageni tunaowaita wawekezaji watatucheka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajua idadi ya rasilimali zetu hapa nchini, tukihojiwa sisi Watanzania je, tunazijua pamoja na mahali zilipo? Lakini tunaowakaribisha wanajua, kwani Serengeti tuliambiwa yule mwekezaji anasafirisha wanyama wetu pamoja na mayai ya mbuni wanatwambia kule kwao ameshakuwa na mbuga inaitwa Serengeti.

Yote hayo ni kutokana na sisi wenyewe ambao tuna uchungu na rasilimali zetu kutokuwa na uwezo wa kujiwekeza. Sasa tuzinduke watoto wetu watatupiga, wanasomea nje, sasa tuna kauli mbiu kilimo kwanza, sasa imekuwa wimbo kila siku, bajeti hii kweli itaweza kukidhi mahitaji ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia nchi yetu ilivyo na wananchi wetu hasa walivyo maskini jembe la mkono litasaidia nini au ndio hivyo vy a bajeti yetu inayolenga miaka mitano tu, je, itaweza kununua matrekta? Mikoa mingapi inahitaji pembejeo mbolea? Je, tutaweza au ndio tutegemee pesa za wahisani na je sisi tuna nusu au robo tatu tupate pa kuanzia? Naomba kujua. Hivi tunakwenda kwenye soko la pamoja sisi watanzania wenyewe rasilimali nydingi tumejiandaa vipi pamoja na wenzetu au tutakua wasindikizaji tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili soko ni zuri lakini tuwe makini nalo sana tusije tukauza nchi yetu bila kujua kwa ajili ya bajeti yetu ambayo tunapitisha bila kufikiria au kujifunza wapi tumekosea na wapi pa kurekebisha. Dalili naziona kutokana na nchi ya Uganda wanavyotuvamia na ndizi pamoja na Kahawa, sisi tunawauzia bei ya chini wenyewe wanaauza bei ya juu sana kulingana na wenyewe wana kiwanja cha ndege kikubwa, wanapeleka nje. Hapa nashauri tuwe makini, tuwe na mipango na mikakati ya kukuza uchumi sio kama MKUKUTA na MKURABITA, kwa hiyo, tusije na haya tunayoyapanga ya kilimo kwanza yakaishia hapo hapo kwenye vitabu kwani uchaguzi unakaribia tutaulizwa haya, je, tutajibu nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuingie kwenye elimu. Wimbo wa elimu ni kipaumbele wakati tunakuwa na kitabu kimoja, hapa mmechemsha kweli kweli. Kwa wazazi ambao uwezo wao ni mdogo hawawezi kuwapeleka watoto katika shule za jirani zetu, je, tunawatakia heri? Tuangalie sana tusirudi kwenye mikataba hewa kama tulikotoka na tutumie vizuri rasilimali zetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichanganue mambo muhimu kabisa ambayo yananisumbua sana kuona tunaondoka miaka mitano bila kukamilisha mambo tunayoyaimba ndani ya Bunge hata kinachokamilika hakipo kabisa na vyanzo tunavyo ila twaleta mchezo wa ukusanyaji usio mzuri. Mimi niko *PAC*, ukiangalia vitabu vy *CAG* unakuta misamaha mingi kwenye makampuni binafsi kwanini tuwasamehe na ndio

paumbele vyetu vya kutuingizia mapato? Madini tunawachimbaji wadogo wadogo, Serikali iwatafutie zana za kisasa hata wenyewe wachangie uchumi wetu hasa Rais anakotembea kwa nchi rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele mimi kwa mawazo yangu, ukusanyaji mapato kwenye nchi yetu uongezwe, tupunguze misamaha, Kilimo kwanza, elimu miundombinu, iongezwe. Bandari ya Mtwara, Tanga, Kigoma na barabara ambavyo vinakwamisha maendeleo viboreshwe. Kwa mfano, tukiboresha bandari hizi wawekezaji tusiwape uhuru wa kutosha, tunaibiwa tunaona, tuache kulala, tuamke, nchi yetu ni tajiri sana, tuna rasilimali nydingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tumechoka na mikataba mibovu hasa wa reli, tumechoka kwa Watanzania umekuwa wimbo hapa nchini, kwani Serikali inashindwa nini kuendesha yenewe? Kwa hayo, naomba yachukuliwe yalivyo, ni matakwa ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watumishi wote kwa kutuhusisha kwenye bajeti.

MHE. MARGARETH S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa mpango mzuri, naomba Kilimo kwanza kiwafikie akina mama vijijini amba ni asilimia sabini ya wanaolima. Pia ziwafikie na pembejeo ikiwa ni pamoja na teknolojia rahisi za kulima.

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkulo, na Manaibu wake Mheshimiwa Sumari na Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee pamoja na viongozi watendaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kazi hii nzuri. Sh. Bilioni kumi na tisa siyo kiasi kidogo na naishukuru Serikali kwa uamuzi huu muafaka. Uamuzi wa kuzipeleka *TIB* kuendeleza Kilimo ni muafaka hasa wakati huu wa kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo yapo malalamiko ya wakulima kwamba kiwango cha chini cha kuweka fedha cha asilimia 20 ni kikubwa mno maana kiwango cha *Tanzania Agricultural Input Trust Fund* na *FBME Bank* cha asilimia 10. Wakulima wa Jimbo langu kuititia *DEMACO* walishaweka shilingi milioni tano kwenye *SACCOS* zao (kama *MALINYI SACCOS*) ili wapate mkopo wa Matrektta, lakini sasa kutookana na uamuzi wa Wizara ya Fedha na Uchumi wa asilimia 20, nina maana waongeze tena shilingi milioni tano zaidi.

Jambo hili kwa wakati huu wakulima wanapalilia mashamba yao ya mpunga na mahindi haliwezekani, kwa hiyo, hawana uwezo wa kuongeza kiasi hicho. Nashauri *TIB* hii hasa kwa “Dirisha la Mikopo ya Kilimo” itoe mikopo yenyenye masharti nafuu zaidi kuliko kile cha mabenki ya biashara. Kwa mantiki hii natoa mapendekezo ya kupunguza riba na masharti.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mhe Mustafa Mkulo pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuutayarisha mwongozo wa mpango tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni muhimu sana wananchi wengi wa kawaida wanufaika na taarifa zenyelugha nyepesi zinazoeleza mafanikio tuliyofikia ya malengo ya maendeleo ya milenia. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anajibu hoja za michango ya Waheshimiwa Wabunge aeleze ni asilimia ngapi (wastani) tumefanikiwa kwa kila lengo la milenia, kama yalivyoorodheshwa ukurasa wa pili (2) wa ripoti aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri Bungeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya MKUKUTA napenda kumjulisha Mheshimiwa Waziri kuwa bado kuna udhaifu mkubwa wa kufikisha elimu ya kuandika au maandiko kwa vikundi vyatayari vya wananchi wa ngazi ya chini. Udfaifu huu ndio husababisha vikundi vingi kukosa mikopo inayotolewa na mifuko mingi ya fedha za Serikali zilizotengwa kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vidogo vidogo.

Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inabidi iwasimamie kwa umakini mkubwa Maafisa Maendeleo na kuwafuatilia kwa karibu zaidi ili kuhakikisha wanatimiza kazi yao. Vinginevyo wananchi wadogo wadogo wataendelea kukosa mikopo na kulalamika kuwa wanabaguliwa kwa kunyimwa mikopo inayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuiwezesha *TIB* kuwa Benki inayotoa mikopo kwa ajili ya miradi ya kilimo, napendekeza itengeti mafungu matatu ya mikopo. Yaani fungu moja la fedha zitengwe kwa ajili ya wakopaji wa miradi mikubwa. Fungu la pili liwe maalum kwa wakopaji wa ngazi ya kati na la tatu litengwe maalum kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo. Kwa mpango huu kila kundi la wakulima litapata fursa ya kukopa katika Benki hii ya Wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kubadilika kwa vipaumbele vya mpango na au bajeti ya mwaka hadi mwaka binafsi nakubali mabadiliko yafanyike pale inapobidi kwa kuzingatia mazingira yaliyo nje kabisa ya uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, tangu ilipoingia madarakani ilianza kwa nchi kukumbwa na mafuriko makubwa yaliyoharibu sehemu kubwa ya miundombinu. Mwaka uliofuata njaa kubwa iliikumba nchi yetu, kutokana na ukame karibu nchi nzima na uliendelea hadi mwaka uliofuata. Mwaka jana 2009, mtikisiko wa uchumi duniani haukutuacha bila athari! Mhe Spika katika mazingira haya si busara wala hekima kung'ang'ania vipaumbele ambavyo ni *rigid* wakati mazingira yanabadilika. Kwa hiyo kubadili vipaumbele kwa sasa wakati mazingira ya uchumi wetu sio *stable* bali ni *volatile* ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni yangu kuwa upatikanaji wa maji safi na salama hasa vijijini ni suala linalopaswa kupewa kipaumbele cha juu zaidi kuliko liliyuo

sasa. Nina wasiwasi mkubwa sana kuwa takwimu za tathmini iliyofanyika kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama sio sahihi kwa sababu pampu nydingi za visima vifupi nchini zimeharibika bila matengenezo kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikifanywa sensa ya Kitaifa kuhusu hitaji la kwanza la wananchi vijijini, naamini watasema kuwa ni maji safi na salama. Naiomba Serikali ilitazame suala hili upya na kipaumbele chake kipangwe juu zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo haya, naunga mkono hoja hii.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo zuri kutoa maoni juu ya mwongozo wa bajeti ya nchi. Maoni yangu kwanza nashauri kabla hatujachangia kuhusu jinsi gani tutapanga vipaumbele vyta matumizi kisekta, bora tunganeza na kujadili vyanzo vipyta vyta fedha kwani bado vyanzo havitoshi na ndio maana tunategemea wahisani na kadri nchi inavyoendelea kuwa tegemezi haiendelei.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nchi yetu haijatuma vizuri rasilimali zetu kama chanzo cha mapato. Tukianza na madini, nchi ina madini mengi lakini bado sera zetu hazijawekwa vema kulifaidisha Taifa letu.

Vivyo hivyo jiografia ya nchi yetu nayo ni rasilimali kwani inategemewa na nchi nane ila bado hatujatumia fursa hii. Vivyo hivyo, tuna maziwa, bahari, mito mikubwa ila shughuli za uvuvi hazijaliongezea Taifa pato la kutosha na wala haionekani kama ni fursa ya kupata kipato, tuna misitu na vingine vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya kupotea kwa pato la Taifa kwa makusudi mfano tabia ya kukagua magari nje ya nchi mfano, Dubai, Japan na maeneo mengine. Kila gari hukaguliwa kati ya Dola za Kimarekani 100-150 na nchi hupata *USD* 10-25 tu. Ni vema stika hizo za ukaguzi zifanyike hapa nchini ili tusizidi kupoteza pato hilo. Vyanzo viko vingi, tunahitaji wataalam wetu wafanye kazi yao ipasavyo watavigundua vingine vingi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Waziri wa Fedha awe anatoa taarifa kila mwisho wa bajeti kiasi gani kimebakia baada ya mwaka wa bajeti kwisha. Vilevile awe akitoa taarifa ya bajeti iliyopita kabla ya kuitisha bajeti mpya ili tujue tumefanikiwa wapi na tumeshindwa wapi na sababu zipi zimesababisha hayo, hapo itakuwa rahisi kupanga vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa *PAC*, nimegundua miradi mingi haitekelezeki kwa kuwa tunategemea zaidi wahisani, hivyo wasipotoa fedha tunakwama. Tujitahidi kutafuta vyanzo vingine vyta fedha ili miradi yetu itumie pesa za ndani. Kwa kuwa tunategemea sana wahisani barabaraa nydingi hazikamiliki. Miaka mingi sasa toka tumeanza Bunge lakini barabara kama za Kigoma-Nyakanazi, Manyoni-Itigi, Tabora haziishi na nydingi hazianzi, tunakuwa tu na mipango mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijielekeza kwenye vipaumbele, nashauri tuendelee na Elimu ili ikishakuwa *stable* tuanze mengine kama miundombinu halafu kilimo kwani

bila miundombinu hatutafungua nchi na mazao ya wakulima hayatafika sokoni. Tufungue uchumi wa nchi kwa kuanza na miundombinu kwa maana ya barabara zote kuu, bandari zote, bahari na maziwa na viwanja vya ndege na reli viboreshwe na hapo tuelekee kwenye Nishati na Viwanda kwani nishati itasaidia kusukuma maendeleo yetu, bila umeme hakuna viwanda bila viwanda hakuna kilimo chenye tija. Umeme unasukuma maji, unasaidia huduma za afya kwani vifaa vingi vinatumia umeme, Shule nazo zinahitaji nishati ya umeme. Hivyo tujifunge mkanda tutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Serikali ni makubwa hayaendani na hali halisi ya uchumi wetu. Mwaka 2010/2011 bajeti ya maendeleo itakuwa 31% wakati matumizi ya Serikali yatakuwa 69%. Tupunguze matumizi tuongeze kwenye bajeti ya maendeleo. Tupunguze magari ya kifahari hatuna haja ya kutumia VX- *New Model* V8 wakati wananchi hawana huduma za kijamii! Wakati huohuo twategemea wahisani, inashangaza kuona safari za nje ni nyngi kuliko za ndani kwenye matatizo ya wananchi. Tupunguze safari za nje, tumeshasafiri sana tubaki nchini tutatue matatizo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kiongozi anasafiri kwa ndege kwenda kikazi mkoani wakati huo huo gari inamfuata alikokwenda wakati angeweza kukodi gari au gari la Halmashauri lingetumika mpaka anaporudi Dar es Salaam. Hapo kuna *service* ya gari, mafuta, posho ya dereva na tiketi ya ndege, vya nini vyote hivyo wakati hatuna uwezo tusiwe wabinafsi tujali nchi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Serikali iangalie, miongozo mingi inachanganya, tunafuata upi, *vision* 2025, *tiger* 2020, MKUKUTA, MKURABITA, MKUMBITA, MKUZA, MDGS au Ilani ya CCM? Sasa je, miongozo yote hiyo haiwachanganyi kweli? Tuangalie matatizo yetu ili tujue pa kuanzia.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa kutuletea na kuujadili Mwongozo wa utayarishaji wa mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2010/11 hadi 2012/13. Mwongozo huu, unatoa fursa kwetu kuijadili na hatimaye kutoa ushauri na mapendelezo kwa Serikali ili kuweza kuangalia upya vipaumbele vilivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tupate uhuru, nchi yetu (viongozi wetu) waliweka bayana maadui wetu wakubwa wa maendeleo amba ni ujinga, umaskini na maradhi. Pamoja na kuwataja maadui hao viongozi wetu walitaja na silaha ya kupambana nao. Silaha hizo ni Watu, Ardhi, Siasa safi na Uongozi bora. Silaha hizi kama tutazitumia ipasavyo maendeleo ya nchi hii yatapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikijitahidi kupambana na maadui hao kwa kushirikiana na wananchi wote wa Tanzania. Kwa kiasi kikubwa mafanikio ya kupunguza umaskini, ujinga na maradhi yapatikana. Ukilinganisha hali ya mwaka 1961 na hali ya sasa 2010, hakuna shaka kuwa kuna maendeleo makubwa katika mapambano hayo na maisha ya Watanzania yanazidi kuwa bora. Kinachotakiwa kufanywa na Serikali yetu pamoja na wananchi kwa ujumla ni kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya maadui hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza nguvu katika mapambano hayo Serikali imeleta mwongozo huo ambao ndani yake kuna vipaumbele vinavyotarajiwa kuwekwa kwenye bajeti zijazo kama zilivyobainishwa kwenye ukurasa wa 32 na mwongozo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha kwanza ni Kilimo na maendeleo ya mifugo. Sina shida sana na kipaumbele hiki ila napenda kujua kuwa hivi sasa ni asilimia ngapi ya Watanzania wanashiriki kwenye kilimo? Kwa takwimu za miaka ya nyuma ni 80% ya Watanzania ndio wanaoshiriki kwenye kilimo, kwa sasa naamini kabisa kuwa idadi ya wakulima itakuwa chini ya 80% kwani vijana wengi wanatoka vijiji na kuhamia mijini ili kufanya biashara ndogondogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kilimo chenyewe katika maeneo mengi ya nchi yetu hakina tija kutokana na mabadiliko makubwa ya hali ya hewa (*climate change*) yanayosababisha maeneo mengi ya nchi yetu kukosa mvua. Naishukuru sana Serikali kwa kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji kwa kuweka miundombinu mizuri ya kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo za Serikali; je tuna maeneo ya kutosha ya kutumia kilimo cha umwagiliaji na kuwashirikisha Watanzania wote? Kwa vyovoyote vile kilimo hiki kitawashirikisha wakulima wachache sana na wengi wataendelea kutegemea neema za Mwenyezi Mungu ili alete mvua za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo basi si vizuri kwa Serikali kuweka kipaumbele jambo ambalo halihusishi watu wengi. Kwa mtazamo wangu eneo muhimu linalotakiwa kupewa kipaumbele ni huduma za jamii na hasa Elimu. Kipaumbele hiki ambacho Serikali ya Awamu ya Nne imekiweka kwa takribani miaka mitatu sasa ndicho chenyeye kuwashusisha watu wote hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, adui yetu mkubwa ujingga ndio chanzo cha maadui wengine waliotajwa na viongozi wa awamu ya kwanza, yaani maradhi na umaskini. Tafiti nyingi zinaonesha kuwa mtu aliyepata elimu si rahisi kwake kuwa maskini au kupata maradhi kirahisi. Kama tutaboresha sekta ya elimu na kutoa kwa kila mmoja nchi hii haitokuwa na umaskini wala maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa eneo hili la elimu hadi sasa lina matatizo lukuki, ombi langu kwa Serikali na kuangalia upya vipaumbele vyake na hatimaye kuvibadilisha na kisha kuipa elimu nafasi ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuishauri Serikali kuwa hivi vipaumbele vidumu kwa miaka kati ya mitano na kumi ili kuhakikisha kuwa malengo yanayotarajiwa katika vipaumbele hivyo yanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuishauri Serikali kuwa kwa kila kipaumbele kinachowekwa kinatakiwa kifanyiwe tathmini ili kuona mafanikio na matatizo kila mwaka wa fedha hii itasaidia sana kuona kama tunafanikiwa au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. OMARI S. KWAANGW': Mheshimiwa Naibu Spika, pato linakua lakini umaskini unaendelea kwa mwananchi mmoja mmoja. Ni muhimu kuhusisha umaskini na idadi ya watu inayoongezeka kwa kazi kulinganisha na ongezeko la pato la Taifa. Vijana wengi wanafanya kazi isiyo na tija ya kutembea na bidhaa katika miji mbalimbali. Kundi hili la nguvu kazi ni lazima liondolewe na lielekezwe kufanya kazi kwa maarifa na juhudhi. Hivyo, kwa hali ilivyo ni kwamba, kuna mikono michache inayofanya kazi, lakini midomo mingi ya kula. Mipango ya nchi ilenje katika kuondoa hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misaada na mikopo. Tayari wafadhili wameanza kupunguza misaada, wengine kutochangia na wengine wamesitisha, hivyo sekta ya Afya kama *HIV/AIDS*, Malaria na TB *programmes* zitaathirika sana. Ni muhimu tuwe na mipango endelevu ya kuanza kujitegemea kwa kuweka fedha zetu kwenye bajeti. Ni hatari kutegemea 96% ya *funds* za *HIV/AIDS* na kadhalika kutoka kwa wafadhili. Watu wengi wataathirika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rasilimali watu. Unapoifanya sekta ya huduma za jamii hasa Afya kuwa ya III katika kipaumbele ni sawa na kukubali kuwa na Hospitali bila maabara kwa sababu upungufu wa rasilimali watu kwa sekta ya afya ni 62%, hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele na I kwangu bado ni Elimu na kwa kweli tumepanua sana sekta ya elimu tumefanya *Rapid expansion* kupita programu za MMEM na MMES, elimu ya juu nayo tumeipanua sana. Sekta hii bado inahitaji vifaa, Maabara kwenye shule za sekondari, bado tuna tatizo la uhaba wa walimu pamoja na *programme* kubwa ya kusahili wanafunzi. Sasa ukiifanya Elimu kipaumbele cha III maana yake *programme* zingine sasa ziahirishwe. Hakuna nchi inayofanikiwa kwa kubadili kila mwaka vipaumbele. Tubaki kwenye elimu kuwa ya I kwa miaka isiyopungua 15 ili kuondokana na adui ujinga. Ujinga ndio mama wa umaskini na maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo tatizo ni usimamizi, hata ukipeleka rasilimali zote. Kuna wakati, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliwahi kusema wakulima wana uwezo wa kulima na kuvuna bila mabwana shamba kwa sababu hawafanyi ile kazi ya ugavi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kutuletea mpango wa mwelekeo wa bajeti hii 2011 – 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Kilimo Kwanza. Baada ya kusoma maandishi na maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika vipaumbele vyake Kilimo Kwanza ijikite katika Umwagiliaji Mkubwa wala tusipumbazwe na *Scheme* ndogo ndogo za umwagiliaji zinazoendelea nchini. Umwagiliaji mkubwa wa Bonde la Mto Rufiji (*The Rufiji River Basin Irrigation Agriculture*) ndio suluhisho na jibu maadui wetu umaskini na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa dunia nzima imekataa kuuza chakula sasa hivi chakula ni nguvu za kiuchumi na nguvu za kisiasa duniani. Serikali sasa ijiingize katika umwagiliaji mkubwa hasa wa Bonde la Mto Rufiji. Kama hatuwezi kujenga miundombinu kwa fedha zetu basi tutumie hata mfumo wa fedha za *Sovereign bonds facility and PPP (Public Private Partnership)*.

Pili, *Stieglers Gorge Hydro power project*, huu ni ukombozi wetu, uwezo wake mkubwa *up to megawatt* 2000 ya umeme. Matatizo ya viwanda na mahitaji ya umeme kwa uzalishaji yangekwisha. Tanzania ingeweza kupunguza gharama za uzalishaji katika viwanda vyetu na tungeweza kushindana na viwanda nya majirani zetu katika EAC na SADC.

Aidha, kwa vile *Electricity* ni bidhaa, Tanzania ingeweza kuuza umeme kwa majirani zetu na hapa nchini tungeweza kuongeza matumizi ya umeme kwa nishati katika viwanda vidogo vidogo na tungetumia umeme zaidi kama nishati mbadala ya kupikia. Hivyo, tungehifadhi mazingira kwa kuinusuru misitu yetu na uchafuzi wa hewa kwa mkaa (*Co₂*).

Tatu, bado elimu iendelee kuwa kipaumbele chetu, bila elimu hakuna kitu kinachowenza kwenda vizuri. Walimu ndio ufunguo.

Mwisho, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali bajeti ya mwaka huu na ujao izingatie yafuatayo:-

Kwanza, kuwekeza katika maeneo yatakayoleta fedha za nje haraka kama vile:-

- Reli ya kati ikarabatiwe haraka ili tusipoteze biashara na nchi za Kongo, Burundi, Rwanda, Malawi, Uganda (Wachina).
- Reli ya Tazara ikarabatiwe haraka (Wachina).
- Vituo nya ushuru mipakani vipewe malengo (Mtukula, Sirari, Namanga, Tarakea, Holili, Horohoro, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara, Kigoma, Manyoni, Kibanga, Rusumo na kadhalika). Bado ukusanyaji ni duni sana.
- Bandari zetu ziongeze ufanisi (Dar es Salaam na Kigoma na kadhalika) na tuwe na malengo.

- Malori makubwa ya mizigo (mbao, mafuta yaongezwe kodi).
- Semina, warsha zifutwe kwani fedha nyingi zinafujwa na uwajibika unakufa.
- Takrima maofisini, chai, tafrija zinaangamiza nchi. Vipunguzwe kwa asilimia sitini kwa kuanzia 2010, swali kwani Ofisini ni mahali pa kula na kunywa?
- Mmatumizi yapunguzwe kwa asilimia ishirini na magari ya gharama kubwa.
- Mikutano maofisini iachwe kwa sababu kazi hazifanyiki.
- Dhana ya kujitegemea irudishwe nchini, leo wananchi wanategemea Serikali na wahisani kwa maendeleo.
- *TRA* waongeze ufanisi kwa asilimia thelathini kwani bado fedha nyingi haikusanywi.
- Fedha za kilimo kwanza zitumike katika kilimo (Mheshimiwa Waziri apunguze magari, *computer*, makaratasi, pikipiki, majengo, Wataalamu wengi bila sababu, semina na kadhalika), pia aongeze ruzuku ya mbolea ndipo kilimo kitakwenda.
- Mheshimiwa Waziri arudishe elimu mahali pake, iwe *Priority number 1*. Tusiudhi wananchi bila sababu.
- Jiografia yetu ni mgodi usioendesheka. Naomba awekeze huko haraka, Kenya watatumaliza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii *project* muhimu sana ya *Clean Development Mechanism (CDM)* ambapo *carbon* (ambayo huzalishwa kutokana na miti) hugeuka bidhaa na kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani, imegeuka kuwa bidhaa muhimu sana ambapo kama nchi ikijipanga vizuri, kisera na kimkakati inaweza ikawa ni fursa kubwa sana ya kuongeza pato la Taifa, wakati huohuo tukishiriki katika kutunza mazingira na kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu kwa kuwa unajulikana kuwa na faida kubwa duniani, Mataifa mengi yameanza kuja nchini, wakionyesha kwamba wana dhamira ya kuendeleza mashamba makubwa. Lakini lengo lao kuu ni kupata maeneo makubwa yatakayowawezesha wao kupanda miti kwa wingi, kwa kutumia fedha zinazotolewa na taasisi ambazo zinahusika na utunzaji wa mazingira. Ningependa kujua Serikali imejipangaje kimkakati kuhakikisha kwamba kama nchi na sio kupitia wageni tunafaidika na fursa hii ambayo ina faida kubwa na ni endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu pia, kabla hatujaanza kukaribisha wawekezaji toka nje tuhakikishe kwamba tunaandaa sera ya Kitaifa, mkakati na mwongozo ili tusije tukajikuta tunapata hasara na tukaanza kushtuka wakati tutakuwa tumeshachelewa kama ilivyotokea kwenye madini? Wakati sisi tunazembea, mtaalam wetu katika masuala hayo (Mtanzania) ameombwa na Serikali ya Rwanda awatengeneze sera ili kama nchi, wawe na mwongozo ulio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itakuwa tayari, nitawaunganisha na mtaalam huyo ambaye amebobeaa na ni mmoja wa wajumbe wa Bodi ya chombo hicho cha Kimataifa kilicho na jukumu la kuitisha miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike wakati, tutumie wataalam wetu, walio kwenye vyombo mbalimbali vya Kimataifa ili nchi iweze kusogea kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuambatanishie hizo *documents* zisome kwa umakini, zaweza kusaidia Wizara yako (kwa kujua kampuni za ndani ambazo zimeshapeleka maombi ya ufadhili wa *projects* husika ili Serikali iangalie ni kwa namna gani inajiandaa kuzibana kimapato kampuni husika, hasa ukizingatia kwamba, wameomba *projects* husika wakati wamesajiliwa (baadhi yao) wakiwa na biashara nyingine, isije ikawa sehemu ya kukwepa kodi? Pia Wizara ya Nishati na Madini, yaweza kabisa kutatua tatizo la umeme kama kukiwa na ufuatiliaji wa umakini kwenye miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napongeza Wizara kwa kutuletea vipaumbele vitano vifuatavyo katika *budget* ya mwaka 2010/11 – 2012/13. Vipaumbele hivyo ni kilimo na maendeleo ya mifugo, miundombinu, huduma za jamii, Elimu, Maji na Afya, Ardhi na Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika vipaumbele hivi vimeteuliwa kwa ufanisi mkubwa kwani vyote vinategemeana katika mzunguko. Bila ardhi hakuna Kilimo na bila Kilimo hakuna Viwanda na bila Miundombinu bidhaa hazifiki kiwandani lakini bila huduma za jamii hakuna rasilimali watu ambao ndio nguzo muhimu. Mtu aliyekamilika ni yule mwenye afya nzuri na elimu bora na bila maji hakuna uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza kauli mbiu ya kilimo kwanza na nina imani kuwa itatuwezesha. Bahati mbaya sana napata shida pale ninapowafikiria wanawake wa Tanzania na hali duni waliyonayo kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, hivi wanawake wa vijijini watanufaikaje na Kilimo kwanza? Enzi za Mwalimu, alihakikisha kuwa alipeleka miradi vijijini ikiwemo ile ya mifugo ya ng'ombe wa kisasa, mbuzi wa kisasa na kuku wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je Serikali iko tayari sasa kwenye *budget* hii kuja na mkakati wa kuboresha mifuko ya mikopo mbalimbali itakayowanufaisha wanawake? Pamoja na kuishukuru Serikali kutuanzishia Benki ya Wanawake itakuwa ni jina tu kama hatutaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la tatu, je Serikali iko tayari kuhakikisha kuna viwanda vidogodogo vya kusindika mazao hayo ili kuongeza thamani? Mfano, usindikaji wa ndizi mbivu na kupata *banana wine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mingi iliyopita ndizi zilikuwa zinatumika kwa chakula na kutengenezea pombe ya kienyeji mbege ambayo haiwezi kusindikwa. Siku za karibuni kumefunguliwa kiwanda cha *Banana Wine* Arusha ambacho kimefanya hata zao la ndizi likapandishwa bei, je, Serikali itasaidiaje viwanda hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali, je, *Budget* inasema nini kuhusu viwanda vilivyofungwa? Vikiwemo *General Tyre* Arusha, *Machine Tools* Moshi, Kiwanda cha Magunia Moshi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la miundombinu, kipimo cha maendeleo ni aina ya usafiri suala la miundombinu ni jema sana, hakika kurejesha usafiri wa Reli hakukwepeki. Nchi yoyote inayoendelea kwa kasi huwa inaweka usafiri amba ni wa bei nafuu na wa uhakika, reli ndiyo yenye kwani itafanya hata barabara zetu ziwe na maisha marefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu usafiri wa reli uharibike, ajali barabarani zimeongezeka, barabara zinaharibika, gharama za nauli zimepanda, ucheleweshwaji barabarani, ujambazi na kadhalika. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba, reli itengewe hela za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vyote vimeorodheshwa lakini bila kuimarisha suala la usalama kwa kuwajengea mazingira mazuri Polisi amba ndio wanaosimamia amani na usalama nchini itakuwa balaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri bajeti ijayo iboreshwe pia kwenye sekta ya Mahakama, ili kesi zinazorundikana zikiwemo zile za Benki zenye thamani ya trilioni tatu zimalizike haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha mchango wangu.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa maelezo ya mwongozo huu. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii. Naunga mkono hoja na maudhui ya mwongozo na vipaumbele vyake. Yote yaliyokusudiwa tuombe Mungu yatekelezwe kwa ufanisi. Lakini ili tuweze kufanya kazi kwa ufanisi na mpango wenye ufanisi lazima ulinzi na usalama wa nchi, mali na

wananchi uimarishwe. Bila ulinzi imara wa mipaka ya nchi yetu na mali zetu, mpango wote si kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kuwa umuhimu wa kibajeti wa masuala ya kiulinzi hauonyeshi waziwazi. Kilimo na mifugo kunahitajika ulinzi, miundombinu inahitajika ulinzi na rasilimali watu wanahitajika ulinzi na kadhalika. Mpango huu lazima uainishe uimarishaji wa ulinzi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara ya fedha kwa kuleta mwongozo huo na naiunga mkono hoja hii. Baada ya hayo, nina haya ya kuchangia:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele katika mipango huenda na uwezo wa kifedha, fedha zikiwa nyingi vipaumbele vyaweza kuwa vingi. Uwezo wa nchi yetu haujawa mkubwa, hivyo vipaumbele vinatakiwa viwe vichache. Mwongozo tulioletewa una vipaumbele vingi mno. Ushauri wangu ni kwamba, tuwe na vipaumbele vitano tu kama ifuatavyo:-

Kwanza, elimu. Tuendelee kuimarisha elimu kwa wananchi wetu. Bado umuhimu wa elimu haujawa wazi kwa wananchi wetu. Wengi wanaona elimu ni kama *fashion* tu. Bado si kwa hiari ya kutoka ndani inayotokana na kutambua umuhimu wa elimu wanapeleka watoto wao shule. Aidha, watoto nao wanakwenda shuleni kutimiza wajibu tu. Hivyo elimu iimarishwe katika maeneo yafuatayo:-

- i. Katika ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya elimu kama madarasa, nyumba za walimu, maabara, ofisi za walimu, kumbi na maktaba.
- ii. Kusimamia sheria za elimu ambazo ni nyingi lakini hatuzisimamii, tukizisimamia elimu itapanda katika hadhi.
- iii. Kufufua na kuiongezea thamani elimu ya watu wazima kwa lengo la kuwakumbusha wananchi umuhimu wa elimu.

Pili, kupeleka kwa makusudi huduma za jamii vijijini huduma zinazotakiwa kuwa za viwango vya juu. Kwa kipindi kirefu sasa nchi yetu imekuwa ikiweka elimu kama moja ya vipaumbele, lakini elimu kama ufunguo wa maisha inaonyesha dhahiri nafasi yake katika kuleta maendeleo katika Taifa hili. Kwa upande mwingine elimu inachangia katika kuiongeza umaskini wa familia na eneo, mifano iko dhahiri. Wasomi wengi ambao ndio matunda ya elimu hupenda kwenda kufanya kazi mijini tu. Sababu ni kwa kuwa mijini huduma za jamii ni nzuri. Hivyo pamoja na kuwekeza katika elimu lakini faida kubwa ya elimu inaishia mijini. Miji yetu inavuta vijana wengi na wasomi ambao ndiyo nguvu kazi ya nchi yetu.

Vijiji vinaachwa bila nguvu kazi na utaalama wowote, vijijini, shule ni duni, zahanati ni duni, barabara ni mbovu na maeneo makubwa hayana umeme na havina wasomi wa kutosha ukilinganisha na mijini! Lakini huko ndiko kuna asilimia kubwa ya Watanzania. Je, elimu tuliyonayo italetaje maendeleo na kupunguza umaskini vijijini kuliko na watu wengi? Mipango mahsusini na ya makusudi ipangwe kupeleka maji vijijini, ipeleke umeme vijijini na vijiji viunganishwe na miji ni mikubwa na midogo. Naamini tukifanikiwa katika haya wataalam wetu ambao ndio matunda ya elimu hawatakataa kwenda vijijini kama atakuta nyumba, maji, umeme na huduma bora za afya. Hapo ndipo tutakuwa tumeipatia elimu nguvu halali ya kuendeleza nchi yetu.

Tatu, nishati vijijini, vijana wetu wengi wanaohitimu mashulen na vyuo hukataa kwenda vijijini kwa kukosekana nishati (umeme). Naamini umeme ukifikishwa katika vijiji vyetu, shule zetu zitajaa walimu, zahanati na vituo vyetu vya afya vitajaa watumishi, vijana wahitimu wa shule na vyuo wangependa wawe na *TV*, *Radio*, *Computer* na vyombo vingine kama hivyo vinavyohitaji nishati ya umeme. Bila umeme kijana hawezi kwenda vijijini hata akienda kwa shingo upande na hatafanya kazi kwa upendo. Nashauri *REA* waongezewe fedha, wapate uwezo wa kusambaza umeme vijijini (afikirie kukata umeme na maji katika miji yote, aunganishe umeme na maji vijijini je, watumishi wote hawatahamia vijijini?)

Nne, miundombinu vijijini. Vijiji viunganishwe na miji na mawasiliano ya ndani ndani ya vijiji viimarishwe kuwe na barabara na mawasiliano mengine vijijini yawepo.

Tano, ni kuhusu ulinzi na usalama, maendeleo hayawezekani bila amani na usalama, viimarishwe majeshi yetu yote yawe ya kisasa.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kupata nafasi hii muhimu ili nami nichangie kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Serikali ni muhimu iwe makini katika kuzingatia vipaumbele katika nchi yetu ambayo inahitaji kupata maendeleo. Kwa maoni yangu kipaumbele cha kwanza katika nchi yoyote ile ni Elimu. Watanzania wanahitaji kupata elimu ili tuweze kupata vijana wengi wenye elimu ambao watasimamia ukulima, ufugaji, uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufanikiwa kimaendeleo kama tutakuwa na Taifa ambalo wananchi wake hawana elimu. Je, tutapataje walimu katika shule za msingi, sekondari na katika vyuo mbalimbali? Je, tutapata wapi wataalam wa kilimo na mifugo? Je, tutapata wapi Madaktari na Wauguzi. Ni muhimu Serikali kwa makini na kuamua kuwalipa walimu mishahara ya kutosha ili wanaohitimu wapende ualimu ili waweze kuajiriwa katika shule zetu za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamejitahidi sana kujenga shule za Kata, nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania kwa kujenga shule za Kata. Kinachohitajika sasa ni walimu, vifaa vya maabara, vitabu, pamoja na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari, barabara, reli, viwanja vyatia, viwanda ni vitu vyatia muhimu sana kuzingatiwa. Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu hiyo. Nchi yetu haiwezi kuendelea na kupata maendeleo kama tutakuwa na nchi ya watoa rushwa na wapokea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile katika kifungu No. 42, ukurasa 29 wa Mwongozo, Serikali imekiri kuwa mabadiliko ya tabia nchi yanaleta athari kubwa sana kwa binadamu na mazingira yake kuhusiana na miundombinu, hatua zinazochukuliwa kukarabati miundombinu na kutoa misaada kwa waathirika siyo “solution” endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatozo hili limetokana kwa sehemu kubwa na uharibifu wa mazingira kutohakisha na ongezeko kubwa la watu pamoja kuongezeka kwa matumizi makubwa na duni ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna ya kutatua matatizo haya ni kuhakikisha miundombinu inakuwa imara na endelevu; kilimo cha mvua na umwagiliaji kinakuwa endelevu kwani maji yakiwepo kadhalika mvua, chakula na malisho ya wanyama yanakuwa endelevu, na kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya ardhi iliyopimwa na matumizi yanasisimamiwa. Matumizi bora ya ardhi, ni pamoja na kuhifadhi vyanzo vyatia maji, kuhifadhi misitu na maeneo ya miteremko na kandokando ya mito na maeneo oevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kipaumbele changu cha kwanza ni, ardhi ambapo pendekazo la Serikali ni kipaumbele cha IV, yale yanayopendekezwa chini ya kipaumbele No. IV – Ardhi, yakifanywa kwanza vipaumbele No. 1 na II yaani Kilimo na Miundombinu, vitawezekana kuwa endelevu.

Kwa hiyo, vipaumbele vyang'vyatia pili ni vichochezi vyatia uchumi (Viwanda, Madini, Nishati). Vipaumbele vyatia tatu ni Kilimo huduma za jamii na matokeo ya utekelezaji wa vipaumbele I – III.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vizingatie nishati mbadala yenye kuleta matokeo makubwa (*impact* ya mara moja). Hapa napendekeza makaa ya mawe - liganga na gesi. Ikibidi kuzingatia umeme wa maji basi ni *Stieglers Gorge* kwa vile michango ya muhimu ya mto Luwegu na Kilombero (80%) ni endelevu, maji yanatoka maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vizingatie kumhudumia ndege anayetega mayai ya dhahabu yaani miundombinu ya vijijini, maeneo ya viwanda mama (Liganga na Mchuchuma Ludewa).

Mheshimiwa Naibu Spika, tupunguze sana kuwategemea wafadhili kwa vile wanatupa “*False Hopes*” tunapanga mikakati kisha inavurugwa kwa kutunyima fedha tulizoahidiwa.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii, kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Wakuu na wataalamu wote waliohusika katika maandalizi ya utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 – 2012/2013. Nimeusoma mpango ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba mpango ni mzuri, naomba nitumie fursa hii kuzungumzia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa namna ilivyoanda vipaumbele. Nakubaliana navyo kabisa, hata hivyo, kwenye Sekta ya Kilimo, eneo la mbolea, nashauri zitengwe pesa za kutosha ili kaya nyingi zaidi ziweze kufaidika na mbolea ya ruzuku. Aidha, mbolea ya ruzuku inayopelekwa kwa wakulima kiasi fulani huibowi, kama mbolea ya ruzuku iliyopelekwa mbozi mwaka huu 2009/2010, karibu vocha za thamani ya Tshs. 100,000,000/= (Shilingi milioni mia moja) zimeibiwa. Naomba Serikali iweke mkakati wa kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kipaumbele cha pili, naomba nishauri kwamba Serikali iongeze kodi kwenye madini, hili ni eneo ambalo tunapoteza mapato mengi sana. Inasemekana Tanzania ni moja ya nchi ambazo zinatoa tozo dogo sana kwenye madini. Kwa kuwa tunahitaji pesa zaidi kwa ajili ya shughuli za maendeleo, naomba Serikali ichukue hatua madhubuti na bila kwaogopa, kuwaonea huruma wafadhili kuweka kodi zinazostahili. Ikiwezekana watalaan wetu wa masuala ya kodi, watembelee na kuona uzoefu wa nchi nyingine. *This in my opinion, is a very potential area which is not fully utilized in as far as tax collection is concerned.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha huduma za jamii; hapa naomba nishauri Serikali kukamilisha miradi yote ya nyuma hasa katika Sekta ya Elimu. Tunajua Elimu ndiyo ilikuwa kipaumbele cha kwanza kwa miaka miwili mfululizo. Hivyo shughuli zote zilizoanza hasa ujenzi wa madarasa na maabara, ziendelee kutengewa pesa za kutosha ili kuzikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda, nchi yetu kimsingi inategemea kilimo kwa zaidi ya asilimia 80, hivyo suala la kuanzisha viwanda vya zana za kilimo ni lazima lipewe kipaumbele kikubwa. Wote tunakumbuka huko nyuma tulikuwa na viwanda vya kutengeneza vifaa vya kilimo kama vile UFI – Ubungo na Zana za kilimo (ZZK) – Mbeya. Kwa bahati mbaya sana, viwanda vyote hivyo havifanyi kazi. Naomba Serikali ije na mpango mzuri wa kujenga au kufufua viwanda vya kutengeneza zana za kilimo. Ni vema pia ikumbukwe kwamba dhana ya Kilimo Kwanza haiwezi kukamilika kama hatuna viwanda vya kutengeneza vifaa vya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu 2010, ni jambo jema sana kutenga pesa za kutosha kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi huo. Hata hivyo, Serikali iweke utaratibu wa kudhibiti pesa haramu zisije zikaingia kwenye uchumi kupitia uchaguzi. Hilo likiachwa bila kudhibitiwa, kuna hatari ya kuwa na

inflation maana pesa ambazo haziko kwenye mzunguko rasmi zitaingia na hiyo ni hatari kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la ukusanyaji kodi, bado lina mianya minge ya ukwepaji kodi pamoja na jitihada zilizopo na shauri udhibitim zaidi uongezwe. Kwa bahati mbaya zaidi, Maafisa wengi wa *TRA* siyo waaminifu kwani wanashirikiana na wafanyabiashara wasio waaminifu kuibia Serikali mapato. Eneo kubwa zaidi tunaloibwa ni kwenye mizigo inayoenda nje ya nchi yetu. Aidha, mizigo mingi, hasa mafuta yakiwa '*Labeled on transit*' lakini yanatumika nchini, kinachotokea ni ukwepaji kodi kwa kuwa mizigo ya aina hiyo haitozwi kodi. Tuimarishe udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nidhamu kwa matumizi, pamoja na jitihada za ukusanyaji fedha unaofanywa na Serikali, bado nyangi ya fedha hizo zinatumika vibaya. Tumeshuhudia kila mwaka Waziri wa Fedha akija na ombi Bungeni akiomba madeni sugu ya upotevu wa fedha za Serikali yafutwe, tumeona taarifa za *CAG* zikionyesha upotevu mkubwa wa fedha za Serikali; hakuna nidhamu ya matumizi. Nashauri mpango huu uje na mkakati maalumu wa kurejesha nidhamu ya matumizi ya pesa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, hasa kwa vile wameleta mpango mzuri kuelekea kwenye bajeti ya mwaka huu wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua, hali za nchi zetu hizi za dunia ya tatu na Serikali zake, lazima tuwe na utaratibu na mpango endelevu ili tuweze kupiga hatua kwenye maendeleo la sivyo tutakuwa hatuna tulifanyalo kwani matatizo yetu ni mengi na rasilimali zetu ni chache. Kwa hiyo dhana ya kuwa na mpango madhubuti na vipaumbele ni njia sahihi kuelekea tuendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Waziri, kama ilivyo katika taarifa ya mpango wa bajeti, Ukurasa wa 32 na 46, I, II na III, ila kutokana na hali ya dunia ilivyo ya upungufu wa chakula na kwa kuwa sisi Tanzania tuna rasilimali watu, ardhi, maji ya kutosha na kwa vile kilimo ndio mchangiaji mkubwa wa mapato nchini, (hasa fedha za kigeni) lakini vilevile kilimo ndio *sector* pekee inayoajiri watu zaidi ya asilimia 75% hapa nchini, lakini ni dhana iliyoanzishwa na Mheshimiwa Rais kwa tamko la **KILIMO KWANZA**.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana moja kwa moja kwamba kilimo kipewe kipaumbele cha kwanza kati ya vipaumbele vilivyoasisiwa au kusisitizwa! Kilimo ndio ufumbuzi wa tatizo la nchi hii, bila ya kilimo hakuna maendeleo. Lakini ni sawa kabisa na ni sahihi uvuvi, mifugo ni sehemu kubwa ya kilimo bali kilimo bila ya kulitaja na kutamka suala la maji, moja kwa moja halitakamilika tukifanya mzaha.

Kwa hiyo basi, tunataka kuona waziwazi kwenye mipango hii, suala la kilimo liambatane na tamko la KILIMO NA UMWAGILIAJI KWANZA. Naelewa *commitment* ya mbolea, mbegu bora, madawa ‘*crop attendant*’ lakini historia inatuonesha hata haya yote ukiwa nayo bila ya kilimo cha umwagiliaji ni kazi bure. Kwa mtazamo wangu, tujikite kikamilifu katika Kilimo cha Umwagiliaji na hapana shaka mengine yatafuatilia. Ni kweli barabara na masoko ni muhimu, lakini bila ya bidhaa yenyewe miundombinu tajwa haitasaidia kusukuma mbele gurudumu hili la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuwakumbusha, Watanzania lazima tubadilike katika hilo tusifanye mzaha, tupunguze maneno mengi, tutumie vitendo. Fedha zikipatikane tujipange vyema, rasilimali watu ipewe nafasi, itengwe maeneo na tuwe kwa sasa na mazao machache ili rasilimali fedha kidogo zitumike kuleta *impact*.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atenge fedha nyingi zaidi za ndani na tupunguze kutegemea misaada hasa hili la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila umwagiliaji hakuna kilimo.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie somo tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubaliane kwamba Kilimo Kwanza, yaani kilimo ndio msingi wa maendeleo, ndio uti wa mgongo kwani 80% ya Watanzania wote ni wakulima. Lakini si hilo tu, kwenye kilimo ndio tunapata chakula na mazao ya biashara. Hii ina maana kwanza chakula, mtu akiganga njaa, akila ndio anaweza kufanya kazi vizuri zaidi. Mtu akiwa ana njaa wala hamuelewani, ndio maana Wanyamwezi wana msemo unaosema “IGEMBE NSABO” maana yake “jembe ni mali” hivyo, Kilimo Kwanza iwe *priority*. Naomba kwa mtazamo wa kwanza wa sasa, nadhani na naamini maji kwanza. Kwa misingi hiyo, naomba *budget yetu first priority* iwe maji, kwani bila maji, hakuna Kilimo Kwanza, bila maji hakuna uhai wa viumbe na mimea na wanadamu wanaotawala hivi viumbe na mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali halisi ya hali ya hewa na mabadiliko ya dunia yanavyoenda, hatuwezi kuendelea kulima kilimo cha kutegemea mvua. Kwa misingi hiyo, tunapotaka kupambana na njaa na umaskini basi kilimo, lakini kilimo cha kisasa, yaani kilimo cha umwagiliaji, hii ina maana uvunaji wa maji ya mvua. Mimi naamini, *first priority* ni maji na umwagiliaji, kwa maana ya kilimo, uvuvi na ufugaji ili wananchi wapate chakula na biashara, hivyo kuondokana na umaskini. Hatua ya pili, naamini ndio iwe elimu na afya sababu bila elimu na afya, mtu hawezi kujikwamua umaskini. Baada ya kulima, mazao ya chakula na ya biashara, tunahitaji barabara za kutoa mazoa mashambani kupeleka masokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopeleka watoto wetu wanakwenda hadi *Form IV* katika shule za Sekondari za Kata lakini hawa wanafunzi hawapati “*Practical*” ya masomo mengine kama yale ya sayansi, kwa misingi hii, tunahitaji umeme. Hivyo, tutakuwa na wataalamu wa sayansi na mabingwa wa masomo/taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na la muhimu zaidi ni idadi ya watu, (*family planning*). Mimi naamini kabisa lazima elimu itolewe na iwe sehemu ya maisha yetu. Watu tuzae kwa mipango na watoto ambao mtu anaweza kuwahudumia. Mara nyingine, umaskini na njaa inatokana na wingi au ukubwa wa familia. Tukiweza kujipanga, tuseme kila familia iwe na watoto wanne (4) au chini ya hapo, akina mama na watoto watapata matunzo bora, afya bora na hivyo hatutakuwa na shida ya watoto wa mitaani au ombaomba hapa na pale. Kwani kila mtu atazaa watoto anaoweza kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi sana kwa Serikali kwa Kilimo Kwanza. Pia kwa kuchagua kilimo kuwa kipaumbele cha kwanza. Kilimo kikifanikiwa, Watanzania wengi wataondokana na umaskini. Pato la Taifa litaongezeka na kuweza kuhudumia huduma tegemezi kama elimu, afya na maji. Binafsi nimepokea kwa shauku kubwa jinsi Serikali ilivyopanga vipaumbele katika bajeti hii ijayo kwani ni mkombozi kwa Mtanzania.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kutoa tathmini ya bajeti ya mwaka 2009/2010 na kuleta mwongozo wa bajeti ya 2010/2011 ili tuweze kuuongezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Mtanzania kwenye maeneo yake hutegemea mapato kwenye Halmashauri yake kuititia bajeti iliyowekwa. Katika makusanyo ya mapato, kuna udhaifu mkubwa ukilinganisha na wenzetu. Mfano kwenye mipaka yetu bidhaa zinachelewa mpakani kuliko wenzetu wa nchi jirani na kusababisha watu kuitisha mizigo njia za panya na kuikosesha Serikali mapato, ni afadhali kuweka mazingira mazuri kwenye makusanyo kuliko wafanyabiashara kuogopa vyombo vyaa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele ni muhimu kwa kila eneo kwenye bajeti ya Taifa na Halmashauri. Kuna Halmashauri ambazo hawakuweza kubadilisha vipaumbele kutokana na elimu kuwa duni kwenye Wilaya husika katika mipango ya Serikali, ni afadhali kuzingatia mipango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la jiografia, ni muhimu sana kujua tunapopanga vipaumbele, kwa mfano, kwenye eneo la wafugaji ambao wako eneo la ukame huwezi kulima mazao ya aina yoyote, huwezi kutumia dhana ya Kilimo Kwanza, kwao wanasema Mifugo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukuza utalii, bado hatujaibua vivutio mbalimbali kwenye maeneo mengi. Ni afadhali tubuni maeneo mengi ya kuwezesha kuendeleza utalii ambao siyo gharama sana kama ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukuza upatikanaji wa madini, bado kuna maeneo mengi ambayo hayakugundulika madini, utafiti ufanyike na kubaini vito vilivyoko kwenye maeneo ya Taifa letu. Hatupati mapato bila kujua au kutumia rasilimali nyingi ambazo bado hatujazitumia, tuzitumie kwa ajili ya kugundua sehemu kubwa na rasilimali nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya kusindika nyama, ni muhimu, viwanda ni sawa na wakulima kuwa na mazao wakose soko hakutakuwa na sababu ya kulima chakula kingi huku hakuna masoko. Kwenye eneo la wafugaji tuandae viwanda na masoko kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mikopo kwenye maeneo ya vijijini bado ni jambo ambalo halikuleta tija na ufanisi. Ardhi ni muhimu ipimwe kwenye maeneo ya vijijini waweze kutumia kama rasilimali ya kupata mikopo. Huduma ya mabenki ni watu wachache sana ambao wanafaidika kupata mikopo. Serikali iwezeshe wananchi kupata mikopo kutokana na rasilimali ardhi. Wajasiriamali hawawezi kuinua hali ya maisha yao bila kupata kianzio cha biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Wizara ya Fedha kwa mwongozo huu. Naomba maboresho kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono mwongozo huu.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi mwongozo wa mpango na bajeti ya Serikali. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na Manaibu wote, kwa kazi nzuri na nzito ya kutayarisha hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tuna mambo mawili kwanza mipango na bajeti. Mipango ni dira na kwa mwongozo huu, tunaishukuru sana Serikali kwa kuwa kama kuna mipango mizuri ni wazi tutatumia fedha chache tulizonazo. Pili, tuna bajeti ya Serikali ambapo ndiyo nataka kuchangia. Tukiwa tuna mipango mizuri na kuiwekea vipaumbele, je, tunaweka vipaumbele kwenye shilingi “ngapi” tulizonazo? Mipango bila pesa haitatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Bunge, zaidi ya kutekeleza matakwa ya wapiga kura, ni pamoja na kuhakikisha fedha za umma zinapatikana, zinatumika vizuri na zinatolewa taarifa (*accountability*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo umeainisha jinsi mapato yalivyokuwa mwaka uliopita kutoka ndani na nje. GBS = 66% na baadhi ya wafadhili kujitoa ingekuwa vizuri kutoa linganisho kwa takwimu ili tujielewe tuko wapi na tunakosea wapi kwa nini Kenya na Uganda wana uchumi ulio bora kuliko sisi wakati (Tanzania) tuna *resources* za (*be it natural resources, maliasili/utalii*) kutosha kuwapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi 2008 na 2009 tulivalia njuga suala la mikataba mibovu, tukaona kama ndiyo inapotezea Taifa mapato. Je, tumerekebisha hali hii kwa kiwango gani? Inaelekea Tanzania tunajua matatizo yetu ya uchumi wetu kushuka, lakini sijajua ni kwa nini hatuna uthubutu wa kutekeleza yote tunayosema kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulizungumzia sana suala la kufufua Reli na Bandari, hakuna kinachotekelzeza kama ipo Mheshimiwa Waziri atueleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ni *engine* ya Bunge, naomba Wizara ya Fedha kupendekeza kuanzisha Kamati ya Bajeti, hii itasaidia sana kufuutilia mambo kwa karibu na kuhimiza uwajibikaji kwa masuala tunayoridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba bajeti ya Serikali iwe na mtizamo wa kijinsia. Haina maana ya bajeti ya wanawake ina maana bajeti itakayolenga makundi yote muhimu ndani ya jamii wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu, vijana, wazee n.k. Bila *gender responsive budget*, makundi fulani ndani ya jamii wanasaaulika kama wanawake, wanahitaji barabara ufile zahanati, zahanati ziwe na vifaa na wataalam ili vifo vya wanawake vipungue n.k. Hii ndiyo maana ya bajeti yenye mtizamo wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu, ambaye amenipa uzima hata nikaweza kuchangia Mwongozo huu wa Bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu wake, pamoja na Wataalam wote wa Wizara, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kutupatia mwanga wa mwelekeo na Bajeti ya Taifa. Ninampongeza pia Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, pamoja na Wanakamati wote, kwa kuuchambua kwa makini sana Mwongozo huu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono Mwongozo huu wa Bajeti. Pamoja na ulakini wote wa Mwongozo huu, lakini kama zilivyo nchi nyingi za Afrika, tatizo lipo katika nidhamu (*Discipline*) ya matumizi ya rasilimali. Kwamba, rasilimali zilizokusudiwa kwa ajili ya kilimo ziwafikie walengwa waliokusudiwa na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine inayotukabili katika utekelezaji wa mipango yetu ni ukosefu wa kufanya tathmini kwa yale yaliyofanywa tayari. Kwa mfano, Wizara ya Elimu imeandaa mpango mzuri wa kuboresha elimu, katika utekelezaji wake utaboresha shule zilizoko mijini na siyo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la wakulima katika shule zilizoko vijijini. Kila mwaka wanapelekwa walimu lakini hawakai wanaondoka; je, kwa nini

kusiwe na mkakati mahususi wa kutatua tatizo hilo? Uwiano wa ujumla wa mwalimu na wanafunzi ni 1:54, lakini shule za vijiji kila mwaka inabaki kuwa 1:120 miaka inapita walimu wanabakia kuwa wawili tu katika shule; je, hakuna tathmini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi katika kifungu cha 2:8 kinachoelekeza kuwa mipango yetu ilenge katika kuboresha miundombinu hasa barabara za vijiji. Ni ukweli usiopingika kwamba, barabara ni nyenzo muhimu. Katika ziara yangu ya kutembelea vijiji, nilikwenda katika Kijiji cha Isonso kilichopo umbali wa kilometra 30 kutoka katika eneo la kuuzia mazao; wananchi hawa wana chakula kingi, lakini hawawezi kukiiza kwa sababu barabara ni mbovu na magari hayaendi; debe la mahindi linauzwa TShs. 1500 wakati sokoni ni TShs. 6000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo huu pia ungetupatia mwanga wa mikakati ya kila sekta iliyokusudiwa.

Mwisho, naunga mkono Mwongozo.

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo huu wa vipaumbele ambavyo vimeainishwa sikubaliani nao.

Mapendekezo yangu, vipaumbele tufanye vitatu kwanza, tukianzia na:-

Elimu: Watanzania tutajikomboa kwa kupata elimu bora. Bado upo upungufu mwingi sana, pamoja na hatua nzuri ambazo wananchi na serikali wamefikia.

- Tujenge nyumba za walimu, tujenge majengo ya utawala, tuwe na vifaa vyaa kufundishia na kujifunzia na tukamilishe maabara zetu.
- Tukamilishe au kuondoa tatizo la walimu. Yapo maeneo kuna upungufu mkubwa sana mfano, Shinyanga uwiano ni 1:78.
- Tukoboresha elimu, mauaji ya vikongwe na albino yatapungua. Suala la Utawala Bora litaonekana.
- Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukienda Bukombe, wananchi wanaonewa sana kwa kuwa hawana elimu. Wananchi wanaporwa mali zao na baadhi ya askari wasio waaminifu. Pia wachimbaji wadogowadogo wanaporwa na waganga wa jadi wanaporwa mali zao.
- Tuboreshe maslahi ya watumishi wa kada zote. Tukifanya hivyo, hata Kilimo Kwanza kitafanikiwa.

Naishauri Serikali miundombinu kiwe kipaumbele namba mbili. Serikali ijitahidi iboreshe reli zetu zote ikiwemo Reli ya Kati na Isaka – Kigali.

- Mheshimiwa Naibu Spika, bandari zetu ziboreshwwe na si kuboreshwwe tu ni pamoja na kusimamia vizuri ili kuingiza mapato yatakayotuwezesha kuboresha Kilimo Kwanza.
- Viwanja vya Ndege viboreshwwe; huwezi kuamini ziara ya Mheshimiwa Rais Shinyanga tarehe 19/01/2010 ilimlazimu ateremkie Uwanja wa Ndege Mwanza badala ya Ibadakuli. Migodi mikubwa ipo Shinyanga lakini uwanja haufai.
- Kupandisha hadhi barabara mfano Barabara ya Masumbwe – Ushirika – Ivumwa hadi Geita na Masumbwe – Ushirika – Shibutwe hadi Kahama na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza kiwe kipaumblele namba tatu. Katika eneo hili naomba tufanye yafuatayo:-

- Turasimishe ardhi ili wakulima wakopesheke.
- Tuboreshe masoko ya mazao kwa wakulima wetu kama alivyofanya Mheshimiwa Rais kwenye Zao la Pamba kwa kuongeza shilingi nane kwa kilo ya pamba.
- Wakulima wapate pembejeo kwa wakati; mfano, zao la tumbaku, wakulima wa Bukombe hawana pembejeo.
- Wakulima wakopeshwe maksai na plau badala ya kuwakopesha *power tillers*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *power tiller* moja ni sawa sawa na shilingi milioni nane au tisa, wakati maksai na plau moja ni sawasawa na shilingi milioni moja na laki sita. Ukitoa maksai na plau vikundi saba kwa *power tillers* ni kikundi kimoja.

Kila wilaya iletu Mpango wa Kuendeleza Kilimo Kwanza. Siyo lazima falsafa ya Kilimo Kwanza ifanane nchi nzima kama Biblia.

Miradi ya umwagiliaji kila maeneo iwepo. Mifugo iheshimiwe pawepo na masoko, machinjio, majosho ya kisasa na kupunguza semina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali idhibiti matumizi mabaya ya fedha hasa kupitia Kitengo cha Manunuzi. Inasikitisha kuona Serikali na Taasisi zake bado zinanunua mahitaji toka kwa aidha watu binafsi au makampuni.

Kwa nini Wakala wa Serikali wa Manunuzi wasisimamie zoezi hili na kuzisaidia? Tunaendelea kununua nje na wakala kwa ajili ya 10%?

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya fedha za serikali mfano fedha zinazopelekwa kutengeneza barabara; kwa nini tusijenge utaratibu wa kuboresha eneo fupi kila mwaka badala ya kutengeneza eneo lote kwa hela ndogo na kuharibu. Mfano, barabara yeny urefu wa km 20 kila mwaka mnapeleka shilingi milioni 14; hizi fedha kwa miaka mitano ni nyingi na uwezekano wa kuboresha barabara ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vipaumbele vibadilishwe kwa kufuata mtiririko nilioutaja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitaomba nimwite Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi, ye ye atapewa dakika 15 na Mheshimiwa Waziri mtoha hoja atapewa dakika 45.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja kuhusu Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya Muda wa Kati, 2010/2011 mpaka 2012/2013 na Bajeti ya 2010/2011 ambayo iliwasilishwa jana na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niwashukuru sana Kamati ya Fedha na Uchumi, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa uchambuzi wao wa Mwongozo huu na ushauri wao na kwa ku-set dira ya mazungumzo na majadiliano. Vile vile napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwenye majadiliano haya, kwa kutoa maoni na ushauri, kwa wale ambao wamechangia kwa kuzungumza na wengine ambao wamechangia kwa mandishi. Naamini kwamba, Mheshimiwa Waziri atawatambua kwa kuwataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuzungumzia baadhi ya maoni na hoja ambazo zimetajwa na Waheshimiwa Wabunge. Nianze na umuhimu wa kuwa na mikakati ya kutumia Soko la Pamoja na Afrika Mashariki ili lisaidie kuinua uchumi wa nchi yetu. Mwongozo ambao Mheshimiwa Waziri aliuwasilisha, umeelezea namna ya kutumia soko hili pamoja na masoko mengine yatokanayo na ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda. Ninashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa upanuzi wa fikra ya nini ambacho kinahitajika kufanyika na moja ambalo limesemwa hapa ni kwamba, kuna umuhimu wa kuwahusisha zaidi wananchi na moja ya njia ya kuwahusisha ni kuwapa elimu ambayo itawawezesha kufahamu maana ya soko hili, fursa zilizopo na jinsi ambavyo wanaweza kulitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia ghamra za kufanya biashara nchini na kusema kwamba ziko juu, kuna umuhimu wa kuzipunguza. Jambo hili nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inalifahamu na ilikwishaanza kulifanyia kazi, sasa hivi kuna Mradi unaojulikana kama BEST, ambao ni kifupi cha *Business Environment Strengthening Tanzania* (Mradi wa Kuimarisha Biashara na Mazingira ya Biashara Nchini), ambao unashirikisha sekta

binafsi. Mradi huu unashughulikia urekebishaji wa sera na mfumo wa sheria zinazotawala mazingira ya biashara na uwekezaji. Baadhi ya mafanikio yaliyokwishapatikana katika Mradi huu ni pamoja na kukamilika kwa maandalizi ya sera ya kusimamia utoaji wa leseni na kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa vitambulisho vya kitaifa. Ninakiri kwamba, bado kuna kazi ya kufanya ili kutoa fursa zaidi na kuboresha mazingira ya biashara na kushusha gharama za kufanya biashara nchini, kazi hiyo Serikali itaendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hoja na maoni ambayo yametolewa na Wabunge wengi na hili jambo linajirudia katika mazungumzo yetu ni lile linalohusu umuhimu wa kutumia jiografia yetu, jiografia ya nchi yetu Tanzania katika Bara la Afrika kwamba, tumezungukwa na nchi nane ambazo hazina Bahari na kwamba, tukirekebisha bandari zetu pamoja na miundombinu yetu ambayo inatuunganisha na nchi hizi, basi tunaweza kupata mapato mengi yanayotokana na matumizi ya Bandari zetu za Dar es salaam, Mtwara na Tanga, lakini pia na Reli ya Kati na Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, kule Serikalini tunaumwa vichwa kuhusu jambo hili na Serikali inalifahamu, moja ya vikwazo ni kwamba, tunayoyazungumzia hapa ni miradi ambayo inahitaji uwekezaji mkubwa.

Ninajua kuna mambo vilevile ya kiutawala, ambayo mara nyininge yameingilia uwekezaji huo mkubwa nilioutaja, lakini ndiyo sababu kwa mfano; Serikali katika jitihada za kutafuta fedha za kuwekeza kwenye miundombinu hii, tulisikia Mheshimiwa Waziri alitaja kwamba, Serikali inafanya maandalizi kwanza ya nchi yetu kutathminiwa na kupewa *rating* ili ituwezeshe kukopa kwenye Soko la Mitaji la Kimataifa kwa kutumia *Sovereign Bond*. Tukifikia hapo na tukifanikiwa kupata fedha hizo ambazo tunatarajia kuzipata na tukizielekeza kwenye miundombinu hii ambayo imezungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge, basi ninaamini kwamba, tutaweza kubadilisha hali na kuchuma kutoptaka na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie vilevile Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunaelewa kinachoendelea Kenya, tunajua kwamba Bandari ya Mombasa inapanuliwa na Serikali ya Kenya, tunajua kwamba Kenya na Uganda wameingia kwenye makubaliano ya kujenga reli mpya kutoka Mombasa na ambayo itakwenda mpaka Malaba na kuvuka kwenda Kampala na tunajua kwamba hiyo inatuweka mahali pagumu kama na sisi hatutavuta kasi na kurekebisha mambo yetu. Ninapenda kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kulisemea jambo hili; tusiache kulisemea na tunawashukuru sana kwa kuendelea kulisisitizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge ambayo imetajwa inahusu umuhimu wa kuongeza vyanzo vipyta vya mapato kwenye Halmashauri zetu. Kama tunavyojua, sasa hivi Halmashauri zetu zina vyanzo viwili vya mapato; kwanza, vyanzo vyao wenywewe vinavyotokana na kodi ndogondogo na ada ndogondogo ambazo wanatoza kwenye Halmashauri zao, lakini sehemu kubwa ya matumizi yao yanatokana na ruzuku kutoka

Serikali Kuu. Serikali imeanza kufanya kazi uwiano huu ili baadae tupunguze kiwango cha ruzuku na kuongeza mapato ya moja kwa moja ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kwamba, Bunge letu Tukufu lilipitisha sheria hapa ya kodi ya majengo, ambayo Mamlaka ya Mapato Tanzania inasaidia Halmashauri kukusanya na kwamba sasa hivi kama sheria ile ilivyoainisha, Mamlaka ya Mapato wangeanza kutoza na kupata uzoefu katika Wilaya tatu za Dar es salaam, wako kazini na wanaingia mwaka wa tatu sasa. Wamepewa kipindi cha miaka mitano na baada ya hapo basi, ndipo watakapokwenda kwenye miji mingine na sehemu nyingine za nchi au Halmashauri nyingine za nchi. Pia programu nyingine ambayo ipo na inafanyiwa maandalizi ni uwezekano wa Halmashauri zetu kukopa kwa kutumia Hati Fungani (*Municipal Bonds*), lakini hizi nazo siyo kitu rahisi kukifanya. Kuna aina mbili za Hati Fungani; kuna aina moja ambayo ni lazima Serikali Kuu itoe dhamana kwa Halmashauri hizi kukopa. Sasa kuna kazi kubwa ya kufanya, kuzirekebisha Halmashauri zetu kufikia kiwango cha kuweza kukopa kutoka kwenye Soko la Fedha halafu Serikali Kuu idhamini, maana kwa kufanya hivyo, ni kwamba Serikali Kuu inakubali hilo deni pale ambapo patakuwa na kutokulipwa. Nyingine ni Hati Fungani ambazo zinatolewa ambazo zinalipwa kutokana na pato la miradi ambayo zile fedha zinazokopwa kuitia zile Hati Fungani zinakwenda kuanzisha. Programu hii inakwenda vizuri na tunatarajia kwamba, siku za usoni tutafika mahali ambapo Halmashauri zetu zitaweza kukopa kwa njia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limesemewa sana ni ulinganishi wa kukua kwa uchumi, lakini eti kwamba umaskini au hali ya Mtanzania haijabadilika. Hapa naomba niseme kwamba, ni kweli kwamba, uchumi wa nchi yetu umekua kwa wastani wa takriban asilimi saba katika miaka 10 iliyopita.

Tunakumbuka kwamba, kwa mfano; mwaka 2008 uchumi wetu ulikua kwa asilimia 7.4, lakini kwa sababu ya msukosuko katika Sekta ya Fedha na Uchumi Duniani, imebidi sasa kurekebisha makadirio yetu ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka uliopita wa 2009 kufikia asilimia 5 tu. Bado ni wastani wa juu, ukilinganisha na makadirio ya kukua kwa uchumi wa dunia ama nchi nyingine ambazo zinatuzunguka. Hoja hapa ni kwamba, maisha ya Mtanzania wa kawaida nayo yawe yameboreka kwa kiwango ambacho kinakaribia kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokubali ni kwamba, kuna uhusiano mkubwa kati ya kuongezeka ama kukua kwa shughuli za kiuchumi na kupungua kwa umaskini. Hiyo tunakiri, katika kipindi cha miaka ya 1990 uchumi wetu ulikua kama ambavyo imesemekana kwa asilimia tatu kwa mwaka, huo ndio ulikuwa wastani kwa miaka 1990, lakini utafiti wa matumizi ya kaya uliofanyika mwaka 1990/1991 ulionesha kwamba, asilimia 34.6 ya Watanzania walikuwa wanaishi chini ya mstari wa mahitaji ya msingi. Kwa maana nyingine, asilimia 65.4 walikuwa juu ya huo mstari, kwa hiyo walikuwa na maisha ambayo yanakubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, katika Mkutano huu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili kwa kina Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2010/2011 hadi 2012/2013. Napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe Naibu Spika, pamoja na Mwenyekiti aliyeuwepo wakati nawasilisha Mwongozo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kuongoza kwa hekima kubwa mjadala wa Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Muda wa Kati. Kwa kiwango kikubwa, busara zenu zimetuwezesha kupata maoni ambayo yataboresha Mwongozo na hatimaye kuwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa, kutayarisha Mipango na Bajeti zao kwa ufanisi zaidi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao ambayo itasaidia sana katika kukamilisha Mwongozo huu. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa michango yao muhimu sana na ambayo itasaidia kuboresha Mwongozo huu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kujadili Mwongozo huu wa Utayarishaji Mpango wa Bajeti ya Serikali, Waheshimiwa Wabunge wamepata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza humu ndani na vile vile kwa maandishi na wengi sana wamechangia kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuataa:-

Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda - Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Jeremiah Sumari - Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Daniel Nicodemo Nsanzugwanko, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Luaga Mpina, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Balozi Dkt. Getrude Mongella, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Juma Njwayo na wa mwisho alikuwa Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia. Kama kuna mtu tumemsahau ningeomba nikumbushwe ili tuweze kumtaja. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wafuatao walichangia kwa maandishi:-

Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Salum Hemed Khamis, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakiyembe, Mheshimiwa Salum Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qasmi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Maida Abdallah.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Luaga Mpina, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Halima Mdee.

Naomba kutangaza kwamba, Mheshimiwa Anastazia Wambura alichangia pia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maoni mengi yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, yalikuwa yanashabihiana. Kutokana na hali hiyo, ninaomba kutoa ufanuzi wa ujumla kwa baadhi ya hoja zilizotolewa kama ifuatavyo:-

Hoja mojawapo ilihu hali ya kufanya tathmini ya Mipango na Mikakati ya Kitaifa ili kujua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, changamoto zilizojitokeza na mwelekeo unaopaswa kufuatwa. Napenda kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali imekuwa ikifanya tathmini mbalimbali za utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya Taifa ikiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Mwaka 2015, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015, pamoja na MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hizo zimetuwezesha kujua malengo yaliyofikiwa hadi sasa kama vile kasi ya ukuaji wa uchumi, kiwango cha ukusanyaji wa mapato, kiwango cha kuandikishwa wanafunzi kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu, pamoja na ajira zilizopatikana kutokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Vile vile

changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mipango na mikakati hiyo zimeainishwa na hivyo kusaidia katika kuandaa vipaumbele na mikakati mipyä ikijumuisha awamu ya pili ya MKUKUTA na mipango mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja juu ya upangaji wa vipaumbele, Waheshimiwa Wabunge wengi wamefanua vizuri kwamba, Taifa halina budi kuweka kipaumbele cha kwanza katika huduma za kiuchumi na cha pili katika huduma za kijamii. Ushauri huu umezingatiwa kwenye Mwongozo na sekta za uzalishaji zinapewa kipaumbele ili ziweze kutupatia mapato endelevu ambayo yatatumika kugharimia shughuli nyingine za kutoa huduma za jamii kama elimu, afya na maji. Nashukuru kwamba, Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili, kuna waliounga mkono vipaumbele tulivyovileta Serikalini moja kwa moja. Kuna wale walovichambua kwa kina na kutuelekeza nini tufanye. Nataka kuwaahidi kwamba, ushauri wote tulioopata tutautekeleza na Mwongozo huu utaboreshwu kwa faida ya Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wananchi kuwezesha kupata matrekta makubwa badala ya *power tillers*, Serikali inaanadaa utaratibu wa kuwawezesha wakulima kukopa matrekta makubwa kutoka kwa wauzaji, ikiwa ni pamoja na kuanzisha vituo vitakavyosaidia kukodisha matrekta wakati wa kulima na kufanya matengenezo, kwa watakaokuwa wamekopa matrekta hayo. Kuhusu maeneo yenye matatizo maalum kama utoaji wa huduma, kuanzia mwaka 2009/2010 Serikali imeanza kutenga fedha za kusaidia Halmashauri ambazo zina mazingira magumu kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi na hosteli za wanafunzi na kuziwekea umeme wa nguvu za jua na pia kwa ajili ya ununuzi wa boti ili kurahisisha usafiri katika maeneo kama vile Rufiji Delta na visiwa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kutekeleza Agizo la Mheshimiwa Rais la Utafiti kutengewa asilimia moja ya Pato la Taifa katika kipindi cha muda wa kati. Serikali itatenga fedha kuendeleza utafiti katika sekta mbalimbali na vile vile itaendelea kuimairisha Mfuko unaojulikana kama *The National Fund for Advisement of Science and Technology*, ambao unasimamiwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Matokeo ya hili yataatuwezesha kujua kwa undani ni sekta zipi hasa zinahitaji utafiti na kwa hiyo ziweze kutengewa ile asilimia moja. Kuhusu hoja ya kushuka kwa mapato ya Serikali katika Bandari ya Tanga, hali hii inasababishwa na kupungua kwa idadi ya meli zinazoleta mafuta ya petroli katika Bandari hiyo na makampuni mengi yanayoagiza mafuta ya meli kubwa kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji ambazo zimekuwa zinashushchia mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na baadae kuyapeleka Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, takriban michango yote ya Waheshimiwa Wabunge, imeelekezwa katika maeneo ya vipaumbele hususan kilimo, mifugo, uvuvi, miundombinu, ardhi, nishati, huduma za jamii, elimu, maji, afya pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Maeneo yaliyotajwa na Waheshimiwa Wabunge, ndiyo vipaumbele vya Mwongozo na Mpango na Bajeti niliyowasilisha. Maelezo ya kina yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika maeneo haya, yatazingatiwa katika maandalizi ya Mipango na Bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, kwa masuala yanayohusu kuongeza mapato, Kamati ya Kupitia Mfumo wa Kodi ambayo inaratibiwa na Wizara yangu, itayashughulikia kwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nawasilisha maelezo yangu kuhusu Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti, nilieleleza kuwa baada ya kupokea michango ya Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo utakamilishwa na kusambazwa kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa ili waweze kuandaa Mipango na Bajeti zao kwa mwaka wa fedha ujao na kipindi cha muda wa kat. Mpango wenyewe na Bajeti utawasilishwa hapa Bungeni mwezi Juni 2010, baada ya kupitiwa na Kamati mbalimbali za Bunge lako Tukufu. Napenda kuwashakikishia kuwa, maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge yatazingatiwa katika kukamilisha Mwongozo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi na zile za msukosuko wa kiuchumi duniani, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na matatizo hayo kama nilivyoeleza kwenye Mwongozo. Matumaini ya Serikali ni kuwa, hatua zilizoandaliwa katika Mwongozo huo zitawezza kutuvusha katika matatizo hayo. Pamoja na kwamba, Serikali imejizatiti kuchukua hatua hizo, ushiriki wa Wananchi na Waheshimiwa Wabunge ni muhimu katika kufanikisha azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikiri kwamba, wakati nasikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge, nimejifunza kwamba ndani humu tuna wenzetu wataalamu wa mambo mbalimbali, nimejifunza kwamba kuna wataalamu wa mambo ya mazingira. Ningewaomba wakati tunakamilisha Mwongozo huu na kwa sababu mambo haya ya tabianchi wale wenzetu waliojaliwa kujifunza, mnakaribishwa ofisini kwangu ili kwa pamoja tuweze kuandaa Mwongozo ambao utakuwa na faida kwa wananchi. Sasa hili si kwa mazingira peke yake, pamoja na wale wataalamu wengine. Nimeona kuna Wabunge amba ni wataalamu kweli kweli katika maeneo kadhaa. Sisi pale Hazina pamejaa Wachumi, *Financial Analysts*, watu wa *Statistics, Micro Economics*, kwa hiyo hatuwezi ku-pretend kwamba tunajua kila kitu. Tunawaombeni wote wenye utaalamu, mnakaribishwa pale Hazina ili tuweze kusaidiana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kuwekeza katika michezo na kukuza vipaji vya wanafunzi kuanzia mashulen; Serikali inaendelea kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Michezo kwa kushirikisha wadau mbalimbali katika ngazi za Shule, Vijiji, Kata, Wilaya, Mikoa na Taifa. Aidha, suala hilo tayari limeainishwa katika maeneo ya Mwongozo wa Muda wa Kati mwaka 2010/2011 hadi 2012/2013. Serikali imechukua ushauri uliotolewa na tutaufanyia kazi wakati wa kuandaa Mipango na Bajeti Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Mwongozo huo utakaotayarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzingatiaji wa muda katika kutoa huduma kwa umma na kutekeleza miradi ya maendeleo; ni kweli kwamba, kuna tatizo la baadhi ya watumishi kutozingatia muda katika kuhudumia wananchi. Hata hivyo, Ofisi zimeandaa Mikataba ya Huduma kwa Wateja ili kuhakikisha huduma hizo zinatolewa na mategemeo yetu ni kwamba, hali hii inaweza kuboreka katika muda si mrefu. Kuhusu ubadilishaji wa maslahi ya watumishi, mishahara na marupurupu, Serikali itaendelea kuyaboresha hatua

kwa hatua kulingana na uwezo wake kifedha. Kuhusu hoja ya wakulima wa kahawa ambao hawajafidiwa hasara iliyotokana na msukosuko wa kiuchumi duniani, Serikali inaendelea kulishughulikia suala hili ili kutoa udhamini wa kusogezza mbele muda wa kurejesha mikopo hiyo. Nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akijibu swali jana, alielezea kwa ufasaha sana hili tutalifuatilia. Ni imani yangu kuwa, ufumbuzi wa suala hili utapatikana mwezi huu wa Februari, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatua ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Serikali inaendelea kuhuisha Mipango na Bajeti yake kwa kujumuisha maeneo makuu manane, ambayo yamelengwa kufikiwa ifikapo mwaka 2015. Malengo hayo yanalenga kutatua changamoto kuu za kimaendeleo. Kwa ujumla, Tanzania ipo mbele katika utekelezaji wa baadhi ya Malengo ya Milenia ikilinganishwa na nchi nyingine zinazoendelea. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo, nchi yetu bado inahitaji juhudzi za ziada katika kufikia Malengo ya Milenia kwa asilimia mia moja.

Kwa upande wa elimu kwa wote, Tanzania imekuwa ni nchi ya mfano katika eneo la uandikishaji wa watoto wanaoanza elimu ya msingi. Aidha, kwa upande wa ushirikishwaji wa wanawake katika ngazi za maamuzi, tayari idadi ya wanawake wanaoshiriki katika ngazi hizo imekuwa ikiongezeka kwa kasi zaidi pengine kuliko nchi nyingine. Kwa mfano, hadi sasa Wabunge Wanawake wamefikia asilimia 33 ya Wabunge wote katika Bunge la Tanzania. Aidha, hali kama hiyo ipo katika sekta nyingine mbalimbali. Vile vile suala la uhifadhi wa mazingira nalo linaendelea vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya mfumko wa bei; katika maelezo yangu wakati nawasilisha Mwongozo nilionesha kwamba, mfumko wa bei mwezi Desemba 2009 ulifikia asilimia 12.2 ikilinganishwa na asilimia 13.5 Desemba, 2008. Tathmini inaonesha kwamba, kasi ya mfumko wa bei ilikuwa ni wastani wa asilimia 12.1 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 10.3 mwaka 2008.

Nilitoa sababu ya kwamba, kulikuwa na uhaba wa chakula nchini na kwa baadhi ya nchi jirani kutokana na ukame. Ni matarajio ya Serikali kwamba, bei za vyakula zitashuka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kuongeza uzalishaji, pamoja na jitihada nyingine za kuboresha miundombinu ya usafiri na uwezekano wa kutumia Hifadhi ya Taifa ya chakula ili kuleta utengamano wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufuatiliaji wa mashirika na mali za umma zilizobinafsishwa, Serikali ilifanya uchambuzi wa mwenendo wake na kubaini hoja ya kuwa na utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya ubinafsishaji, *yaani Post Privatisation Valuation and Monitoring* na kushauri kuanzishwa kwa vitengo vya kufuatilia zoezi la ubinafsishaji katika kila Wizara yenye Mashirika yaliyobinafsishwa.

Nilimsahau Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, alichangia pia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kushirikiana na *Consolidated Holding Corporation*, imeanzisha Kitengo Maalum and *Post Privatisation*

Unit chini ya Consolidated Holding Corporation, kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa ubinafsishaji kufuatana na mipango ya uwekezaji *and Business Plan* kwa mujibu wa mikataba ya uuzaaji. Kitengo hiki kinawashirikisha pia Wataalam wa Wizara Mama husika na kimeanza kutembelea Mashirika na mali zote zilizobinafsishwa kwa lengo la kufuatilia *compliance* na kupendekeza hatua za kuchukuliwa kwa mujibu wa kinachojili katika ukaguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mahusiano kati ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Milenia, Ilani ya Uchaguzi ya CCM na MKUKUTA, tayari mahusiano yapo na yameainishwa kwenye Mwongozo huo kama ulivyowasilishwa hapa jana. Kuhusu hoja ya kuifanya Serikali ifanye utafiti juu ya idadi ya rasilimali watu tulionao na fani zao ni kweli kuna umuhimu wa kufanya utafiti huo; hivyo, suala hilo tumelichukua na tutalipeleka kwa mamlaka husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Matumaini yetu ni kwamba, wakati tunaleta hapa mpango kamili, hili litakuwa limeshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kuanza kwa utekelezaji wa Miradi ya *Millennium Challenge Corporation* ili kurudisha imani ya wananchi, Serikali imekamilisha maandalizi yote ya awali na hivyo kazi ya ujenzi itaanza wakati wowote kuanzia sasa. Nataka kuwajulisha kwamba, fedha za *MCC* tayari tumeahidiwa kwamba, zitaanza kupatikana wakati wowote, kwa hiyo miradi yote ile ambayo itafadhiliwa na *MCC* kule kote ambapo wenzetu wanajua kuna miradi ya namna hiyo, wakae tu mkao wa kula, wakati wowote miradi hiyo inaweza kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uamuzi wa Serikali kuzuia Wananchi wa Mikoa fulani Fulani, kwa mfano, Rukwa wasiuze mazao yao nchi jirani; kimsingi, Serikali ilifanya uamuzi huo kwa dharura maalum iliyokuwepo ili kunusuru nchi isikumbwe na uhaba wa chakula kutokana na baa la njaa lililokuwa limejitokeza. Tungeruhusu chakula kiuzwe kiholela, sasa hivi hata ule mfumko wa bei niliokuwa nauzungumzia, ungekuwa umefikia hali ambayo haingekuwa nzuri hata kidogo. Ninataka kusisitiza kwamba, ule ulikuwa ni uamuzi wa dharura. Kwa hiyo, Serikali itafanya marejeo na tutaona tutafanya uamuzi gani tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, Katibu Mkuu Alhaj Ramadhan Khijjah, Naibu Makatibu Wakuu; John Haule, Nashon Msongole na Dkt. Phillip Mpango na Watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na Wizara nydingine, ambao wamewezesha kukamilika kwa kazi hii. (*Makofî*)

Baada ya maelezo haya, naomba kuwashukuru tena kwa michango yenu kuhusu Mwongozo, Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2010/2011 hadi 20012/2013. Nataka kurudia kusema kwamba, michango ilikuwa mingi, mizuri, inayaoelimisha, iliyojaa hekima na iliyojaa utaalamu, tusingeweza kujibu kila kilichozungumzwa hapa Bungeni. Yote tumeyachukua tumeyanakili, nadhani *Hansard* tutaipata na wale walioituandikia tunayo yote na naahidi kwamba, yote yatashughulikiwa na Mwongozo wetu wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Mwaka 20010/2011 na Mpango wa Kati wa

Mwaka 2012/2013 utaboreshw na mtakuja kuona wenyewe tutakaporudi hapa mwezi Juni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Mwongozo wa Mpango na Bajeti Ulipitishwa na Bunge*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mimi binafsi napenda nichukue nafasi hii, kuwapongeza kwa mijadala ambayo ilikuwa ni ya hali ya juu sana. Wasiwasi wangu ulikuwa kwamba, leo ninatafuta maji kijiji fulani, sijui nini kijiji fulani, kwa kweli haikutokea hivyo. Kwa hiyo, nadhani tumekwenda sawa sawa na mahitajio ya Mpango wenyewe tuliokuwa tumeishauri Serikali katika maeneo yale tunayoyaita *Micro Economics*, kitu ambacho kimekuwa *impressive*. Nilikuwa na wasi wasi, tunaanza hapa, tena mwaka wa mwisho si unajua. Mimi mto wangu, mimi daraja, sijui hospitali, nilikuwa nafikiri kitakuwepo, lakini bahati nzuri hamkufanya hivyo, jambo ambalo nadhani yamekuwa majadiliano ya hali ya juu sana. Kwa hiyo, naomba niwapongeze. (*Makofî*)

Mheshimiwa Waziri usingeweza kujibu zaidi ya hivyo ulivyojibu, kwa sababu yote waliyokupa ni ya ushauri; kwa hiyo vile ulivyo fanya *summary* yako nadhani umekidhi mahitaji ya kikao hiki. Naomba niwapongeze wote kwa uvumilivu na juhudhi nyingi, nina matangazo machache. Kwanza kabisa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kesho tarehe 6 kuanzia saa 10 jioni katika Ukumbi Na. 231 kutakuwa na Mkutano wa Kamati hiyo kujadili Azimio la Bunge linalohusu Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*). Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati, tunaomba wahudhurie kwa sababu taarifa tulizonazo ni kwamba, Wajumbe huwa hawahudhurii na ipo kwenye kanuni zetu, kama Mjumbe hahudhurii vikao idadi iliyotajwa kwenye kanuni na Kamati ya Bunge adhabu yake ni kubwa. Kwa hiyo, nategemea kwamba, Wajumbe mtakumbuka kesho saa 10.00 jioni Kamati ya Uchumi na Fedha, mnapaswa kwenda kuhudhuria kikao hicho katika Ukumbi Na. 231.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma kwa Wabunge, Mama Kitolina Kippa, anaomba niwatangazie Wabunge wote kuwa, Chama cha Mtando wa Kutokomeza Ukeketaji Tanzania, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, wanawaalikeni kwenye maandamano ya kupinga ukeketaji, yatakayofanyika kesho tarehe 6 Februari, 2010 kuanzia saa 2.00 asubuhi. Maandamano haya yataanzia Shirika la AFNET kuelekea Barabara ya Nyerere hadi Polisi Jamii; kwa hiyo, nyote mnakaribishwa saa 2.30 asubuhi.

Halafu Waandishi wa Habari walikuwa wameniandikia *ki-note* asubuhi kwamba; je, wanakaribishwa kwenye ile semina ya kesho ambayo tulisema kuna semina ya APNAC kule *African Dreams* kuhusu Muswada wa Kuchangia Gharama za Uchaguzi? Sasa nilipata kwa wahusika hili siyo tangazo la waandaji wa hiyo semina, wanasema kwamba, Waandishi wa Habari wanaopenda watafika kwenye ufunguzi halafu basi; lakini kuna Waandishi wengine 10 ndiyo wamealikwa kutoka TTV, ITV, Star TV na Magazeti. Ninadhani walioalikwa wanazo barua za mwaliko; kwa hiyo, najibu hoja waliyioleta Waandishi wa Habari, msiende kugombana; kuna Waandishi 10 walioalikwa na nina hakika wamealikwa kwa barua.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kesho hatutakuwa na kazi za Bunge kama Bunge; hivyo, ningeshawishi wengi sana mshiriki kwenye ile semina kwa sababu itatusaidia kutupa upeo zaidi kuhusu Muswada wetu na tunakwenda kujadili baada ya kuboreshwa. Kwa hiyo, kama ninavyosema siyo busara kuukataa; ni busara kuuchambua na kuubadili kufuatana na mnavyoona inafaa. Kwa sababu ule Muswada ni muhimu sana kwa maana ya demokrasia yetu na pia kwa sura nzima ya nchi; kwa nini watu wawe huru sana kutumia fedha ambapo hatuwezi kuelewa nadhani hata kama tutakuwa na matatizo lakini m jitahidi kuboresha ule Muswada.

Baada ya kusema haya, *nili-note* kwamba, wengi hamkupata mabadiliko ya ratiba, nadhani kwa sababu mabadiliko yamekuwa mengi; kwa hiyo mmechanganya. Siku ya Jumatatu tutakuwa na kipindi cha maswali kama kawaida halafu tutakuwa na Maazimio yafuatayo; Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya Mabadiliko katika baadhi ya vipengele vya Mkataba ulioanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), ndiyo maana Kamati inaomba kesho Wajumbe wake wakutane saa 10.00. Halafu kuna Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Maji ya Bonde ya Mto Zambezi; Azimio lingine ni la Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za *SADC*. Matangazo mengine yatafuatia siku hiyo hiyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, siku hiyo mjue kutakuwa na Maazimio haya, wanaotaka kuijandaa jiandaeni vizuri yataingia Siku ya Jumatatu.

Baada ya kusema hayo, nawashukuru kwa wiki nzima mmefanya kazi kwa bidii sana na kwa utulivu mkubwa. Ninawatakia *weekend* njema na jioni njema. Ninaahirisha Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.30 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 8 Februari, 2010 Saa Tatuu Asubuhi*)

